# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 16 Mei, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Afya, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa niaba yake Mheshimiwa Tecla Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Mchinga, swali lake litaulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 197

### Hitaji la Ukarabati Shule ya Msingi Kingurungundwa – Mchinga

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA K.n.y. MHE. SALMA R. KIKWETE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa katika Shule ya Msingi Kingurungundwa iliyopo Mchinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsate sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Mchinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna shule za msingi kongwe 2,147 nchini ambazo zilianzishwa kabla ya kupata Uhuru mwaka 1961. Hali ya miundombinu ya shule hizo ni mseto zikiwemo zenye hali nzuri na nyingine zenye miundombinu chakavu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeanza kufanya tathimini ya hali ya miundombinu ya shule zote za msingi kupitia mradi wa *BOOST* ili kubaini mahitaji ya ujenzi wa miundombinu mipya ya shule na hali ya uchakavu wa miundombinu iliyopo. Tathimini hiyo imeanza mwezi Aprili, 2022 na itakamilika mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tathimini hiyo yatatumika kuandaa mpango wa uendelezaji na ukarabati wa miundomibinu ya shule za msingi kwa miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026 ikiwemo Shule ya Msingi Kingurungundwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Lakini kutokana na umuhimu wa shule hii, kama ilivyoelezwa hapa; kwamba ni ya muda mrefu sana; na naona hapa majibu yote yaliyotoka ni ya jumla jumla.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kuomba ni *commitment* ya Serikali; je, Shule hii ya Kingurungundwa ni lini italetewa fedha kufanyiwa ukarabati? Kwa sababu hali ya shule hii ni mbaya zaidi kuliko hizo shule nyingine ambazo umezijumuisha kwenye majibu yao. Naomba kupata *commitment* ya Serikali, hii Shule ya

Kingurungundwa ni lini italetewa fedha ili ifanyiwe ukarabati mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tulijibu katika jibu la msingi, kwamba, mpango wetu wa sasa ni kuzifanyia tathmini shule zote ikiwemo shule ya Kingurungundwa. Tukishamaliza mchakato; maana yake ni kuanzia mwaka huu wa fedha mpaka mwaka 2025/2026. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tutafanya mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha shule hiyo inafanyiwa ukarabati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Na mimi napenda kuuliza swali moja la nyongeza; Shule ya Msingi Chunya Mjini pamoaja na Shule ya Msingi Chunya Kati ni shule kongwe ambazo zilikuwepo tangu kabla nchi yetu haijapata uhuru. Shule hizi zimechakaa sana baaddhi ya majengo yameanguka.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili ukarabati wa majengo hayo uweze kufanyika na ziweze kurudi katika hali kama shule nyingine ambazo zinajengwa sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kitu kikubwa ambacho nikukuhakikishie tu kwamba miongoni mwa shule ambazo ziko katika mpango hizi ni mbili ambazo umezianisha Mheshimiwa Mbunge, na tutahakikisha baada ya tathmini tutazipa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba zinajengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini Shule ya Msingi SUA ambayo ina matatizo ya upungufu wa vyuo itafanyiwa ukarabati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tathmini yetu itaisha mwezi Julai 2022 na tutakuwa na shule zote nchini, ikwemo ya Shule ya Msingi SUA ambayo ameiainisha hapa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba mara baada ya hiyo tathmini kila mmoja atajua shule yake inahudumiwa lini. Ahsante sana

**SPIKA:** Ahsante sana, Francis Leornad Mtega, Mbunge wa Mbarali sasa ulize swali lake.

Na. 198

**Serikali Kuligawa Jimbo la Mbarali**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italigawa Jimbo la Mbarali na kuwa na Halmashauri mbili ili kusogeza huduma karibu na wananchi?

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis leonard Mtega Mbunge wa Jimbo la Mbarali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, halmashauri huanzishwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014. Mwongozo huo umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kuanzisha Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hii, hatua ya awali inahusisha kupata ridhaa ya vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata, Baraza la Madiwani la Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)*. Baada ya hatua hii, maombi hayo yanawasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na tathmini na kuwasilishwa kwa mamlaka husika ili itoe uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais TAMISEMI haijapokea maombi ya kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali. Hivyo, nashauri taratibu za uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala zifuatwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtega.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu maziuri ya Mheshimiwa Waziri, na ya kueleweka nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mchakato wa huu ni mrefu, je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuna ulazima wa kuongeza vyombo vya usafiri katika Halmashauri ya Mbarali, hasa kwenye sekta ya elimu, afya, TASAF na kadhalika ili waweze kuwahudumia wananchi kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa *TARURA* ipo chini ya TAMISEMI, je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kuwa kuna ulazima wa kuhamasisha hii TARURA sasa ikarabati zote zilizoharibiwa na mvua kubwa iliyokuwa inanyesha kipindi kilichopita, ili wananchi waweze kupata huduma za kijamii kwa urahisi na pia kusafirisha mazao yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Leornard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kuhusu usafiri. Nimhakikishie tu kwamba Ofisi ya Rais TAMISEMI tumeshaanza huo mchakato. Mwaka jana tuligawa magari, kwa maafisa elimu sekondari, na mwaka huu vilevile tumeshaagiza magari mengine 184 kwa ajili ya maafisa elimu wa shule za msingi ambayo tumeshapata awamu ya kwanza 35 na mengine yanakuja, lakini yote yameshalipiwa.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo tunatoa magari kwa ajili ya wahandisi wa *TARURA* wa halmashauri, lakini vilevile tutapeleka *ambulance* katika halmashauri zote nchini ambazo zina hospitali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jukumu hili la kusadia Halmashauri nchini ikiwemo ya Mbarali lipo katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu kumalizia ukarabati wa barabara za *TARURA*, tumelichukua hilo katika bajeti yetu na kwamba tutahakikisha kwamba zinajengwa kulingana na mahitaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo tangu mwaka 2017, ilipitia taratibu na vigezo vyote vya kuweza kugawa jimbo. Lakini changamoto iliyorudishwa ni Kamba kuna idadi ndogo ya watu. Je, Serikali itakuwa tayari kuigawa hii halmashauri, baada ya sensa ya mwaka huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Kilolo, ilikuwa imekidhi vigezo vingine isipokuwa ya idadi ya watu; na kinachosubiriwa ni kujua hiyo idadi watu. Mimi ninaamini kwamba kama vigezo vitafikiwa basi mapendekezo yatapelekwa huko mbele na mamlaka husika italiangalia. Kwa hiyo, tusubiri vigezo vikishakuwa vimekamilika, basi hatua hiyo inaweza kukubalika baadaye. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini sasa Serikali italigawa Jimbo la Sumbawanga Vijijini ambalo hata Mwenyezi Mungu aliligawa kati kati, Ufipa wa Chini kata 13 na Ufipa wa Juu kata 14. Sasa ni lini Serikali italigawa jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilijibu katika swali la msingi, ni kwamba wafuate tu utaratibu na sisi tutazingatia endapo

hizo halmashauri zimetimiza vigezo vyao, na baada ya hapo maana yake sisi tutapeleka katika mamlaka husika kwa ajili ya maamuzi. Kwa hiyo, kikubwa tu waanze mchakato halafu mamlaka husika italiangalia hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa uamuzi wa mwisho wa Serikali kugawa halmashauri, wilaya na mikoa ulifanyika mwaka 2012, takribani miaka kumi iliyopita, na kwa kuwa maeneo mengi sasa hivi yana sifa kabisa za kugawiwa, mfano Mkoa wa Tabora, Morogoro, Tanga na mikoa mingine mikubwa na baadhi ya wilaya ambazo ni kubwa kama Sikonge na Mbeya.

Je, maamuzi mengine ya Serikali tuyategemee lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephat Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kwamba Serikali ilifanya maamuzi ya mwisho, mwaka 2012, na muda ambao umepita mpaka sasa hivi ni miaka kumi na bado Serikali inapitia na kutathmini kuona haja ya kuongeza endapo maeneo ya utawala, ama tuendelee na sasa ili tuendelee kuyaboresha na kuwa bora. Kwa hiyo, naamini kabisa Serikali uamuzi wake mpaka sasa hivi upo sahihi na bado tunazingatia; na siyo kwamba mwaka 2012 ndiyo ilikuwa mara ya mwisho. Bado huo mchakato utaendelea baada ya kuona mahitaji ya wakati wa sasa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Wilaya ya Tunduru ilianzishwa mwaka 1905 na mpaka leo bado ni kubwa kulinganisha na wilaya zingine; na kwa kuwa vikao vyote vinavyohusu kugawa halmashauri ile limefanyika mpaka ngazi

ya mkoa; na kwa kuwa Tunduru Kusini ndilo jimbo ambalo linaathirika sana kwa kutokuwa na halmashauri. Je, Serikali itaanzisha lini halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Idd Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, kwamba halmashauri ambazo zimeshamaliza mchakato, bado Serikali inaendelea kupitia vigezo na kutathimini, ili kuona kama haja ya kutangaza kwa wakati uliopo ama tuendelee kuboresha zile halmashauri ambazo ni changa. Kwa hiyo jambo hilo lipo katika ofisi zetu na wasubiri wakati ambapo itakuwa tayari kufanya hivyo, tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kusogeza huduma kwa wananchi. Je, ni lini Serikali itaongeza idadi ya tarafa katika Wilaya ya Nyamagana na Ilemela kwa kuwa zina kata zaidi ya kumi na tano na zina tarafa moja moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Furaha Matondo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuongeza maeneo ya utawala ni moja ya jukumu la Serikali ambalo tumekuwa tukilifana mahali ambapo pana vigezo vyote. Kwa hiyo, kama kunakuwa na eneo halina vigezo maana yake tunakuwa hatuna hiyo fursa ya kuongeza. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Furaha Matondo kwamba endapo maeneo hayo yaliyoainishwa yakifuata taratibu zote na zikafika katika Serikali Kuu, basi Serikali itazingatia kulinga na vigezo vilivyowekwa kikatiba. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mariam Azzan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 199

**Mikakati ya Kulinda Vyanzo vya Maji**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakomesha shughuli za ukataji miti, kilimo na ujenzi karribu na vyanzo vya maji ili kulinda vyanzo vya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imekamilisha uandaaji wa Mipango ya Muda Mrefu ya Kuhifadhi Vidakio vya Maji *(Catchment Conservation Plans)* katika mabonde yote tisa nchini. Mipango hiyo imeweka dira, vipaumbele na utaratibu mzuri wa utunzaji wa vyanzo vya maji

katika maeneo ya vidakio vya maji na mipango hiyo itatekelezwa hadi mwaka 2035.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuhakikisha inakomesha shughuli za ukataji miti kilimo na ujenzi karibu na vyanzo vya maji, hadi sasa jumla ya vyanzo vya maji 191 vimewekewa mipaka ikiwa ni hatua za kuzuia shughuli za kibinadamu katika vyanzo hivyo na vyanzo 44 vipo katika hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili vilindwe kisheria. Vilevile, jumla ya Jumuiya za Watumia Maji 162 zimeanzishwa katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuwashirikisha wananchi katika shughuli za utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji itaendelea kutolewa kwa wananchi ili wafanye shughuli za kiuchumi katika maeneo ambayo hayana athari kwa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na sheria zote zilizonukuliwa katika Ofisi ya Waziri. Je, Ofisi hiyo inashirikiana vipi na Ofisi ya TAMISEMI, Ardhi, Kilimo na Mifugo katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji vinahifadhiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa nini Serikali isianzishe tuzo maalum kwa ajili ya vijiji na Kamati za Maji zinazohifadhi vyanzo hivyo kikamilifu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara tunashirikiana na hizi wizara ambazo tunaingiliana kimajukumu na hili tumeendelea kulifanya hasa katika ziara ya Wizara za Kisekta tumekuwa tukiendelea kutoa elimu ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na tuzo maalum kama nimemsikia vizuri. Tuzo maalum ni moja ya vitu ambavyo tunavitoa kwenye Jumuiya za Watumia Maji. Tunatoa tuzo kwa maana ya kuwapa motisha ili kuona kwamba wananchi wanashiriki moja kwa moja kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji. Vilevile kama ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, kwa niaba ya Waziri, naomba niseme nimepokea, tutaendelea kuongeza nguvu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 200

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi - Wilaya ya Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chemba uliokwama kwenye ngazi ya lenta kwa miaka mitatu sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chemba ulianza mwezi Novemba mwaka 2018. Gharama za jumla za ujenzi huu ni Sh.296,000,000. Ujenzi huo umeshirikisha nguvu za wananchi pamoja na Mdau aitwaye *Local Investment Climate* ambaye alitoa kiasi cha Sh.43,000,000. Ujenzi umefikia kwenye hatua ya lenta na ulisimama kutokana na kukosekana kwa fedha. Kiasi cha Sh.53,000,000 tayari kimeombwa kwenye mfuko wa tuzo na tozo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ili kumalizia ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Nina swali moja tu la nyongeza. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwa sababu mradi huu umeanza muda mrefu sana. Wilaya yetu ya Chemba miji yake mingi ipo pembezoni na ni ukweli kwamba eneo la mjini lina watu wachache sana. Sasa nataka kujua nini mpango wa Serikali wa kupeleka hii huduma ya Vituo vya Polisi kwenye miji hiyo mikubwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Chemba sehemu kubwa ni Wilaya ya Vijijini na ina miji inayozunguka mji wenyewe wa Chemba, pale panahitajika pia utaratibu wa kuimarisha ulinzi kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwahidi tu Mheshimiwa Monni kwamba tulikubaliana nitafanya ziara, moja ya lengo ni kuangalia maendeleo ya ujenzi huu, lakini la pili ni kuangalia maeneo ambayo

kimkakati yanastahili kupewa huduma za kipolisi ili kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Tutakapofika huko Mheshimiwa tutakubaliana ni maeneo gani yapewe kipaumbele. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Wananchi wa Kishapu, Mfuko wa Jimbo wa Mbunge wa Jimbo la Kishapu, lakini pia na wadau wa maendeleo kama Mwadui na wengine wameweza kuchangia jumla ya Sh.53,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inaunga mkono nguvu na jitihada za wananchi na wadau wa maendeleo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tumpongeze Mheshimiwa Butondo kwa kufuatilia kwa karibu masuala yanayohusu usalama wa raia na mali zao na uhamasishaji wa wadau kuchangia hizi fedha. Nimwahidi tu kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi tuna mpango mkakati wa kuimarisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Mikoa na Wilaya ambazo hazina kabisa. Kwa hiyo hali ya fedha itakaporuhusu, Wilaya ya Kishapu ni moja ya maeneo yatakayopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ujenzi wa Vituo vya Polisi unakwenda sambamba na ujenzi wa makazi ya askari ili kuwawezesha Askari Polisi kupata makazi mazuri na kuweza kufanya

kazi zao vizuri. Je, ni upi mpango wa Wizara kusaidia suala la nyumba za askari polisi katika eneo la Kigoma Mjini ambazo ziko katika hali mbaya sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ng'enda, Mbunge wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba askari wanahitaji makazi hususan yawe karibu na vituo vya polisi, lakini tunajua pia kwamba makazi mengi hasa vituo vya zamani ni mabovu, ndio maana kipaumbele kimewekwa kwenye ukarabati wa majengo yaliyochakaa. Hata hivyo, tutaendelea kuimarisha ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya askari kadiri tutakavyoweza kupata fedha kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Saja, Kijombe, Uhenga ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe wako mbali sana na huduma za kipolisi. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi ndani ya Kata ya Saja ili kuwapa unafuu wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Neema amekuwa mara kwa mara anaulizia masuala ya ulinzi, lakini jambo moja

analonivutia ni kwamba kiwango cha uhalifu Njombe hakilingani na maeneo mengine hasa ile ya mipakani. Kwa hiyo niwapongeze wananchi kwa kuzingatia hilo. Kwa hivyo kadri hali ya fedha itakavyoruhusu tutaendelea kuimarisha kujenga vituo vya polisi katika maeneo yanayohitajika ikiwemo hii Kata aliyoitaja ya Saja kule Njombe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chrristina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kilichopo Selamagasi kimejengwa toka enzi ya mkoloni na kimechakaa sana. Je, ni nini mpango wa Serikali kukarabati kituo kile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, Shinyanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu ya baadhi ya maswali ya Wabunge, tunatambua uwepo wa uchakavu mkubwa kwa baadhi ya Vituo vya Polisi kikiwemo hiki alichokitaja.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema alivyosoma hotuba ya bajeti ya Wizara hii mpango wa Serikali kuanza ukarabati wa Vituo vya Polisi na makazi katika mwaka ujao na fedha zimepitishwa, tutaangalia kiwango cha uchakavu ili kuweza kuweka kipaumbele vikiwemo hivi vya Wilaya ya Shinyanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 201

**_CSR_ kwa Halmashauri zinazozunguka Mbuga na Hifadhi za Taifa**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia Halmashauri zinazozunguka Mbuga na Hifadhi kwa kutoa *CSR* kwenye mapato ya utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa Sera ya Uwajibikaji Kijamii *(Community Social Responsibility - CSR),* Serikali inatekeleza miradi ya ujirani mwema kwa jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa zikiwemo Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi za Wanyamapori za Jamii *(WMAs)*. Katika kutekeleza Sera hiyo, Halmashauri za Wilaya pamoja na jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa, zinanufaika na mapato yanayotokana na utalii ikiwemo kupatiwa miradi mbalimbali ya kijamii inayoibuliwa na wananchi kwenye sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya, Sekta ya elimu, Sekta ya Maji na Sekta ya Ujenzi. Miradi hii hutekelezwa na Taasisi za Uhifadhi nchini ambazo ni *TANAPA, TAWA* na *NCAA*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uwindaji wa Kitalii, Serikali pia imekuwa ikitekeleza Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na.5 ya 2009 ambayo inaelekeza kuwa asilimia 25 ya fedha zinazotokana na ada za wanyamapori waliowindwa katika vitalu vya uwindaji wa

kitalii zirudishwe kwenye halmashauri zinazopakana na maeneo ya uwindaji. Aidha, katika maeneo ya *WMAs*, Kanuni za *WMAs* za mwaka 2018 zinaelekeza kuwa asilimia 75 ya ada ya kitalu, asilimia 55 ya ada ya wanyamapori wanaowindwa na asilimia 45 ya gharama za uhifadhi zinazotokana na uwindaji wa kitalii zirudishwe kwa jamii inayomiliki maeneo husika. Wizara imekuwa ikitekeleza matakwa haya kupitia *TAWA*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa nia ni kuleta unafuu kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo; na kwa kuwa halmashauri ndio zinazojua zaidi mahitaji ya watu wale, hatuoni kwamba ni muda sasa tuzipeleke fedha hizo kwenye halmashauri badala ya kutekeleza miradi kama inavyofanyika migodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa katika Mkoa wa Kilimanjaro suala la uoteshaji miti ni hiari, lakini ukataji miti ni suala ambalo lazima upate kibali na miti hiyo wanatumia kwa ajili ya nishati ya moto. Je, Serikali haioni kutafuta namna nyingine ya kuwapatia nishati mbadala kupitia *CSR*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufatilia hizi *CSR* katika eneo lake analowakilisha. Katika swali lake ambalo ameuliza Serikali haioni haja kupeleka fedha katika halmashauri. Kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba halmashauri pia zinapata asilimia na pia wananchi wanapata asilimia. Lengo ni kufikisha hii miradi kwa

jamii ambao ndio hasa walinzi wa haya maeneo ambayo tunayahifadhi.

Mheshimiwa Spika, jamii ikijisikia kwamba ni sehemu ya uhifadhi sisi kama Serikali tunafarijika kwamba wanaona uthamani wa eneo lile na ni rahisi sasa hata unapowaelezea uhifadhi namna yake ni nini na thamani ya uhifadhi ni nini. Kwa hiyo kupeleka kwenye jamii ni muhimu zaidi kuliko kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba uoteshaji wa miti Serikali kupitia hifadhi ya *TANAPA* ilianzisha mradi wa majiko banifu katika eneo linalozunguka Mlima Kilimanjaro. Majiko haya yalikuwa ni fanisi na walienda kufundishwa kaya mbalimbali katika maeneo hayo na pia tumeingia kwenye mpango wa kuanzisha upandaji wa miti katika maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, upandaji huu ulianza toka mwaka jana na sasa hivi ni endelevu. Hivyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu utatekelezwa ambapo wananchi wengi wanaozunguka maeneo hayo watapata miche ambayo itapandwa katika maeneo ya vijiji nje ya hifadhi ili irahisishe kupata nishati mbadala. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nusu ya Wilaya ya Meatu imepakana na Hifadhi ambazo ni Ngorongoro, Serengeti na Maswa *Game Reserve*. Je, ni lini Serikali itaendelea kunufaisha miradi katika Wilaya ya Meatu, miradi ile ilikuwa inatolewa na ujirani mwema kutokana na utalii unaofanywa katika Hifadhi ya Serengeti na Ngorongoro ikiwemo ujenzi wa mabweni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimwambie tu kabisa Mheshimiwa Mbunge kwamba, asiwe na wasiwasi na niendelee kumpongeza kwa sababu wananchi wanaozunguka yale mapori ya akiba tunatambua umuhimu wa namna ya kunufaika na *CSR*. Hata hivyo, kwenye eneo hili Mheshimiwa Leah amekuwa akileta maombi katika ofisi zetu, lakini tutambue tu kwamba katika kipindi cha miaka miwili hii iliyopita tulikuwa tuna changamoto ya UVIKO 19 ambapo hifadhi zetu ziliathirika sana. Hivyo Serikali ilichukua jukumu la kuzisaidia hizi hifadhi ili ziweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeshaanza kuimarika vizuri, *CSR* zitarudi kama ilivyokuwa mwanzo na pengine zaidi hasa ukizingatia *Royal Tour* imeibua mambo mengi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mamlaka ya Wanyamapori *(TAWA)*, imefanya maboresho makubwa Kilwa Kisiwani ambao ni mji wa kitalii na Kilwa Kisiwani imetangazwa kuwa ni sehemu ya urithi wa dunia, lakini makubaliano yalikuwa kwamba wananchi wa Kilwa Kisiwani wapate *CSR* kupitia kujengewa shule pamoja na zahanati, lakini mpaka sasa hawajajengewa shule wala zahanati.

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, swali langu, je, Waziri yuko tayari kufuatilia kuona kwamba shule na zahanati inajengwa Kilwa Kisiwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hili, lakini kama ambavyo nimeeleza mwanzo kwamba kabla ya UVIKO-19 tulikuwa tunatekeleza kupeleka haya maeneo *CSR*, lakini hii changamoto ya UVIKO-19 ndio iliyoturudisha nyuma lakini kwa sasa hivi tumeshaanza kuimarika vizuri. Hivyo nimwahidi Mheshimiwa Mbunge katika eneo lake nitaenda pia nitaenda kuongea na wananchi wa jimbo hilo ili kuwaambia umuhimu wa kupata *CSR* pia umuhimu wa utunzaji wa maeneo ya hifadhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ilikuwa tuelekee Wizara ya Afya lakini tutaelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, halafu tutarejea Wizara ya Afya. Naibu Waziri anayetakiwa kujibu maswali ana udhuru kidogo.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, sasa aulize swali lake.

Na. 205

**Mpango wa Ujenzi wa Reli ya Kusini**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, mpango wa ujenzi wa reli ya Kusini kutoka Mtwara hadi Ruvuma na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma umefikia wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli ya Mtwara-Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma kilomita 1,000. Upembuzi uliofanyika ulipendekeza kuwa utekelezaji wa mradi huo ushirikishe sekta binafsi. Kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za kumwajiri Mshauri Elekezi *(Transaction Advisor)* kwa ajili ya kuandaa Andiko, makabrasha ya zabuni ili kumpata mwekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Spika, aidha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika -*SADC* imeahidi kutoa kiasi cha Dola za Marekani 6,000,000 kwa lengo la kumgharamia Mshauri Elekezi. Utaratibu wa kupata fedha hizi unaendelea na kazi hii inatarajiwa kufanyika Mwaka wa Fedha 2022/2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa mradi huu upo katika mpango wa maendeleo ya miaka mitano. Je, Serikali inaweza kuona kuwa kuna haja sasa ya kuharakisha upatikanaji wa huyo Mwekezaji. Pia kufanya mazungumzo makini ili mradi huo uweze kuanza kwa haraka kwa muda uliokusudiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili,...

**SPIKA:** Umeshauliza maswali mawili kwenye swali lako hilo la kwanza Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kuharakisha mazungumzo ambayo yanaendelea kwa ajili ya mradi

huu wa Liganga na Mchuchuma. Ni kweli majadiliano yameendelea na bahati nzuri sana nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba majadiliano yako katika hatua za mwisho kabisa ili mradi huu uanze utekelezaji wake. Na kwa maana hiyo mara tu mazungumzo yatakapokamilika na sisi upande wa *TRC* kwa kuwa tayari fedha kutoka Umoja wa *SADC* wametuahidi kutoa hizo Dola 6,000,000 na sisi tutaanza utekelezaji wa mradi huu kwa ujenzi wa *standard gauge*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anataka kufahamu kwamba ni lini sasa mradi huu utaanza. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tu mazungumzo yatakapokamilika mradi huu tutaanza utekelezaji wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed Mbunge wa Shaurimoyo sasa aulize swali lake.

Na. 206

***ATCL* kulipa madeni**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED** aliuliza:-

Je, Shirika la Ndege nchini *(ATCL)* limeshaanza kulipa madeni ya Makampuni yaliyokuwa yanatoa huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed Mbunge wa Shaurimoyo kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni ya makapuni yanayotoa ama yaliyokwisha kutoka huduma kwa *ATCL* baada ya kuyafanyia uhakiki. Mwaka 2016 kabla ya Serikali kuanza mpango wa kuifufua *ATCL* Kampuni ilikuwa inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 141.77 na watoa huduma mbalimbali wa ndani na nje.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Serikali imelipa madeni jumla ya shilingi bilioni 127.07.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuiwezesha *ATCL* kulipa madeni yaliyobaki kulingana na uwezo wa kibajeti. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza hivi sasa shirika letu la Ndege Tanzania limeanza safari zake za kubeba mizigo kwa ajili ya safari Guangzhou China, inaondoka China na kupitia Zanzibar na baadaye inarudi Zanzibar. Shirika hivi sasa wanatumia ndege yake ya *Boeing 787* kwa ajili ya kubeba mizigo hiyo. Ndege hii imeundwa kwa ajili ya kubeba abiria na mizigo lakini eneo kubwa ya ndege hii ni kwa ajili ya kubeba abiria. Shirika letu sasa linabeba mizigo bila ya abiria kwa kwenda huko China.

Je, Shirika halioni hivi sasa kuendelea kufanya hivyo ni kuendelea kulitia hasara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la abiria kati ya Zanzibar, Pemba na Dar es Salaam. Je, ni lini Shirika la Ndege la *Air Tanzania* litaanza safari zake katika Kisiwa cha Pemba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. FREDY A. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Juma Mohamed Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna Ndege aina ya *Dreamliner 787-8* ambayo inafanya biashara kati ya Tanzania na China na

Ndege hii imekuwa ikibeba abiria lakini kipindi cha *Covid 19* China kama tunavyofahamu kuingia abiria yeyote ndani ya nchi ya China. Kwa hiyo tukaona ni heri na bora Ndege hii aina ya *787-8 Dreamliner* ambayo ina uwezo wa kubeba tani 40 ifanye biashara ya kubeba mizigo kuliko tungeiacha kuwa *grounded* na ingekuwa gharama zaidi kuliko hivi sasa ambavyo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge anatamani ama anapenda kwamba tuanzishe safari za kwenda Pemba. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wa Zanzibar kwamba Shirika letu la *ATCL* litaanza safari zake za Pemba mwaka wa fedha 2023/2024 kwa maana ya kwamba mwaka ujao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tunaenda Wizara ya Afya. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 202

**Kutatua changamoto Chuo cha Afya Hospitali ya Kitete - Tabora**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya vifaa vya kufundishia na uhaba wa Wakufunzi katika Chuo cha Afya kilichopo Hospitali ya Kitete.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya vifaa vya kufundishia katika Chuo cha Afya Tabora na tayari imepeleka

vifaa vyenye thamani ya Shilingi Milioni 115.7 kwa ajili ya kuboresha mafunzo kwenye chuo hicho. Pamoja na ununuzi wa vifaa hivyo, Serikali imepeleka Shilingi Milioni 267.8 kwa ajili ya ukarabati wa maabara Nne za kufundishia. Aidha, mpaka sasa Serikali imepeleka watumishi 11 wanaofundisha chuoni hapo ili kupunguza upungufu wa wakufunzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwanza ninasikitika sana kwa majibu ya Serikali ya jumla namna hii, kwa sababu mpaka naleta swali hili tayari nilikuwa nafahamu kwamba kuna mapungufu ya Wakufunzi pamoja na vifaa vya kufundishia. Wakati wanafunzi wakiwa 24 ndiyo fedha zilipelekwa, leo kuna wanafunzi zaidi ya 280 hakuna walimu, walimu ni hao unaowasema hawa 11 hao wakufunzi ndiyo waliyopo. Ninaomba nipate *commitment* ya Serikali, ni lini mtapeleka wakufunzi ili chuo hichi kiweze kufanya vizuri kama vilivyo vyuo vingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hizi Maabara zinafanyiwa ukarabati lakini mpaka sasa hata vifaa vya kufundishia kwenye hizi Maabara bado hazijaenda Mheshimiwa Naibu Waziri. Hebu naomba mnipe majibu halisi watu wa Tabora wasikie, ni lini mtapeleka fedha ili vifaa vipelekwe na wanafunzi hawa waweze kupata mafunzo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Afya Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kukipenda chuo chake. Pamoja na swali lake hili Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini aliandika barua, nimuombe sasa *specifically* mimi na yeye tukishamaliza hapa, tukishamaliza leo Bunge hili na tukamaliza bajeti yetu, tuende mimi pamoja na yeye akathibitishe hivi vyote ambavyo nimemwambia hapa. Tutakwenda mimi na wewe, najua ulikwenda ukakuta hayo matatizo na hukurudi tena, baada ya wewe kuuliza hili swali Mheshimiwa Waziri wa Afya alielekeza na kazi imefanyika.

Twende pamoja ili usimamie hizi fedha ambazo zimeshapelekwa uhakikishe zimefanya kazi ambayo wewe ulitegemea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 203

**Serikali kutoa Bima za Afya bure kwa watu wenye ulemavu wa kudumu**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani ina mpango gani mahsusi wa kutoa Bima za Afya bure kwa watu wenye Ulemavu wa kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya imetoa utaratibu wa kusaidia watu wenye mahitaji maalum wasio na uwezo. Hata hivyo Serikali inakamilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ambapo utawezesha watu wote wakiwemo watu wenye ulemavu kupata huduma katika vituo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Taya swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali kwa majibu mazuri na mipango mizuri na mikakati mizuri kwa ajili ya Bima ya Afya kwa watu wote. Naomba niulize swali langu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba watu wenye ulemavu ni watu ambao hawajiwezi wengine. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuweka dirisha maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu kama vile kwa Wazee?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa Bima ya Afya mara nyingine vipimo vingine havifanyiki. Je, Serikali haioni haja sasa kwamba vipimo vya Kansa ya Saratani ya Ngozi viweze kufanyika bure katika hizo Bima ambazo mnaziandaa kuja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, moja amesema kuwa na dirisha maalum kwa ajili ya watu wenye Ulemavu. Hili ni wazo zuri sana tunalichukua, vilevile pamoja na kuwa na dirisha lakini ni katika kila *infrastructure* ya hospitali kwenye wodi na kila mahali kuwepo na sehemu ambazo ni maalum zinazowezesha watu wenye ulemavu kuweza kupata huduma kirahisi kama wanavyopata watu wengine.

Meshimiwa Spika, nimeona vilevile amezungumzia na watu wenye ulemavu wa ngozi. Sasa hivi kwa mfano kwenye Hospitali ya Kanda ya *KCMC* wamepelekwa watu kutoka Hospitali mbalimbali za Mikoa. Moja kujifunza kwa ajili ya kuzalisha dawa maalum kwa ajili ya wale watu wenye ulemavu wa ngozi hasa ile *screening* ile ya kujipaka kwa ajili ya kuzia miale ya jua. Kwa hiyo, hayo yanaboreshwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni suala la kwamba kuna baadhi ya mahitaji ambayo ya kitiba ambayo wanahitaji baadhi ya Walemavu ambayo hayapo kwenye Mfuko wa Bima ya Afya. Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tunaenda kuboresha kuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa watu wote, ni wakati wa muafaka wa sisi kuhakikisha kwamba vitu vyote hivyo vimeingia kwenye utaratibu. Lakini wakati kabla hatujafikia hilo la Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya, naomba mimi na wewe tukae unianishie hayo

mambo maalum ili Mheshimiwa Waziri wa Afya aweze kuyafanyia kazi mapema, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa Bima za Afya kwa wote, je, ni hatua ipi imefikiwa ili kupata Bima hizo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, hatua zilizofikiwa. Kwanza zimefikiwa hatua zote za kitaalam, tuko kwenye hatua ambayo nafikiri uliona Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri wa Afya alileta ushauri wake na akawaleza Wabunge hatua tuliyofikia ambavyo Wabunge mmetoa *input* muhimu na mmeturuhusu tuendelee na mchakato.

Kwa hiyo, hatua ambayo tunaendelea sasa ni zile hatua ambazo kwa kweli inatakiwa maoni yenu Wabunge nasi pamoja Serikali na Wabunge tuweze kulisukuma na Muswada huo uje mapema Bungeni. Kikubwa tunategemea mchango wenu mzuri ili mwisho wa siku tukishapitisha basi pasiwepo na kasoro ambazo tutaziona baadae. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Sambamba na Bima kwa Walemavu umezuka ugonjwa kwa wanawake wanaojifungua watoto ambao wana mgongo wazi, hasa kule Mkoa wa Mbeya kwenye Hospitali ya Rufaa pale wanachaji fedha kuanzia 500,000 mpaka 1,000,000. Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia kuwapunguzia mzigo wa kulipa gharama hizo wanawake wanaojifungua watoto wa mgongo wazi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa wa Waziri wa Afya alishaelekeza na ameshasema mara nyingi kwamba akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano wanatakiwa wapate huduma bure, hilo ni la kwanza. Lakini ninyi ni mashahidi Waheshimiwa Wabunge jinsi ambavyo Serikali imeendelea kuboresha *infrastructure* kwa miaka sasa mingi sasa hivi tunaenda ndani ya miezi miwili hakutakuwepo na hospitali ya Mkoa haina na *CT scan* na vile vifaa ambavyo vitatusaidia kufanya *operation* zile ambazo zinahitaji utaalam wa juu kama hizo. Kwa hiyo kikubwa ni kwamba tutaboresha hiyo, ili iwe inaenda sambamba na suala la watoto njiti. Kwa hiyo watoto njiti na hao wanaozaliwa na *malformation* mbalimbali imewekwa utaratibu na ma-*specialist* wanapelekwa kwenye maeneo kwa ajili ya kuhakikisha hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge mkikutana na matatizo *specific* kwa sababu binaadam ndiyo wale wale mnatuambia mimi na Waziri na hata *information* kutoka popote zinafanyiwa kazi kwa wakati wake. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru. Kuna utafiti ulifanywa na Jumuiya ya Viongozi wa Dini kuhusiana na mambo ya Bima ambao unaonyesha takribani Watanzania milioni 15 hawana uwezo wa kabisa wa kujikatia hii Bima ya Afya.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kuwakatia hawa Watanzania Milioni 15 waweze kupata matibabu wakati huo wakisubiria Bima ya Afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali zuri la Mbunge. Kwanza, moja kupanga ni kuchagua na

tunaopitisha bajeti ni sisi, kwa hiyo kikubwa tayari Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu imejulikana kweli kwamba kuna asilimia 28 ya watu ambao hawawezi kujilipia, Rais wetu ameshakubali itengwe kila mwaka bilioni 149.77 kwa ajili ya kuwahudumia watu hao ambao unasema.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapanga nikuambie tu ni rahisi sana kungojea wewe LUKU iingie kwenye nyumba ukaacha kuwa na giza lakini ukiugua haisubiri. Kikubwa tunachowaambia wakati wa kupanga na kuamua vipaumbele tukate kodi wapi hasa kwenye Bima ni wakati wa sisi Wabunge kuchagua tunaelekea upande gani.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza Mbunge wa Chumbuni sasa aulize swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Mtoni.

Na. 204

**Nchi zilizofungua Ofisi za Ubalozi Dodoma**

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, ni nchi ngapi zimeshafungua Ofisi zao za Ubalozi Jijini Dodoma baada ya zoezi la kuhamisha Makao Makuu ya Serikali Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pondeza Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hadi sasa nchi tatu zimeshafungua Ofisi Ndogo za Ubalozi Jijini Dodoma. Nchi hizo ni Uingereza, Ujerumani na China. Hata hivyo, Wizara inaendelea kuzishawishi nchi nyingine kufungua Ofisi zao hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine baadhi ya Mashirika ya huduma za jamii na maendeleo ya Umoja wa Mataifa yameshafungua Ofisi zake Jijini Dodoma. Mashirika hayo ni pamoja na *UNDP, UNICEF, UN Women, WFP, WHO, UNFPA, FAO, IFAD, IOM, UNAID, UNCDF* na *UNIDO*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-HAFAR I. JUMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningetamani pia kujua kwa niaba ya muuliza swali Je, ni Balozi ngapi ambazo walau zimeshakuwa na viwanja japokuwa hazijafungua ofisi rasmi kuelekea kuwa na Ofisi rasmi katika Makao Makuu ya nchi?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Balozi zote nchini zimegawiwa viwanja Dodoma na Taasisi zake na kila Ubalozi ulitengewa karibu heka tano tano kwa ajili ya kuwekeza makazi yake pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Naibu. Mheshimiwa Kunti Majala swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa swali. Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba Balozi zote nchini zimepewa viwanja Dodoma.

Je, ni changamoto gani kubwa inayosababisha Balozi hizi zishindwe kuja kuendeleza viwanja hivyo na kuhamia Dodoma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria (K.n.y Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza utaratibu wa kuhamisha makazi ya Kibalozi kutoka iliyokuwa makao makuu ya nchi yetu kuja Dodoma ni utaratibu sawa na nchi nyingine zilivyofanya wakati huo. Kwa mfano, sisi tulihama kutoka *Borne* kwenda Berlin lakini tulichukua muda mrefu sana kwa sababu, hili ni suala la mipango ya kila nchi kujiwekea mpango wa uhamisho ambao unahitaji fedha. Kwa hiyo, upo uwezekano kabisa mkubwa wa nchi hizi *ku-delay* kuhamia hapa Dodoma kwa sababu, lazima ziingie kwenye mipango yao ya fedha na ziruhusu katika utaratibu wa kawaida Balozi zao kuhamishia makazi yake hapa makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo tukumbuke wakati tunafanya mchakato wa uhamisho baadhi ya Balozi zetu hapa ambazo zinawakilisha nchi zao hapa ndio zilikuwa zinamaliza majengo yao mapya Dar es Salaam. Kwa hiyo, unaweza ukaona namna ambavyo kunakuwa na misukosuko ile ya kimaandalizi kuanza kufikiria upya kuhamia Dodoma, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge kwa kawaida ningewaletea matangazo sasa, lakini matangazo ya wageni wetu hayako tayari sijaletewa bado kwa hiyo nitawatangaza baadaye kidogo, lakini sasa tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya. Ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu ikubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2021/2022 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka, 2022/2023. Aidha, ninaliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka, 2022/2023.

Mheshmiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Afya. Ninafahamu unyeti wa Sekta hii ya Afya ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitaifanya kazi hii kwa ueledi,

uaminifu na ubunifu mkubwa ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za Afya. Kipekee nimpongeze Rais Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake imara na pia kwa dhamira yake, maono yake na uthubutu wake ambao umekuwa dira sahihi inayoongoza utendaji wangu katika kuimarisha utoaji wa huduma za Afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wake wa kuboresha huduma za afya. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na kwa kutusimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba Wizara inatekeleza majukumu yake ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 6 Aprili, 2022 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha wa 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge letu Tukufu napenda kukuhakikishia kuwa Sekta ya Afya, itaendelea kutekeleza wajibu wake wa kutoa huduma za afya kwa kuzingatia Sheria mbalimbali zinazopitishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge na Makamu wake, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba kwa ushauri na maelekezo wanayoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara hususani katika kipindi cha maandalizi ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu na kuendelea kuwapa ushirikiano, katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama ulivyo utaratibu nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Emmanuel Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha aliyeteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie pia Bunge lako Tukufu kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi wa Jimbo la Ngorongoro kwa kifo cha Mheshimiwa Wiliam Ole Nasha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro. Aidha, natoa pole kwa familia na wananchi hususani wanawake wa Mkoa wa Rukwa, kwa kifo cha Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalam Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa Watanzania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo Hospitalini na majumbani. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka wagonjwa wetu ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2021/2022, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/2023 kama inavyooneshwa kwenye kitabu changu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 3 - 94. Kwa upande wa mwenendo wa bajeti Wizara na Taasisi zake zilizochini yake ilikadiriwa kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 507.2 na hadi kufikia mwezi Machi, 2022 jumla ya Shilingi Bilioni 403 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 79 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilipitishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya jumla ya Shilingi Trilioni 1,034,134,295,000 hadi kufikia Machi, 2022 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni 700.1 sawa na asilimia 68 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, Bunge lako lilipitisha nyongeza ya bajeti ya kiasi cha Shilingi Bilioni 263.7 kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Hadi kufikia Machi, 2022 Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni 230.6 sawa na asilimia 87 ya bajeti ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu kazi mbalimbali zilizotekelezwa yapo katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 11-103, lakini kwa kuwa taarifa hiyo ni ndefu nitaomba nijikite katika maeneo makubwa machache. Eneo la kwanza kwa upande wa huduma za kinga naomba hotuba yangu iingie *Hansard* yote kama nilivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za kinga eneo kubwa ambalo tumelifanyia kazi ni huduma za chanjo katika kipindi hiki cha Julai, 2021 hadi Machi, Wizara ilihakikisha chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana. Lengo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunawafikia watoto milioni 2 wenye umri wa chini ya mwaka mmoja, wajawazito milioni 2.2 na wasichana wenye umri wa miaka 14 ni 685,580.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji hadi kufikia Machi, 2022 hali ya utoaji wa chanjo nchini imeendelea kuimarika. Kwa mfano, chanjo kwa watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kwa chanjo ya PENTA kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya dondakoo, kifaduro, kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha Shirika la Afya Duniani cha kupima utoaji wa chanjo katika nchi ilifikia asilimia 96 ya lengo. Aidha, chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana tuliweza kuwafikia wasichana 535,298 ambao walipata dozi moja dozi ya kwanza, sawa na asilimia 78 ya lengo na wasichana waliopata dozi ya pili au dozi zote mbili walikuwa 420,015 sawa na asilimia 61 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mtaona kwamba wasichana wengi wanashindwa kukamilisha dozi ya chanjo ya kuwakinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Hivyo, kuanzia mwaka wa fedha, 2022/2023 Serikali itakuwa inatoa dozi moja ya chanjo ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi badala ya dozi mbili, baada ya kupatikana kwa matokeo ya utafiti wa kisayansi yaliyobainisha kwamba dozi moja inauwezo wa kuwakinga wasichana kupata maambukizi dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Hivyo nitoe wito kwa wazazi na walezi wenzangu wenye watoto wa umri wa miaka 14, kuhakikisha wanawapatia chanjo hii ya saratani ya mlango wa kizazi ili kuwakinga kuja kupata saratani siku zao za mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya na usafi wa mazingira tumeendelea kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za kuimarisha afya na usafi wa mazingira, ikiwemo kutekeleza awamu ya pili ya kampeni ya Taifa ya usafi wa mazingira yenye kauli mbiu *"USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO"*. Kupitia kampeni hii napenda kutoa taarifa ndani ya Bunge lako kwamba idadi ya kaya zenye vyoo bora nchini imeongezeka kutoka asilimia 64 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 72 mwezi Machi, 2022.

Mheshimiwa Spika, nitumie tena Bunge lako Tukufu kuendelea kuwahimiza watanzania kuzingatia kanuni za usafi binafsi na usafi wa mazingira ili kujikinga na magonjwa mbalimbali kwani kinga ni bora kuliko tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za lishe tumeendelea kutoa afua mbalimbali za lishe ikiwemo matone ya *Vitamin* A kwa watoto waliochini ya miaka mitano. Tulipanga kutoa matone ya *Vitamin* A kwa watoto milioni 8.2 nchi nzima kati ya wenye umri wa miezi sita hadi miezi 59. Zoezi hili lilikamilika kwa kuweza kuwafikia walengwa milioni 8 sawa na asilimia 97.2 ikilinganishwa na asilimia 95 ya mwaka, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto tumeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma

kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua, wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua. Kwa upande wa huduma kabla ya ujauzito Wizara ilinunua na kusambaza vidonge vya uzazi wa mpango dozi milioni 1.7 sawa na asilimia 82 ya lengo, sindano za uzazi wa mpango dozi milioni 2.1 sawa na asilimia 93 ya lengo na vipandikizi 206,000 sawa na asilimia 78 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu sijaonesha idadi ya huduma za uzazi wa mpango kwa wanaume. Katika kipindi hicho wateja waliotumia njia za uzazi wa mpango walikuwa milioni 4.8 ikilinganishwa na wateja milioni 4.3 mwaka, 2020. Kupungua kwa watu waliotumia huduma za kisasa za uzazi wa mpango imetokana pia na uwepo wa mlipuko wa UVIKO – 19.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma wakati wa ujauzito *Antenatal Care* tunakadiria kwamba, wakina mama wapatao milioni 2.3 hutarajiwa kupata ujauzito nchini Tanzania. Katika kipindi hiki jumla ya wanawake wajawazito 1,700,000 walihudhuria *Clinic* na kupatiwa huduma za afya na kati yao asilimia 99.7 ya wakinamama wajawazito walifanya mahudhurio manne au zaidi ikilinganishwa na asilimia 85 mwaka, 2020. Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza tunaona katika kila wanawake 100 wajawazito, wanawake 99 wanahudhuria *clinic* angalau mara nne wakati wa ujauzito wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, changamoto iliyopo ni wanawake wajawazito kuchelewa kuhudhuria *Clinic* wapatapo ujauzito. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya hao wajawazito milioni 1.7 ni wajawazito 656,000 tu sawa na asilimia 37.6 walianza kupata huduma za wajawazito chini ya wiki 12 za mwanzo wa ujauzito. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwahimiza wajawazito kuhudhuria *Clinic* mapema ndani ya wiki 12 za mwanzo za ujauzito wao na kukamilisha mahudhurio yote manne, ili kuepuka kupata changamoto mbalimbali zinazoweza kusababisha vifo vyao na vichanga vyao. Kwa upande wa huduma za afya wakati wa kujifungua tumeendelea pia kutoa elimu juu ya umuhimu wa wakina mama wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutoa

huduma za afya. Katika kipindi hiki wajawazito milioni 1.3 walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya, ikilinganishwa na wajawazito 890,000 waliojifungulia *Clinic* kipindi kama hicho mwaka, 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni kutokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeufanya katika kuboresha huduma kwa wakina mama wajawazito. Aidha, katika kipindi hiki wajawazito milioni 1.3 walihudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi ikilinganishwa na wajawazito 851,000 mwaka uliopita. Takwimu zinazokusanywa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini zinaonesha, vifo vitokanavyo na uzazi vimeendelea kupungua kutoka vifo 1,640 mwaka, 2020 hadi vifo 1,580 mwaka, 2021.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi hata hivyo hazijumuishi vifo vinavyotokea kwenye ngazi ya jamii lakini pia, takwimu hizi ni zile ambazo tumezikusanya katika vituo vya kutolea huduma za afya na sio za mazoezi ya Kitaifa au tathmini za Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatarajia kupitia Sensa ya idadi ya watu itakayofanyika Agosti, 2022 na utafiti wa demografia na afya Tanzania *Demographic and Health Survey* ambao umeanza kufanyika toka Septemba, 2021. Tunatumaini kwamba tutapata matokeo halisi ya Kitaifa kuhusu hatua ambayo nchi yetu imefikia, katika kupunguza vifo vya wakina mama wajawazito na watoto wachanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI Wizara imeendelea kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za kupima, ili kutambua hali zao za maambukizi ya virusi vya Ukimwi lakini pia tunawapatia huduma za ushauri, upimaji, matunzo na huduma za dawa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi Disemba, 2022 nchi yetu inakadiriwa kwamba kuwa na Watanzania milioni 1.7 ambao wanaishi na virusi vya Ukimwi na kati ya hao Watanzania milioni 1.5 wanaokadiriwa kuishi na virusi vya Ukimwi wameweza kutambua hali zao. Kati ya

hao wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na wanaotambua hali zao asilimia 99.3, walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI. Aidha, hadi sasa asilimia 95.8 ya wananchi waliokuwa wanatumia dawa za *ARV* walikuwa wamefubaza wingi wa virusi vya UKIMWI ambao ni sawa na chini ya nakala 1,000.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwahimiza Watanzania kupima virusi vya UKIMWI ili kuweza kutambua hali zao. Katika hili nimshukuru sana Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwa kuwa balozi wa kuhamasisha wanaume kupima virusi vya UKIMWI ili waweze kutambua haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia, kutoa huduma za UKIMWI katika vituo vyetu vikiwemo vituo vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto. Kwa upande wa kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, huduma hizi sasa zinatolewa katika vituo 6,996 sawa na asilimia 98 kati ya vituo 7,138 vinavyotoa huduma za afya ya uzazi na mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tumeweza pia kuwapima wajawazito kama wana virusi vya UKIMWI kwa asilimia 99. Kwa hiyo, katika wajawazito 100 waliofika katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya, wajawazito 99 waliweza kupimwa kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameendelea kuwa asilimia 11 kwa kipindi kama hicho mwaka 2020 hadi 2021.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia na jitihada za kudhibiti ugonjwa wa Malaria ikiwemo kusambaza dawa pamoja na vipimo vya haraka vya Malaria. Taarifa yangu inaeleza kwa kina katika ukurasa wa 31 hadi 34. Hata hivyo, nitumie Bunge lako Tukufu pia kuwataka watoa huduma za afya nchini kuzingatia mwongozo wa Serikali, kupima Malaria kwa kutumia kipimo cha haraka *(MRDT),* ni bure; kupata dawa za Malaria ni bure pamoja na sindano ya Malaria kali. Kwa hiyo, nawataka watumishi wa afya kuzingatia mwongozo huu, kwamba matibabu na vipimo vya malaria ni bure kwa wananchi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa udhibiti wa magonjwa ya miliupuko. Tumeendelea kupambana na maambukizi ya magonjwa ya mlipuko ambayo pia yanatolewa taarifa Kimataifa, ikiwemo Kipindupindu, Kimeta, Ebola, UVIKO-19 ambapo tumetoa elimu ya afya kwa umma. Katika kipindi hiki cha Julai, 2021 hadi Machi tumeendelea kuona ugonjwa wa Kipindupindu katika Halmashauri za Nkasi, Kigoma Manispaa, *Kigoma Dc,* Tanganyika na Uvinza, ambapo jumla ya wagonjwa 390 na vifo vinne viliripotiwa. Aidha, ugonjwa wa UVIKO-19 umeendelea kuripotiwa hapa nchini ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2022 jumla ya wagonjwa 14,198 wamethibitishwa kuugua na vifo vilivyoripotiwa ni 403.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sasa hivi tunaona kupungua kwa wastani wa wagonjwa na vifo vinavyotokana na UVIKO kuanzia mwezi Machi, 2022. Hata hivyo, ninaendelea kuwasihi Watanzania kuchanja chanjo ya UVIKO-19 kwa sababu hatujui wimbi linalokuja la UVIKO litakuja kwa nguvu gani.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa nitoe kwa ufupi shughuli zilizotekelezwa kwa upande wa huduma za tiba. Tumeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma hizi kupitia vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kufikia 8,549 ikilinganishwa na vituo 8,458 mwaka 2020. Kati ya hivyo, hospitali ni 404, vituo vya afya *(health centers)* ni 956 na zahanati ni 7,189.

Mheshimiwa Spika, pia tumeendelea kuangalia mwenendo wa magonjwa yanayowasumbua Watanzania katika kipindi hiki. Kwa upande wa wagonjwa wa nje wenye umri chini ya miaka mitano walisumbuliwa na magonjwa ya mfumo wa hewa, Malaria na maambukizi katika mkojo. Kwa watu wa umri wa miaka mitano na zaidi magonjwa makuu yaliyowasumbua ni maambukizi katika mfumo wa hewa, maambukizi katika njia ya mkojo na Malaria. Kwa kipindi hiki pia kwa upande wa wagonjwa wa kulazwa; kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ni kichomi, Malaria na kuharisha sana, ambapo kwa watu

wa umri wa miaka mitano na kuendelea magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ni Malaria, kichomi na maambukizi katika njia ya mkojo *(UTI)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia tumeona ongezeko kubwa la watu wanaolazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambikiza ikiwemo kisukari, shinikizo la damu, pamoja na saratani, hali inayoashiria kukua kwa tatizo la magonjwa yasiyoambukiza katika nchi yetu. Hivyo, nitoe pia wito kwa Watanzania kulinda na kujikinga afya zao ikiwemo kufanya mazoezi, kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa pamoja na kupima afya zao mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili pia tumeangalia upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa-tiba ambapo Wizara kupitia bohari ya dawa *(MSD)* hununua, hutunza na kusambaza zaidi ya aina 2,976 za dawa, vifaa na vifaa-tiba na vitendanishi. Kati ya aina hizi 2,976 tumebainisha kwamba, aina 290 za dawa ni dawa muhimu na za kipaumbele kwa Wizara ya Afya na hivyo zinapaswa kupatikana kipindi chote katika bohari ya dawa, *(MSD)*. Aidha, katika kipindi hiki Wizara ya Afya kupitia Wizara ya Fedha tumepeleka *MSD* kiasi cha Shilingi bilioni 129.8 kwa ajili ya kugharamia mnyororo mzima wa upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa aina 290 za dawa imefikia asilimia 51 katika ngazi ya *MSD,* asilimia 43 ngazi ya zahanati, asilimia 42 vituo vya afya, asilimia 50 hospitali za wilaya, asilimia 76 hospitali za rufaa za mikoa na asilimia 51 katika hospitali za kanda maalum na Taifa. Taarifa hii inapatikana pia katika ukurasa wa 39 hadi 44 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia, Serikali kupitia Wizara ya afya imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa ili kuokoa maisha ya Watanzania wengi, sambamba na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi. Katika kipindi hiki hospitali zetu za Taifa ziliwasilisha Wizarani idadi ya wagonjwa 49 waliosema kwamba wanahitaji kupatiwa matibabu nje ya nchi, ambapo wagonjwa 37 walipatiwa kibali cha

kwenda kutibiwa nje ya nchi. Katika kipindi hiki pia hospitali zetu za Taifa, kanda maalum, ziliendelea kutoa huduma za matibabu ya ubingwa bobezi ikiwa ni pamoja na upandikizaji wa figo *(renal transplant)* kwa wagonjwa 14 na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa 99 toka huduma hii ilipoanzishwa nchini kwetu mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa watoto 14 ulifanyika, unaitwa *Cochlea implants* na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa 49 toka huduma hii ilipoanzishwa mwaka 2017, lakini pia tuliendelea kutoa huduma ya upandikizaji wa uroto *(born marrow transplant)* ambapo jumla ya wagonjwa 11 walifanyiwa upandikizaji huo. Kwa mara ya kwanza huduma hii ya kupandikiza uroto *(born marrow transplant)* imefanyika katika nchi yetu na ndio ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza tumeweza kutoa huduma hii kwa wagonjwa 11.

Mheshimiwa Spika, pia tumeendelea kutoa huduma za upasuaji mkubwa wa moyo kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa 439 pamoja na wagonjwa 1,425 walipata huduma za upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum, upasuaji mkubwa wa ubongo kwa wagonjwa 5,098 na huduma za kibingwa na tiba za saratani. Katika kipindi hiki cha kutekeleza majukumu yetu, jumla ya wagonjwa 107 kutoka nje ya nchi walifika nchini kupatiwa huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi. Nchi hizo ni pamoja na Visiwa vya Comoro, Zambia, *DRC,* Kenya, Botswana na Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaahidi Watanzania kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu, ununuzi wa vifaa tiba na watumishi wenye weledi ili kuimarisha uwezo wa ndani wa kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ikiwemo kuvutia wananchi kutoka nchi jirani kupata huduma hii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Hospitali za Kitaifa, Maalum na Kanda, ambazo ni Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Moi, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Saratani *Ocean Road,* Hospitali ya

Kibong'oto, Hospitali ya Mirembe, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini *(KCMC),* Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando na Hospitali za Rufaa za Mikoa, zipo kuanzia ukurasa wa 49 hadi 71 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji wa Hospitali ya Mloganzila ambayo hivi sasa ipo chini ya usimamizi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu na wananchi kuwa kuanzia tarehe 01 Julai, 2022, hospitali hii itaanza kujiendesha yenyewe. Tunaamini kuwa hatua hii itaiwezesha hospitali kutoa huduma bora na kwa haraka sambamba na kuipunguzia mzigo Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ikiwemo ubora wa huduma za afya ambapo tulifanya uhakiki wa ubora wa huduma *(clinical audit)* katika hospitali 28 za rufaa za mikoa. Uhakiki huu unaonesha utoaji wa huduma bora ni asilimia 45 chini ya kiwango cha ubora kinachotakiwa. Hivyo, tumeweka mikakati ya kuboresha maeneo yote yenye upungufu na kuendelea kufanya uhakiki katika vituo vyote vya huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa rasilimali watu katika sekta ya afya pamoja na changamoto zinazoikabili sekta ya afya kutokana na upungufu wa raslimali watu, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kupunguza pengo kati ya upatikanaji watumishi ikilinganishwa na mahitaji halisi. Katika hili tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa kibali cha ajira mpya kwa wataalam wa afya, ambapo jumla ya nafasi za ajira 10,285 zimetolewa, nafasi 7,612 kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za Halmashauri chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; ajira 1,650 kwa ajili ya hospitali za kanda na mikoa; na ajira 1,023 kwa ajili ya vituo vya afya *DDH,* pamoja na *Voluntary Agencies Hospitals* zimetolewa. Maelezo haya pia yapo katika ukurasa wa 75 hadi 77 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa huduma za afya. Tumeendelea pia kuongeza kiasi cha fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia huduma za afya pamoja na fedha ambazo tunazipata kutoka kwa wadau wetu wa maendeleo. Mwenendo wa ugharamiaji wa huduma za afya umeonesha ongezeko la fedha za ndani kutoka Shilingi bilioni 406.1 mwaka 2015/2016 hadi Shilingi bilioni 909 mwaka 2021/2022 ambapo fedha za nje zimeendelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia huduma za afya inaonesha dhamira ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha tunaboresha huduma za afya kwa kutumia mapato yetu ya ndani. Sekta ya afya tuna matumaini makubwa na *Royal Tour* kwamba pia itatuongezea mapato katika sekta ya afya ili tuweze pia kuboresha huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchangiaji, Watanzania wamepata huduma za afya aidha kwa kulipa fedha taslimu papo kwa hapo au kulipa kabla ya kuugua kwa kupatiwa kadi ya bima ya afya kama Sera ya Afya inavyoeleza. Hadi Desemba, 2021 jumla ya Watanzania milioni tisa sawa na asilimia 15 ya Watanzania wote ndio walionufaika na mfumo wa bima ya afya ambapo asilimia 85 wapo nje ya mfumo wa bima ya afya. Hali hii inawaweka Watanzania wengi hususan wa kipato cha chini katika hatari ya kutopata huduma za afya pindi wanapohitaji na wakiwa hawana fedha za kuchangia. Katika kutatua changamoto hii Wizara inaendelea kukamilisha muswada wenye lengo la kutunga sheria itakayowataka Watanzania wote kujiunga na bima ya afya na hivyo kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya pindi wanapozihitaji.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana wewe na Bunge lako tukufu, wiki iliyopita ulitupatia kibali cha kuendelea mbele kukamilisha Muswada huu wa Bima ya Afya kwa Wote *(Universal Health Insurance)*.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu pia nimeeleza miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ambapo nimeweka katika hotuba yangu ikiwemo miradi iliyogharamiwa na fedha za UVIKO-19 inayohusu ujenzi wa *ICU* 38, wodi za huduma za dharura *(emergency department)* 21, nyumba za watumishi 26, uboreshaji wa hospitali za rufaa za mikoa saba, maalum moja, kituo cha magonjwa ya kuambukiza pamoja na elimu ya afya kwa umma. Kwa wastani, utekelezaji wa miradi yote ya uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya umefikia wastani wa asilimia 75. Vilevile kupitia fedha hizi Wizara imeratibu ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa ambapo kila Halmashauri pia itapata; vifaa vya uchunguzi: *CT-Scan, MRI, X-Ray* na *ECO,* vifaa vya *EMD, ICU* na *Telemedicine*.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu pia nimeeleza kazi mbalimbali zilizotekelezwa na taasisi sita zilizo chini ya Wizara ikiwemo bohari ya dawa, mfuko wa Taifa wa bima ya afya, mamlaka ya dawa na vifaa tiba, taasisi ya chakula na lishe, wakala wa maabara wa mkemia mkuu wa Serikali na taasisi ya utafiti wa magonjwa kuanzia ukurasa wa 79 hadi ukurasa wa 90 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimeeleza majukumu ya mabaraza na bodi za kitaaluma ambapo mabaraza ya kitaaluma yako nane na bodi mbili ambayo ni Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalamu wa Macho, Baraza la Radiolojia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya na Bodi ya Ushauri wa Hospitali. Kazi zao nimezieleza kuanzia ukurasa wa 90 hadi ukurasa wa 109 katika hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vyetu ni vipi katika mwaka wa fedha wa 2022/2023. Tuimebainisha vipaumbele 13. Kipaumbele cha kwanza ni kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ili kuweza kuwakinga na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Kipaumbele cha pili ni

kusimamia viwango vya ubora wa huduma za kinga na tiba katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, katika eneo hili tumeona tusiendelee kujisifu kwa kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali, lakini tunataka twende mbali zaidi tujiulize; je, Watanzania wanapata huduma bora za afya? Kwa hiyo, tutawapima watoa huduma zetu, hospitali zetu kwa kuangalia ubora wa huduma. Tutaangalia kwanza, je, mgonjwa alipofika katika kituo cha kutoa huduma, alipata huduma nzuri ikiwemo kuchukuliwa historia ya mgonjwa; Ikiwemo kufanyiwa *physical examination;* amepata *consultation* nzuri; amepata vipimo na dawa zote anazopaswa kupata?

Mheshimiwa Spika, pia tutaangalia lugha na muda ambao mgonjwa ametumia katika kupata huduma za afya. Kwa hiyo, tutahesabu zahanati na majengo tuliyojenga, lakini tutajikita zaidi katika kusimamia ubora wa huduma za afya *(quality of healthcare services)*.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, tunaenda kuimarisha huduma za afya ya uzazi ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, vifo vya watoto wachanga pamoja na mimba za utotoni. Tutaimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kuimarisha huduma za lishe hususan kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, vijana balehe na wanawake wa umri wa kuzaa. Tutaimarisha huduma za afya na usafi wa mazingira ili kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na hivyo kupunguza idadi ya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili la afya na usafi wa mazingira kuna mambo madogo tu yakifanyika tunaweza kupunguza Watanzania wanaokwenda katika vituo vya kutoa huduma za afya. Hivi ni kwa nini katika vijiji vyetu katika mitaa yetu kuna uchafu na mambo ambayo yanaweza kuhatarisha afya zetu ikiwemo kusababisha magonjwa ya matumbo, pamoja na kuhara?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, eneo hili pia tutalipa kipaumbele, msisitizo wa kutosha. Tutaimarusha miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali za rufaa, mikoa na kanda, matibabu ya kibingwa, kudhibiti magonjwa ya mlipuko pamoja na TEHAMA na ugharamiaji wa huduma za afya pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivi, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha Shilingi trilioni 1.1 ambazo zitatumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa ofisi. Shilingi bilioni 74.4 tumezitenga kwa ajili ya chanjo za watoto, Shilingi bilioni 10 tumezitenga kwa ajili ya kujenga hospitali maalum ya huduma za mama na mtoto Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine Rais Samia anakwenda kuandika historia nchini. Kwa mara ya kwanza tutakuwa na Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Akinamama na Watoto *(Women and Children Hospital)*. Kwa hiyo, tumetenga Shilingi bilioni 10 na tunaamini kwamba hospitali hii pia itawezesha matibabu ya kibingwa. Pia tutajenga vyumba vya huduma za watoto wachanga mahututi katika hospitali 100 za wilaya *(Neonatal Intensive Care Unit),* tutawajengea uwezo watoa huduma wa afya kuwa na stadi, weledi na tabia bora, kuweka vifaa na watumishi, tumetenga shilingi bilioni 23.5. shilingi bilioni 200 tumezitenga kwa ajili ya dawa, vifaa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, bilioni 18.6 tumezitenga kwa ajili kukamilisha Hospitali (5) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa ya Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu. Bilioni 26 tumetengwa kwa ajili ya hospitali Hospitali za Rufaa za Shinyanga, Singida na Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Bilioni 14 ni miundombinu ya hospitali nane za Rufaa za Mikoa; naomba, pale pa Ligula imeonekana ni Lindi, lakini Ligula ni Mtwara; bilioni 15.9 pia kwa ajili ya huduma za matibabu ya kibingwa. Tumetenga pia bilioni 10 kujenga jengo la matibabu ya saratani ya mionzi katika hospitali yetu ya Benjamin Mkapa, pamoja na bilioni tatu kwa ajili ya ubingwa bobezi, bilioni 65 kulipia *intense* wanaofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niseme tu vipaumbele hivyo ambavyo tumevitengea fedha nimevieleza katika hotuba yangu ikiwemo masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na huduma nyingine.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na sekta nyingine. Napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuwashukuru wadau wetu wanaochangia Mfuko wa Afya ya Pamoja *(Health Basket Fund),* ambazo ni nchi za Canada, Denmark, Ireland, Uswisi, Korea Kusini, Benki ya Dunia na *UNICEF*.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimekuwa zikifadhili miradi mbalimbali ya afya. Nayashukuru pia Mashirika ya Kimataifa yote ambayo nimeyataja katika hotuba yangu ikiwemo *(UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN, WHO* na *International Atomic Energy Agency*); Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB); GAVI; PEPFAR; CDCUS, IMF, USAID PMI; Abbott Fund; DFID; EGPAF; GIZ; Global Fund (for HIV, TB* na Malaria); *Bill and Melinda Gates Foundation; GSI, (JSI); JICA; KfW;* wako wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya Kiserikali ambao wengi pia wamehudhuria hapa kwa kuendelea kusaidia au kuchangia sekta ya afya; na wadau wetu hawa nimewataja katika aya ya 187 ya hotuba yangu. Navishukuru Vyuo Vikuu na vyuo vya mafunzo ya kada za kati nchini pamoja na vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wangu wa kazi nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Kipekee namshukuru sana jembe langu Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya. Aidha, naomba kuwashukuru Prof. Abel Makubi Katibu Mkuu na Dkt Seif Shekalaghe, Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawashukuru Dkt Aifello Sichalwe, Mganga Mkuu wa

Serikali, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Kipekee napenda kuwashukuru Wakurugenzi wa Hospitali zetu zote za Rufaa za Kanda na Taifa na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za usajili. Nawashukuru waganga wakuu wa mikoa na wilaya. Waganga wafawidhi wa hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za halmashauri vituo vya afya na zahanati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kengele ya pili niombe hela, lakini kabla sijaomba hela nitumie fursa hii kuishukuru kwa dhati familia yangu kwa upendo na uvumilivu mkubwa na kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu. Lakini nawashukuru sana watu wa Tanga Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Nawaahidi wana Tanga mjini kwamba nitawatumikia na kuwapenda na kuwaenzi ili tuweze kulifanya jimbo letu liwe la mahaba ukarimu na maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niombe fedha. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi 619,538,808,257. Kati ya fedha hizo, shilingi 140,813,114,464.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu. Wizara itakusanya shilingi 85,739,668,813.00 ambazo pia zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, shilingi 392,986,024,980.00

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hebu soma tena hiyo ya bilioni 85.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo 619,538...

**SPIKA:** Ngoja, hiyo ya bilioni 85 ndiyo uisome upya

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 85,739,968,813 zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa

**SPIKA:** Hapo kwenye laki sita umesoma lakini tisa hapa kwenye maombi yako 85....

**WAZIRI WA AFYA:** Shilingi bilioni 85,739,668,813

**SPIKA:** Sawa hii namba naona imekataa ni shilingi 85,739,668,813 haya endelea kusoma nyingine.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, shilingi 85,739,668,813 zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, shilingi 392,986,024,980.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika mashirika yaliyo chini ya Wizara. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 22.

Kwa upande wa matumizi Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 1,109,421,722,000.00 ili tuweze kutekeleza majukumu yetu. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 554,289,666,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo Wizara inakadiriwa kutumia shilingi bilioni 555,132,056,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na 50% ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi 410,298,000,000 na fedha za nje ni shilingi 144,834,056,000.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa Wizara inaomba Bunge lako tukufu itupitishie bajeti ya mapato na matumizi ya shilingi 1,109,421,722,000.00.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti za Wizara ya Afya www.moh.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2022/23 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2021/22 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2022/23.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha Hotuba yangu siku ya leo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kwa kuniteua kuwa Waziri wa Afya. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitaifanya kazi hii kwa weledi, uaminifu na ubunifu mkubwa ili kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora za Afya. Kipekee nimpongeze Rais Samia kwa uongozi wake imara na pia kwa dhamira yake, maono yake na uthubutu wake ambao umekuwa dira sahihi inayoongoza utendaji wangu katika kuimarisha utoaji wa huduma za Afya nchini. Aidha, ni dhahiri kuwa katika kipindi cha Uongozi wake Watanzania wameshuhudia kasi kubwa ya uimarishaji na utoaji wa huduma bora za afya nchini ikiwa ni pamoja ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya katika Halmashauri na Mikoa yote nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na huduma za matibabu ya Kibingwa na ubingwa Bobezi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda

na Taifa. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais kuwa, Wizara itaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha huduma za afya nchini zinawafikia watanzania walio wengi na hususan wenye kipato cha chini.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wake wa kuboresha huduma za afya nchini hususani kwa wananchi wa maeneo ya Vijijini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake mahiri ikiwemo kusimamia vyema utekelezaji wa vipaumbele vya Afyanchini. Aidha, ninampongeza kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 6 Aprili 2022 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2022/23.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunapenda kukuhakikishia kuwa Uongozi na Watumishi wa Sekta ya Afya nchini tutakeleza wajibu wetu wa kutoa huduma za afya kwa kuzingatia Sheria na Kanuni mbalimbali zinazopitishwa na Bunge lako tukufu. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu** kwa kuchaguliwa kuwa **Naibu Spika** wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano walionipatia ambao umeiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za Afya. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya

kuhakikisha kuwa watanzania wana afya bora ili washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa viwanda, na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb)**, na Makamu wake, **Aloyce John Kamamba (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara hususani katika kipindi cha maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za Afya. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia Wananchi ndani na nje ya Bunge.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa **Emmanuel Lekishon Shangai** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa **Jimbo la Ngorongoro** na **Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha** aliyeteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa Familia na Wananchi wa Jimbo la Ngorongoro kwa kifo cha **Mheshimiwa Wiliam Ole Nasha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro.** Aidha, naomba kutoa pole kwa familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kifo cha **Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalam mkoa wa Rukwa.** Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wote, waliopoteza ndugu, Jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo Hospitalini na majumbani. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2021/22, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (Health Sector Strategic Plan (HSSP) V 2021/22 – 2025/26) pamoja na makubaliano ya Kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza nchini kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za chanjo, lishe na afya ya uzazi, mama na mtoto;

(ii) Kuimarisha huduma za tiba nchini ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini;

(iii) Kuweka mazingira wezeshi ya ukusanyaji wa damu salama na mazao yake katika mikoa mitano ya Dodoma, Mbeya, Kigoma, Mtwara na Mwanza ili kukidhi mahitaji;

(iv) Kuimarisha huduma za matibabu ya Kibingwa na ubingwa Bobezi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali ya Benjamini Mkapa kufikia viwango vya Kimataifa ili kukidhi mahitaji ya hapa nchini na kuhudumia wagonjwa kutoka nje ya nchi;

(v) Kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote;

(vi) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa kada mbalimbali za afya kwa kuimarisha miundombinu katika vyuo vya afya nchini;

(vii) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalam bingwa na bobezi katika Sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na kutumia utaratibu wa mafunzo ya kibingwa na bobezi wakiwa kazini (Fellowship Training Programme);

(viii) Kuimarisha huduma za dharura katika Hospitali za Kanda ikiwemo Hospitali ya Benjamini Mkapa ili iweze kumudu ongezeko la mahitaji ya huduma za dharura kutokana na Serikali kuhamishia Makao Makuu ya nchi Dodoma;

(ix) Kuimarisha mpango wa Taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, ajali na majanga kwa kuboresha huduma za dharura na uokoaji ikiwemo miundombinu na vitendea kazi;

(x) Kusimamia ubora, usalama na ufanisi pamoja na kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na Tiba Asili na Tiba Mbadala Nchini;

(xi) Kuimarisha utoaji wa huduma za afya kuanzia ngazi ya Afya ya Msingi, hospitali za rufaa ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa kwa kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya;

**Mapato na Matumizi ya Fedha**

13. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Fungu 52, inalo jukumu la kusimamia upatikanaji na utoaji wa Huduma za Afya nchini. Wizara hukusanya mapato kutokana na Huduma za Tiba zitolewazo na Hospitali zilizo chini yake, tozo za huduma katika Taasisi mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

14. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/22 Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **shilingi 507,218,152,321.00** ambapo kati ya fedha hizo, **shilingi 81,717,635,624.00** zilitarajiwa kukusanywa kutokana na vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara na **shilingi 92,044,336,376.00** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa. Aidha, Mashirika yaliyo chini ya Wizara yalikadiriwa kukusanya **shilingi 333,456,180,321.00.** Hadi kufikia mwezi Machi, 2022, jumla ya **shilingi 403,030,966,255.18** zilikuwa zimekusanywa, sawa na **asilimia 79** ya lengo. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 84,812,539,861.00** kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, sawa na **asilimia 104** ya makadirio, kiasi cha **shilingi 48,102,720,587** sawa na **asilimia 52** kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha **shilingi 270,115,705,806.88** sawa na **asilimia 81** kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara.

15. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22 Wizara ilipitishiwa na Bunge lako tufuku bajeti ya jumla ya **shilingi 1,034,134,295,000.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi**

**557,303,059,000.00** ilikuwa kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ikijumuisha **shilingi 252,523,260,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 304,779,799,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Vilevile, Wizara ilipata nyongeza ya bajeti ***(supplimentary Budget)*** ya kiasi cha **shilingi 263,728,066,998.00** kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO 19.

16. ***Mheshimiwa Spika***, fedha zilizopitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 476,830,236,000.00,** kati ya fedha hizo **shilingi 351,700,000,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 125,130,236,000.00** ni fedha za nje kutoka kwa Wadau wa Maendeleo wanaochangia Sekta ya Afya. Aidha, fedha kiasi cha **shilingi 263,728,066,998.00** ambazo ziliongezwa kwenye bajeti ya Wizara pia zililenga kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

17. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2022, Wizara ilipokea jumla ya **shilingi 700,158,699,597.02** sawa na **asilimia 68** ya bajeti iliyoidhinishwa ya **shilingi 1,034,133,295,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida hadi Machi, 2022 ni **shilingi 441,433,858,257.14** sawa na **asilimia 79** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/22. Kati ya fedha hizo **shilingi 212,174,499,103.19** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na **asilimia 84** na **shilingi 229,259,359,153.95** sawa na **asilimia 75** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Afya.

18. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa miradi ya maendeleo kiasi cha **shilingi 258,724,841,339.88 sawa na asilimia 54** kimepokelewa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **shilingi 241,351,889,683.77 sawa asilimia 69** na fedha za nje ni **shilingi 17,372,951,656.11.** Vilevile, Wizara imepokea kiasi cha **shilingi**

**230,667,862,267.28** sawa na **asilimia 87** ya **shilingi 263,728,066,998.00** ya bajeti ya nyongeza (Supplimentary budget) kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Aidha, Wizara imepokea **shilingi 258,127,631,886.17** nje ya mfumo wa malipo wa Hazina (Exchequer system) kutoka kwa Wadau wa maendeleo kwenda moja kwa moja kutekeleza Miradi Misonge ya afya ikiwemo ugharamiaji wa dawa na vifaa tiba. Vilevile, Wizara ilipokea kiasi cha **shilingi 41,195,716,045.96** kutoka **Mfuko wa Afya wa Pamoja** na kukipeleka moja kwa moja OR – TAMISEMI kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za afya katika ngazi ya msingi.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

### HUDUMA ZA KINGA

### Chanjo

*19.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara ilihakikisha chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana kulingana na mahitaji ya Mikoa yote nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa **watoto 2,061,343** wenye umri wa chini ya mwaka mmoja, **wajawazito 2,229,015** na **Wasichana 685,580** wenye umri wa miaka 14 ambao ni walengwa wa huduma za chanjo kwa mwaka 2021/22 wanapata huduma za chanjo kwa wakati.

*20.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa chanjo mbalimbali kama ifuatavyo: sindano ya kukinga polio (IPV) dozi 612,900 kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa Watoto; chanjo ya Pentavalent *Pneumococcal Conjugate Vacine*(PCV) dozi 3,167,400 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa ya Nimonia na homa ya uti wa mgongo; chanjo ya Rota dozi 630,000 za kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa wa kuhara; chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi *Human Papilloma-virus* (HPV) dozi 641,400; chanjo ya *Measle and Rubella* (MR) dozi 2,500,000 dozi ya surua na rubella ; chanjo ya *Bivalent Oral Polio Vaccine* (BOPV) dozi 6,000,000 kwa ajili ya kuzuia virusi

mbalimbali vinavyosababisha ugonjwa wa kupooza kwa watoto; chanjo ya *Tetanus Diphtheria* (Td) dozi 2,000,000 kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa Pepopunda kwa mama wajawazito; chanjo ya *Bacillus Calmette-Guerin*(BCG) dozi 4,000,000 kwa ajili ya kuwakinga watoto wachanga na ugonjwa wa Kifua; na chanjo ya Pentavalent dozi 4,800,500 kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo. Chanjo zilizopokelewa zilisambazwa kwenye mikoa yote kulingana na idadi ya walengwa na uhitaji.

Hadi kufikia Machi 2022, hali ya utoaji wa chanjo nchini imeendelea kuimarika, ambapo chanjo kwa Watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kwa chanjo ya Penta kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha Shirika la Afya Duniani (WHO) cha kupima utoaji wa Chanjo katika nchi ilifikia asilimia 96 kati ya 1,060,726 ya lengo. Chanjo za kukinga ugonjwa wa Polio ya matone (OPV3) ilifikiwa kwa asilimia 79, sindano ya kukinga polio (IPV) kwa asilimia 95, Surua rubella dozi ya 1 asilimia 92, Surua Rubella dozi ya 2 asilimia 78, chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana dozi ya kwanza (HPV 1) asilimia 78 na dozi ya pili (HPV 2) asilimia 61.

*21.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki pia, Wizara iliratibu upatikanaji wa chanjo dhidi ya UVIKO- 19 ambapo jumla ya dozi 9,845,774 zilipatikana kama ifuatavyo: - aina ya Janssen dozi 1,679,550, Sinopharm dozi 4,066,964, Pfizer dozi 3,722,940 na moderna dozi 376,320. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2022 dozi 6,375,456 sawa na asilimia 62 zilizopokelewa zilikuwa zimesambazwa mikoani kwa matumizi. Dozi zilizotumika ni 5,547,743.

*22.* ***Mheshimiwa Spika,*** Takwimu zinaonesha kuwa, tangu ugonjwa huu wa UVIKO-19 uliporipotiwa hapa nchini Machi 2020, hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya watu 14,198 wamethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO – 19 na Watu

**403** wamepoteza maisha sawa na **asilimia 2.8** ya waliougua. Wizara, inaendelea kuratibu utoaji wa chanjo ya UVIKO -19 kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa hapa nchini. Zoezi la utoaji chanjo hapa nchini lilianza rasmi mwezi Julai, 2021. Hadi kufikia 31 Machi, 2022 jumla ya **watu 3,067,877** kati ya **watu 30,740,928** ikiwa ni **asilimia 10** ya Watanzania wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, wamepata chanjo kamili dhidi ya ugonjwa huu. Lengo ni kufika **asilimia 70** ya watanzania wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Wizara pia ilifanya mafunzo ya utoaji chanjo za UVIKO-19 kwa wakufunzi ngazi ya Taifa na baadaye kufuatiwa na mafunzo ya utoaji chanjo kwa wasimamizi wa chanjo katika ngazi za Mikoa 26 na Wilaya 184 na watoa huduma wawili kutoka kila kituo kinachotoa chanjo. Wizara iliratibu mikutano mbalimbali ya uhamasishaji ikiwemo mkutano wa kuhamasisha wadau wa chanjo kwa Sekta binafsi, Asasi za Kiraia na Viongozi wa dini.

*23.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea na kazi ya udhibiti wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo ambapo sampuli 539 za ulemavu wa ghafla ulio tepetepe (AFP), sampuli 24 za ufuatiliaji wa ugonjwa wa polio katika mazingira (Environmental surveillance for polio) na sampuli 1,506 za Wagonjwa waliokuwa na dalili za homa na vipele (FRI) zilichukuliwa na kupelekwa maabara. Majibu ya vipimo vya AFP yalikuwa salama ikithibitisha kuwa hapakuwa na ugonjwa wa Polio nchini.

**Afya na Usafi wa Mazingira**

*24.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia afua za kuimarisha hali ya afya na usafi wa mazingira. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendesha mafunzo kwa Waganga Wakuu, Wahandisi na Maafisa Afya katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri kutoka Mikoa 17 ya Tanzania Bara juu ya matumizi ya Mwongozo wa Maji na Usafi wa Mazingira kwenye Vituo vya Kutolea Huduma za Afya yaani "*Water, Sanitation and Hygiene in Healthcare Facilities – 2017*".

Aidha, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kwa kushirikiana na WHO ilifanya tathmini ya udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za Afya katika Mikoa 26 ya Tanzania bara, kazi hii imefanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilifanyika mwezi Septemba 2021 ikihusisha Mikoa 13 ambayo ni Kigoma, Tabora, Iringa, Mbeya, Manyara, Arusha, Sumbawanga, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Pwani, Mwanza na Shinyanga na Awamu ya pili ilifanyika mwezi Oktoba 2021 katika Mikoa iliyofanyiwa tathmini awamu ya pili ambayo ni Songwe, Njombe, Katavi, Lindi, Tanga, Dar es salaam, Simiyu, Geita, Kilimanjaro, Mara, Singida, Kagera na Ruvuma. Matokeo yalibainisha kuwa katika Vituo vya kutolea huduma za afya asilimia 65 ya vituo vyote vina uelewa wa mfumo wa udhibiti taka hatarishi kwa kutenganisha taka kwa kutumia "3 clour coded bin system". Aidha, imebainika kuwa katika Hospitali za rufaa za mikoa asilimia 75 zina viteketezi vinavyokubalika na miongozo ya wizara ya afya na asilimia 40 kwa hospitali za wilaya na asilimia 38 kwa vituo vya afya na zahanati. Hivyo Wizara itaendelea kuimarisha Mifumo ya udhibiti wa taka nchini.

*25.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira yenye kaulimbiu isemayo "***USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO***" yenye lengo la kuhimiza ujenzi na matumizi ya vyoo bora na vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni katika ngazi ya kaya na Taasisi. Kupitia kampeni hii, idadi ya kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka **asilimia 64** mwaka 2020 hadi kufikia **asilimia 72** mwezi Machi, 2022. Vilevile, kaya zenye vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni zimeongezeka kutoka **asilimia 40** Mwaka 2020 kufikia **asilimia 41** mwezi Machi, 2022**.** ***Nitumie Bunge lako tukufu kuendelea kuwahimiza watanzania kuzingatia kanuni za usafi binafsi na usafi wa mazingira ili kujikinga na magonjwa mbalimbali kwani Kinga ni Bora kuliko Tiba.***

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za Afya ya jamii mipakani, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Wizara imetekeleza afua mbalimbali ikiwemo:

i. Kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Wasafiri (*Travel advisory*) Namba 10 ambao umeanza kutekelezwa katika Viwanja vyote vya Ndege, Bandari zote na Mipakani

ii. Upimaji wa wasafiri umeendelea kufanyika katika mipaka yote nchini, ambapo katika kipindi hiki jumla ya Wasafiri 784,822 wameweza kupimwa hali ya maambukizi ya UVIKO-19

iii. Kufanya Mafunzo ya kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ya msingi na Kamati za Ulinzi na Usalama ngazi ya Wilaya, mafunzo hayo yalihusu kujikita zaidi katika kukabiliana na changamoto ya wasafiri wanaotumia njia zisizo rasmi kuingia nchini katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Arusha, Rukwa, Kagera na Kigoma. Mafunzo hayo pia yalijikita katika mbinu za kumtambua na utoaji wa taarifa za msafiri mwenye dalili za magojwa na njia za kujikinga ili kuzuia maambukizi wakati wa kumhudumia msafiri huyo.

iv. Kuongeza vituo vya kupimia UVIKO-19 kutoka kituo 1 hadi vituo 9 ambavyo ni Maabara ya Taifa, hospitali ya Mount Meru (Arusha), Ngorongoro (Arusha), Hospitali Bugando (Mwanza), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Kanda ya Mbeya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bukoba (Kagera), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni (Kigoma), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Pia Vituo viwili vitaanza kutoa huduma hivi karibu ambavyo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Musoma (Mara) na Hospitali ya Mji wa Kahama

v. Wizara pia imeendesha mafunzo kwa watalaam 20 wanaofanya kazi mipakani kuhusu namna ya kuingiza

taarifa kwenye ramani yaani (Geographical Information System).

**Huduma za Lishe**

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha lishe na afya ya watoto wachanga na wadogo kwa kuendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto walio chini ya miaka mitano. Malengo ya kampeni ya mwaka 2021/22 yalikuwa ni kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto 8,248,450, kati ya umri wa miezi (6 – 59). Zoezi hili lilikamilika kwa kuweza kuwafikia walengwa 8,015,463 sawa na asilimia 97.2 ikilinganishwa na asilimia 95 ya mwaka 2020. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto kwa kuimarisha upatikanaji wa chakula dawa, upatikanaji wa vifaa vya kufanyia tathmini ya hali ya lishe pamoja na kuboresha miundombinu ya kufanyia matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto. Pia vituo vinavyotoa matibabu ya utapiamlo mkali kwa kulaza vimeongezeka kutoka vituo 365 mwaka 2020 kufikia vituo 385 vya kutolea huduma za afya hadi kufikia Machi, 2022.

28. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya utafiti wa hali ya lishe kwa wanafunzi wa shule za msingi za Serikali nchi nzima, ambapo jumla ya wanafunzi 63,000 kutoka shule 650 wamefanyiwa tathmini ya hali ya lishe na kudodoswa masuala ya ulaji na wanafunzi 21,000 wamepimwa kiasi cha damu. Utafiti huu umefanyika mwezi Agosti na Oktoba, 2021, uchakataji wa takwimu unaendelea. Ni matumaini ya Wizara kuwa matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kuboresha hali ya lishe kwa vijana hususani walioko mashuleni**.**

29. ***Mheshimiwa Spika***, Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo kuchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imeandaa na kuratibu

Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama ambayo yalifanyika mwezi Agosti, 2021 Mkoani Songwe. Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka 2021 ilikuwa ni; "*Kulinda unyonyeshaji wa maziwa ya mama ni jukumu letu sote*". Pia Wizara ilifanya warsha kwa wanahabari Mkoani Dodoma na Iringa mwezi Agosti, 2021 ambapo jumla ya waandishi wa habari 60 (magazeti, radio, luninga, blogs, social media) walijengewa uwezo kuhusu masuala mbalimbali ya Lishe ili kuweza kuibua changamoto za Lishe katika jamii zetu pamoja na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Lishe-bora kwa maendeleo ya mtu na Taifa kwa ujumla.

*30.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa lishe nchini imefanya maadhimisho ya Siku ya Lishe Kitaifa tarehe 18 – 23 Oktoba, 2021. Uzinduzi na Kilele cha Maadhimisho hayo umefanyika Mkoani Tabora. Aidha, Wizara ilifanya uraghibishi na mafunzo kwa timu za uendeshaji wa huduma za afya za Mikoa na Halmashauri (RHMT na CHMT) pamoja na watoa huduma za Afya kuhusu uanzishwaji wa vitengo vya kuratibu huduma za Lishe kwenye Vituo vya kutolea huduma za Afya katika Mikoa ya Tabora, Manyara na Dodoma, ambapo jumla ya watoa huduma **150** wamejengewa uwezo.

**Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

*31.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za Afya ya Uzazi, ikiwa ni pamoja huduma kabla ya kujifungua, Wakati wa ujauzito, Wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, kwa upande wa **huduma kabla ya ujauzito** ambapo Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) ilinunua na kusambaza vidonge vya uzazi wa mpango dozi 1,755,349 sawa na asilimia 82 ya lengo, sindano za uzazi wa mpango aina ya depo-provera dozi 2,125,625 sawa na asilimia 93 ya lengo na vipandikizi 206,000 sawa na asilimia 78 ya lengo. Dawa hizi zilisambazwa katika Halmshauri zote nchini. Katika kipindi hicho, wateja waliotumia njia za uzazi wa mpango walikuwa 4,189,787 ukilinganisha na wateja 4,357,151 wa

mwaka 2020. Njia hizo za uzazi wa mpango zilizotolewa katika vituo mbalimbali vya huduma za afya nchini ni pamoja na vipandikizi asilimia 57.1, sindano asilimia 18.5, vidonge asilimia 10.1, kondomu asilimia 5.3, kufunga kizazi mama asilimia 0.4, Kitanzi asilimia 7.2 na njia zingine asilimia 1.4

*32.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya wakati wa ujauzito (Antenatal Care)** ambapo inakadiriwa kuwa **kila mwaka akinamama wapatao milioni 2.3 hutarajiwa kupata ujauzito nchini Tanzania**. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, jumla ya **Wanawake wajawazito 1,784,809** walihudhuria Kliniki na kupatiwa huduma za Afya na kati yao, asilimia 99.7 ya akinamama wajawazito walifanya mahudhurio manne au zaidi ikilinganishwa na asilimia 85 mwaka 2020. Hata hivyo changamoto iliyopo ni wanawake wajawazito kuchelewa kuhudhuria klinik wapatapo ujauzito. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya wajawazito 1,784,809 ni wajawazito 656,040 sawa na asilimia 37.6 walianza kupata huduma za wajawazito chini ya wiki 12 za mwanzo wa ujauzito, ikilinganishwa na asilimia 36 ya kipindi kama hiki mwaka 2020. Aidha, katika kipindi Julai 2021 hadi Machi 2022, asilimia 99.7 ya akinamama wajawazito walifanya mahudhurio manne au zaidi ikilinganishwa na asilimia 85 mwaka 2020. Ongezeko hili kubwa la matumizi ya huduma za kliniki wakati wa ujauzito limetokana na kubadilika kwa mwongozo wa huduma muhimu wakati wa ujauzito kutoka mahudhurio ya kila baada ya miezi mitatu na kuwa mahudhurio ya kila mwezi (Jumla mahudhurio 8 au zaidi kwa kipindi chote cha ujauzito) pamoja na kuongezeka kwa uhamasishaji juu uhumimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki ngazi ya jamii. ***Nitumie Bunge lako Tukufu kuhimiza wajawazito kuhudhuria kliniki mapema ndani ya wiki 12 za mwanzo wa ujauzito na kukamilisha mahudhurio yote 8 ili kuepuka kupata changamoto mbalimbali zinazoweza kusababisha vifo vyao na vichanga vyao wakati wa kujifungua.***

*33.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa **huduma ya afya wakati wa kujifungua**, Serikali imeendelea kutoa elimu ya

umuhimu wa akina mama wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, wajawazito 1,398,778 walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya sawa na asilimia 79.5 ikilinganishwa na wajawazito 890,909 sawa na asilimia 80 ya waliojifungulia kliniki kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, wajawazito 1,340,239 walihudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi, ikilinganishwa na wajawazito 851,040 waliohudhuria kliniki kipindi kama hicho mwaka 2020. Takwimu zinazokusanywa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini zinaonesha vifo vitokanavyo na uzazi vimeendelea kupungua kutoka vifo 1,640 mwaka 2020 hadi vifo 1,580 mwaka 2021. Takwimu hizi hazijumuishi vifo vinavyotokea kwenye ngazi ya jamii, hata hivyo zinatuonyesha mwenendo wa kupungua vifo vitokanavyo na uzazi. Kupitia tafiti mbalimbali zinazoendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na Tanzania Demographic Health Survey (iliyoanza kufanyika Septemba 2021, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoka mwezi Septemba 2022) zitaonesha hali iliyofikiwa katika jitihaza za nchi yetu za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

*34*. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeratibu ujenzi na ukarabati mkubwa wa vituo vya Afya 304 ili kuviwezesha kutoa huduma kwa wajawazito wanaopata uzazi pingamizi wakati wa kujifungua (CEmONC), huduma ambayo imesaidia kuokoa maisha ya mama na mtoto. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya vituo vya Afya 250 sawa na asilimia 82.2 vilikuwa vimeanza kutoa huduma kamili ya CEmONC ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Wizara inaendelea kuhakikisha vituo vyote vya afya vilivyojengwa ambavyo havijaanza kutoa huduma vinapata watumishi wenye ujuzi hasa Madaktari, watoa dawa za usingizi na wakunga pamoja na vifaa tiba kwa lengo la ykuharakisha kuanza utoaji wa huduma. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wametoa mafunzo ya huduma muhimu za dharura kwa matatizo yatokanayo na uzazi na watoto wachanga pamoja na utoaji wa dawa za

usingizi na ganzi kwa watoa huduma za afya 598 kutoka Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Simiyu, Mtwara, Lindi, Mwanza na Morogoro.

*35.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha **huduma za Watoto wachanga** ambapo katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 jumla ya Vyumba/Wodi za Watoto Wachanga Mahututi (Neo- natal Intensive Care Unit - NICU) 30 zimeanzishwa katika hospitali za Halmashauri na hivyo kuwa kuwezesha kuwepo kwa jumla ya NICU 165. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imeziwezesha hospitali zote za Rufaa za Mikoa kuwa na NIC. Vilevile maboresho yamefanyika katika NICU ya Hospitali ya Taifa Muhimbili. Wizara pia imeendelea kufanya ufuatiliaji wa watoto wanaozaliwa na ulemavu katika Halmashauri za Ifakara TC, Mlimba DC, Kahama TC, Mbulu DC na Mbeya CC. Takwimu zilizokusanywa zinaonyesha kuwa jumla ya watoto wenye ulemavu 32,586 walizaliwa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, na kati yao Watoto 31,640 sawa na asilimia 97 walizaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kati ya watoto waliozaliwa, 54 walibainika kuwa na ulemavu wa kuzaliwa ambapo 14 walizaliwa wafu na 40 walikuwa hai na walipatiwa rufaa kwa matibabu zaidi ya kitaalamu. Huu ni wastani wa watoto 2 kuzaliwa na ulemavu kwa kila vizazi 1,000. Vilevile, Wizara imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu za kutibu na kuzuia magonjwa kwa Watoto ikiwemo Dawa ya kidonge myeyuko cha Amoxicillin kwa ajili ya Kichomi kwa Watoto *(bacterial pneumonia*) dozi 25,646,700 zilinunuliwa na kusambazwa sawa na asilimia 84 ya lengo. Aidha dawa ya zinki na ORS kwa ajili ya kutibu kuharisha zilizofungashwa kwa pamoja dozi 439,760 sawa na asilimia 86.5 ya lengo zilinunuliwa na kusambazwa.

*36.* ***Mheshimiwa Spika***, Kulingana na takwimu zinazokusanywa kutoka katika vituo vya kutolea huduma zinaonesha kuwa vifo vya Watoto vimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka ambapo vifo vya Watoto wachanga vimepungua kutoka vifo 8,190 mwaka 2020 hadi vifo 6,741

mwaka 2021; vifo vya Watoto wa chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 2,657 mwaka 2020 hadi vifo 1,092 mwaka 2021 na vifo vya Watoto umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 3,482 mwaka 2020 hadi vifo 1,512 mwaka 2021. Takwimu hizi hazijumuishi vifo vinavyotokea kwenye ngazi ya jamii, hata hivyo zinatuonyesha mwenendo wa kupungua vifo vya Watoto wa umri chini ya miaka mitano nchini. Kupitia tafiti mbalimbali zinazoendelea kufanyika ikiwa ni pamoja Tanzania Demographic Health Survey (iliyoanza kufanyika Septemba 2021, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoka mwezi Septemba 2022) zitaonesha hali iliyofikiwa katika vifo vya watoto.

*37.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 huduma kwa waliopatwa na **vitendo vya ukatili wa kijinsia na Ukatili Dhidi ya watoto** ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya wateja 97,479 walitoa taarifa katika vituo vya kutolea huduma za afya, kati yao waliotoa taarifa ndani ya masaa sabini na mbili (72) walikuwa 26,364 sawa na asilimia 27. Ili kupanua wigo wa huduma kwa waliofanyiwa vitendo vya Ukatili wa kijinsia na Ukatili Dhidi ya Watoto, vituo vya kutolea huduma jumuishi kwa waliofanyiwa vitendo vya ukatili vimeendelea kuongezeka ambapo kwa sasa vimefikia 18 kutoka vituo 13 mwaka 2020. Aidha, Watoa huduma wa afya 745 na watoa huduma wa ngazi ya jamii 155 wamejengewa uwezo wa namna ya kutoa huduma za kitabibu na kisaikolojia pamoja na utoaji wa elimu kwenye ngazi ya jamii. Wizara pia iliboresha huduma za kitabibu na kisaikolojia ambapo Mwongozo wa Kuzuia na Kupambana na Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia umehuishwa na kuongeza afua ya huduma kwa wanawake na wasichana waliofanyiwa ukeketaji ili kuweza kutoa huduma stahiki kwa wahanga ikiwemo wakati wa kujifungua. ***Nitoe wito kwa wahanga wa ukatili kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya ndani ya saa 72 baada ya tukio. Aidha, ninawataka watoa huduma za afya kutowanyanyapaa wahanga wa vitendo hivyo bali wawapatie***

***huduma haraka kwa kuzingatia miongozo mbalimbali iliyowekwa.***

*38.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kupambana na changamoto za afya wanazokutana nazo vijana jumla ya Watoa huduma za afya 650 kutoka Mikoa ya Njombe, Dodoma, Morogoro, Kigoma, Tanga, Geita, Singida, Shinyanga, Iringa na Arusha walijengewa uwezo kuhusu kutoa huduma za afya rafiki kwa vijana. Vilevile, jumla ya Waelimishaji rika 350 kutoka Mikoa ya Iringa, Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Tanga, Singida, Geita, Kigoma na Rukwa wamejengewa uwezo ili wawe na ujuzi wa stadi za maisha na elimu ya afya. Aidha, jumla ya vijana 397,613 sawa na asilimia 32 ya vijana balehe walipatiwa elimu na matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango. Vilevile, ili kupunguza changamoto za afya ambazo vijana wanakumbana nazo, Mwongozo umeandaliwa wa namna ya kuanzisha program za kuwafikia vijana walioko kwenye taasisi za elimu ya juu na kati ili kutoa elimu na huduma za kujikinga na maambukuzi ya Virusi vya UKIMWI, Ukatili wa Kijinsia na elimu ya afya ya uzazi. Kamati za afya ya Mkoa na Wilaya zote za Mkoa wa Rukwa wamefanyiwa uraghibishi wa agenda ya Kitaifa ya kuwekeza katika afya na ustawi wa vijana ili afua zilizoainishwa zianze kutekelezwa.

*39.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha **huduma za saratani ya mlango wa kizazi** Wizara iliweka malengo ya kufanya uchunguzi wa saratani ya Mlango wa Kizazi kwa wanawake 459,822 sawa na asilimia 12 ya wanawake walio kati ya miaka 30 hadi 50 kwa mwaka. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, jumla ya wanawake 162,773 sawa na asilimia 71 walifanyiwa uchunguzi. Kati ya hao, wanawake 3,847 walipatiwa matibabu ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi. Vilevile, jumla ya vituo vya kutolea huduma za saratani ya Mlango wa Kizazi viliongezeka kutoka 794 mwezi Juni, 2021 hadi kufikia vituo 801 mwezi Machi, 2022. Mpango wa Wizara ni kuhakikisha kuwa huduma za kupima saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti zinapatikana kwa

urahisi katika ngazi za chini hususani kwenye Zahanati na Vituo vya Afya lengo likiwa ni kupunguza mzigo wa kutiba magonjwa ya saratani na kuwaepusha wananchi na vifo kwani saratani inatibika ikigundulika mapema.

**Udhibiti wa VVU/UKIMWI**

*40.* ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara imeendelea kuboresha afua mbalimbali ambazo zinahamasisha wananchi kwenda kupima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU/UKIMWI, ili waweze kupatiwa huduma za ushauri, upimaji, matunzo na huduma za dawa kwa haraka pale inapoonekana kuwa wameambukizwa. Hadi kufikia Desemba 2021 Jumla ya wateja 1,519,013 sawa na **asilimia 84.6** ya watu 1,795,905 wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI nchini walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi (95 ya kwanza). Kati yao, wateja 1,507,686 sawa na **asilimia 99.3** walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI (95 ya pili). Aidha, hadi sasa **asilimia 95.8** ya wateja waliokuwa wanatumia dawa za ARV nchini walikuwa wamefubaza wingi wa virusi vya UKIMWI ambayo ni sawa na chini ya nakala 1,000 (95 ya tatu).

*41.* ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Idadi ya **vituo vinavyotoa huduma ya Tiba ya UKIMWI** (CTC) vimefikia 6,759 kutoka vituo 5,555 mwaka 2015 na kati ya hivyo CTC kamili ni 3,075 na vituo vya huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto (RCHS) vinavyotoa huduma ya kutoa dawa ya kufubaza Virusi vya UKIMWI vipo 3,684. Aidha, Wizara ilisaini mwongozo wa utekelezaji wa utoaji dawa kinga na kuanza kwa huduma hiyo, ambapo hadi sasa jumla ya walengwa 13,285 walianza huduma hiyo katika Mikoa yote nchini.

*42.* ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya **Kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT)** zinatolewa katika **vituo 6,996** sawa na **asilimia 98** kati ya **vituo 7,138** vinavyotoa huduma za afya ya uzazi na Mtoto. Aidha, Wizara imeweza

kupanua huduma ya upimaji wa pamoja wa VVU na kaswende kwa wajawazito ambapo jumla ya vituo 3,497 kati ya 7,138 sawa na asilimia 49 vinavyotoa huduma za afya ya uzazi na mtoto vimeanza kupima VVU na kaswende kwa kutumia kitepe kimoja, lengo ni vituo vyote viweze kutoa huduma ya upimaji huo. Vilevile, katika kipindi cha 2021/22 wajawazito waliopatiwa huduma za upimaji wa VVU walifikia asilimia 99. Wizara imeendelea kupanua **huduma za upimaji wa Watoto wachanga** waliozaliwa na akina mama wenye VVU kutoka Idadi ya vituo vinavyotoa huduma hizi kutoka vituo 50 mwaka 2020 hadi vituo 141 mwaka 2021. Upimaji huo hufanyika kwa kutumia vinasaba vya VVU mahali zitolewapo huduma (EID Point of Care). Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, jumla ya watoto 54,134 waliozaliwa na akina mama wanaoishi na VVU walipimwa vinasaba vya VVU na kati yao watoto 1,299 sawa na asilimia 2 walikutwa na maambukizi ya VVU na wote waliunganishwa na huduma ya matibabu lengo ni kuzuia kabisa maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto. Kwa ujumla maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameendelea kuwa asilimia 11 kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2021.

*43.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha afua mpya ya **Mama Kinara** katika ngazi ya Jamii kwa ajili ya kuwezesha ufuatiliaji wa wajawazito na akina mama wanaonyonyesha ambao wamekwisha thibitika kuwa na maambukizi ya VVU. Kitendea kazi cha “Mama Kinara” kimetengenezwa na jumla ya Mama Kinara 818 na Wakufunzi 40 walipata mafunzo yaliyofanyika katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga, Dodoma, Manyara, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Geita na Tabora. Hadi sasa jumla ya akinamama 68,028 wanaonyonyesha walio na VVU wamefikiwa kati ya akinamama 73,935. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha wanawake wenye maambukizi ya VVU/UKIMWI wananyonyesha Watoto wao ili kuweza kuwafanya wawe na afya bora.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma**

*44.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za Kifua Kikuu na Ukoma sanjari na Mpango Mkakati wa Sita wa mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma. Lengo kuu katika mpango huu ni Kuongeza kasi ya uibuaji wa wagonjwa, kupunguza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu na kutokomeza Ukoma katika Halmashauri zenye wagonjwa wa Ukoma. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara ilipanga kuibua wagonjwa 44,993 ambapo wagonjwa 46,104 waliibuliwa, sawa na asilimia 102. Aidha, hadi kufikia Machi, 2022 asilimia 96 ya wagonjwa waliopatiwa matibabu ya Kifua Kikuu walipona ambapo ni juu ya lengo la Shirika la Afya Duniani (WHO) la kuponyesha asilimia 90 ya wagonjwa wanaoanza matibabu. Mafanikio haya ni matokeo ya ufuatiliaji wa kimkakati wa karibu wa wagonjwa vituoni na ushirikishwaji wa watoa huduma katika ngazi ya jamii na ushiriki mzuri wa Jumuia ya Mwitikio wa Kudhibiti Kifua Kikuu na UKIMWI Tanzania (MKUTA). Vilevile, katika kipindi hicho, jumla ya wagonjwa 275 wa Kifua Kikuu Sugu waligundulika ikilinganishwa na wagonjwa 214 waliogundulikwa katika kipindi cha mwaka 2021. Wagonjwa waliogunduliwa kuwa na Kifua Kikuu Sugu walianzishiwa matibabu kikamilifu.

*45.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha huduma za **upimaji wa Kifua Kikuu**, Serikali imeongeza mashine za kisasa za GeneXpert zinazopima Kifua Kikuu kwa ufanisi na muda mfupi kutoka 268 mwaka 2020/21 hadi mashine 336 mwezi Machi, 2022. Mashine hizo hupima na kutoa majibu ndani ya masaa 2 ikilinganishwa na darubini ambazo hutoa majibu baada ya masaa 48. Pia katika kipindi hiki, Wizara imenunua na kusambaza mashine 179 za ECG kwa ajili ya ufuatiliaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu.

*46.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeanzisha **huduma mkoba za kliniki tembezi** (Mobile vans outreach services) zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya watu 14,000 walio katika maeneo hayo walichunguzwa na kupimwa Kifua Kikuu. Kati ya waliopimwa 1,076 sawa na asilimia 8 waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu na kuanzishiwa matibabu.

*47.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha njia za uibuaji wa wagonjwa wapya wa Ukoma na utoaji wa tiba kinga kwa makundi hatarishi. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya Kaya 110 zilifikiwa na kufanyiwa uchunguzi. Katika zoezi hili, wagonjwa wapya wa Ukoma 15 waliibuliwa na kuanzishiwa matibabu. Pia katika kipindi hiki watu 2,131 waliokuwa katika makundi hatarishi walipewa tiba kinga na watu 1,050 waligundulika kuwa na magonjwa mengine ya ngozi walianzishiwa matibabu. Sanjari na utoaji wa huduma za Ukoma, Wizara imeendelea kutoa vifaa tiba kwa waathirika wa Ukoma kwa kugawa jozi za viatu 1,800 ili kupunguza athari za ulemavu kwa waathirika wa Ukoma. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza tafiti kubwa tatu za Ukoma; (i) Tafiti inayolenga kubainisha maeneo hatarishi ya maambukizi ya Ukoma "Geo Spatial Methods of clustering Leprosy cases", (ii) Tafiti ya kubaini njia ya ufuasi ya utoaji tiba kinga "PEP4LEP study" na (iii) Tafiti ya kubaini njia bora ya kuanza ufuatiliaji wa mwenendo wa usugu wa dawa za Ukoma "Antimicrobial resistance study".

**Udhibiti wa Malaria**

*48.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali katika jitihada za kupunguza na kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini kama ilivyo ainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Malaria wa mwaka 2021-2025. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2022

ni pamoja na; Kufuatilia wingi (density), tabia (Behavior), aina (Species) na uwepo wa vimelea vya malaria (sporozoites) kwenye miili ya mbu waenezao malaria katika Halmashauri zenye vituo maalumu (sentinel sites) vinavyotumika katika ufuatiliaji huo. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, **ufuatiliaji na usimamizi shirikishi** ulifanyika katika Halmashauri 24 zenye vituo maalumu ambavyo ni; Uvinza DC, Kigoma Ujiji, Kasulu DC, Uyui DC, Igunga DC, Sikonge DC, Tanganyika DC, Mlele DC, Muleba DC, Missenyi DC, Ngara DC, Geita DC, Bukombe DC, Bagamoyo DC, Rufiji DC, Mtwara MC, Tandahimba DC, Ruangwa DC, Kilwa DC, Ilala MC, Kinondoni MC, Kilosa DC, Mvomero DC na Ulanga DC. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya entomolojia kwa ajili ya kazi ya utegaji wa mbu wapevu kwenye vituo maalumu 32 pamoja na uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli kwa njia ya PCR/ELISA ili kuweza kutambua aina ya mbu na uwepo wa vimelea wa malaria katika vituo maalumu 32 kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya **vyandarua vyenye dawa ya kuzuia mbu 2,514,276** vimesambazwa katika **Mikoa 5** ya Mwanza, Geita, Kigoma, Kagera na Mara kwa lengo la kupambana na maambukizo ya ugonjwa wa malaria.

*49.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na maambukizo ya ugonjwa wa malaria, Wizara pia imeendelea kutekeleza afua ya **upuliziaji dawa ukoko katika kuta za nyumba** katika mikoa yenye kiwango kikubwa cha maambukizo ya ugonjwa wa malaria. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, upuliziaji wa dawa umefanyika katika Halmashauri 6 za Kasulu, Kakonko, Kibondo, Biharamulo, Bukombe na Ukerewe ambapo jumla ya nyumba 592,444 zimepuliziwa na wananchi 2,665,998 wamekingwa dhidi ya maambukizi ya malaria katika maeneo hayo.

*50.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi, inatekeleza Mradi wa **Kuelekea Utokomezaji wa Malaria** (*Towards Elimination of Malaria in Tanzania-TEMT*)

unaotekelezwa kwenye Mikoa 5 na Halmashauri 15 za Tanzania Bara ambayo ni Kilimanjaro (Rombo DC, Same DC na Moshi DC), Dodoma (Kondoa DC, Chamwino DC na Mpwapwa DC), Tanga (Handeni DC, Lushoto DC na Tanga Jiji), Kigoma (Kibondo DC, Kigoma-Ujiji MC na Uvinza) na Ruvuma (Tunduru DC, Nyasa DC na Songea MC). Kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ni pamoja na; kutoa mafunzo kwa washiriki 969 katika mkoa wa Tanga ambapo washiriki hao walitoka ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na vijiji kuhusu upuliziaji dawa ukoko, ununuzi wa pampu 532 pamoja na viuadudu (lita 342 aina ya *Bactivec* na lita 147 aina ya *Griselesf*).

*51.* ***Mheshimiwa spika,*** Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) ilipokea kutoka kwa Wadau wa Maendeleo Dawa mseto ya kutibu Malaria (ALu) dozi 14,977,710, Vipimo vya haraka vya malaria (mRDT) jumla ya vitepe 20,991,875 na dawa ya sindano ya kutibu Malaria kali (Inj. Artesunate) vichupa 2,356,930. Dawa na vitendanishi hivi vinaendelea kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kupitia Bohari ya Dawa (MSD), kulingana na mahitaji ya vituo husika. Huduma za uchunguzi wa malaria kwa kutimia vipimo vya haraka na matibabu ya Malaria zinatolewa bila malipo. ***Nitumie Fursa hii kuwataka watoa huduma za afya nchini kuzingatia Mwongozo wa Serikali wa kutoa huduma bure za uchunguzi na matibabu ya malaria.***

**Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko yanayotolewa Taarifa kimataifa**

*52.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara imeendelea kupambana na maambukizi ya magonjwa ya mlipuko ikiwemo Kipindupindu, Kimeta, Ebola, UVIKO-19, ambapo jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwemo kutoa Elimu ya Afya kwa Umma na kuandaa miongozo kuhusu kujikinga na magonjwa. Mafunzo ya Epidemiolojia na Usimamizi wa Maabara kwa ngazi zote za utoaji mafunzo (mafunzo ya awali, ya kati na ya muda mrefu)

yanaendelea kutolewa. Jumla ya Wanafunzi 44 wa mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa pamoja na Epidemiolojia na usimamizi wa Maabara wameendelea na mafunzo yao ya darasani na ya vitendo ambapo wameweza kufanya tafiti mbalimbali za magonjwa, kutathmini mifumo mbalimbali ya ufuatiliaji wa magonjwa na matukio yenye athari kiafya, kufanya uchunguzi wa milipuko ya magonjwa (Kimeta na Kipindupindu) pamoja na kusaidia mapambano dhidi ya UVIKO-19.

*53.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022, ugonjwa wa kipindupindu uliripotiwa katika Halmashauri za Nkasi, Kigoma Manispaa, Kigoma DC, Tanganyika na Uvinza ambapo jumla ya wagonjwa 390 na vifo 4 viliripotiwa. Aidha ugonjwa wa UVIKO19 umeendelea kuripotiwa hapa Nchini ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Novemba 2021 ugonjwa umeripotiwa kwa wastani wa visa 55 kwa siku na vifo 2 kwa wiki moja. Hali ya ugonjwa iliongezeka katika kipindi cha Disemba 2021 hadi Januari 2022, ambapo viliripotiwa wastani wa visa 121 kwa siku na vifo 7 kwa wiki moja. Hali ya ugonjwa huu iliendelea kupungua kwa wastani wa visa 7 kwa siku na kifo 1 kwa wiki kuanzia mwezi Februari 2022 hadi Mei, 2022

*54.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na Ufuatiliaji wa magonjwa ya njia ya hewa yanayofanana na *influenza* katika vituo maalum *(Sentinel sites)* vilivyopo katika Mikoa 15 ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Manyara, Arusha, Dodoma, Mwanza, Tabora, Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa na Kigoma. Vituo vinavyo toa huduma ya upimaji vimeendelea kuongezeka kutoka 9 mwaka 2020 hadi vituo 18 Machi, 2022 Lengo ni kuwa na angalau na kituo kimoja katika kila Mkoa ili kuendelea na ufuatiliaji wa mwenendo wa magonjwa ya njia ya hewa yaliyopo na mapya.

*55.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inakamilisha mfumo wa ki-elekroniki wa ufuatiliaji wa tetesi za Magonjwa na matukio yenye athari za kiafya unaotegemewa kukamilika mwezi Mei, 2022. Pia Madawati ya ufuatiliaji wa tetesi za magonjwa ngazi ya Mkoa yamehuishwa katika Mikoa 6 (Kagera, Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Tanga na Arusha) na Watumishi 640 na Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii 800 katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Dar es Salaam wamepatiwa mafunzo ya ufuatiliaji wa Taarifa za tetesi za Magonjwa na Matukio yenye athari kiafya.

**Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele**

*56.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na **magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele** ikiwa ni pamoja na Usubi, matende na mabusha, kichocho na trakoma, Wizara imehakikisha kuwa wataalam, dawa, vifaa na vifaa tiba vya kutosha vinapelekwa katika maeneo ambayo yameonekana yanasumbuliwa zaidi na magonjwa hayo. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) ilisambaza dawa aina ya *Ivermectin (Mectizan)* vidonge 26,620,500 na *Albendazole* vidonge 7,817,400 vya kudhibiti na kukinga magonjwa ya **Usubi, Matende na Mabusha**. Aidha, Wizara ilisambaza dawa aina ya *Praziquantel* vidonge 7,966,000 kudhibiti na kukinga ugonjwa wa Kichocho; *Zithromax* vidonge 1,944,500 na Zithromax ya maji, chupa 16,088 kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa **Trakoma** katika halmashauri za Ngorongoro, Longido, Kiteto na Simanjiro.

*57.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Wizara ilitoa Kingatiba za kutokomeza **ugonjwa wa Matende na Mabusha** kwa Wananchi wa Wilaya za Kilwa, Pangani Temeke, Ilala na Kinondoni. Wananchi wengi walijitokeza kumeza kinga tiba dhidi ya ugonjwa wa matende ikilinganishwa na lengo lililopangwa katika maeneo husika kama ifuatavyo; Kilwa asilimia 80 ya lengo, Pangani asilimia 83. Temeke asilimia 80, Jiji la Dar es Salaam asilimia 70, Kinondoni asilimia 76, Mtwara DC asilimia 79, Mtama asilimia

82 na Mafia asilimia 71. Jumla ya watu 4,055,719 walimeza kingatiba hiyo ambayo ni sawa na asilimia 77.6 ya walengwa wote. Mafanikio haya yametokana na upatikanaji wa madawa kwa wakati, rasilimali fedha, uhamasishaji na mwitikio mzuri wa Jamii.

*58.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya **Wagonjwa 2,473** wa **vikope** walifanyiwa usawazishaji wa kope katika Mikoa ya Pwani, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Singida, Rukwa na Dodoma. Mafanikio haya yametokana na mwitikio chanya wa jamii katika kupokea huduma hii ya usawazishaji wa kope. Aidha ugawaji wa kingatiba ya kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa trakoma ulifanyika katika Halmashauri za Chamwino, Kongwa na Kiteto. Wananchi wengi walijitokeza kumeza dawa hizi kwa asilimia kubwa dhidi ya malengo yaliyokuwa yamewekwa katika maeneo husika kama ifuatavyo;

Ngorongoro asilimia 88, Chamwino asilimia 83, Kongwa asilimia 96, na Kiteto asilimia 93. Jumla ya watu 714,273 walimeza Kingatiba hiyo. Vilevile, Wizara iliendelea na shughuli za kudhibiti ugonjwa wa usubi, ambapo ugawaji wa dawa za kingatiba kwa jamii ulifanyika katika Mikoa 7 na Halmashauri 28 ambapo mafanikio dhidi ya malengo yaliyokuwa yamewekwa katika maeneo husika ni kama ifuatavyo; Iringa asilimia 86, Mbeya asilimia 82, Morogoro asilimia 86, Njombe asilimia 85, Ruvuma asilimia 83, Songwe asilimia 84, Tanga asilimia 86. Jumla ya watu 5,730,442 walimeza kingatiba hiyo ambayo ni sawa na asilimia 85 ya walengwa wote.

**Elimu ya Afya kwa Umma**

*59.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya lishe, huduma za mama na mtoto, afya ya mazingira, magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza na namna ya kujikinga na

majanga mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara iliandaa na kusambaza vielelezo vya kutoa elimu kwa jamiii kama ifuatavyo; Mabango 693,000, Vipeperushi 500,050 pamoja na kurusha matangazo ya Runinga 12,734 na 21,572 ya Redio. Aidha Wizara imeratibu Vipindi 618 vya Redio, vya Runinga 308 na kurusha kupitia mitandao ya kijamii vipeperushi 5,690, picha za sauti 286 na kusambaza *USB flash* 621 zenye ujumbe wa elimu ya afya.

*60.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha na kushirikisha jamii kuchukua hatua dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza pamoja na kupata uelewa wa masuala mbalimbali ya afya, Wizara ilitoa mafunzo na uelimishaji kwa makundi mbalimbali ya kijamii ambapo Viongozi wa Dini 1,230, Wanahabari na Wahariri wa vyombo vya habari 230, Wazee Mashuhuri 1,560 na Wasanii 45. Mafunzo haya yalilenga kuhamasisha masuala mbalimbali ya kiafya hususan kinga dhidi ya UVIKO-19 na matumizi ya chanjo. Wizara imefanya mafunzo na kampeni ya Mpango Harakishi na Shirikishi wa Kinga dhidi ya UVIKO-19 pamoja na matumizi ya chanjo awamu ya pili. Mafunzo yalihudhuriwa na washiriki 249 kutoka Wizara ya Afya, OR-TAMISEMI, Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu wa Bunge, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Wizara nyingine, Wadau wa maendeleo, Wawakilishi wa viongozi wa Kidini, viongozi wa Serikali za Mitaa na Viongozi wa Kimila.

## HUDUMA ZA TIBA

### Usimamizi wa Vituo vya kutolea huduma za Afya

*61.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya nchini zinazotolewa kupitia **Vituo vya kutolea huduma** vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vilivyosajiliwa vimeongezeka

kufikia 8,549 ikilinganishwa na vituo 8,458 mwaka 2020. Kati ya hivyo, Hospitali ni 404, Vituo vya Afya 956 and Zahanati 7,189.

**Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa, 2021/22**

| **Aina ya Vituo** | **Julai 2020-Juni 2021** | | | | **Julai 2021 – Machi, 2022** | | | | **Idadi ya vituo Vilivyo ongezeka (Julai 2021 – Machi, 2022** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Serikali** | **Mashirika ya Dini** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Mashirika ya Dini** | **Binafsi** | **Jumla** | **Jumla** |
| Hospitali | 185 | 117 | 67 | 369 | 207 | 112 | 85 | 404 | **35** |
| Vituo vya Afya | 645 | 124 | 157 | 926 | 679 | 150 | 127 | 956 | **30** |
| Zahanati | 5,395 | 676 | 1,092 | 7,163 | 5,491 | 622 | 1,076 | 7,189 | **26** |
| **Jumla ndogo** | **6,225** | **917** | **1,316** | **8,458** | **6,377** | **884** | **1,288** | | **91** |

***Chanzo: HFR***

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Hospitali za Watu Binafsi imesajili vituo vya kutolea huduma katika ngazi mbalimbali ambavyo ni; Hospitali ngazi ya Wilaya 12, Hospitali ngazi ya Mkoa mbili (2), Hospitali za Kibingwa 1, Vituo vya Afya 7, Zahanati 89, Polyclinic 57 na kliniki za kawaida 47. Kwa ujumla vituo vilivyosajiliwa na bodi hadi kufikia Machi 2022 ni 3,198. Aidha, Wizara imetengeneza Mfumo wa Usajili wa Kielektroniki, ambao utatumiwa na wamiliki wa Hospitali Binafsi na Umma kutuma maombi yao ya usajili na kulipia ada mbalimbali kupitia mfumo huu ambao umeunganishwa na Mfumo wa Mfuko Mkuu wa Serikali (GePG). Kwa kufanya hivi, Mfumo huo utarahisisha upatikanaji wa haraka wa huduma ya usajili wa vituo na kupokea malipo mbalimbali ili

kupunguza gharama za usafiri badala ya kufuata huduma hii Dodoma na hivyo kuepuka usumbufu usio wa lazima.

63. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za tiba nchini ambapo katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya Wagonjwa 21,230,469 walipatiwa huduma, ambapo Wagonjwa 20,428,932 ni wa nje na Wagonjwa 801,537 walilazwa. Wagonjwa hao walipatiwa huduma katika Hospitali za ngazi ya Taifa, Kanda, Mikoa, Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati zote nchini kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo chini.

**Idadi ya Wagonjwa waliohudhuria katika Vituo vya kutolea huduma za afya kwa kipindi Julai 2020 hadi Machi, 2021.**

| AINA YA VITUO | Mahudhurio katika Vituo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai, 2020 hadi Machi, 2021 | | | | | |
| | OPD (wagonjwa wa nje) | Asilimia | IPD (wagonjwa wa kulazwa) | Asilimia | JUMLA | Asilimia |
| Hospitali | 5,372,495 | 26 | 566,853 | 66 | 5,939,348 | 28 |
| Vituo vya Afya | 4,614,193 | 22 | 275,185 | 32 | 4,889,378 | 23 |
| Zahanati | 10,297,155 | 50 | 0 | 0 | 10,297,155 | 48 |
| Kliniki | 447,894 | 3 | 12,442 | 1 | 460,336 | 3 |
| **Jumla** | **20,731,737** | | **854,480** | | **21,586,217** | |

***Chanzo: DHIS2***

64. ***Mheshimiwa Spika***, kulinganisha na takwimu zilizoainishwa katika jedwali hapo juu, idadi kubwa ya Wagonjwa wa Nje walipatiwa huduma katika ngazi ya Zahanati kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 na asilimia kubwa ya Wagonjwa wa kulaza walipata huduma katika Hospitali. Hali hii imejidhihirisha pia katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo chini.

**Idadi ya Wagonjwa waliohudhuria katika Vituo vya kutolea huduma za afya kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022.**

| AINA YA VITUO | Mahudhurio ya Vituo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai 2021 hadi machi 2022 | | | | | |
| | OPD (wagonjwa wa Nje) | Asilimia | IPD (wagonjwa wa kulazwa) | asilimia | JUMLA | Asilimi a |
| **Hospitali** | 8,693,153 | 28.4 | 823,973 | 67.66 | 9,517,126 | 30 |
| **Vituo vya Afya** | 6,565,696 | 21.5 | 380,024 | 31.20 | 6,945,720 | 22 |
| **Zahanati** | 14,101,020 | 46.1 | 13,305 | 1.09 | 14,114,325 | 44 |
| **Kliniki** | 1,222,227 | 4 | 600 | 0.05 | 1,222,827 | 4 |
| **Jumla** | **30,582,096** | | **1,217,902** | | **31,799,998** | |

***Chanzo: DHIS2***

**Magonjwa yaliyoongoza kuwaathiri wananchi (Top ten Diseases)**

65. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, magonjwa yaliyoongoza kwa **wagonjwa wa nje (OPD)** wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa, Malaria na maambukizi katika njia ya mkojo; na kwa umri wa miaka mitano na zaidi magonjwa yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa, Maambukizi katika njia ya mkojo na Malaria (Kiambatisho Na.1)

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, magonjwa yaliyoongoza kwa **wagonjwa wa kulazwa (IPD)** kwa wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni Kichomi (Severe and non- Severe), Malaria na kuharisha sana (Acute diarhoea), ambapo kwa watu walio na umri wa miaka mitano na zaidi, magonjwa yalioongoza yalikuwa ni Malaria, Kichomi (Severe and non-Severe) na maambukizi katika njia ya mkojo (UTI) (Kiambatisho Na.2). Katika kundi hili la wagonjwa, magonjwa yasiyoambukiza yalikuwa ni moja ya chanzo cha watu kwenda kulazwa katika vituo vya kutolea

huduma za afya; hali inayoashiria kukua kwa kiwango cha tatizo la magonjwa ya aina hiyo hapa nchini.

**Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

*67.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya unakuwa wa kuridhisha. Wizara kupitia Bohari ya Dawa hununua, hutunza na husambaza zaidi ya aina **2,976** za dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Kati ya hizo aina **290** zimeainishwa kuwa ni dawa muhimu na za kipaumbele cha Wizara ya Afya kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinapatikana nyakati zote katika Bohari ya Dawa (MSD). Aidha hadi sasa, Wizara ya Afya kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imeshapeleka MSD kiasi cha **shilingi 129,851,510,000.00** kwa ajili ya ugharamiaji wa mnyororo mzima wa upatikanaji wa dawa. Kupatikana kwa fedha hizi kumewezesha upatikanaji wa aina 290 za dawa, vifaa tiba na vitendanishi muhimu kufikia asilimia 51 katika ngazi ya MSD na asilimia 43 ngazi ya Zahanati, asilimia 42 kwa ngazi ya Vituo vya Afya, asilimia 50 kwa ngazi ya hospitali za Wilaya, asilimia 76 kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa na asilimia 51 katika Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa. Wizara itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha MSD wananunua na kusambaza dawa, vifaa na vifaatiba vyenye ubora na kwa gharama nafuu. Aidha Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI itaendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa dawa katika Vituo vya kutolewa huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali.

*68.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za afya nchini, MSD imeendelea kusimamia uzalishaji wa barakoa ambapo hadi Machi, 2022 kiwanda cha *KEKO Phamaceautical* kimezalisha barakoa 1,988,200 zenye thamani ya shilingi 1,361,985,200. Aidha, Ujenzi wa Kiwanda cha Mipira ya kuvaa mikononi (Gloves) umekamilika kwa asilimia 90 na uzalishaji wa majaribio tayari umeanza. Ujenzi

wa kiwanda hicho umeenda sanjari na ujenzi wa nyumba tatu za wafanyakazi ambazo tayari zimekamilika. Vilevile, MSD imenunua mitambo ya kutengeneza na kufungasha dawa rojorojo (*ointment and cream*) ambayo imekwishawasili nchini, ambapo ujenzi kwa ajili ya kiwanda hicho umeendelea kukamilishwa na baadhi ya malighafi zimekwishawasili nchini na mkandarasi wa kusimika mitambo ya kiwanda tayari amepatikana. Ni matarajio ya Wizara kuwa viwanda hivi vitawezesha upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya kwa wakati na kwa gharama nafuu.

**Upatikanaji wa Damu Salama**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama ilipanga kukusanya chupa za Damu Salama 375,000 ili kukidhi mahitaji ya Damu Salama nchini katika kipindi cha mwaka mzima wa 2020/21. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, Wizara ilifanikiwa kukusanya **chupa za damu 252,372** sawa na **asilimia 67** ya lengo la mwaka, ikilinganishwa na idadi ya chupa za damu salama 250,933 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2010/21. Damu zote zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu, pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni UKIMWI (HIV), Homa ya ini B na C (HBV & HCV) na Kaswende (Syphilis). Jumla ya chupa za damu 222,444 sawa na asilimia 88 ya chupa zilizokusanywa zilikuwa salama na kusambazwa hospitalini kwa ajili ya matumizi. Wizara imepanga kukusanya jumla ya chupa za damu 550,000 ikiwa ni ongezeko la chupa 175,000 sawa na ongezeko la asilimia 46. Na katika kuimarisha upatikanaji wa damu salamu, Wizara imeamua kutoa bure mifuko ya kukusanyia damu kwa Halmashauri zote nchini. Hii ni kutokana na kuwa Damu salama ni bidhaa ya afya ambayo haiuzwi au kupatikana katika maduka au benki binafsi isipokuwa Serikalini tu. Hivyo Wizara imeona ni vyema kuondoa vikwazo vilivyopo vya upatikanaji wa damu salama ili kuokoa Maisha. Kutokana na uamuzi huu wa Wizara wa kugawa bure mifuko ya damu, Halmashauri na Mikoa sasa watawajibika kugharamia shughuli za kuelimisha na

kuhamasisha wananchi kuchagia damu pamoja na kuandaa kampeni za kuchangia damu katika maeneo yao.

Aidha katika kipindi hicho Jumla ya chupa za Damu Salama 27,616 sawa na asilimia 11 ya chupa zote zilizokusanywa zilitengenezwa mazao ya damu, ambapo jumla ya **mazao 48,079** (Chembe sahani 4,887, Plasma mgando ni 15,566 na Chembe hai nyekundu ni 27,626). yalitengenezwa

*70.* ***Mheshimiwa Spika*** Wizara imeendelea kuhakikisha huduma za damu salama zinaimarika na kusogea karibu na wananchi kupitia ujenzi unaoendelea wa Kituo cha Kanda ya Kati Dodoma, pamoja na vituo **vitano (5)** vya Mikoa kwenye Mikoa ya Njombe, Rukwa, Tanga, Kigoma na Manyara. Vilevile, mpango utawezesha Hospitali za Mikoa kutengeneza mazao ya damu kwa mwaka 2022/2023 ili kuongeza vituo vinavyotengeneza mazao ya damu vya sasa ambavyo ni Vituo saba vya Kanda, Hospitali za Rufaa za kanda, Pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

**Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza**

*71.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zilizolenga katika kukabiliana na magonjwa **yasiyoambukiza** ambayo yameendelea kuwa changamoto katika Sekta ya Afya. Afua zilizotekelezwa kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ni pamoja na;

- Ukarabati wa Kliniki zinazotoa huduma za Selimundu na Hemofilia katika Hospitali ya KCMC, Muhimbili, Benjamin Mkapa, Bugando, Mbeya ZRH na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro umefanyika.
- Kuendelea na upanuzi wa huduma za usafishaji wa damu (dialysis) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kuongeza Hospitali nyingine 12 za awamu ya pili zitakazotoa huduma hizo ambapo awamu ya kwanza ilihusu Hospitali 7. Mkakati huo unatekelezwa kwa kushirikisha MSD na NHIF, ambao utawezesha huduma za usafishaji wa damu kuongezeka kutoka asilimia 47, yaani

watu 2,749 wanaopata huduma za dialysis sasa kati ya 5,800 wanaokadiriwa kuhitaji huduma hiyo kufikia asilimia 60 ifikapo Juni 2023. Mkakati wa Wizara ni kuziwezesha Hospitali zote za Rufaa za Mikoa kutoa huduma ya kusafisha damu.

- Kuandaa Sheria ya uvunaji na upandikizwaji wa Viungo ambayo mchakato wake umefikia hatua ya kukusanya maoni ya Wadau wa Sheria hiyo.
- Kuandaa na kuzindua Mpango Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza wa mwaka 2021-2026 unaotoa dira ya mapambano dhidi ya Magonjwa yasiyoambukiza nchini.
- Kufanya uchambuzi wa Sera na Sheria mbalimbali zinazohusu afua za lishe na mazoezi ili kuweza kurekebisha Sheria na Sera katika kuongeza kasi ya mapambano ya vihatarishi (risk factors) vya magonjywa yasiyoambukiza. Uchambuzi huu umekamilika na ushawishi na uraghibishi kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge unaendelea.
- Kuandaa na kuzindua Mwongozo wa mazoezi ya kuushughulisha mwili na kuepuka tabia bwete ambao pia umeainisha aina ya mazoezi kwa makundi mbalimbali.
- Kuandaa vipindi mbalimbali na machapisho ya utoaji wa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza. Hii ikiwa ni pamoja na kuadhimisha wiki ya Magonjwa yasiyoambukiza iliyoadhimishwa tarehe 07 hadi 13 Novemba 2021, ambapo machapisho zaidi ya 250 yaliwasilishwa katika Kongamano la Kisayansi, na Wananchi zaidi ya 300,000 walifikiwa na huduma mbalimbali za upimaji wa Magonjwa yasiyoambukiza zilizotolewa.
- Kuandaa mtaala wa mafunzo ya Magonjwa yasiyoambukiza kwa watoa huduma za afya katika ngazi ya Afya ya Msingi. Hadi sasa, Wizara imeweza kufanya mafunzo kwa watoa huduma 159 kutoka katika vituo vya afya 57 vya Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam.

- Kukamilisha Mkakati wa Kifaifa wa Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku nchini kwa miaka (5) kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26.
- Kufanya mafunzo ya utoaji huduma za kisukari na *diabetic foot* kwa Hospitali zote za Rufaa za Mikoa.
- Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha tathmini ya hali ya huduma za utengamao ambayo ilitumika kuandaa mkakati wa uimarishaji wa huduma za utengamao wa mwaka 2021-2026. Sambamba na mkakati huo serikali imeendelea kuimarisha karakana za tiba mtengamao katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Iringa na Mtwara ili kuziwesha kuwa na vifaa vya kisasa katika utoaji wa huduma hizo.

**Uimarishaji wa huduma za Matibabu ya Kibingwa nchini**

*72. **Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa nchini, ili kuokoa maisha ya wananchi wengi sambamba na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa ziliwasilisha Wizarani idadi ya wagonjwa 49 waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi, ambapo wagonjwa 37 walipatiwa kibali cha kwenda kutibiwa nje ya nchi.

*73. **Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum zimehudumia jumla ya wagonjwa 1,782,264. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 1,566,536 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 215,728 ikilingalinishwa na wagonjwa 1,686,395 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21 kama inavyoonesha katika kiambatisho Na.3. Aidha, kati ya wagonjwa 1,782,264 waliohudumiwa katika Hospitali hizo, wagonjwa 84,109 walikuwa ni wagonjwa wa msamaha, na walizigharimu Hospitali hizo za Rufaa za Taifa, Kanda na Maalum jumla ya shilingi 35,469,895,902.19 kama inavyoonesha katika **kiambatisho Na.4**.

**Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)**

*74.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) imehudumia jumla ya wagonjwa 367,213. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 328,938 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 38,275. Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 46,591 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi bilioni 14.1 katika kipindi hicho.

*75.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali imetoa **huduma ya upandikizaji figo (renal transplant)** kwa wagonjwa 6 ambapo gharama ya huduma hiyo ni shilingi milioni 30 kwa mgonjwa mmoja ambapo huduma hiyo hugharimu shilingi milioni 120 nchini India. **Wagonjwa waliopandikizwa figo tangu huduma hiyo ilipoanzishwa hapa nchini mwaka 2017, wamefikia wagonjwa 70**. Hivyo wagonjwa 70 waliopata huduma hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wangegharimu shilingi 8,400,000,000 iwapo wangepata huduma hiyo nchini India. Kwa kuanzisha huduma hii hapa nchini Serikali imeokoa jumla ya shilingi 6,300,000,000.

*76.* ***Mheshimiwa spika,*** Katika kipindi cha Julai 2021 mpaka Machi, 2022, Hospitali imetoa **huduma ya upandikizaji vifaa vya usikivu (cochlea implant)** kwa watoto 14 ambapo gharama ya huduma hiyo ni shilingi milioni 36 kwa mgonjwa mmoja ambapo huduma hiyo hugharimu shilingi milioni 100 nchini India. **Wagonjwa waliopandikizwa vifaa vya usikivu tangu huduma hiyo ilipoanzishwa hapa nchini mwaka 2017, wamefikia 49 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.764**. Hivyo watoto 49 waliopata huduma hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wangegharimu shilingi bilioni 4.9 Kwa kuanzisha huduma hii hapa nchini Serikali imeokoa jumla ya shilingi bilioni 3.136.

*77.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali ya Taifa Muhimbili imetoa huduma za Matibabu ya Radiolojia kwa njia ndogo (*Intervertional*

*Radiology*) kwa wagonjwa 1,692 na kufanya jumla ya wagonjwa waliopata huduma hii kufikia 2,343 tangu huduma hii ilipoanzishwa Novemba, 2018. Gharama ya kumpeleka mgonjwa mmoja nje ya nchi kwa huduma hii ni shilingi milioni 96 ambapo Hospitali ya Taifa Muhimbili inatoa huduma hiyo kwa gharama ya shilingi milioni 8 tu. Kwa wagonjwa 2,343 Hospitali imetumia shilingi bilioni 18.7, na endapo wangeenda nje Serikali ingetumia shilingi bilioni 224.9. Hivyo jumla ya shilingi bilioni 206.2 zimeweza kuokolewa.

**Hospitali ya Mloganzila**

*78.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Hospitali ya Mloganzila imehudumia jumla ya Wagonjwa 91,744 ukilinganisha na Wagonjwa 82,339 waliohudumiwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2020/21. Kati ya wagonjwa hao, Wagonjwa 82,804 walikuwa ni wa nje (OPD) na wagonjwa 8,940 walikuwa ni wa ndani (IPD). Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 2,928 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha Shilingi bilioni 1.9 katika kipindi hicho. Hali ya upatikanaji wa damu katika Hospitali imefikia wastani wa asilimia 94 ya mahitaji.

*79.* ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imefanikiwa kusimika **mtambo wa kuzalisha hewa tiba** *(Oxygen generating plant)* wenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 yenye ujazo wa 8.5 $M^3$ kwa siku, ambapo mitungi ya ziada takribani 100 itauzwa na hivyo kuongeza mapato ya ndani. Aidha, mtambo huu umegharimu Dola za Marekani 300,000. Vilevile, Hospitali imefanya ukarabati wa **wodi ya watoto wachanga mahututi *(Neonatal Intensive Care Unit -NICU)*** ambapo ukarabati huu umeongeza vitanda vya *NICU* kutoka vitanda 30 mwaka 2020 hadi hadi kufikia vitanda 60 kwa mwaka 2021. Pia, mradi huu unahusisha uanzishwaji wa Wodi ya Watoto wachanga, na wodi ya wajawazito mahututi (*Maternal ICU)* yenye uwezo wa vitanda 4 pamoja na wodi ya wajawazito wanaohitaji uangalizi maalum (*HDU)* yenye uwezo wa vitanda 6. Ukarabati huu umegharimu jumla shilingi milioni 168.2.

*80.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali ya Mloganzila kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili ilifanikiwa kutoa huduma ya **upandikizaji wa uloto *(bone marrow transplant)*** ambapo jumla ya wagonjwa 11 walifanyiwa upandikizaji huo. Huduma hii ni mara ya kwanza kufanyika nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Gharama za kumpeleka mgonjwa mmoja nje ya nchi ni **shilingi milioni 250** wakati katika Hospitali ya Mloganzila ni **shilingi milioni 70 tu**. Hivyo Hospitali imetumia **shillingi milioni 770** na kama wagonjwa hao wangeenda nje ya nchi, Serikali ingetumia **shillingi bilioni 2.75** na hiyo jumla ya **shilingi bilioni 1.98** zimeweza kuokolewa.

*81.* **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha utendaji wa hospitali ya Mloganzila ambayo ipo chini ya usimamizi wa hospitali ya Taifa Muhimbili naomba kuchukua fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa kuanzia tarehe 1 Julai 2022, hospitali hii itaanza kujiendesha yenyewe**.** Wizara inaendelea na uchambuzi wa huduma mahususi za ubingwa bobezi ambazo Hospitali hii itajikita katika kuzitoa kwa wananchi. Tunaamini kuwa hatua hii itaiwezesha Hospitali kutoa huduma bora na kwa haraka sambamba na kuipunguzia mzigo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

*82.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Machi, 2022 Taasisi ya Mifupa (MOI) iliendelea kutoa huduma ambapo jumla ya Wagonjwa 154,260 walihudumiwa. Kati yao, Wagonjwa wa nje (OPD) ni 147,847 na Wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni 6,413 ikilinganishwa na Wagonjwa 155,843 waliohudumiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021.

*83.* ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ilifanya upasuaji kwa Wagonjwa 5,098 ambapo upasuaji wa Mifupa mbalimbali Wagonjwa 1,765; upasuaji wa kubadilisha nyonga Wagonjwa 121; upasuaji wa goti Wagonjwa 90; upasuaji wa goti kwa

kutumia matundu Wagonjwa 131; upasuaji wa mfupa wa kiuno Wagonjwa 59; upasuaji wa uti wa mgongo Wagonjwa 142; upasuaji wa ubongo Wagonjwa 157; upasuaji wa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi Wagonjwa 288; upasuaji wa mfupa wa paja (femur) Wagonjwa 345; na upasuaji kwa wagonjwa wa dharura 1,793. Vilevile Taasisi imefanya upasuaji wa kunyoosha vibyongo (Scoliosis Surgery) kwa Watoto 22 na upasuaji wa kuondoa uvimbe ulio kwenye sakafu ya ubongo kupitia tundu la pua (transphenadial hypophysectomy) Wagonjwa 23, na upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye mshipa wa damu kwenye ubongo (Aneurysm clipping) ilikuwa Wagonjwa 162.

*84*. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Taasisi kwa kutumia maabara maalum ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu (Angio – Suite) imefanya upasuaji kwa kutumia maabara hii kwa wagonjwa 161. Aidha, kwa mara ya kwanza Taasisi imeweza kutoa matibabu ya kifafa (Epilepsy) kwa njia ya upasuaji.

*85.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi iliendelea kutoa huduma za Mkoba ikiwa ni pamoja na upasuaji wa mifupa kwa lengo la kusogeza huduma kwa Wananchi. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Madaktari Bingwa wa MOI wamewahudumia Wagonjwa 1,465 katika Hospitali ya Nyangao (Lindi); Hospitali ya Misheni Ndanda (Lindi) wamehudumiwa Wagonjwa 1,051; Hospitali ya Mkoa wa Geita wamehudumiwa Wagonjwa 315; Hospitali ya Arusha HDC wamehudumiwa Wagonjwa 60 na Hospitali ya Benjamini Mkapa (Dodoma) wamehudumiwa Wagonjwa 32.

**Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**

*86.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Taasisi ilihudumia jumla ya Wagonjwa 87,332 ikilinganishwa na Wagonjwa 75,716 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2020/21. Kati yao, Wagonjwa 84,045

walikuwa wa nje (OPD) na Wagonjwa wakulazwa (IPD) walikuwa 3,287. Miongoni mwa waliopata huduma ni pamoja na Wagonjwa 58 kutoka nchi za Visiwa vya Comoro, Zambia, DRC, Kenya, Botswana na Burundi. Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 2,135 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi milioni 814.8.

*87*. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeweza kufanya upasuaji wa moyo kwa Wagonjwa 439, kati ya wagonjwa waliofanyiwa upasuaji, Wagonjwa 311 walifanyiwa **upasuaji mkubwa wa kufungua kifua bila kusimamisha Moyo,** kati yao Watu wazima walikuwa 113 na Watoto walikuwa 198. Aidha, Wagonjwa wengine 128 ambao ni Watu wazima wenye matatizo ya mishipa ya damu walifanyiwa upasuaji kwa njia ya kisasa (Vascular surgery), upasuaji huu umefanywa na Wataalam wa ndani.
Aidha, jumla ya Wagonjwa 1,425 walipata **huduma za upasuaji wa Moyo kwa kutumia mtambo maalum (*Catheterization Laboratory)*** ikiwa ni ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na Wagonjwa 1,262 waliofanyiwa huduma hiyo kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/21, kati yao Watu wazima walikuwa 1,288 na Watoto 137.

**Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)**
*88*. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ilihudumia jumla ya wagonjwa 37,882 kati ya Wagonjwa hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 33,621 na Wagonjwa wa kulazwa walikuwa 4,261. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa katika kipindi hiki, wagonjwa 15,153 walipatiwa huduma za tiba mionzi, wagonjwa 9,849 walipatiwa huduma ya tiba kemia na wagonjwa 12,880 walipata tiba ya kemia na mionzi. Baada ya huduma za uchunguzi na tiba ya Saratani kuimarishwa, wagonjwa kutoka nje ya nchi wameendelea kufika katika Taasisi ambapo katika kipindi hicho wagonjwa wapya 59 walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya Saratani.

89. ***Mheshimiwa Spika***, aidha **huduma za uchunguzi wa Saratani** umeendelea kufanywa na Taasisi kwa njia ya Mkoba. Uchunguzi huo ulifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Lindi, Ruvuma, Dodoma, Arusha, na Mtwara. Katika kipindi hiki, jumla ya wanawake 9,219 walifanyiwa uchunguzi wa Saratani ya Matiti na Saratani ya mlango wa kizazi; kati yao wanawake 2,977 walifanyiwa uchunguzi katika Taasisi na wanawake 6,242 walifanyiwa uchunguzi kupitia huduma za Mkoba. Kati ya Wanawake waliofanyiwa uchunguzi wa Saratani ya Matiti na Saratani ya mlango wa kizazi, wanawake 364 walionekana kuwa na dalili za awali za Saratani na wanawake 26 waligundulika kuwa na Saratani. Pia, jumla ya wanaume 686 walifanyiwa uchunguzi wa Saratani ya tezi dume; kati yao wanaume 165 walifanyiwa uchunguzi katika Taasisi na wanaume 521 walifanyiwa uchunguzi kupitia huduma za Mkoba. Katika uchunguzi huo, wanaume 21 sawa na asilimia 3 waligundulika kuwa na Saratani ya tezi dume. Pia, uchunguzi wa Saratani ya ngozi (*kaposi sarcoma*) na utumbo mpana ulifanyika kwa watu 302 ambapo watu 33 sawa na asilimia 10 waligundulika kuwa na Saratani.

Katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata **elimu kuhusu ugonjwa wa Saratani**, Taasisi iliendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali zikiwepo vipindi 34 vya runinga, redio vipindi 51 na machapisho 46 ya magazeti kuhusu namna ya kujikinga na Saratani. Utoaji wa elimu kwa umma ulitekelezwa kwa asilimia 90 ya lengo. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kwa njia ya mitandao ya kijamii kupitia (@oceanroadcancerinstitute, @wizara_afya). Vilevile, jumla ya wanafunzi 262 kutoka shule za Sekondari walipatiwa elimu kuhusu Saratani.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Upatikanaji wa **dawa za Saratani** kwa Wagonjwa ilikuwa ni asilimia 99 ikilinganishwa na asilimia 98 mwaka 2020/21. Taasisi imeendelea kusimamia utoaji wa dawa za Saratani kwa mgonjwa kuchangia kadiri anavyomudu ambapo wagonjwa wasiomudu gharama

walipatiwa msamaha wa kupata dawa za tiba ya Saratani kupitia dawati la Afisa Ustawi wa Jamii ambapo jumla ya wagonjwa 2,792 walipatiwa misamaha mbalimbali ya gharama za uchunguzi wa Kimaabara, Radiolojia na tiba.

Huduma zilizotolewa kwa msamaha katika kipindi hicho zina thamani ya **shilingi bilioni 13.9** Taasisi iliendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa za saratani katika Duka la Dawa la Jamii. Upatikanaji wa dawa za Saratani katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 uliendelea kuwa asilimia 100 na imesaidia kuongeza mapato kwa Taasisi. Vilevile, bei ya dawa katika duka la dawa la Jamii la Taasisi ni nafuu kwa wastani wa asilimia 30 ikilinganishwa na bei ya dawa hizo katika maduka binafsi nje ya Taasisi.

*91.* ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na uboreshaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na Serikali katika eneo la matibabu na uchunguzi wa Kibingwa na ubingwa Bobezi kwa wagonjwa wa saratani, Rufaa za matibabu nje ya nchi zimepungua. Kutokana na maboresho hayo, Taasisi ilitoa rufaa ya matibabu nje ya nchi kwa mgonjwa mmoja (1) tu katika kipindi cha miaka miwili mfululizo.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ilitoa tiba Shufaa (palliative care) kwa jumla ya wagonjwa 25,224 na wagonjwa 2,013 walipatiwa *oral morphine* kwa ajili ya kupunguza maumivu. Pia huduma za Maabara zimezidi kuimarika ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, jumla ya vipimo vya Maabara 148,676 vilifanyika, ambapo kati yake, vipimo 147,339 vilikuwa vipimo vya kawaida na vipimo 1,337 ni vya patholojia. Vipimo mahsusi vya Saratani vya *histopathology, cytology, Immunoassay (tumor markers), haematology, clinical chemistry, immunology, parasitology, na blood transfusion* vinafanyika na kusaidia kutoa tiba mahsusi kwa wagonjwa wa Saratani.

*93.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha taarifa hii, Taasisi ilitoa jumla ya tiba mionzi 168,255 kwa wagonjwa kwa kutumia

mashine 5 za mionzi ya nje (2 za *Cobalt-60*, 1 ya *Caesium* na 2 za LINAC) na mashine 2 mionzi ya ndani *(brachytherapy)*. Taasisi ilifanikiwa kutoa jumla ya vipimo 18,633 vya radiolojia, kati ya vipimo hivyo, vipimo 7,192 ni vya *X-ray*, 7,535 vya *ultrasound*, 3,759 vya *CT Scan* na 147 vya *mammograph* ikiwa ni sawa na asilimia 105 ya lengo.

*94.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi iliendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba za dawa nyuklia ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, jumla ya wagonjwa 1,082 walipatiwa huduma sawa na asilimia 95 ya lengo. Wagonjwa 369 walifanyiwa uchunguzi *(diagnostic scans)* katika Mifupa, Figo, Ubongo, na Tezi ya shingoni na wagonjwa 36 walipatiwa tiba ya nyuklia. Aidha, Maabara ya Taasisi ilifanyiwa tathmini kwa ajili ya ithibati ya Kimataifa *(International accreditation)* na kupewa ithibati katika vipimo vya aina tano. Cheti cha ithibati cha ubora kimetolewa kutoka Shirika la Viwango la Ukaguzi la Kimataifa SADCAS na hivyo Maabara ya Taasisi imeingizwa katika orodha ya maabara bora inayotoa huduma za vipimo Duniani.

*95.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa mafunzo kwa Wanafunzi 67 wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi (Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology), wanafunzi 34 wa Shahada ya Uzamili ya Onkolojia (Masters of Medicine in Clinical Oncology) na wanafunzi 10 wa Shahada ya Uzamili ya Uuguzi katika Onkolojia (Masters of Science in Nursing Oncology). Mafunzo haya yameongeza uwepo wa Wataalamu wa huduma za Saratani hapa nchini; kwa sasa Taasisi ina Madaktari Bingwa 37.

*96.* ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi iliendelea kutekeleza mradi wa kusimika mashine ya *PET/CT Scan* ambapo unahusisha ujenzi wa *Bunkers* na ununuzi na usimikaji wa mashine za PET/CT Scan na Cyclotron, kwa gharama ya shilingi bilioni 18.2. Ujenzi

wa jengo ulianza Mei, 2021, na unategemewa kukamilika Juni, 2022 ambapo hadi sasa umefikia asilimia 80 ya utekelezaji.

**Hospitali ya Benjamin Mkapa**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali ya Benjamin Mkapa imeendelea kutoa huduma ambapo jumla ya Wagonjwa 168,479 walihudhuria na kupata matibabu, ikilinganishwa na Wagonjwa 126,196 waliopata huduma kwa kipindi kama hiki mwaka 2020/21. Kati ya hao, Wagonjwa 160,942 walikuwa wa nje (OPD) na wagonjwa waliolazwa (IPD) Walikuwa 7,537. Wagonjwa wanaopatiwa huduma katika Hospitali wameendelea kuongezeka sawa na ongezeko la asilimia 34 ikilinganishwa na mwaka 2020/21.

Ongezeko hilo limetokana na uboreshwaji wa huduma zinazotolewa kutokana na uwepo wa vifaa vya kisasa na wataalam wenye ujuzi. Aidha, wagonjwa wa msamaha walikuwa 2,228 ambao waligharimu Hospitali kiasi cha shilingi milioni 281 katika kipindi hicho.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Jumla ya **vipimo vya moyo** 9,270 vimefanyika kwa kipindi cha mwaka 2021/22, ikilinganisha na vipimo 7,104 vilivyofanyika kipindi kama hiki mwaka 2020/21 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31. Vilevile Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2022, jumla ya wagonjwa 4,872 walipata **huduma ya upasuaji**, ikilinganishwa na wagonjwa 3,188 waliopewa huduma hiyo kwa kipindi kama hicho mwaka 2020/21, ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 53. Wagonjwa waliofanyiwa **huduma za upasuaji kwa kutumia matundu madogo** walikuwa 846 ikilinganishwa na 509 waliofanyiwa kipindi kama hiki mwaka 2021 ambalo ni ongezeko la asilimia 66.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2022, jumla ya Wagonjwa nane (8) walipata **huduma ya**

**Upandikizwaji wa Figo** na kufikisha jumla ya wagonjwa 29 waliopata huduma hii toka Hospitali ilipoanza kutoa huduma za kupandikiza figo mwezi Machi, 2018. Gharama ya upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa ni kati ya Shilingi milioni 27 hadi Milioni 35 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na Shilingi milioni 75 hadi Milioni 100 mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Upatikanaji wa huduma hizo hapa nchini kumeiwezesha Serikali kuokoa jumla ya Shilingi bilioni 2.1

**Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

*100.* ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ilihudumia jumla ya wagonjwa 28,325 kati yao 26,761 ni wagonjwa wa akili wa nje (OPD) na wagonjwa wa akili wa ndani (IPD) 1,564. Aidha, wagonjwa wa msamaha waliopewa huduma walikuwa 3,985 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 60,217,746 katika kipindi hicho. Jumla ya Wagonjwa 123, walipata huduma za kibingwa za Saikolojia na wagonjwa 443 wa Neuro-psychiatry na wagonjwa wapatao 123 walifanyiwa uchunguzi na kuandikiwa taarifa za Kisheria. Vilevile, katika kliniki ya afya ya akili kwa Watoto na vijana wagonjwa 1,121 walihudumiwa. Taasisi pia, ilipokea wagonjwa wapya 225 wenye matatizo ya utumiaji wa madawa ya kulevya na hivyo kufanya jumla ya waraibu wanaohudumiwa na kituo cha Itega kufikia 548 toka kilipoanza kutoa huduma mwaka 2020.

**Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto**

*101.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Hospitali ilihudumia jumla ya Wagonjwa 26,884 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 13,953 na wagonjwa waliolazwa walikuwa 636 na wagonjwa waliohudumiwa katika Jamii (community outreach) walikuwa 12,295. Kati ya Wagonjwa waliolazwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu walikuwa 104. Aidha, Wagonjwa wa kifua kikuu sugu

waliomaliza matibabu ni asilimia 75 na kati yao asilimia 70 walithibitishwa kupona kifua kikuu sugu.

*102.* ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeweza kufanya ubainishaji wa vinasaba vya UVIKO-19 katika sampuli 69 ambapo sampuli 29 ziliweza kuleta majibu kati ya sampuli hizo zilizoleta majibu, sampuli 19 zilikuwa na vinasaba vya delta and Beta. Hospitali imeendelea pia kutoa huduma kwa wagonjwa wa msamaha, ambapo jumla yao walikuwa 497 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha Shilingi 114,541,967 katika kipindi hicho.

**Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**

*103.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Hospitali imehudumia jumla ya Wagonjwa 237,186, ikilinganishwa na Wagonjwa 330,947 waliopatiwa huduma mwaka 2020/21. Kati yao, Wagonjwa 205,329 walikuwa wa nje na Wagonjwa 31,857 walilazwa. Hospitali imeendelea pia kutoa huduma kwa Wagonjwa wa msamaha, ambapo jumla ya Wagonjwa 18,547 walihudumiwa na waliigharimu Hospitali kiasi cha Shilingi 185,478,000 katika kipindi hicho. Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuendelea kuongeza Wataalam wa kada mbalimbali. Hadi kufikia Machi 2022 huduma zilizoongezeka ni za upasuaji wa mishipa ya fahamu na ubongo. Huduma ya tiba ya Saratani imeendelea kutolewa ambapo Hospitali imehudumia jumla ya Wagonjwa 820 waliopata matibabu ya Saratani kwa kutumia dawa (chemotherapy) na upasuaji.

*104.* ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ambapo jengo la huduma za daraja la kwanza lilikarabatiwa na kuongeza vitanda 50, na kufanya Hospitali kuwa na jumla ya vitanda 603. Aidha, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi bilioni 9.2 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) la kutolea huduma za afya ya uzazi na Mtoto lililopo eneo la Meta. Jengo hili linajengwa kwa utaratibu wa "Force Account" na ujenzi umefikia asilimia 95.

Kukamilika kwa jengo hili kutaongeza vitanda 220 na kufikia jumla ya vitanda 823.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando**

*105.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Hospitali ilihudumia jumla ya Wagonjwa 291,837 ikilinganishwa na Wagonjwa 311,610 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 269,019 na Wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 22,818. Aidha, Hospitali imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa msamaha, ambapo Wagonjwa 548 walihudumiwa na waliigharimu Hospitali kiasi cha Shilingi 308,651,412. Vilevile, Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuanza kutoa uchunguzi wa Saratani ya matiti baada ya kununua mashine iitwayo *mammogram* kwa Shilingi million 800.

Taasisi ilihudumia jumla ya Wagonjwa 9,542 wa matibabu ya Saratani ikilinganishwa na Wagonjwa 12,320 waliopata huduma hiyo mwaka 2020/21. Kati yao, Wagonjwa 2,765 walipatiwa tiba ya Saratani kwa kutumia dawa (Chemotherapy) na Wagonjwa 598 walipatiwa tiba ya mionzi (Radiotherapy). Upatikanaji wa huduma hii umepunguza Rufaa za Wagonjwa wa Saratani wa Kanda ya Ziwa kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)**

*106.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Hospitali ya KCMC ilipokea jumla ya Wagonjwa 297,810. Kati yao Wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 208,467 na Wagonjwa wa ndani (IPD) ni 89,343, ambapo asilimia 87 ya wagonjwa wote wanatoka katika Mikoa iliyopo ndani ya maeneo yanayohudumiwa na Hospitali kwa Kanda ya Kaskazini.

*107.* ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali pia imeendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa kununua na

kufunga mitambo mipya ya *MRI, CT na Digital X- ray*. Maboresho hayo yamewezesha wagonjwa kuendelea kufanyiwa kipimo cha MRI Wagonjwa 735, vipimo vya *CT Scan* wagonjwa *5,678*, vipimo vya *Ultrasound* Wagonjwa 6,213 na Wagonjwa 9,873 vipimo vya *X-ray*. Huduma za upasuaji zimefanyika kwa Wagonjwa 4,674.

*108*. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali pia imeendelea kutoa huduma katika idara ya Saratani, ambapo katika kipindi tajwa jumla ya wagonjwa 6,806 wa Saratani, kati yao Wagonjwa 4,878 walikuwa ni Watu wazima na Wagonjwa 1,928 walikuwa ni watoto. Hospitali kupitia idara ya Urolojia iliweza kufanya upasuaji kwa Wagonjwa 761 waliokuwa na changamoto mbalimbali katika njia ya Mikojo, kati yao Wanaume walikuwa 695 na wanawake ni 66. Idara ya ngozi, imeendelea kutoa huduma za matibabu na upasuaji, ambapo katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Machi 2022 jumla ya Wagonjwa 11,893 walifikiwa. Hospitali pia imeendelea kutoa huduma za Mkoba (outreach services) katika maeneo mbalimbali nje ya Hospitali ambapo katika kipindi tajwa jumla ya Wagonjwa 5,254 wamepatiwa huduma mbalimbali.

*109*. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuadhimisha miaka 50 ya Hospitali ya KCMC tangu kuanzishwa kwake mwaka 1971, Hospitali ilitoa huduma ya upimaji kwa Wananchi bure, ambapo jumla ya Watu 1,930 walipimwa magonjwa mbalimbali ikiwemo utoaji wa chanjo ya UVIKO - 19. Hospitali pia imetoa huduma ya macho ambapo jumla ya wagonjwa 17,281 kati yao wagonjwa wapya walikuwa ni 15,989 na Wagonjwa wakujirudia ni 1,292. Katika kipindi tajwa Hospitali imetoa msamaha kwa wagonjwa 703 ambapo jumla ya Shilingi bilioni 3.5 zimetumika, kati ya hizo Shilingi bilioni 2.9 zimetumika kwa Wagonjwa wa Saratani.

*110.* ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za kibingwa ambapo, ujenzi wa wodi maalumu ya wagonjwa wa Saratani imekamilika kwa asilimia 100 na inaendelea kutoa huduma. Katika kipindi tajwa Hospitali pia inaendelea na ujenzi wa jengo la mionzi (Bunker) ambapo jumla ya gharama ya ujenzi ni Shilingi Bilioni 4.7, kati ya hizo Shilingi Bilioni 2 zimetolewa. Mradi huu umetekelezwa kwa asilimia 48. Hospitali pia imeendelea na ujenzi wa mabweni ya kulala Wagonjwa wa Saratani na ndugu wa Wagonjwa ambao watakuwa wanatokea maeneo ya nje ya Mkoa wa Kilimanjaro, malazi yatakuwa kwa gharama nafuu sana, ujenzi huu umefikia asilimia 52 na unategemewa kugharimu Shilingi bilioni 2 hadi kukamilika kwake.

*111.* ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali inaendelea kutoa huduma ya uzalishaji wa hewa ya Oksijeni kupitia kinu chake chenye uwezo wa kuzalisha mitungi 400 kwa siku hivyo kuokoa zaidi ya shilingi 150,000,000 kwa mwezi. Upatikanaji wa hewa hii katika hospitali umekuwa msaada mkubwa hasa kipindi cha mfumuko wa UVIKO- 19 na hivyo kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 3.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato**

*112.* ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato ilianza kutoa huduma Julai, 2021 ambapo hadi kufikia Machi 2022, Hospitali imeweza kuhudumia jumla ya wagonjwa 5,607 ambapo Wagonjwa wa nje *(OPD)* walikuwa 4,810 na wagonjwa wa ndani *(IPD)* walikuwa 797. Huduma za kibingwa zilizoanza kutolewa ni pamoja na upasuaji kwa Wanawake *(obstretics & Gyanocology)* kama vile *Hysterectomy intravaginal & Abdominal, Laparatomy, VVF Repair, Colporhaphy Anterior & posterior, Vulvectomy + Biopsy taking*.

*113.* ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya utoaji huduma ambapo kwa

kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Machi 2022, Hospitali imeendelea na ujenzi wa majengo 6 na nyumba 20 za Watumishi, ambayo yanajengwa kwa awamu. Katika Awamu ya kwanza ilihusu Ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa nje (OPD), jengo la Famasi na uchunguzi (Maabara), Jengo la huduma za dharura (EMD) na Jengo la Wagonjwa wanaohitaji Uangalizi maalumu (ICU) na utekelezaji wake umefikia asilimia 98. Ujenzi wa awamu ya pili unahusisha Majengo yafuatayo, Wodi yenye ghorofa mbili (2) na likikamilika litakuwa na uwezo wa kuwa na vitanda 201 ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 45, jengo la Mionzi limefikia asilimia 95, kazi za nyongeza za ujenzi wa Jengo la kuhifadhia maiti *(Mortuary),* jengo la kutakasisha vifaa *(CSSD)* na jengo la kufulia nguo.

*114*. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuboresha huduma, Hospitali imeanzisha utengenezaji wa mifuko ya kuwekea taka mbalimbali *(Bin liners)* na kuuza kwa vituo vya kutoa huduma za afya vya karibu, pia Hospitali imeshaanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa dharura (EMD). Aidha, hospitali ipo katika taratibu za kuanzisha Kitengo cha kuchanganya Dawa (*compounding* na *infusion unit)*, kuanzisha huduma ya kitengo cha ICU, kitengo cha Mionzi ambapo kutakuwa na huduma ya CT Scan na MRI, na kuanzisha Huduma ya kuchuja Damu kwa Wagonjwa ambao Figo zao zimeshindwa kufanya kazi *(Dialysis)*.

**Hospitali za Rufaa za Mikoa**

*115*. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zilihudumia jumla ya wagonjwa 2,636,890 ikilinganishwa na wagonjwa 2,814,390 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa katika kipindi cha 2021/22 wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 2,415,431 na wagonjwa waliolazwa (IPD) walikuwa 221,459. Mchanganuo wa wagonjwa waliohudumiwa upo katika **kiambatisho Na.5**. Aidha, kati ya wagonjwa hao waliohudumiwa katika Hospitali

za Rufaa za Mikoa, jumla ya wagonjwa 145,797 walikuwa ni wagonjwa wa msamaha, na walizigharimu Hospital hizo jumla ya shilingi 3,473,134,105 ikilinganishwa na Wagonjwa 353,139 wa msamaha mwaka 2020/21 waliozigharimu Hospitali hizo kiasi cha shilingi 4,286,784,135 kama ilivyofafanuliwa katika **kiambatisho Na.6**

*116.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa **Huduma za Kujifungua** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya akinamama 65,616 walijifungua katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ukilinganisha na akinamama 77,563 waliojifungua mwaka 2020/21 kama inavyoonekana katika **kiambatisho Na.7.** Aidha, katika kipindi hicho vilitokea vifo 231 vinavyohusiana na uzazi ukilinganisha na vifo 272 vilivyoredokiwa mwaka 2020/21. Kupungua kwa idadi hii ni kutokana na jitihada za Serikali za kuboresha Vituo vya Afya katika Halmashauri mbalimbali nchini, ambavyo vimewezeshwa kutoa huduma bora za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC).

*117.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa katika ngazi ya mikoa ambapo huduma mbalimbali za kibingwa zimeendelea kutolewa ikiwemo **huduma ya usafishaji wa damu (dialysis)** kwa wagonjwa wenye magonjwa ya figo. Jumla ya wagonjwa 62 wameendelea kupata huduma za kusafisha damu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 7 ambazo ni Bombo (Tanga), Bukoba (Kagera), Mount Meru (Arusha), Ligula (Mtwara), Maweni (Kigoma), Musoma (Mara) na Sekou-Toure (Mwanza). Wagonjwa hawa wanapata huduma za kusafisha damu mara tatu kwa wiki. Aidha, Serikali inaendelea kuzijengea uwezo hospitali zote za rufaa za Mikoa ziweze kutoa huduma za kusafisha damu.

*118.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa kwenye mazingira ya karibu na wananchi, ambapo katika kipindi cha Julai 2021 hadi

Machi, 2022 Hospitali za Rufaa za Mikoa 18 zilitoa **huduma za mkoba (outreach services)** katika fani za ubingwa zifuatazo; magonjwa ya macho, magonjwa ya watoto, dawa za usingizi, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ndani, upasuaji wa kawaida, afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, magonjwa ya sikio, pua na koo, afya ya akili, radiolojia, afya ya kinywa na meno, magonjwa ya damu, magonjwa ya ngozi na huduma za tiba kwa mazoezi (physiotherapy). Katika kliniki hizo, jumla ya wagonjwa 23,976 walihudumiwa, kati yao 2,934 walifanyiwa upasuaji.

**HUDUMA ZA DHARURA NA MAAFA**

*119.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za dharura na kutekeleza afua mbalimbali za kukabiliana na maafa yanayotokea nchini ambayo huathiri afya za Wananchi. Katika kipindi cha taarifa hii nchi yetu imeendelea kukabiliana na janga la ugonjwa wa UVIKO-19 ambalo limeathiri nchi nyingi Duniani. Katika kukabiliana na janga hilo, Wizara imetekeleza afua zifuatazo;

i. Kuratibu kuanzishwa kwa vituo vinne (4) vya Operesheni ya matukio ya dharura (PHEOCs) na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa vituo hivyo katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza na Dar es Salaam. Aidha, kwa sasa Wizara inaratibu maandalizi ya uanzishaji wa vituo vitano (5) vya Operesheni ya matukio ya Dharura katika mikoa ya Songwe, Dodoma, Katavi, Mtwara na Iringa ili kuimarisha ufanisi wa kukabiliana na dharura katika Mikoa hiyo.

ii. Kuratibu utekekelezaji wa ununuzi na ufuatiliaji wa usimikaji wa Mitambo saba (7) ya kuzalisha na kujaza hewa tiba ya oksijeni chini ya fedha za Benki ya Dunia. Mitambo hiyo imesimikwa katika Hospitali za rufaa za Mikoa ya Amana (DSM), Ligula (Mtwara), Mbeya, Dodoma, Geita, Manyara na Songea (Ruvuma). Mitambo mingine 12 imeshanunuliwa na Serikali na inaendelea kufungwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

ya Sekou Toure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Katavi, Songwe, Sokoine (Lindi), Morogoro, Njombe, Simiyu, Musoma (Mara), Kitete (Tabora), Sumbawanga (Rukwa) na Shinyanga. Lengo la Wizara ni kuhakikisha hospitali zote za Rufaa za Mikoa, Taifa, Maalumu, Kanda na baadhi ya Hospitali za Wilaya zinakuwa na mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni ili kuondoa changamoto ya uhaba wa hewa tiba hiyo na kuimarisha huduma za Dharura na Maafa, ambapo jumla ya Mitambo 55 inatarajiwa kununuliwa na kusimikwa ifikapo Desemba, 2022 na,

iii. Kuratibu utekelezaji wa mradi wa mwendelezo wa huduma za msingi wakati wa dharura na majanga "*Continued Essential Health services*" unaotekelezwa kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI pamoja na Shirika la Amref katika Mikoa 11 ya Dar es salaam, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Mwanza, Iringa, Njombe, Songwe na Mbeya. Zaidi ya Watumishi wa afya 8,600 wamepata mafunzo ya tiba na kuzuia maambukizo ya ugonjwa wa UVIKO-19, Nakala 6000 za Miongozo ya Matibabu imesambazwa kwenye Vituo vya kutolea huduma za afya na Vituo 8 vimefanyiwa ukarabati wa majengo ya *triage* na kuwekewa vifaa. Vituo hivyo ni; Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa, Kituo cha Afya cha Magugu (Manyara), Hospitali ya Mji ya Mafinga (Iringa), Hospitali ya Mji ya Kibena (Njombe), Hospitali ya Wilaya ya Makete (Njombe), Kituo cha Afya cha Ruanda (Mbeya) na Kituo cha Afya cha Tunduma (Songwe).

**UDHIBITI WA UBORA WA HUDUMA ZA TIBA**

*120.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha ubora wa huduma za Afya katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini, Wizara ilifanya uhakiki wa ubora wa huduma za matibabu (Clinical Audit) katika Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa. Lengo

ilikuwa ni kupata hali halisi (baseline) ya ubora wa huduma kwa kulinganisha na kiwango cha ubora cha utoaji wa huduma za Afya. Uhakiki huu ulionyesha wastani wa utoaji wa huduma bora ni sawa na asilimia 45 ambayo ni chini ya kiwango cha ubora kinachotakiwa. Wizara imeweka mikakati ya kuboresha maeneo yote yenye mapungufu na kuendelea kufanya uhakiki katika vituo vyote vya huduma. Sambamba na ubora wa huduma kwa ujumla, ubora wa huduma za Maabara umeendelea kuimarika ambapo jumla ya Maabara 48 zimepata ithibati ya Kimataifa na Maabara zingine 47 zipo katika hatua mbalimbali za mchakato wa kupata ithibati ya Kimatifa katika utoaji wa huduma bora za Maabara.

*121.* ***Mheshimiwa Spika,*** Tathmini ya kutoa nyota (Star Rating Assessment) kwenye Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ya Msingi imefanyika kwenye Mikoa mitano (5) ya Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Singida na Songwe. Tathmini hiyo ilifanyika Novemba 2021 na imeonesha kuwa ubora wa huduma kwenye Mikoa hiyo unaendelea kuimarika ambapo vituo ambavyo vimepata nyota 0 viko chini ya asilimia 4 (isipokuwa kwa mkoa wa Njombe ambapo ni asilimia 8). Mkoa wa Kilimanjaro umefanya vizuri ukilinganisha na Mikoa mingine minne ambapo kwa Kilimanjaro Vituo vilivyopata nyota 3 au zaidi ni asilimia 27. Aidha, tathmini inaendelea kwenye Mikoa mingine mitano ya Katavi, Kigoma, Mara, Njombe na Rukwa.

*122.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usalama wa wagonjwa na watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kukinga na kudhibiti Maambukizo (Infection Prevention and Control). Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022, tathmini na mafunzo maalumu (mentorship) yalifanyika katika Hospitali 37 za rufaa, ikijumuisha Hospitali za Rufaa za Mikoa 28, Hospitali 4 za Rufaa za Kanda na Hospitali Maalum tano (5).

**RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

*123.* ***Mheshimiwa Spika,*** uwepo wa watoa huduma za Afya ni moja ya nguzo muhimu inayohitajika kwa ajili ya kuwa na mfumo imara na fanisi kwa ajili ya utoaji wa huduma za Afya. Upatikanaji wa Rasilimali watu katika Sekta ya Afya upo katika kiwango cha asilimia 47 ya mahitaji yote na hivyo kuwepo kwa upungufu kwa kiwango cha asilimia 53. Moja ya sababu inayosababisha kuwepo na upungufu wa Watumishi ni pamoja na kasi kubwa ya ongezeko la vituo vya kutolea huduma za Afya ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa uchumi isiyoruhusu kuajiriwa kwa Watumishi wanaokidhi mahitaji halisi.

*124.* ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto zinazoikabili Sekta ya Afya kutokana na **upungufu wa rasilimaliwatu**, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kupunguza pengo kati ya upatikanaji wa Watumishi ikilinganishwa na mahitaji halisi. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kibali cha ajira mpya kwa wataalam wa afya ambapo kwa mwaka 2022/23 jumla ya nafasi za ajira 10,285 zimetengwa. Hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na: kuandaliwa kwa mwongozo utakaotumika na vituo vya kutolea huduma za Afya kutoa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani; kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika Sekta ya Afya kwa kuwashawishi kutumia sehemu ya rasilimali fedha zinazotumika katika kutekeleza program mbalimbali kugharamia ajira za muda mfupi kwa wataalam wa afya; na kuendelea kufanya upembuzi wa uzito wa majukumu katika kila kituo cha kutoa huduma za afya dhidi ya idadi ya watumishi kwa kila kituo na hatimaye kuwa na uwiano sahihi katika ngazi zote za utoaji huduma za afya.

*125.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha **uzalishaji wa wataalam wa afya** wenye ujuzi na weledi unaotakiwa, Wizara imeendelea kuratibu uendeshaji wa Vyuo 44 vya Kada za

Afya ngazi ya Kati pamoja na kushirikiana na Taasisi zinazosimamia uzalishaji wa wataalam katika ngazi ya vyuo vikuu. Aidha katika kusimamia uendeshaji wa Vyuo ngazi ya Kati, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 37,941 sawa na asilimia 62 ya wanafunzi 61,276 waliotuma maombi kujiunga na vyuo vya Afya ngazi ya kati katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022. Kati yao wanafunzi 4,768 sawa na asilimia 12.6 walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali vya afya na wanafunzi 33,173 sawa na asilimia 87 walichaguliwa kwenye vyuo binafsi na taasisi za dini katika program za Uuguzi na Ukunga na Sayansi Shirikishi za Afya.

*126.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi katika Sekta ya Afya, ili kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo imefanikiwa kutoa fursa za mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika nyanja mbalimbali za ubingwa na ubobezi, ambapo jumla ya watumishi 783 wameendelea kulipiwa gharama za masomo ya uzamili (postgraduate studies) katika vyuo vikuu vya ndani watumishi 756 na nje ya nchi watumishi 27. Katika kipindi hicho, jumla ya wataalam bingwa 124 walihitimu mafunzo ya shahada ya uzamili kwa ufadhili wa Serikali ikilinganishwa na wataalam bingwa 137 ambao walihitimu mafunzo hayo mwaka 2020/21.

## UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA

*127.* ***Mheshimiwa Spika***, Upatikanaji na utoaji wa huduma za Afya nchini umeendelea kugharamiwa na fedha za ndani pamoja na wadau wa maendeleo wanaochangia katika Sekta ya Afya. Mwenendo wa ugharamiaji wa huduma katika Wizara umeonesha kuwepo kwa ongezeko la fedha za ndani kutoka shilingi 406,122,271,000.00 mwaka 2015/16 hadi shilingi 909,003,059,000.00 mwaka 2021/22 ambapo fedha za nje zimeendelea kupungua kutoka shilingi 374,618,452,000.00

mwaka 2015/16 hadi shilingi 125,130,236,000.00 mwaka 2021/22. Ni dhahiri kuwa mwenendo huo unaonyesha kutekeleza kwa vitendo dhamira ya Serikali inayolenga katika kugharamia afya za wananchi kwa kutumia vyanzo vya ndani.

*128.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007, wananchi wote wenye uwezo wa kiuchumi hutakiwa kuchangia gharama za huduma za afya pindi wanapozihitaji. Utaratibu wa uchangiaji unaotumika hivi sasa ni kwa kutoa fedha taslimu papo kwa papo au kulipa kabla ya kuugua na kupatiwa kadi ya bima ya afya ambayo hutumika pindi muhusika anapohitaji huduma za afya. Hata hivyo uzoefu umeonesha kuwa wananchi wanaotumia utaratibu wa malipo ya papo kwa papo wapo katika hatari ya kutopata huduma pindi wanapohitaji na wakiwa hawana fedha za kuchangia. Hadi Desemba 2021 jumla ya watanzania 9,094,624 sawa na asilimia 15 ya Watanzania wote ndiyo wanaonufaika na mfumo wa bima ya afya ambapo asilimia 85 wapo nje ya mfumo wa Bima ya Afya. Katika kutatua changamoto ya Watanzania wengi kuwa nje ya mfumo wa bima ya afya, Wizara inaendelea na maandalizi ya Muswada wenye lengo la kutunga sheria itakayowataka watanzania wote kujiunga na Bima ya Afya na hivyo kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya pindi wanapozihitaji bila ya kikwazo cha fedha.

**MIRADI YA MAENDELEO**

*129.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo mbambali nchini. Jumla ya Miradi 22 ilikuwa inasimamiwa na Wizara katika maeneo mbalimbali hadi kufikia Machi, 2022. Miradi mitatu (3) imekamilika, miradi 12 inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2022 na miradi saba (7) itakamilika ifikapo Desemba, 2022. Kwa upande wa Miradi inayogharamiwa na fedha za UVIKO-19 yote inatarajiwa kukamilika kati ya Mwezi Mei na Juni, 2022. Kwa Wastani

utekelezaji wa miradi yote ya uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya imefikia wastani wa asilimia 75. Taarifa ya kina ya utekelezaji wa miradi hiyo imeambatishwa katika taarifa hii **(kiambatisho Na. 8)**

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

### Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

*130.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2022, Mfuko Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa na lengo la **kusajili wanachama** wapya 489,058. Mfuko ulifanikiwa kusajili wanachama wapya 453,294 sawa na asilimia 93 ya lengo ikilinganishwa na wanachama 418,972 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2021. Idadi hiyo ya wanachama waliosajiliwa, imewezesha Mfuko kuwa na wanachama wachangiaji 1,548,958 na wanufaika 4,826,978 sawa na asilimia 8 ya Watanzania wote hadi kufikia Machi, 2022. Serikali inaendelea na juhudi za kutoa elimu ya dhana ya bima ya afya na umuhimu wa kujiunga na bima ya afya kabla ya kuugua, ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini (NHIF na CHF) ili kuwawezesha Wananchi wengi kuwa na bima ya afya.

*131.* ***Mheshimiwa Spika***, Vyanzo vikuu vya mapato ya Mfuko ni pamoja na michango ya wanachama, mapato yatokanayo na uwekezaji na mapato mengineyo. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2022, Mfuko ulikuwa na lengo la **kukusanya fedha zitokanazo na michango** ya wanachama shilingi bilioni 419.12. Mfuko ulifanikiwa kukusanya fedha za michango shilingi bilioni 356.75 sawa na asilimia 85 ya lengo.

*132.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha uboreshaji wa huduma za matibabu nchini, mfuko unatoa **mikopo nafuu** ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo. Tangu kuanzishwa kwa mpango huu, jumla ya vituo 367 vimefaidika na utaratibu huu ambapo kiasi cha shilingi bilioni 35.33 zilitolewa kwa vituo

vilivyokidhi vigezo. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2022, shilingi bilioni 1.8 zilitolewa kwa vituo 21 vilivyokidhi vigezo. Utaratibu huu umesaidia kujenga uwezo wa vituo katika kutoa huduma za afya kwa wanachama na wananchi kwa ujumla. Mfuko unaendelea kuwahamasisha watoa huduma kutumia fursa hii ya mikopo katika kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wananchi. Aidha, majadiliano baina ya Mfuko na Bohari ya Dawa (MSD) yamefanyika kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini ambapo Mfuko utakuwa na jukumu la kutoa fedha za mikopo kwa vituo vya matibabu vitakavyoomba na MSD itakuwa na jukumu la kutoa vifaa tiba.

*133.* ***Mheshimiwa Spika*** Mfuko umeendelea kuongeza mtandao zaidi wa vituo vya kutolea huduma za afya ambapo hadi Machi 2022, ulikuwa umesajili vituo 9,025 vya matibabu vya ngazi na umiliki wa watoa huduma mbalimbali mijini na vijijini ili kutoa huduma za matibabu kwa wanachama na wanufaika wa huduma zake nchi nzima ikilinganishwa na vituo 8,482 mwaka 2021. Kati ya vituo hivi, vituo vya Serikali ni 6,361 sawa na asilimia 71, vituo vya Mashirika ya Dini ni 854 sawa na asilimia 9, na vituo vya watu binafsi ni 1,810 sawa na asilimia 20.

*134.* ***Mheshimiwa Spika***, maeneo makubwa ya matumizi ya Mfuko ni malipo ya madai kwa watoa huduma na gharama za uendeshaji wa shughuli za Mfuko na Maendeleo. Mfuko umeendelea kutoa mchango katika **uchangiaji wa gharama za matibabu katika Sekta ya afya** ambapo kwa mwaka 2020/21 shilingi bilioni 540.55 zililipwa kwa watoa huduma. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2022, jumla ya Shilingi bilioni 371.03 zililipwa kwa vituo vya kutolea huduma ikilinganishwa na shilingi bilioni 365.68 zilizolipwa mwaka 2021. Takwimu zinaonesha kuwa, fedha za NHIF kwa sasa zinachangia wastani wa asilimia 80 ya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi husika, Mfuko umelipa madai kwa wastani wa siku 57 ambazo ni ndani ya

matakwa ya Sheria, lengo ni kufikia wastani wa siku Mfuko umeanzisha mfumo wa uwasilishaji na uchakataji wa madai kwa njia ya Kielekitroniki kwa lengo la kuhakikisha madai ya watoa huduma yanalipwa kwa wakati. Hadi Machi 2022, jumla ya watoa huduma 81 kati ya 9,025 waliosajiliwa na Mfuko walikuwa wamejiunga katika mfumo huu.

*135.* ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko unaendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara katika vituo vya kutolea huduma kwa lengo la kusimamia ubora wa huduma na kutoa elimu ya miongozo mbalimbali ya tiba inayotolewa na Serikali. Vilevile, ili kuhakikisha Mfuko unakuwa endelevu, utaendelea kufuata mapendekezo yanayotolewa na taarifa ya Tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko (actuarial valuation).

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

*136.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka ilifanya tathmini ya maombi 714 ya **usajili wa dawa za binadamu** kati ya 868 sawa na asilimia 82 ya yaliyokuwepo katika kipindi husika. Maombi 421 kati ya maombi yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa na hivyo kusajiliwa. Aidha, maombi 293 ambayo hayakukidhi vigezo, wahusika walishauriwa kurekebisha maeneo yaliyokuwa na upungufu. Vilevile, Mamlaka ilipokea maombi 79 ya **usajili wa dawa za mifugo** ambapo maombi 71 yalifanyiwa tathmini na kati ya hayo maombi 58 sawa na asilimia 82 yalikidhi vigezo na hivyo kusajiliwa. Maombi 206 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa ambapo maombi 192 yalifanyiwa tathimini na kati ya hayo, maombi 164 sawa na asilimia 85 yalikidhi vigezo vya usajili.

*137.* ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ilifanyia kazi maombi 496 ya **usajili wa maeneo ya biashara ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi** kati ya maombi 497 yaliyopokelewa. Maombi 467 sawa na asilimia 94 yaliyofanyiwa kazi yalikidhi vigezo na hivyo maeneo husika kusajiliwa na kupewa vibali vya kuanza biashara za bidhaa hizo. Aidha, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa

viwanda vipya vitatu (3) vya uzalishaji dawa ndani ya nchi ambapo viwanda vyote vilikidhi vigezo vya uzalishaji. Vilevile, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda tisa (9) vya uzalishaji wa vifaa aina ya barakoa na vyote vilikidhi vigezo na kupewa usajili. Maeneo 7,291 yanayojihusisha na biashara ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi yalifanyiwa ukaguzi ambapo maeneo 6,351 sawa na asilimia 87 yalikidhi vigezo. Maeneo ambayo hayakukidhi vigezo yalipewa maelekezo ya kufanya marekebisho stahiki.

*138.* ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Sampuli 2,930 kati ya Sampuli 3,272 sawa na asilimia 90 za bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi zilichunguzwa ambapo Sampuli 2,862 sawa na asilimia 98 zilikidhi vigezo. Bidhaa ambazo Sampuli zake hazikukidhi vigezo hazikusajiliwa na nyingine kuondolewa kwenye Soko kwa njia ya ukaguzi. Kiwango cha asilimia 98 cha bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi zilizokidhi vigezo kwa kipindi hiki, kinaashiria uhakika wa uwepo wa bidhaa bora na salama kwenye soko kwa watumiaji. Katika kulinda afya za watumiaji wa bidhaa za dawa, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa tani 1,234.15 za bidhaa za dawa na vifaa tiba zenye thamani ya takriban shilingi bilioni 5.33 kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

*139.* ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka iliendelea kudhibiti ubora wa bidhaa za dawa, vifaa na vifaa tiba vinavyoingizwa au kusafirishwa nje ya nchi. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 7,573 ya kuingiza nchini bidhaa za dawa, vifaa na vifaa tiba, vitendanishi na malighafi ya kutengeneza dawa nchini yalipokelewa na kufanyiwa tathmini ambapo maombi 6,837 sawa na asilimia 90 yalikidhi vigezo na kuidhinishwa. Aidha, Mamlaka ilipokea na kufanyia kazi jumla ya maombi 732 ya kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa na vifaa tiba ambapo maombi 674 sawa na asilimia 92 yalikidhi vigezo na hivyo kuidhinishwa.

**Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)**

*140.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, jumla ya sampuli mbalimbali 70,981 zilizopokelewa sawa na asilimia 115 ya lengo. Sampuli zilizochunguzwa ni 64,685 sawa na asilimia 91 ya sampuli zilizopokelewa. Ongezeko la sampuli zilizopokelewa limetokana na kuwepo kwa kazi maalum zilizotekelezwa na vikosi kazi vya vyombo vya ulinzi na usalama. Matokeo ya uchunguzi wa Kimaabara yameendelea kuchangia katika utoaji wa haki na ulinzi wa Afya za Wananchi na mazingira.
Aidha, katika kipindi husika ukaguzi wa Maghala, usajili wa Wadau wa Kemikali na utoaji wa vibali ulifanyika, ambapo jumla ya kampuni 438 zinazojihusiha na kemikali zilisajiliwa sawa na asilimia 82 ya lengo na jumla ya vibali 31,333 vya kemikali vilitolewa sawa na asilimia 180 ya lengo. Maghala yaliyokaguliwa yalikuwa 1,000 sawa na asilimia 114 ya lengo. Ukaguzi umeimarisha utekelezaji wa sheria na kuchangia kulinda usalama wa Afya ya binadamu na mazingira.

*141.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Mamlaka imeendelea na ujenzi wa jengo lenye ghorofa nne (4) la Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Makao Makuu ya nchi Dodoma. Ujenzi huu unagharimu shilingi bilioni 8.14 na ulianza mwezi Julai 2021 na unategemewa kukamilika mwezi Julai 2022. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 45. Pia, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa wadau ambapo jumla ya Wadau 9,360 walielimishwa juu ya majukumu ya Mamlaka na wajibu wa Wadau katika kutekeleza Sheria, taratibu na kanuni zinazosimamiwa na Mamlaka.

*142.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Mamlaka iliweza kufanya tafsiri ya Sheria tatu zinazotekelezwa chini ya Mamlaka kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili kuweza kutoa uelewa mpana wa sheria hizo na kurahisisha utekelezaji wake. Sheria hizo ni: Sheria ya Mamlaka

ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sheria Na.8 ya Mwaka 2016; Sheria ya udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu, Sheria Na.8 ya Mwaka 2009; na Sheria ya usimamizi na udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sheria Na.3 ya Mwaka 2003.`

**Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)**

*143.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Utafiki wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) imeendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kupambana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, pamoja na kuimarisha mifumo ya afya. Katika kipindi hiki miradi 120 iliendelea kutekelezwa ikilinganishwa na lengo la mwaka la kutekeleza miradi 135. Taasisi ilikamilisha utafiti wa usalama na ufanisi wa dawa za tiba asili za NIMRCAF, Covidol, Convotanxa, Bingwa, Planet ++, Uzima na Bupiji kwa wagonjwa wa UVIKO-19. Matokeo yalionesha kuwa, hakukuwa na matatizo kwenye figo au ini kwa wagonjwa wa UVIKO-19 waliotumia dawa hizi; Utafiti mwingine uliangalia uwezo na utayari wa wananchi kulipia bima ya afya ili kufikia malengo ya upatikanaji wa afya kwa wote. Matokeo yalionesha kuwa asilimia 73 ya Wananchi walioshiriki katika utafiti huu walionesha utayari wa kujiunga na mifuko ya bima ya afya.

*144.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi iliendelea kutekeleza tafiti zingine ikiwa ni pamoja na; Utafiti wa usalama na ufanisi wa chanjo ya TANCoV 1.3.20 ya UVIKO-19 iliyotengenezwa hapa nchini; Utafiti wa kufuatilia hali ya maambukizi ya malaria nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika Mikoa 13 ya Tanzania bara; Utafiti unaolinganisha utoaji huduma wa pamoja kwa magonjwa ya VVU, kisukari na shinikizo la damu na mfumo wa utoaji huduma unaotumika sasa (Integrated diabetes, hypertension and HIV care); Utafiti wa majaribio ya chanjo ya VVU ulienda sambamba na utafiti wa dawa kinga za TAF/FTC na TDF/FTC kwa watu walio katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU ( PrEPVacc TRIAL). Kwa ujumla, muda wa kukamilika kwa tafiti zinazoendelea ni kati ya

mwaka mmoja hadi miaka mitano ambapo Taasisi imejipanga kutoa matokeo pindi hizo tafiti zitakapokamilika.

*145.* ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ilipokea na kuratibu tathmini za maadili na usalama kwa maombi ya tafiti 213 ikilinganishwa na lengo la mwaka la tafiti 275 sawa na asilimia 77. Katika maombi haya, zaidi ya asilimia 21 ya tafiti hizi zililenga kwenye Mifumo ya afya, asilimia 12 magonjwa yasiyoambukiza, asilimia 9 UKIMWI, asilimia 10 Malaria, asilimia 8.5 UVIKO-19, na asilimia 10 Kifua Kikuu. Miradi hii imelenga kutoa majibu na takwimu zinazohusu magonjwa ya Malaria, Virusi vya Ukimwi (VVU), Kifua kikuu, Magonjwa ya kitropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, na magonjwa yasiyoambukiza.

*146.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa uzalishaji wa dawa za tiba asili, Taasisi imeendelea na utekelezaji wa ujenzi wa jengo la uzalishaji wa dawa za tiba asili katika eneo la Mabibo Dar es Salaam, ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 95. Kwa sasa Taasisi inaendelea na taratibu za usimikaji wa Mitambo ya Uzalishaji.

**Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC)**

*147.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Chakula na Lishe inajukumu la kuratibu na kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kuimarisha huduma za lishe nchini. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Taasisi imetekeleza miradi Mitano (5) ya kiutafiti inayolenga kutatua changamoto za hali duni ya lishe (utapiamlo) katika Jamii. Miradi hiyo ni pamoja na *"Food Intake Survey Among Non-Pregnant Lactating Women Of Reproductive Age In Mbeya Region*", *"Barriers of Health-Seeking Behaviours Among Parents or Caregivers of Children Who Suffer From Severe Acute Malnutrition In Tanzania", "Assessment of Food Taboos and Preferences in Mainland Tanzania and Zanzibar", "Definining the Optimal Standards for Iodized Salts" na "The Efficacy of a developed Ready to Use (RUTF) Therapeutic Food for Children aged 6 – 59 months in Dodoma and Singida Regions.*

*148.* ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na miradi hii ya utafiti iliyoorodheshwa hapa juu Maabara ya Taasisi imeteuliwa na imeanza kufanya uchambuzi na kuchakata Sampuli zinazohusu viashiria vya chakula na lishe katika Utafiti wa Taifa wa Afya na Demografia *(Tanzania Demographic and Health Survey 2021/22)* ambao unaendelea nchi nzima. Uamuzi huu umetokana na Taasisi kujiimarisha zaidi katika eneo la uchambuzi wa Kimaabara kwa kununua mashine mpya ya kisasa ijulikanayo kama "*Cobas Integra*+" ambayo ina uwezo mkubwa wa kuchakata Sampuli za aina tofauti na kutoa matokeo ya viashiria vingi kwa usahihi na kwa muda mfupi.

*149.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha afua za kukabiliana na tatizo la upungufu wa vitamini na madini, katika kipindi hiki Taasisi kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo, kupitia VETA imenunua mashine tano (5) za kuchanganya madini joto katika chumvi zenye thamani ya Shilingi Milioni 55 ambazo zimesambazwa katika Mikoa mitatu (3) na Halmashauri Tano (5); Tanga (Halmashauri za Tanga Jiji na Mkinga), Pwani (Halmashauri za Bagamoyo na Mkuranga) na Mtwara (Halmashauri ya Mtwara Vijijini). Aidha, kwa kutengeneza mashine hizi ndani ya nchi, Serikali imeweza kuokoa takribani Shillingi Millioni 80.

*150.* ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu uandaaji na uzinduzi wa Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa masuala ya lishe *(2nd National Multisectoral Nutrition Action Plan 2021-2025)* ambao unatoa Mwongozo kwa Wadau wote kuhusu vipaumbele katika utekelezaji wa afua za lishe katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo. Uzinduzi wa mpango huu ulifanyika sambamba na uzinduzi wa Mkakati wake wa kutafuta Rasilimali fedha (Resouce Mobilization Stratergy). Pia, katika kipindi hiki Taasisi imeendelea kuratibu maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Lishe ambapo kwa mwaka huu wa fedha hafla ya kilele cha maadhimisho ilifanyika Mkoani Tabora.

## E. MABARAZA YA WANATAALUMA NA BODI ZA USHAURI ZA AFYA

*151.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya. Katika kutekeleza hilo mabaraza na bodi mbalimbali za kitaaluma ziliundwa kisheria kwa ajili ya kusimamia majukumu hayo. Mabaraza na bodi za kitaaluma ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Macho, Baraza la Radiologia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB) na Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Mabaraza na bodi hizi zimetekeleza majukumu yafuatayo:-

**Baraza la Madaktari Tanganyika**

*152.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Baraza limesajili wanataaluma wa kada mbalimbali kama ifuatavyo; Madaktari na Madaktari wa Kinywa Watarajali *(Provisional Registration)* 1,494; Uhuishaji wa Usajili (*Retention)* ya Madaktari na Madaktari wa Kinywa 15; na Usajili wa Kudumu *(Full registration)* Madaktari na Madaktari wa kinywa 2,395**.** Hadi kufikia Machi, 2022, **Jumla ya madaktari 26,090 wamesajiliwa na Baraza**.

*153.* ***Mheshimiwa Spika***, Baraza liliendesha na kusimamia Mitihani ya kabla ya utarajali (Pre- internship examinations) iliyofanyika katika Vituo vitano ambavyo ni Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Dar es Salaam na Mwanza. Mitihani hii ilihusisha Watahiniwa 1,198 kutoka katika Vyuo tisa (09) nchini, ambapo Madaktari walikua 1,153 na Madaktari wa Meno walikua 36.

*154.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, Baraza liliendesha na kusimamia mtihani wa baada ya utarajali (post-internship examination) iliyofanyika katika vituo 6 ambavyo ni Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam na

Pwani. Mitihani hii ilihusisha watahiniwa 2,186 kutoka katika vyuo 9 Nchini kwa mchanganuo ufuatao; Madaktari walikuwa 2,084, Madaktari wa meno walikuwa 43, *Physiotherapist* walikuwa 26, *Prosthetics and Orthotics* walikuwa 12 na *Clinical Psychiatrists* 21

*155.* ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanya uhamasishaji wa mafunzo endelevu ya kitaaluma kuanza kutekelezwa na wanataaluma ambapo kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Baraza kupitia Kamati ya Mafunzo Endelevu ya kitaaluma (CPD Committee) imefanya uhamasishaji kwa wanataaluma mbalimbali katika ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Aga Khan Dar es Salaam, Hospitali ya Rufaa ya kanda ya Mkoa wa Mbeya, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando Mwanza, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora-Kitete, Arusha Lutheran Medical Centre na Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru - Arusha. Lengo la vikao hivi ni kuhamasisha wataalamu juu ya usajili na utoaji wa Mafunzo Endelevu ambapo Baraza limeweza kusajili jumla ya Taasisi 21 zitakazotoa kozi mbalimbali za Mafunzo Endelevu

*156.* ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Baraza limesikiliza jumla ya Mashauri 34 ya uvunjifu wa maadili ya kitaaluma. Baada ya kusikiliza mashauri hayo, Baraza limefanya maamuzi ya Mashauri hayo kwa kuzingatia Sheria ya Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi Sura Na. 152 ya mwaka 2017 pamoja na kanuni zake, ambapo mashauri 11 yameshafanyiwa maamuzi, na mashauri 23 uchunguzi bado unaendelea.

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**

*157.* ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kufuatana na mpango kazi ambapo katika kipindi cha Julai 2021 mpaka Machi 2022 Baraza limefanikiwa kusajili jumla ya **Wauguzi na Wakunga wapya 4,567** wenye sifa ambao ni sawa na asilimia 82 ya wote waliyotarajiwa kusajiliwa. Aidha Wauguzi na Wakunga wanaendelea

kuhuisha leseni zao, ambapo kati ya Julai 2021 hadi Machi 2022, Jumla ya Wauguzi na Wakunga 1,148 wamehuisha leseni zao kwa wakati na jumla ya Watarajali 571 wanaendelea na mafunzo yao katika vituo mbalimbali. Hivyo hadi Machi 2022 baraza lina **jumla ya wauguzi na wakunga waliosajiliwa 47,973.**

*158.* ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuratibu, kuhamasisha na kufuatilia mafunzo ya kujiendeleza kazini (CPD) kwa Wauguzi na Wakunga kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na njia ya mtandao na masomo yanayoandaliwa katika Taasisi za mafunzo. Katika kipindi cha Julai, 2021 mpaka Machi, 2022 jumla ya wauguzi na wakunga 4,695 wamehudhuria mafunzo mbalimbali yakiwemo ya huduma bora kwa mteja (customer care), weledi wa kuhudumia wagonjwa mbalimbali, uwekaji wa kumbukumbu sahihi (documentation) na maadili ya wanataaluma.

*159.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Baraza lilipokea tuhuma mbalimbali za ukiukwaji wa maadili kutoka katika Mikoa wa Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Ruvuma. Baraza lilichunguza na kusikiliza tuhuma hizo na kufanya maamuzi kama ifuatavyo: Tuhuma 10 zilifanyiwa maamuzi ambapo Muuguzi mmoja (1) alikutwa na hatia na alisimamishwa kazi kwa muda wa miaka mitatu (3), Muuguzi mmoja (1) alipewa onyo la maandishi, Wauguzi wawili (2) walipewa karipio, Wauguzi wanne (4) mashauri yao yatasikilizwa tena, Muuguzi mmoja (1) aliachiwa huru na Muuguzi mmoja (1) shauri lake lipo kwa Afisa Ustawi wa Jamii. Mashauri mapya manne (4) yaliyopokelewa katika kipindi hiki, bado yapo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa.

**Baraza la Famasia**

*160.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Baraza lilisajili jumla ya wanataaluma 1724 ambapo kati yao Wanataaluma 1359 (wafamasia 397, fundi dawa sanifu 918 na fundi dawa wasaidizi 44) walipatiwa usajili wa kudumu, na

Wafamasia 365 walipatiwa Usajili wa muda (Provisional Registration). **Hivyo hadi Machi 2022, Baraza lina jumla ya wanataaluma 8,580** (8,215 wamepata usajili wa kudumu na 365 wana usajili wa muda). Kati ya 8,215 wenye usajili wa kudumu, wafamasia ni 2998, Fundi dawa 4432 na fundi dawa Wasaidizi 785).

*161.* ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile, katika kipindi hiki, Baraza lilifanya ukaguzi katika majengo 2,199. Kati ya hayo, 960 ni majengo mapya, na 1,239 ni maduka ya dawa muhimu yanayotoa huduma. Kati ya maeneo mapya yaliyokaguliwa maeneo 533 yalikidhi vigezo na kuruhusiwa kuendelea na biashara. Maeneo ambayo hayakukidhi vigezo wamiliki walishauriwa kurekebisha upungufu ulioonekana. Vilevile, Baraza lilihuisha vibali 2,082 na hakuna vibali vya maduka ya famasi vilivyofutwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukiukwaji wa utaratibu wa uendeshaji wa maduka hayo. Vilevile, ilani za kufunga famasi (closure order) ziliandikwa kwa famasi 196.

*162.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Baraza limeratibu mitihani ya usajili kwa waombaji 4,029 wakiwemo Wafamasia 694, Fundi dawa sanifu 3,000, Fundi dawa wasaidizi 292 na Watoa dawa 43 wa mwaka mmoja. Kati yao, watahiniwa 1782 (Wafamasia 491, Fundi dawa sanifu 1,136, Fundi dawa wasaidizi 134 na Watoa dawa 21) waliofanya mitihani katika Mwezi oktoba 2021, jumla ya watahiniwa 847 (47.5%) walifaulu na kupatiwa Leseni za utendaji kazi za taaluma, wakiwemo wafamasia 350, Fundi dawa Sanifu 487, Fundi dawa wasaidizi 6 watoa dawa 4 na hivi sasa wanatoa huduma katika maeneo mbalimbali nchini. Watahiniwa 2,245 wakiwemo wafamasia 203 Fundi dawa sanifu 1,864, Fundi dawa wasaidizi 158 Watoa dawa 22 walifanya mitihani yao mwezi Februari 2022, na matokeo ya watahiniwa hawa yanasubili kuidhinishwa na Bodi. ***Katika kuimarisha usimamizi wa dawa nchini naomba kuujulisha umma wa Tanzania kuwa Wizara inasitisha kwa muda Mafunzo ya ADDO kuanzia tarehe 1 Julai 2022.***

**Baraza la Wataalam wa Maabara**

*163.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Baraza limetoa usajili na leseni kwa Wataalam 5,111 na hivyo kuwa na jumla ya **Wataalam wa Maabara 22,348 waliosajiliwa**. Kati ya Wataalam waliopewa usajili kati ya kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, Wataalamu 1,303 walipewa usajili wa awali, na Wataalamu 748 walipewa usajili wa kudumu. Vilevile, Baraza liliandikisha Wataalamu 217 katika ngazi ya Cheti, na Wataalamu 2,843 wa kada ya afya ambao wanatoa huduma za Kimaabara, lakini sio Wataalamu waliosomea Maabara, kwa ajili ya kutoa huduma za upimaji wa vipimo vya haraka walipewa leseni za upimaji.

*164.* ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanya ukaguzi katika Vyuo vitatu (3) ambavyo ni *Kibaha College of Health and Allied Sciences, Mwanza City College* na *Arusha City College* kwa ajili ya kuanzisha kozi ya Maabara kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Kati ya Vyuo hivyo, Vyuo viwili (2) ambavyo ni *Kibaha College of Health and Allied Sciences na Mwanza City College* havikukidhi vigezo vya kupewa kibali cha kutoa mafunzo hayo kutokana na mapungufu makubwa yaliyobainika. Chuo cha *Arusha City College* kilikidhi vigezo vya kupewa kibali cha kuanzisha kozi ya Maabara na hivyo sasa kuwepo kwa jumla ya Vyuo 46 vinavyotoa mafunzo hayo.

*165.* ***Mheshimiwa Spika,*** Jumla ya Vyuo 7 vilifanyiwa ukaguzi shirikishi wa kufuatilia ubora wa utoaji wa mafunzo. Vilevile, Baraza limewatahini Wataalamu wa Maabara kwa ngazi ya Astashahada Wataalam 256, Stashahada Wataalamu 1,468 na Shahada Wataalamu 387 kwa ajili ya usajili wa leseni za kudumu.

**Baraza la Wataalamu wa Radiolojia**

*166.* ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, jumla ya maombi 321 yalipokelewa kwa ajili ya usajili, uandikishaji na uorodheshaji wa Wataalamu wa

Radiolojia. Maombi 312 yalipitishwa na kupata usajili, na maombi 9 hayakukidhi vigezo. Aidha, jumla ya Wataalamu 1,000 kati ya 1,647 wamehuisha leseni zao. Vilevile, Watarajali 59 walisajiliwa na kupangiwa vituo vya kufanyia mazoezi kwa vitendo (Watarajali 28 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Watarajali 31 kwa mwaka wa fedha 2021/2022). Kundi la kwanza lilimaliza mwezi Oktoba 2021 na kundi la pili lilianza Novemba 2021 na ukaguzi wa Watarajali umekuwa ukifanyika kila baada ya miezi mitatu.

*167*. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia maadili na miiko ya taaluma ya Radiolojia, jumla ya Mashauri matatu ya uvunjifu wa Miiko na Maadili ya Taaluma yaliripotiwa. Mashauri mawili yalijadiliwa kwenye kikao cha Kamati ya nidhamu ya Baraza na kutolewa maamuzi. Aidha, shauri la tatu lipo katika ngazi ya Mahakama. Baraza limekuwa likifuatilia Wataalamu wake kupitia ukaguzi shirikishi katika maeneo mbalimbali. Katika kipindi hiki Baraza liliweza kutembelea Vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya Radiolojia kwa Kada mbalimbali na kutoa elimu juu ya Miiko na Maadili. Baraza limekamilisha mfumo wa usajili wa Wataalamu (Health Practioners Registration System) ambapo Wataalamu wameanza kupata mafunzo ya namna ya kuutumia mfumo huo.

**Baraza la Afya Mazingira**

*168.* ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 Baraza limesajili Wataalamu wapya 132, Waliohuisha leseni 1,183, na Usajili wa awali (provisional registration) 99. Aidha Baraza limefanya usimamizi elekezi na shirikishi katika Vyuo vitano (5) vinavyotoa mafunzo ya Sayansi ya Afya Mazingira kwa lengo la kutoa elimu ya masuala ya usajili na leseni kwa Wanafunzi wanaoelekea kuhitimu, wafanyakazi (Wakufunzi) wa vyuo husika na kufanya ufuatiliaji wa Watarajali 63 waliokuwa wakifundisha katika Vyuo hivyo ili kujua maendeleo, changamoto na kuzitafutia ufumbuzi. Hivyo hadi **Machi 2022 Baraza lina jumla ya wanataaluma 4,002 waliosajiliwa.**

*169.* ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limetengeneza Mtaala unaojitegemea wa elimu ya kujiendeleza (CPD) na nyenzo za kufanyia tathimini. Aidha, majukumu mengine yaliyotekelezwa na Baraza ni pamoja na: kufanya majaribio ya mfumo mpya wa usajili wa kieletroniki na kuanza zoezi la kuingiza taarifa za wataalamu 1,627 waliosajiliwa ili waanze kutambuliwa na mfumo huo; Kushiriki katika utekelezaji wa Kampeni ya usafi wa mazingira; na kuandaa Mwongozo wa ufundishaji wa masuala ya afya na mabadiliko ya tabia ya nchi ambao utatumika na Vyuo vya Afya Mazingira nchini.

*170.* ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limefanya ufuatiliaji na usimamizi elekezi katika Mikoa ya Ruvuma, Songwe, Mtwara, Singida, Arusha, Tabora, Manyara na Kilimanjaro kwa lengo la kufuatilia tuhuma za uvunjifu wa maadili, kusimamia watarajali waliopo katika mikoa tajwa na kuhimiza masuala ya Usajili wa wataalamu, vikundi na taasisi zinazotoa huduma za afya Mazingira na uhuishaji wa leseni za wataalamu wa Mikoa husika na kutoa elimu kwa Maafisa Afya wa Mikoa tajwa juu ya mfumo mpya wa kujisajili kwa njia ya kielektroniki.

*171.* ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kutoa elimu ya masuala ya kuzingatia maadili na miiko ya kada kama sheria inavyosisitiza, kazi hii inafanyika kwa ushirikiano kati ya Baraza, Chama cha Maafisa Afya (CHAMATA) na Maafisa Afya wa Mikoa na Halmashauri kwa kusisitiza Wataalamu kufanya kazi kwa weledi na uaminifu pasipo kuvunja miiko na maadili ya kada. Ambapo kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2021 hadi Machi, 2022 mashauri ya uvunjifu wa maadili yaliyoshughulikiwa ni matatu (3).

**Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala**

*172.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala limesajili jumla ya Waganga wa tiba asili na tiba mbadala pamoja na wasaidizi wao 3,271, vituo vya kutolea huduma za tiba asili 91, dawa za asili 8 na uhuishaji wa leseni kwa Waganga wa tiba asili 707. Aidha, katika kipindi hicho Baraza limeendelea

kusimamia, kuratibu na kuendeleza huduma za tiba asili na tiba mbadala ambazo ni miongoni mwa huduma za afya zinazotolewa hapa nchini. Hivyo hadi Machi 2022 baraza lina jumla ya waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala 31,064 waliosajiliwa

*173.* ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza liliendesha zoezi maalumu la uhamasishaji na utengenezaji wa leseni za Waganga wa tiba asili kwa papo hapo, zoezi hili lilifanyika katika mikoa ya Simiyu na Shinyanga ili kupunguza changamoto ya Waganga wengi kufanya kazi bila kuwa na leseni. Katika zoezi hili lililofanyika katika Halmashauri zote za mikoa ya Simiyu na Shinyanga jumla ya Waganga 2,742 walisajiliwa.

*174.* ***Mheshimiwa Spika***, Baraza lilifanya ukaguzi katika vituo vya kutolea huduma za Tiba Mbadala mkoa wa Dar es Salaam ambapo watoa huduma 105 na vituo 82 vya kutolea huduma za tiba mbadala (Masaji) walifikiwa na kuelimishwa juu ya sheria na taratibu za usajili wa vituo na watoa huduma. Katika zoezi hili ilibainika kuwa watoa huduma za tiba mbadala (masaji) hawakuwa na uelewa juu ya mamlaka inayowasimamia na taratibu wanazopaswa kuzifuata kwa mujibu wa sheria ili kuendesha huduma zao kama sehemu za tiba mbadala zilizorasimishwa.

*175.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Baraza kupitia kamati ya maadili imefanyia kazi mashauri matatu ya uvunjifu wa maadili ambayo yamewasilishwa kwenye kikao cha kisheria cha Baraza kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi. Mashauri hayo yanahusika na; Uchakachuaji wa dawa asili zinazoombewa usajili (Adulteration) na dhuluma ya haki miliki ya ugunduzi wa dawa asili.

*176.* ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuhakikisha taaluma ya tiba asili na tiba mbadala inasimamiwa na kukuwa, Baraza limeendelea kutoa mafunzo kwa waratibu wa tiba asili na tiba mbadala ngazi ya halmashauri na mikoa juu ya sheria,

kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali ili waratibu hao ambao ndiyo wasimamizi wa shughuli za tiba asili katika maeneo yao wakawe chachu ya usimamizi na uendelezaji wa tiba asili.

**Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi**

*177.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Bodi ya Ushauri ya Hospitali binafsi imesajili Hospitali Binafsi 250, kati ya Vituo hivyo, Vituo 230 viliomba usajili mpya, viliomba kupandishwa hadhi na vituo 3 viliomba kuongeza huduma. Katika Vituo vilivyoomba kusajiliwa, Vituo 5 viliomba kusajiliwa katika Hospitali ngazi ya mkoa, 4 ngazi ya Wilaya, 6 huduma ya kuchuja damu, 115 usajili wa Clinic aina mbalimbali, 10 ngazi ya Vituo vya Afya na 104 ngazi ya Zahanati. Aidha, Bodi imeidhinisha Mashirika 95 kati ya 98 yaliyoomba kusimamia na kuendesha Vituo vya kutolea huduma za afya.

*178.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia utoaji wa huduma bora kulingana na Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu Bodi ya Ushauri ya Hospitali binafsi ilifanya ukaguzi wa Hospitali Binafsi 366 katika mikoa ya Arusha, Tanga na Mbeya. Kati ya Vituo vilivyokaguliwa Vituo 39 vilisitishiwa huduma kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutokuwa na usajili, kutokuwa na watumishi na miundombinu mibovu.

*179.* ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ilipokea tuhuma moja (1) ya ukiukwaji wa miongozo na sheria za usajili wa hospitali binafsi kutoka mkoa wa Iringa. Tuhuma hii ilifanyiwa kazi kwa pamoja na Bodi ya Hospitali Binafsi (PHAB), Bodi ya Vituo vya Maabara Binafsi (PHLB) na Kurugenzi ya Tiba na Kituo kilikutwa na makosa na hivyo kupewa adhabu. Mmiliki wa Kituo cha Afya ambaye pia ndiye mmiliki wa Chuo aliagizwa kutenganisha eneo la Chuo na kituo cha Afya. Mmiliki alipokea maagizo na kuahidi kuhamisha chuo kutoka kwenye Kituo cha Afya kwenda eneo jingine ndani ya miezi sita (6).

**Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB)**

*180.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya imesajili jumla ya Maabara Binafsi za Afya 346 na kufikia jumla kuu ya **Maabara Binafsi za Afya 2,839 zilizosajiliwa kote nchini hadi mwezi Machi 2022**. Aidha, katika kuhakikisha kuwa wamiliki wa maabara binafsi za Afya nchini wanazingatia sheria, kanuni na miongozo, Bodi imefanya ukaguzi shirikishi wa maabara za Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Mbeya na Iringa na jumla ya maabara 562 zilifikiwa.

*181.* ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Maabara Binafsi ya Afya pia ilitoa elimu ya ubora wa huduma za maabara, sheria, kanuni za maabara kwa wamiliki na watendaji wa maabara ili kuondoa mazingira hatarishi kwa mgonjwa, kuhakikisha wamiliki wanasajili maabara zao kwa mujibu wa Sheria Na. 10 ya 1997 na kanuni zake kuboresha huduma za maabara na pia kuhuisha leseni zao pindi zinapoisha muda wake. Bodi ya Maabara Binafsi za Afya imeweza kufanya mafunzo kwa waratibu wa huduma za maabara nchini katika Wilaya 49 za Mikoa 8. Katika mafunzo hayo jumla ya Waratibu wa huduma za Maabara ngazi ya Wilaya 49 walipata nafasi ya kujengewa uwezo kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya Bodi ya Maabara Binafsi za Afya. Aidha, walielimishwa juu ya mbinu za ukaguzi, malipo ya tozo mbalimbali za Bodi kupitia mfumo wa malipo ya Serikali "GePG", maadili ikiwa ni pamoja na kuepuka Rushwa na kutumia lugha nzuri kwa wateja kwa lengo la kuboresha huduma za maabara na vipimo kwa ustawi wa umma wa watanzania.

## F. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

*182.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ya Afya imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha huduma za afya nchini: -

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano;
ii. Kusimamia viwango vya ubora wa huduma za kinga na tiba katika ngazi zote za utoaji huduma za afya nchini;
iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, vifo vya watoto wachanga pamoja na mimba za utotoni,
iv. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya
v. Kuimarisha huduma za lishe hususani kwa watoto wa umri wa chini ya miaka 5, vijana balehe na wanawake wa umri wa kuzaa;
vi. Kuimarisha huduma za afya na usafi wa mazingira ili kudhibiti magonjwa ya kuambukizi na hivyo kupunguza idadi ya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini;
vii. Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwemo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa;
viii. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi;
ix. Kudhibiti magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyo ya kuambukiza;
x. Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalamu katika Sekta ya Afya;
xi. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;
xii. Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika utoaji huduma za afya; na
xiii. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu katika utoaji wa huduma za afya nchini.

*183.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vilivyoanishwa katika mwaka 2022/23, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha **shilingi 1,109,421,722,000** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na

uendeshaji wa Ofisi na miradi wa maendeleo. Baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na: -

i. Kununua, kutunza, kusambaza na kutoa Chanjo kwa watoto nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 74,473,286,354** zimetengwa.
ii. Kujenga Hospitali Maalum ya Mama na Mtoto Jijini Dodoma ili kuimarisha huduma za tiba kwa magonjwa ya wanawake na watoto ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 10** kimetengwa. Aidha kiasi cha **shilingi bilioni 23.36** kimetengwa kwa ajili ya kujenga vyumba vya huduma za Watoto wachanga katika hospitali 100 za wilaya, kuwajengea uwezo watoa huduma kuwa na stadi, weledi na tabia bora katika kutoa huduma za mama na mtoto, kujenga, kuweka vifaa na watumishi wenye weledi kwenye ICU za Wazazi katika hospitali za Kanda na mikoa
iii. Kuwezesha Ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuzisambaza katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 200** zimetengwa.
iv. Kukamilisha ujenzi wa Hospitali (5) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya **Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu** ambapo jumla ya **shilingi bilioni 18.6** kimetengwa.
v. Kukamilisha ujenzi wa Hospitali mpya tatu (3) za Rufaa za Mikoa katika mikoa ya **Shinyanga, Singida na Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Mara** ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 26** kimetengwa.
vi. Kuendelea kukamilisha upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali nane (8) za Rufaa za Mikoa ambayo mikataba yake bado inaendelea. Hospitali hizo ni pamoja na Ligula (Mtwara) Tumbi (Pwani), Bombo (Tanga), Kagera, Maweni (Kigoma), Kitete (Tabora), Sekou – Toure (Mwanza) na Mawenzi (Kilimanjaro) ambapo kiasi cha **Shilingi 13,698,000,000** kimetengwa.
vii. Kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa na Kanda kwa kuimarisha miundombinu na ununuzi wa vifaa katika Taasisi ya

JKCI, Hospitali za Rufaa za Kanda za Chato, Mtwara, KCMC, Bugando, Mbeya na kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi. Vilevile, Hospitali Teule ya Ukerewe itaimarishwa katika eneo hili ambapo jumla ya **Shilingi 16,900,000,000** zimetengwa.

viii. Kuendelea na ujenzi wa wodi ya wagonjwa binafsi (Private word katika hospitali ya Taifa Muhimbili) ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4** kimetengwa

ix. Kuanza ujenzi wa jengo la kutolea huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikiwemo huduma ya Mionzi katika hospitali ya Benjamini Mkapa- Dodoma, kiasi cha **shilingi bilioni 10** kimetengwa

x. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali mbili (2) mpya za Mikoa ya Ruvuma na Sokoine (Lindi) ambapo kiasi cha **Shilingi 2,000,000,000** zimetengwa.

xi. Kuwezesha Mafunzo ya Ubingwa Bobezi Nje ya Nchi ambapo kiasi cha **Shilingi 3,000,000,000** kimetengwa.

xii. Kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi tarajali (Interns) ambapo kiasi cha **shilingi 65,000,000,000** zimetengwa.

xiii. Kuimarisha udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza ambapo kiasi cha **Shilingi 12,609,396,973** zimetengwa.

xiv. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 26,608,315,374** zimetengwa.

xv. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 14,833,845,612** zimetengwa.

xvi. Kutekeleza afua nyingine mbalimbali za afya ambapo kiasi cha **Shilingi 57,409,211,687** zimetengwa.

## G. SHUKRANI

*184*. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za Afya na Ustawi wa Jamii.

*185*. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), Ireland (Irish Aid), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini hususani afya ya msingi. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali ikiwemo kufadhili miradi mbalimbali inayotekelelezwa na Serikali kwa kushirikia na Mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuboresha huduma za afya nchini.

*186*. ***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN-Women, WHO na IAEA); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); IMF, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); GAVI; PEPFAR; CDC; USAID; PMI; Abbott Fund; DFID; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; Global Fund (for HIV, TB na Malaria); Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; KfW; Save the Children; World Vision; Benki ya STANBIC; Walter REED; Jhpiego na Delloite

*187*. ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin Mkapa Foundation, AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International,

SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Kivulini, WiLDAF, TCRF na FSDT.

*188.* ***Mheshimiwa Spika,*** navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya.

*189.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.),** Naibu Waziri wa Afya. Aidha, naomba kuwashukuru **Prof. Abel N. Makubi** Katibu Mkuu na **Dkt Seif A. Shekalaghe,** Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawashukuru **Dkt Alfello W. Sichalwe**, Mganga Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia Wakurugenzi Wakuu wa Hospitali za Taifa na Kanda ambao ni **Prof. Lawrence M. Museru** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Dkt. Respicious L. Boniface** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Prof. Mohamed Janabi** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Julius Mwaiselage,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Leonard Subi** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dkt. Paul S. Lawala** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Dkt. Alphonce Chandika** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Mawala** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Fabian A. Massaga**(Hospitali ya Bugando) na **Dkt. Geleard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC).

*190.* ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru wakurugenzi na wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara

ambazo ni MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TFNC pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili. Vilevile ninawashukuru Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa watanzania kujali na kulinda afya zao ikiwemo kwa kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa, kufanya mazoezi ya viungo mara kwa mara na kujiepusha na unywaji wa pombe kupita kiasi. Ni muhimu watanzania wakatambua kuwa Afya ni Mtaji.

*191.* ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru Familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Jimbo letu la Tanga Mjini.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2022/23

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/23

*192.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha **shilingi 619,538,808,257**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 140,813,114,464.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, **shilingi 85,739,668,813.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, **shilingi 392,986,024,980.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Makusanyo hayo ni

sawa na ongezeko la **asilimia 22** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2021/22 ambayo yalikuwa ni kukusanya shilingi **507,218,152,321.00**.

**Matumizi ya Kawaida**

*193.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **shilingi 554,289,666,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 50** ya bajeti tengwa, ambapo kiasi cha **shilingi 331,566,406,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha **shilingi 222,723,260,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

*194.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inakadiria kutumia **shilingi 555,132,056,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 50** ya bajeti tengwa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **shilingi 410,298,000,000.00** na fedha za nje ni **shilingi 144,834,056,000.00**

*195.* ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni **shilingi 1,109,421,722,000.00** ili kuweza kutekeleza malengo iliyojiwekea.

| **Na.** | **Fungu** | **Matumizi ya Kawaida** | **Miradi ya Maendeleo** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 52 | 554,289,666,000.00 | 555,132,056,000.00 | 1,109,421,722,000.00 |
| | **Jumla** | **554,289,666,000.00** | **555,132,056,000.00** | **1,109,421,722,000.00** |

*196.* ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya *www.moh.go.tz*.

*197.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**Kiambatisho Na.1.** Magonjwa 10 yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje (OPD) 2021/22

| | Umri chini ya Miaka 5 | | | Umri miaka mitano na zaidi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi ya Wagonjwa** | **Asilimia/ (wagonjwa wote)** | **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi ya wagonjwa** | **Asilimia/ (Wagonjwa wote)** |
| 1 | Maambukizi katika mfumo wa hewa | 3,270,329 | 33.3 | Maambukizi katika mfumo wa hewa | 3,675,506 | 18.6 |
| 2 | Malaria | 1,183,965 | 12.0 | Maambukizi katika njia ya mkojo | 3,059,487 | 15.5 |
| 3 | Maambukizi katika njia ya mkojo | 828,205 | 8.4 | Malaria | 1,356,865 | 6.9 |
| 4 | Kuharisha (With No Dehydration) | 750,940 | 7.6 | Shinikizo la juu la moyo | 1,017,106 | 5.2 |
| 5 | Kichomi, (Non-Severe & Severe) | 695,861 | 7.0 | kichomi (severe & Non severe) | 636,422 | 3.2 |
| 6 | Magonjwa ya mfumo wa chakula | 323,072 | 3.3 | Vidonda vya tumbo | 610,264 | 3.1 |
| 7 | Minyoo ya tumboni | 284,642 | 2.9 | Magonjwa ya mfumo wa chakula | 560,330 | 2.8 |
| 8 | Magonjwa ya ngozi | 207,314 | 2.1 | Minyoo yatumboni | 488,209 | 2.5 |
| 9 | Kuharisha (With Dehydration) | 206,927 | 2.1 | Kisukari | 488,054 | 2.5 |
| 10 | Magonjwa ya ngozi | 143,508 | 1.5 | Upasuaji | 400,256 | 2.0 |

**Kiambatisho Na 2:** Magonjwa 10 yaliyoongoza kwa Wagonjwa wa Kulazwa (IPD) 2021/22

| | Umri chini ya Miaka 5 | | | Umri miaka mitano na zaidi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi ya Wagonjwa** | **Asilimia/ (Wagonjwa wote)** | **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi ya wagonjwa** | **Asilimia/ (Wagonjwa wote)** |
| 1 | Kichomi (Severe & Non severe) | 64,599 | 18.9 | Malaria | 76,834 | 9.8 |
| 2 | Malaria | 52,554 | 15.4 | Kichomi (severe & non severe) | 65,904 | 8.4 |
| 3 | Kuharisha sana (<siku 14) | 36,052 | 10.6 | Magonjwa ya mfumo wa mkojo | 50,723 | 6.5 |
| 4 | Upungufu wa damu | 25,937 | 7.6 | Upungufu wa damu | 45,997 | 5.9 |
| 5 | Kuzaliwa na uzito mdogo (<2.5kg) | 13,282 | 3.9 | Shinikizo la juu la moyo | 43,974 | 5.6 |
| 6 | Maambukizi katika damu | 13,040 | 3.8 | Vidonda vya tumbo | 30,316 | 3.9 |
| 7 | Maambukizi ya mfumo wa upumuaji | 12,939 | 3.8 | Magonjwa ya kina mama | 29,445 | 3.8 |
| 8 | Maambukizi ya mfumo wa mkojo | 11,508 | 3.4 | Mimba kutoka (Abortion) | 26,720 | 3.4 |
| 9 | Magonjwa ya mfumo wa chakula | 10,396 | 3.1 | Kisukari | 25,777 | 3.3 |
| 10 | Kukosa hewa (Birth Asphyxia) | 9,329 | 2.7 | Magonjwa ya mfumo wa chakula | 23,990 | 3.1 |

*Chanzo: DHIS2*

**Kiambatisho Na.3.** Idadi ya Wagonjwa waliohudumiwa katika Hospitali ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022

| NA. | HOSPITALI | WAGONJWA WALIOHUDUMIWA 2021/22 | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | | Nje (OPD) | Wakulazwa (IPD) | |
| 1 | HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI(UPANGA) | 328,938 | 38,275 | 367,213 |
| 2 | HOSPITALI YA MUHIMBILI (MLOGANZILA) | 82,804 | 8,940 | 91,744 |
| 3 | TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE (JKCI) | 84,045 | 3,287 | 87,332 |
| 4 | TAASISI YA MIFUPA MUHIMBILI (MOI) | 147,847 | 6,413 | 154,260 |
| 5 | TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD | 33,621 | 4,261 | 37,882 |
| 6 | HOSPITALI YA MIREMBE | 26,761 | 1,564 | 28,325 |
| 7 | HOSPITALI YA RUFAA KANDA MBEYA | 205,329 | 31,857 | 237,186 |
| 8 | HOSPITALI YA MAGONJWA AMBUKIZI KIBONG'OTO | 13,953 | 636 | 14,589 |
| 9 | HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA | 160,942 | 7,537 | 168,479 |
| 10 | HOSPITALI YA BUGANDO | 269,019 | 22,818 | 291,837 |
| 11 | HOSPITALI YA KCMC | 208,467 | 89,343 | 297,810 |
| 12 | HOSPITALI YA KANDA YA CHATO | 4,810 | 797 | 5,607 |
| | **JUMLA** | **1,566,536** | **215,728** | **1,782,264** |

**Kiambatisho Na.4.** Idadi ya Wagonjwa wa Msamaha katika Hospitali ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022

| NA. | HOSPITALI | WAGONJWA WALIOPATA MISAMAHA (Julai 2021 hadi Machi, 2022) | |
|---|---|---|---|
| | | MISAMAHA | THAMANI |
| 1 | HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI UPANGA | 46,591 | 14,100,000,000 |
| 2 | HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI MLOGANZILA | 2,928 | 1,900,000,000.00 |
| 3 | TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE (JKCI) | 2,135 | 814,848,257.29 |
| 4 | TAASISI YA MIFUPA MUHIMBILI (MOI) | 3,152 | 318,307,889.90 |
| 5 | TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD | 2,792 | 13,885,950,630 |
| 6 | HOSPITALI YA RUFAA KANDA MBEYA | 18,547 | 185,478,000.00 |
| 7 | HOSPITALI YA MAGONJWA AMBUKIZI KIBONG'OTO | 497 | 114,541,967.00 |
| 8 | HOSPITALI YA MIREMBE | 3,985 | 60,217,746.00 |
| 9 | HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA | 2,228 | 281,000,000.00 |
| 10 | HOSPITALI YA BUGANDO | 548 | 308,651,412.00 |
| 11 | HOSPITALI YA KCMC | 703 | 3,500,000,000.00 |
| 12 | HOSPITALI YA KANDA YA CHATO | 3 | 900,000.00 |
| | **JUMLA** | **84,109** | **35,469,895,902.19** |

**Kiambatisho Na.5.** Wagonjwa waliohudumiwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022

| Na. | Hospitali | Mkoa | Idadi ya Vitanda | Wagonjwa Julai 2021 hadi Machi, 2022 | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | NJE (OPD) | WAKULAZWA (IPD) | |
| 1 | Amana | DSM | 341 | 123,905 | 14,115 | 138,020 |
| 2 | Bombo | Tanga | 457 | 58,090 | 8,700 | 66,790 |
| 3 | Bukoba | Kagera | 312 | 64,234 | 4,699 | 68,933 |
| 4 | Dodoma | Dodoma | 423 | 148,785 | 20,927 | 169,712 |
| 5 | Geita | Geita | 227 | 39,494 | 4,488 | 43,982 |
| 6 | Iringa | Iringa | 377 | 58,675 | 8,990 | 67,665 |
| 7 | Katavi | Katavi | 149 | 47,527 | 6,199 | 53,726 |
| 8 | Kitete | Tabora | 240 | 37,998 | 6,917 | 44,915 |
| 9 | Ligula | Mtwara | 222 | 40,823 | 3,794 | 44,617 |
| 10 | Manyara | Manyara | 111 | 21,490 | 2,987 | 24,477 |
| 11 | Maweni | Kigoma | 178 | 38,152 | 4,572 | 42,724 |
| 12 | Mawenzi | Kilimanjaro | 210 | 75,541 | 6,594 | 82,135 |
| 13 | Mbeya | Mbeya | 180 | 31,128 | 1,548 | 32,676 |
| 14 | Morogoro | Morogoro | 375 | 88,810 | 13,193 | 102,003 |
| 15 | Mt. Meru | Arusha | 420 | 86,896 | 10,710 | 97,606 |
| 16 | Musoma | Mara | 269 | 39,002 | 5,139 | 44,141 |
| 17 | Mwananyamala | DSM | 309 | 453,833 | 11,976 | 465,809 |
| 18 | Njombe* | Njombe | 54 | 9,718 | 953 | 10,671 |
| 19 | Sekou Toure | Mwanza | 331 | 86,048 | 26,278 | 112,326 |
| 20 | Shinyanga | Shinyanga | 276 | 45,041 | 6,880 | 51,921 |
| 21 | Simiyu* | Simiyu | 24 | 13,367 | 935 | 14,302 |
| 22 | Singida | Singida | 300 | 66,829 | 4,338 | 71,167 |
| 23 | Sokoine | Lindi | 176 | 23,032 | 3,927 | 26,959 |
| 24 | Songea | Ruvuma | 321 | 80,932 | 9,087 | 90,019 |
| 25 | Songwe | Songwe | 156 | 81,979 | 4,147 | 86,126 |
| 26 | Sumbawanga | Rukwa | 217 | 29,161 | 13,318 | 42,479 |
| 27 | Temeke | DSM | 370 | 443,910 | 10,354 | 454,264 |
| 28 | Tumbi | Pwani | 236 | 81,031 | 5,694 | 86,725 |
| | **Jumla** | | **7,261** | **2,415,431** | **221,459** | **2,636,890** |
| | | | | | | |

**Kiambatisho Na.6.** Idadi ya Wagonjwa wa Msamaha waliohudumiwa pamoja na gharama zao katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022

| Na | Hospitali | Idadi ya Wagonjwa Waliosamehewa | Gharama za Msamaha |
|---|---|---|---|
| 1 | Amana-DSM | 9,020 | 128,615,836 |
| 2 | Bombo-Tanga | 12,055 | 270,908,988 |
| 3 | Bukoba-Kagera | 4,672 | 112,184,704 |
| 4 | Dodoma | 16,687 | 596,349,500 |
| 5 | Geita | 7,891 | 178,820,171 |
| 6 | Iringa | 2,005 | 35,909,420 |
| 7 | Katavi | 1,968 | 80,224,870 |
| 8 | Kitete-Tabora | 7,387 | 185,995,965 |
| 9 | Ligula-Mtwara | 716 | 3,945,350 |
| 10 | Manyara | 1,902 | 129,779,354 |
| 11 | Maweni-Kigoma | 1,457 | 42,880,210 |
| 12 | Mawenzi-Kilimanjaro | 11,175 | 104,686,389 |
| 13 | Mbeya | 52 | 1,731,470 |
| 14 | Morogoro | 2,357 | 39,275,516 |
| 15 | Mount Meru-Arusha | 5,543 | 102,011,830 |
| 16 | Musoma-Mara | 4,061 | 109,244,396 |
| 17 | Mwananyamala -DSM | 5,422 | 238,127,590 |
| 18 | Njombe | 175 | 6,039,390 |
| 19 | Sekou Toure-Mwanza | 21,640 | 351,342,118 |
| 20 | Shinyanga | 2,242 | 49,093,830 |
| 21 | Simiyu | 81 | 3,235,810 |
| 22 | Singida | 3,499 | 244,439,034 |
| 23 | Sokoine-Lindi | 1,146 | 5,488,820 |
| 24 | Songea-Ruvuma | 7,375 | 86,132,940 |
| 25 | Songwe | 5,717 | 235,668,860 |
| 26 | Sumbawanga-Rukwa | 1,827 | 23,466,903 |
| 27 | Temeke-DSM | 6,024 | 65,401,000 |
| 28 | Tumbi-Pwani | 1,701 | 42,133,841 |
|  | **Jumla** | **145,797** | **3,473,134,105** |

**Kiambatisho Na.7:** Idadi ya akina mama waliojifungua na vifo vilivyotokana na uzazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi,2022.

| Na | Hospitali | Waliojifungua | Vifo Vilivyotokana na Uzazi |
|---|---|---|---|
| 1 | Amana-DSM | 5,293 | 10 |
| 2 | Bombo-Tanga | 2,802 | 13 |
| 3 | Bukoba-Kagera | 1,175 | 9 |
| 4 | Dodoma | 5,828 | 18 |
| 5 | Geita | 3,668 | 16 |
| 6 | Iringa | 1,754 | 7 |
| 7 | Katavi | 1,129 | 6 |
| 8 | Kitete-Tabora | 1,772 | 28 |
| 9 | Ligula-Mtwara | 946 | 10 |
| 10 | Manyara | 2,294 | 8 |
| 11 | Maweni- Kigoma | 773 | 7 |
| 12 | Mawenzi-Kilimanjaro | 1,290 | 0 |
| 13 | Mbeya | 2,179 | 6 |
| 14 | Morogoro | 3,759 | 17 |
| 15 | Mount Meru-Arusha | 3,602 | 8 |
| 16 | Musoma-Mara | 1,566 | 7 |
| 17 | Mwananyamala-DSM | 4,352 | 7 |
| 18 | Njombe | 272 | 6 |
| 19 | Sekou Toure- Mwanza | 4,418 | 7 |
| 20 | Shinyanga | 1,524 | 4 |
| 21 | Simiyu | 0 | 0 |
| 22 | Singida | 1,915 | 4 |
| 23 | Sokoine-Lindi | 787 | 1 |
| 24 | Songea- Ruvuma | 2,612 | 3 |
| 25 | Songwe | 3,408 | 3 |
| 26 | Sumbawanga-Rukwa | 1,189 | 16 |
| 27 | Temeke-DSM | 3,932 | 7 |
| 28 | Tumbi-Pwani | 1,377 | 3 |
| **Jumla** | **65,616** | **231** | |

**Kiambatisho Na.**8. Jedwali linaloonesha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

| Na. | Hospitali Husika | Lengo la Mradi | Gharama za Mradi | Chanzo cha Fedha | Kiasi kilichotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1: Ujenzi na Upanuzi wa Majengo mbalimbali ya kutolea huduma katika Hospitali Ngazi ya Taifa** | | | | | | |
| **Na.** | **Hospitali Husika** | **Lengo la Mradi** | **Gharama za Mradi** | **Chanzo cha Fedha** | **Kiasi kilichotolewa** | **Hatua ya utekelezaji (%)** |
| 1 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | Ujenzi wa Jengo la Wodi Maalum (Private wards) Ujenzi unatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza (hadi hatua ya jamvi) iligharimu 1.2bil. Awamu ya pili (Framed Structure) itagharimu 4.36 Bil. | 26,000,000,000.00 | GOT | 4,000,000,000.00 | Asilimia 26 |
| | | Ukarabati wa vyumba vya ICU 5 | 1,000,000,000.00 | IMF | 900,000,000.00 | Asilimia 80 |
| | | Ukarabati wa vyumba vya Radiologjia (MRI 1, CT SCAN 1 na X-ray 2 | 40,000,000.00 | IMF | 40,000,000.00 | Asilimia 90 |
| **JUMLA KUU HOSPITALI NGAZI YA TAIFA** | | | **27,040,000,000.00** | | **4,940,000,000.00** | |
| **2: Ujenzi na Upanuzi wa Majengo mbalimbali ya kutolea huduma katika Hospitali za Rufaa za Kanda** | | | | | | |
| **Na.** | **Hospitali Husika** | **Lengo la Mradi** | **Gharama za Mradi** | **Chanzo cha Fedha** | **Kiasi kilichotolewa** | **Hatua ya utekelezaji (%)** |
| 1 | Chato | **Awamu ya kwanza** OPD, | 16,072,813,776.31 | GOT | 16,072,813,776.31 | Asilimia 98 |

| Na. | Hospitali Husika | Lengo la Mradi | Gharama za Mradi | Chanzo cha Fedha | Kiasi kilichotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maabara, Pharmasia, EMD Upasuaji na ICU | | | | |
| | | **Awamu ya pili:** Radiologia na wodi za wagonjwa | 17,705,497,182.27 | GOT | 9,756,138,647.49 | Asilimia 70 |
| | | Awamu ya tatu ujenzi wa Nyumba 20 za watumishi | 1,143,582,899.00 | GOT | 1,092,842,899.00 | Asilimia 99 |
| | | Uzio (Fence) | 1,125,666,900.00 | GOT | 933,202,033.00 | Asilimia 85 |
| | | Njia za kupita wagonjwa (Walk ways) na Barabara za ndani ya eneo la Hospitali | 2,010,000,000 | GOT | 1,970,000,000.00 | Asilimia 86 |

| Na. | Hospitali Husika | Lengo la Mradi | Gharama za Mradi | Chanzo cha Fedha | Kiasi kilichotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ukarabati Mdogo kuwezesha usimikaji wa vifaa vya radilogia (MRI1, CT scan 1 na X-ray 1) | | IMF | | Vyumba viko tayari maboresho madogo yatakamilish wa wakati wa ufungaji mashine. |
| 2 | Kanda ya kusini Mtwara | Ujenzi wa jengo la OPD Complex kwa ajili ya huduma mbalimbali kwa ngazi ya Kanda. Upanuzi wa huduma utaendelea kwa kujenga majengo mengine kadri master plan ya hospitali | 16,488,012,643.02 | GOT&WB | 15,111,404,882.65 | Asilimia 98 |

| Na. | Hospitali Husika | Lengo la Mradi | Gharama za Mradi | Chanzo cha Fedha | Kiasi kilichotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | na upatikanaji wa fedha. | | | | |
| | | Ukarabati Mdogo kuwezesha usimikaji wa vifaa vya radilogia (MRI1, CT scan 1 na X-ray 1) | 40,000,000 | MFI | | Vyumba vipo katika jengo Jipya. Maboresho madogo yatafanyika wakati wa ufungaji mashine |
| 3 | Kanda ya Nyanda za juu - Mbeya | Ujenzi wa jengo la pekee kwa ajili ya Huduma za uzazi (Maternity Complex) unafanyika katika Hospitali ya Rufaa, Kanda ya Nyanda za juu Kusini Mbeya tawi la Meta. Jengo lina Ghorofa Sita | 9,392,191,914.99 | GOT | 9,392,191,914.99 | Asilimia 94 |
| | | Ukarabati Mkubwa wa eneo la ICU | 500,000,000.00 | | 497,920,186.71 | Asilimia 60 |
| | | Ukarabati wa EMD | | | | Asilimia 25 |
| 4 | Kanda ya ziwa - Bugando | Ujenzi wajengo la ghorofa nne la wodi maalumu ya Saratani | 5,400,000,000.00 | GOT&BMC | 1,990,000,000.00 | Asilimia 85 |
| | | Ukarabati Mkubwa wa ICU | 516,000,000.00 | IMF | 500,000,000.00 | Asilimia 30 |
| | | Ukarabati kwa ajili chumba cha X-Ray | | IMF | | Chumba kipo tayari |
| 5 | Kanda ya Kaskazini | Ujenzi wa Jengo la | 4,700,000,000.00 | GOT | 2,000,000,000.00 | Asilimia 60 |

| Na. | Hospitali Husika | Lengo la Mradi | Gharama za Mradi | Chanzo cha Fedha | Kiasi kilichotolewa | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | (KCMC) | huduma za tiba - Mionzi kwa matibu ya magonjwa ya cancer (Radiotherapy) | | | | |
| | | Ukarabti Mkubwa wa jengo la ICU | 499,318,800.00 | IMF | 499,318,800.00 | Asilimia 70 |
| 6 | Kanda ya Kati, Hospitali ya Benjamini Mkapa | Jengo la Tiba Mionzi (Radiotherapy) | 32,000,000,000.00 | GOT | | Asilimia 0 |
| | | Ukarabati Mkubwa wa eneo la ICU | 100,000,000.00 | IMF | 100,000,000.00 | Asilimia 90 |
| | | Ukarabati kwa ajili chumba cha X-Ray | | IMF | | Asilimia 90 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU HOSPITALI ZA KANDA** | | | **107,693,084,115.59** | | **59,915,833,140.15** | |
| **3: Ujenzi na Upanuzi wa Majengo mbalimbali ya kutolea huduma katika Hospitali Maalumu** | | | | | | |
| 1 | Kibong'oto | Ujenzi wa Maabara ya Kisasa (BSL 3) | 13,732,409,704.50 | GOT, WB & GF | 7,773,061,071.97 | Asilimia 96 |
| | | Ujenzi na ukarabati Mkubwa wa jengo la Radiologia kwa ajili ya kusimika CT Scan | 262,000,000.00 | ORIO | 262,000,000.00 | Asilimia 10 |
| | | Ukarabati Mkubwa na upanuzi wa wa jengo kwa ajili ya huduma za wagonjwa mahututi (ICU) | 350,000,000.00 | IMF | 350,000,000.00 | Asilimia 60 |
| 2 | Taasisi ya Moyo, | Ukarabati Mkubwa wa | 509,466,480 | IMF | 500,000,000.00 | Asilimia 60 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jakaya Kikwete (JKCI) | Jengo la ICU | | | | |
| 3 | Ocean Road | Ukarabati Mkubwa wa Jengo la ICU | 714,649,507 | IMF | 714,649,507.00 | Asilimia 60 |
| | | Ukarabati Mkubwa kwa ajili ya chumba cha kufunga MRI | 280,000,000 | IMF | 280,000,000.00 | Asilimia 60 |
| 4 | Mirembe | Ukarabati kwa ajili ya chumba cha X-ray na Ultrasound | | ORIO | | Asilimia 60 |
| | | Ujenzi na ukarabati mkubwa wa wodi na majengo mbalimbali ya Hospitali | 3,000,000,000 | IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD | 1,200,667,641 | IMF | 750,000,000.00 | Asilimia 40 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | na ICU | | | | |
| 5 | Ukerewe | Ujenzi wa jengo la OPD, RCH, Mortuary na Pharmacy | 3,000,000,000 | IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 10 |
| **JUMLA KUU HOSPITALI MAALUM** | | | **23,049,193,332.65** | | **16,629,710,578.97** | |

**4.0 UJENZI NA UKARABATI HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA**

**4.1 : Ujenzi wa Hospitali Mpya tano (Njombe, Simiyu, Geita, Songwe na Katavi)**

| Na. | Hospitali Husika | Lengo la Mradi | Gharama za Mradi | Chanzo cha Fedha | Kiasi kilichotolewa | Hatua ya Utekelezaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Njombe | Ujenzi unatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ilihusu ujenzi wa OPD ambalo kwa sasa linatumika, ujenzi wa awamu ya pili | 27,478,274,300.00 | GOT&GF | 22,192,716,800.00 | Asilimia 96 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | umehusisha majengo yafuatayo, Jengo la Afya ya uzazi (Maternity), EMD&ICU, Upasuaji & Mifupa na wodi, laundry, Damu Salama na Incinerator na nyumba tano za watumishi | | | | |
| | | Ujenzi wa jengo la CT Scan na nyumba 1 ya Mtumishi | 390,000,000.00 | IMF | | Asilimia 40 |
| 2 | Simiyu | Ujenzi wa Maternity Block | 5,774,992,393.00 | GOT&GF | 3,250,745,328.86 | Asilimia 80 |
| | | Ujenzi wa jengo la EMD na ICU | 1,210,000,000.00 | IMF | 1,210,000,000.00 | Asilimia 55 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ukarabati mdogo Chumba cha CT Scan na nyumba 1 ya Mtumishi | | IMF | | Vyumba vipo, ukarabati mdogo utafanyika wakati wa kufunga mashine |
| 3 | Geita | Ujenzi unatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ulianza ujezi wa OPD block (Ghorofa 1) Theatre &Radiology Block (Ghorofa 1) Laundry Building na jengo la Mgahawa (Cafeteria) | 8,612,994,260.00 | GOT | 8,612,994,260.00 | Asilimia 95 |
| | | Ujenzi wa Jengo la | 998,628,336.00 | GF | 998,628,336.00 | Asilimia 99 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maabara | | | | |
| | | Ujenzi wa Jengo la Afya ya Uzazi (Maternity Wing) | 6,999,848,824.00 | GOT & Global Fund | 3,865,986,022.39 | Baada ya Mradi kusimama hatua za kuendeleza mradi kupitia Mkandarasi mwingine ziko hatua ya kusainiwa Mkataba zinakamilishwa |
| | | Ujenzi wa jengo la EMD na ICU | 1,210,000,000.00 | IMF | 1,210,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Ukarabati mdogo Chumba cha CT Scan na nyumba 1 ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 55 |
| 4 | Songwe | Ujenzi wa Jengo la OPD | 6,246,443,640.00 | GOT | 6,246,443,640.00 | Asilimia 99. |
| | | Ujenzi wa Jengo la | 999,448,336.00 | GF | 999,448,336.00 | Asilimia 99 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maabara | | | | |
| | | Ujenzi wa jengo la wazazi (maternity) | 9,745,114,617.81 | GOT | 2,668,663,229.77 | Asilimia 22 |
| | | Ujenzi wa jengo la EMD na ICU | 1,210,000,000.00 | IMF | 1,210,000,000.00 | Asilimia 20 |
| | | Ujenzi wa Nyumba 1 ya Mtumishi na ukamilishaji wa chumba cha CT Scan na X-ray | 120,000,000.00 | IMF | Bado | |
| 5 | Katavi | Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa | 9,915,512,420.00 | GOT | 9,915,512,420.00 | Asilimia 72 |
| | | Ujenzi wa Maabara | 998,628,336.00 | GF | 998,628,336.00 | Mradi umekamilika na kukabidhiwa |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD | 1,188,849,798.00 | IMF | 860,000,000.00 | Asilimia 28 |
| | | Ujenzi wa Jengo la ICU | | IMF | | Asilimia 7 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Vyumba vya CT Scan na X-ray | 178,518,660.00 | IMF | 178,518,660.00 | Vyumba viko ndani ya jengo la Hospitali |
| **JUMLA KUU KUNDI LA 4.1** | | | **83,457,253,920.81** | | **64,598,285,369.02** | |
| **4.2: Ukarabati na upanuzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa iliyopokelewa kutoka OR-TAMISEMI mwaka 2017. ikijumuisha Singida, Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (Mara - Kwangwa), Shinyanga, Manyara, Mawenzi (Kilimanjaro), Mbeya RRH** | | | | | | |
| **Na.** | **Hospitali Husika** | **Lengo la Mradi** | **Gharama za Mradi** | **Chanzo cha Fedha** | **Kiasi kilichotolewa** | **Hatua ya utekelezaji (%)** |
| 1 | Singida | Ujenzi unatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya sasa ni kujenga sakafu ya chini jengo lenye ghorofa 3 kwa ajili ya wodi za kulaza wagonjwa | 19,525,525,130.75 | GOT & GF | 6,021,614,224.19 | Asilimia 70 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (Wards), vyumba vya upasuaji (Theatres), huduma za famasi (Pharmacy), huduma za maabara (Laboratory) na huduma za wagonjwa mahututi (ICU) | | | | |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD na ICU | 1,426,254,074.86 | IMF | 1,426,254,074.86 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Ukarabati Mkubwa kwa ajili vyumba vya radiologia (CT Scan na X-ray) | 66,696,678.00 | IMF | 66,696,678.00 | Asilimia 80 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Kwangwa-Mara | Ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwal. Nyerere Kwangwa - Mara ni jengo moja lenye sehemu ya kutolea huduma za wagonjwa wa nje, wagonjwa wa kulazwa, maabara, radiolojia, upasuaji, famasia na dharura. Ujenzi unaendelea vizuri ambapo tayari upande wa kitalu C umekabidhiwa na unatoa huduma. upande wa | 22,959,162,959.26 | GOT | 14,321,021,916.48 | Asilimia 95 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kitalu A na B bado vinaendelea kukamilishwa kwa ujumla, hatua ya awali ya mradi iko katika | | | | |
| | | Ujenzi wa Nyumba 1 ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | | Asilimia 40 |
| 3 | Shinyanga | Jengo la huduma za kupambana na ugonjwa wa UVIKO (Covid 19) linaendelea pamoja na maandalizi ya Jengo la Afya ya Uzazi | 2,071,850,094.32 | GOT&GF | 1,941,058,554,56 | Asilimia 97.5 |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD na ICU | 1,210,000,000.00 | IMF | 1,210,000,000.00 | Asilimia 65 |
| | | Ujenzi wa Jengo la Radiologia (CT | | | | Asilimia 10 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Scan na X-Ray) | | | | |
| | | Nyumba 1 ya Mtumishi | 400,000,000.00 | IMF | | Asilimia 10 |
| 4 | Manyara | Ukamilishaji wa Jengo la wagonjwa wa Nje (OPD) | 1,499,000,000.00 | GF | 1,499,000,000.00 | Asilimia 98 |
| | | Ujenzi wa Jengo la Damu Salama | 1,133,059,693.50 | GOT | 647,770,207.00 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD na ICU | 1,210,000,000.00 | IMF | 1,210,000,000.00 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa Jengo la CTScan na Nyumba 1 ya Mtumishi | | IMF | | Asilimia 40 |
| 5 | Mawenzi - Kilimanjaro | Ujenzi wa EMD | 764,995,975.00 | GF | 764,995,974.62 | Asilimia 99 |
| | | Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto | 6,434,028,320.00 | GOT & GF | 4,778,059,098.00 | Asilimia 70 |
| | | Ukarabati Mkubwa wa Jengo la ICU | 149,067,895.00 | IMF | 149,067,895.00 | Asilimia 55 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 25 |
| | | Ukarabati wa vyumba vya radiologia (CT scan na Nyumba 1 ya Mtumishi) | | IMF | | Vyumba vipo na ukamilishwaji unafanyika na Mkandarasi aliyeko site |
| 6 | Mbeya RRH | Ujenzi wa Jengo la EMD | 683,664,745.00 | GF | 683,664,745.00 | Asilimia 100 |
| | | Ujenzi wa jengo la upasuaji (theatre, ICU & CSSD) | 5,339,493,180.24 | GOT & GF | 5,339,493,180.24 | Asilimia 90 |
| | | Ukarabati Mkubwa wa Jengo la ICU | 150,000,000.00 | IMF | 150,000,000.00 | Asilimia 80 |
| | | Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 35 |
| | | Ujenzi wa Jengo la CTScan | | IMF | | Asilimia 10 |
| **JUMLA KUU KUNDI LA 4.2** | | | **65,382,798,745.93** | | **38,537,637,993.39** | |

| 4.3: Upanuzi wa majengo katika Hospitali ya Sekou Toure – Mwanza, Mwananyamala - Dar es Salaam, Ruvuma, Tanga, Maweni- Kigoma, Sumbawanga (Rukwa), Iringa, Kitete -Tabora, Dodoma, Sokoine Lindi, Mount Meru - Arusha, Temeke na Amana | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Hospitali Husika** | **Lengo la Mradi** | **Gharama za Mradi** | **Chanzo cha Fedha** | **Kiasi kilichotolewa** | **Hatua ya utekelezaji** |
| 1 | SekouToure (Mwanza) | Ujenzi wa Jengo la Afya ya Uzazi Ni ujenzi wa jengo la sakafu 5 | 10,106,468,902.31 | GOT | 9,876,453,413.53 | Asilimia 96 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Ukarabati wa chumba cha X-ray pamoja na ujenzi wa Nyumba 1 ya Mtumishi | 12,770,080.00 | IMF | 12,770,080.00 | Asilimia 60 |
| 2 | Mwananya mala | Ukamilishaji wa Jengo la Afya ya Uzazi lenye ghorofa 4 kutoa huduma zote mama na mtoto | 2,604,937,502.91 | GOT & GF | 2,604,937,502.91 | Asilimia 98 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD na ICU | 1,050,000,000.00 | IMF | 1,050,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Ukarabati wa chumba cha X-ray | 35,256,000.00 | IMF | | Asilimia 40 |
| 3 | Ruvuma | Ujenzi wa Jengo la huduma za Dharura (EMD) | 630,340,507.00 | GF | 630,340,507.00 | Umekamilika na kuanza kutumika |
| | | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) awamu ya kwanza katika eneo jipya la Hospitali ya mkoa | 3,000,000,000.00 | GOT & IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 30 |
| | | Ukarabati mkubwa wa jengo kwa ajili ya ICU Hospitali ya mkoa ya sasa | 169,246,500.00 | IMF | 152,000,000.00 | Asilimia 94 |
| | | Ujenzi wa Nyumba ya | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 30 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mtumishi | | | | |
| | | Ujenzi wa jengo la CT Scan | 271,079,500.20 | IMF | 271,079,500.20 | Asilimia 10 |
| 4 | BOMBO - Tanga | Ujenzi wa Jengo la Methadone | 736,705,586.00 | GF | 736,705,586.00 | Awamu ya kwanza imekamilika |
| | | Ujenzi wa Jengo la Damu Salama | 1,133,059,693.50 | GOT | 647,770,207.00 | Kusafishaji eneo la kufanya ujenzi |
| | | Ukarabati Mkubwa wa jengo la EMD na ICU | 250,000,000.00 | IMF | 250,000,000.00 | ICU asilimia 99<br>EMD asilimia 90 |
| | | Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Bado (Changamoto ya upatikanaji wa eneo) |
| | | ujenzi wa jengo la CT Scan | | IMF | | Asilimia 10 |
| 5 | Maweni - Kigoma | Ujenzi wa Jengo la Upasuaji | 619,255,321.00 | GF | 619,255,321.00 | Asilimia 100 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ujenzi wa Jengo la Damu Salama | 1,271,033,725.50 | GOT | 647,770,207.00 | Asilimia 60. |
| | | Ujenzi wa jengo la Mortuary na Upanuzi wa jengo la OPD na Maternity | 3,520,000,000.00 | GOT& IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 30 |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD na ICU | 1,335,348,000.00 | IMF | 1,210,000,000.00 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 50 |
| | | Ukarabati wa jengo la CT Scan | | IMF | | bado |
| 6 | Sumbawanga – Rukwa | Ujenzi wa Jengo la Damu Salama | 1,099,993,610.00 | GF | 1,099,993,610.00 | Asilimia 40 |
| | | Ukarabati mkubwa wa jengo la ICU | 247,141,173.00 | IMF | 247,141,173.00 | Asilimia 65 |
| | | Ujenzi wa Nyumba | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 40 |
| | | Upanuzi wa jengo kwa ajili | 205,386,339.60 | IMF | | Asilimia 10 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ya CTScan | | | | |
| 7 | Iringa | Ujenzi wa Jengo la huduma za Dharura (EMD) | 621,993,845 | GF | 621,993,845.00 | Asilimia 100 |
| | | Ukarabati Mkubwa wa Jengo la ICU | 150,000,000 | IMF | 150,000,000.00 | Asilimia 90 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi | 90,000,000 | IMF | 90,000,000.00 | Bado kuanza |
| | | Ujenzi wa Jengo la CT Scan | 271,079,500 | IMF | 271,079,500.20 | Asilimia 10 |
| 8 | Kitete - Tabora | Ujenzi wa Jengo la huduma za Dharura (EMD) | 604,870,350 | GF | 604,870,350.00 | Asilimia 98 |
| | | Ujenzi wa Jengo la Afya ya Uzazi (Maternity Block) awamu ya Kwanza | 6,735,155,134 | GOT & IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 35 |
| | | Ujenzi wa | 560,000,000 | IMF | 130,000,000.00 | Asilimia 45 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Jengo la ICU | | | | |
| | | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi | 90,000,000 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 38 |
| | | Ujenzi wa jengo la CT Scan | | IMF | | Asilimia 7 |
| 9 | Ligula Mtwara | Ukamilishaji wa Jengo la Upasuaji na Miundombinu ya majengo mengine ndani ya Hospitali | 1,000,000,000 | GOT | | Bado |
| | | Ujenzi wa Jengo la EMD na ICU | 1,177,489,386 | IMF | 860,000,000.00 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa Jengo la OPD | 3,000,000,000 | IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 5 |
| | | Ujenzi wa nyumba 1 ya Mtumishi | 90,000,000 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 25 |
| 10 | Dodoma | Ukarabati wa jengo la EMD | 103,235,987.00 | IMF | 100,000,000.00 | Asilimia 95 |
| | | Ujenzi wa Jengo la ICU | 725,006,257.00 | IMF | 560,000,000.00 | Asilimia 80 |
| | | Ujenzi wa | | IMF | | Asilimia 20 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | | 90,000,000.00 | |
| | | ujenzi wa jengo la CT Scan | 300,169,628.00 | IMF | 300,169,628.00 | Asilimia 7 |
| | | Ujenzi wa Kituo cha Kanda ya kati cha Damu Salama Dodoma | 1,702,065,625.00 | UNICEF | 1,157,404,625.00 | Asilimia 90 |
| 11 | Amana | Ukarabati wa ICU | 150,331,260.00 | IMF | 150,000,000.00 | Asilimia 98 |
| | | Ukarabati wa EMD | 457,204,904.00 | IMF & GOT | 120,000,000.00 | Asilimia 95 |
| | | Upanuzi wa jengo kwa ajili ya CT Scan na X-ray | 405,000,000.00 | IMF | | Asilimia 10 |
| 12 | Bukoba - Kagera | Ujenzi wa ICU | 561,000,000.00 | IMF | 560,000,000.00 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa EMD | 660,000,000.00 | IMF | 650,000,000.00 | Asilimia 45 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi na jengo la CT Scan | | IMF | | Bado kuanza |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 10 |
| 13 | Morogoro | Ujenzi wa ICU | 560,000,000.00 | IMF | 560,000,000.00 | Asilimia 65 |
| | | Ujenzi wa EMD | 650,000,000.00 | IMF | 650,000,000.00 | Asilimia 85 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi na | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 60 |
| | | Jengo la X-Ray | | IMF | | Asilimia 80 |
| 14 | Mount Meru Arusha | Ukarabati wa ICU | 194,831,505.00 | IMF | 194,831,505.00 | Asilimia 90 |
| | | Ukarabati wa EMD | 364,000,000.00 | IMF | 335,168,495.00 | Asilimia 80 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 50 |
| | | Ukarabati wa chumba cha CT Scan na X-Ray | 177,375,086.40 | IMF | 177,375,086.40 | Asilimia 80 |
| 15 | Sokoine - Lindi | Ujenzi wa ICU | 560,000,000.00 | IMF | 560,000,000.00 | Asilimia 30 |
| | | Ujenzi wa EMD | 650,000,000.00 | IMF | 650,000,000.00 | Asilimia 30 |
| | | Ujenzi wa | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 20 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | nyumba ya Mtumishi | | | | |
| | | Jengo la CT Scan | 231,280,000.00 | IMF | 231,280,000.00 | Ujenzi bado hujaanza |
| | | Ujenzi wa Jengo OPD | 3,000,000,000.00 | IMF | 3,000,000,000.00 | Asilimia 7 |
| 16 | Temeke | Ukarabati wa ICU | 180,000,000.00 | IMF | 180,000,000.00 | Asilimia 85 |
| | | Ukarabati wa EMD | 130,000,000.00 | IMF | 130,000,000.00 | Asilimia 97 |
| | | Upanuzi wa jengo kwa ajili ya CT Scan na X-ray | 338,495,909.50 | IMF | 338,495,909.50 | Asilimia 20 |
| 17 | Tumbi RRH | Ujenzi wa Jengo la Hospital kwa ajili ya huduma za EMD, Surgical Ward na OPD | | GOT | 3,900,000,000.00 | bado |
| | | Ukarabatai wa EMD | 360,666,416.00 | IMF | 360,666,416.00 | Asilimia 90 |
| | | Ukarabati wa ICU | 326,819,148.00 | IMF | 326,819,148.00 | Asilimia 98 |
| | | Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 | IMF | 90,000,000.00 | Asilimia 35 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ukarabati wa chumba cha CT Scan | 163,022,664.00 | IMF | 163,022,664.00 | Asilimia 55 |
| **JUMLA KUU KUNDI LA 4.3** | | | **56,629,115,045.75** | | **51,309,394,279.74** | |
| **5: Ujenzi na Upanuzi wa Majengo mbalimbali ya kutolea huduma katika Vituo Maalumu** | | | | | | |
| **Na.** | **Kituo Husika** | **Lengo la Mradi** | **Gharama za Mradi** | **Chanzo cha Fedha** | **Kiasi kilichotolewa** | **Hatua ya utekelezaji (%)** |
| 1 | Chanjo, IVD Mabibo | Ukarabati, Upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya kuhifahia Chanjo - IVD Mabibo | 1,388,682,288.50 | CHAI /GAV | 374,485,879.56 | Asilimia 52 |
| 2 | Elimu ya Afya kwa Umma | Ujenzi wa kituo cha Kisasa (Health Promotion services) ambapo jengo linaloanza kujengwa ni Jengo la Uchapishaji (Printing and Press | 2,184,000,000 | IMF | 2,184,000,000.00 | Hatua za awali, maandalizi ya Ujenzi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Building) | | | | |
| 3 | Kituo cha Umahiri kwa Magonjwa hatarishi na Milipuko - Kisopwa Dar es Salaam | Ujenzi wa Kituo cha Umahiri kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na Milipuko | 7,776,000,000 | GOT & IMF | 2,900,000,000.00 | Asilimia 25 |
| **JUMLA KUU 5** | | | **11,348,682,288.50** | | **5,458,485,879.56** | |
| **6: Ujenzi na Upanuzi wa Majengo mbalimbali ya kutolea huduma za Mafunzo, Vyuo vya Afya** | | | | | | |
| **Na.** | **Hospitali Husika** | **Lengo la Mradi** | **Gharama za Mradi** | **Chanzo cha Fedha** | **Kiasi kilichotolewa** | **Hatua ya utekelezaji (%)** |
| 1 | Tabora Clinical Officers Training Centre | Ujenzi wa Jengo la Wodi Maalum (Private wards) | 261,651,078.35 | BSF | 261,651,078.35 | Asilimia 75 |
| 2 | Ngudu Environmental Health School | Ukarabati Mkubwa wa majengo mbalimbali ndani ya chuo | 419,538,606.28 | BSF | 419,538,606.28 | Asilimia 90 |

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, na kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati na kuendelea na utaratibu wetu nitaleta matangazo. Waheshimiwa Wabunge nilete matangazo tuliyonayo hapa mbele. Kwanza ni tangazo la wageni, tutaanza na wageni walioko jukwaa la Spika.

Kwanza ni wageni 12 kutoka Baraza la Taifa la watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi *NACOPHA* wakiongozwa na ndugu Leticia Mourice ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi; karibuni sana sana. Lakini pia ameongozana na Afisa Mtendaji Mkuu wa *NACOPHA* ambaye ni ndugu Deogratius Rutatwa, karibuni sana ndugu zetu kutoka *NACOPHA*.

Lakini pia wapo wageni wangu 16 ambao ni viongozi wa Asasi za Kiraia katika Sekta ya afya chini ya mfuko wa Mkapa *Foundation* wakiongozwa na mwenyekiti wao ndugu Rahim Naseer, karibuni sana.

Ninaye pia mgeni mwingine ambaye ni Dkt. Sebastian Ndege Mkurugenzi Mtendaji wa Jembe *Group*, kutoka Jijini Dar es Salaam karibu sana.

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa Afya, na hawa ni Prof. Abel Nkono Makubi ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana yupo pia Dkt. Aifello Sichalwe ambaye ni Mganga Mkuu wa Serikali, karibu

sana. Mheshimiwa Ummy Mwalimu pia ameambatana na Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo wa Wizara ya Afya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara Mameneja wa Miradi na Wasajili wa Mabaraza ya kitaaluma hawa wasimame wote kwa pamoja karibuni sana Bungeni.

Lakini pia wapo wahisani 15 wa maendeleo katika sekta ya afya wakiongozwa na Dkt. Jema Bisimba ambaye ni Mwenyekiti wa kundi la wadau wa afya *USAID*. Kwa hiyo wadau wote wa afya ama wahisani wote msimame wote kwa pamoja. Sasa wengine huenda hawasikii kiswahili lakini *Development Partners in the Health Sector if you could all stand together in the same group.* Haya naamini ni nyie peke yenu; ahsanteni sana.

Wapo wawakilishi 16 wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali wakiongozwa na Dkt. Ellen Mkondya Senkoro ambaye anawakilisha kundi la NGO’s ndani ya nchi. Sijui wako upande gani? Karibuni sana, naona ni wale ambao walishatambulishwa.

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt Godwin Mollel ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, na hawa ni viongozi wa *Dorice Mollel Foundation* wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa *Doris Mollel Foundation* ambaye pia ni mwanzilishi wa Taasisi hiyo Doris Mollel, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Mollel ambao ni wadau saba wa sekta ya

afya kutoka Shirika la *FREO 2* kutoka Australia wakiongozwa na Dkt. Roger Rassol ambaye ni Rais na Mwanzilishi wa *FREO 2* karibuni sana wageni wetu.

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge ambaye ni Mhadhiri wa Chuo cha Uhasibu Arusha *(IAA)* Dkt Solomon Muguba, karibu sana.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Judith Kapinga ambao ni ujumbe wa viongozi wa dini Tanzania, kamati ya viongozi wa dini kutoka mkoa wa Geita na Jijini Dar es Salaam, karibuni sana.

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni wapiga kura wake na wafanyabiashara wa Soko la Makumbusho kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na mfanyabiashara Selemani Kulele, karibuni sana.

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambao ni wanafunzi na walimu wa Chuo cha Boboya East Africa kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana.

Tunao wageni wengine 11 wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni wafanyakazi wa *Fifty-six Hotel* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana.

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni viongozi wa TWARIQA kutoka Jijini Arusha wakiongozwa na Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Arusha Amini Hatibu Mushi, karibuni sana.

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Bonah Kamoli ambao ni wanafunzi ambao alisoma nao pamoja Chuo cha Diplomasia Kozi ya *Postgraduate in Management of Foreign Relations* mwaka 2013/2014, karibuni sana.

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Joseph Thadayo ambaye ni Mhasibu mapato wa halmashauri ya wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro ndugu Dialo Mahinya, karibu sana.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Oscar Kikoyo ambaye ni mzee Rusticus Anjelo Nshekerwa kutoka Kijiji cha Rubya Wilayani Muleba ambaye pia ni baba wa mtumishi wa Bunge Ndugu Prudence Rweyongeza; naona mtumishi wetu amekaa pale na baba yake, karibu sana.

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni Mkurugenzi wa Media *Assistant Company* ndugu Henry Mdimu kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambaye ni ndugu Meshack Mollel kutoka *Path Finder International* ya Jijini Dodoma, karibu sana.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba ambaye mama ni yake mdogo kutoka Jijini Mwanza ndugu Shamsa Shigela, karibu sana.

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Agnes Hokororo ambaye ni ndugu yake kutoka Mtwara mjini ndugu Asha Moto, karibu sana.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya kwa mafunzo viongozi 15 wa Shirikisho la Walimu Taifa Tawi la Hai mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Mwl. Kiwele Iwvata, karibuni sana.

Tunao viongozi wa *The Nelson Mandela African Institute of Science* cha mkoani Arusha wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Emmanuel Luoga, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge hawa ndiyo wageni tulionao Bungeni siku ya leo, lakini yako matangazo mengine hapa. Kwanza ni tangazo kutoka kwa Waziri wa Elimu Prof. Adolf Mkenda, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mnaalikwa katika ufunguzi wa mashindano ya *MAKISATU* yanayofanyika leo saa 8.00 mchana katika uwanja wa Jamhuri. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana kwenye ufunguzi huo.

Lakini pia lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba leo

kutakuwa na semina kuhusu maboresho ya Sera ya Ubia na mapitio ya Mpango Mkakati wa kuboresha Muundo na utendaji kazi wa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*. Semina hii imeandaliwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hii muhimu sana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tukitoka hapa wote tutaelekea ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya mafunzo hayo.

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine, hili tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba siku ya Jumamosi tarehe 14 Mei 2022 kulikuwa na mchezo kati ya *Bunge Sports Club* na Iringa *Veterans* kwenye uwanja wa Jamhuri na *Fountain Gate Academy*. Kwanza ni matokeo ya mpira wa miguu, *Bunge Sports Club* hawakupata goli lolote lakini pia Iringa *Veterans* hawakupata goli lolote japokuwa kuna nyota wa mchezo Mheshimiwa Haji Mlenge, ndiye alikuwa nyota wa mchezo japokuwa hakupewa nafasi ya kutetema maana hata yeye hakuchezesha nyavu. (*Makofi*)

Lakini pia yapo matokeo ya mpira wa peteambapo Bunge *Queens* walipata magoli 31 Iringa Veterans magoli 27, nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Waheshimiwa Wabunge *Bunge Sports Club* inawashukuru Wabunge wote kwa kujitokeza kwenye michezo hii lakini pia na watumishi wa Bunge walioenda kuwaunga mkono, ahsanteni sana.

Lipo tangazo lingine ambalo limetolewa na Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kwamba Chuo cha Nelson Mandela wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo ambaye tumetoka kumtangaza hapa wapo katika viwanja vya Bunge nyuma ya jengo la Msekwa kwa ajili ya kuonesha dawa tiba ambazo wamezalisha.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa kwenda kuwatembelea mzione dawa hizo, lakini mzitumie na pia maelezo mtakayoyapata yatasaidia sana kwenye kuishauri Serikali kwenye eneo hili.

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine linalohusu mabadiliko ya ratiba yetu ya Bunge hili. Siku ya tarehe 13 Mei, 2022, tulikutana Kamati ya Uongozi na kufanya mabadiliko kwenye ile ratiba ambayo mlikuwa mmegawiwa mwanzo. Mabadiliko hayo yanaathiri siku ya bajeti, lakini pia siku ya kupiga kura hapa ndani. Sababu ya mabadiliko hayo ni kwamba tunayo makubaliano ya Nchi za Afrika Mashariki kusoma bajeti kwa siku moja. Sasa kwa mwaka huu 2022 kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2022/2023, Nchi za Afrika Mashariki zimekubaliana kusoma bajeti siku ya tarehe 14.

Sisi tulikuwa tumepanga bajeti isomwe tarehe 16, kwa hivyo inarudi siku moja nyuma. Kwa hivyo inaathiri bajeti nyingine za kisekta, siku zilizokuwa zimepangiwa, bajeti nyingine zilikuwa zimepangiwa zaidi ya siku moja na hizo bajeti nyingine zilikuwa ziende mpaka siku ya tarehe 15. Kwa

hivyo ratiba yetu itakuwa na mabadiliko kidogo, kwa hivyo badala ya kusoma bajeti kuu siku ya Alhamisi tarehe 16 Juni, 2022, itasomwa siku ya tarehe 14 Juni, 2022. Tumezoea kusoma bajeti yetu siku ya Alhamisi, siku hii haitakuwa Alhamisi itakuwa siku ya Jumanne. Kwa hivyo, siku ya Jumatano ambayo itakuwa ni siku ya tarehe 15 ni ile siku ambayo Wabunge wanapewa nafasi ya kusoma bajeti ili tuanze uchangiaji. Kwa hivyo uchangiaji utaanza tarehe 16, siku ya tarehe 15 mtapewa nafasi kwa ajili ya kujisomea.

Wizara mbalimbali zimeshataarifiwa kuhusu mabadiliko haya na pia Kamati zetu za Bunge ambazo zinatakiwa kuwasilisha taarifa zao sambamba na hizi za Wizara nazo zinajiandaa vilivyo kwa ajili ya mabadiliko haya ya ratiba.

Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko haya mtawekewa kwenye vishkwambi vyenu, lakini ni muhimu kufahamu kwamba sasa tarehe ya kupiga kura pia itakuwa imebadilika ambayo itawataka Wabunge wote wawepo Dodoma. Sasa badala ya kupiga kura siku ya tarehe 28 iliyokuwa imetajwa kwanza, sasa kura itahitimishwa siku ya tarehe 24 Juni, 2022. Kwa hiyo siku hiyo ya tarehe 24 Juni, 2022 kila Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atatakiwa kuwepo Bungeni kwa sababu utaratibu wa kura ya Bajeti ni wa kura ya wazi na unaitwa jina moja baada ya lingine.

Waheshimiwa Wabunge haya ndio matangazo niliyokuwa nayo siku ya leo. Hata hivyo, lipo jambo lingine la muhimu sana ambalo linaendelea katika Taifa letu na nitumie

fursa hii kulisema hilo pia halafu tutaendelea na ratiba yetu. Waheshimiwa Wabunge usiku wa tarehe 11 Mei, 2022 kupitia mitandao ya kijamii tulipata taarifa kwamba Baraza Kuu la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) limeazimia kukubaliana na uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA wa kuwafukuza wanachama Wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia chama hicho.

Siku ya tarehe 12 Mei, 2022, saa saba na dakika kumi na tano na sekunde thelathini na nane mchana kwa njia ya barua pepe, nilipokea barua za Wabunge hawa 19 wakinifahamisha kuwa maamuzi yaliyofikiwa na Baraza Kuu la CHADEMA la kuwavua uanachama wa CHADEMA kwa sababu ya vitendo vyao vya kuteuliwa na kukubali kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwanza kwa maana ya (a) si halali, (b) ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na (c) hayakuzingatia haki ya msingi ya kuwasikiliza ama kuruhusu kujitetea. Kwa mantiki hiyo Wabunge hao wamepinga uamuzi huo na mwenendo mzima wa maamuzi yaliyofanyika ndani ya Chama katika Mahakama Kuu ya Tanzania Dar es Salaam kupitia shauri namba 16 la mwaka 2022 *Miscellaneous Course*, *No. 16 of* 2022, dhidi ya Baraza la Wadhamini wa CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Tarehe hiyo hiyo 12 Mei, 2022 saa tisa na nusu alasiri, Afisa wa CHADEMA aliyejitambulisha kwa jina moja la

Meshack alifika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam kwa ajili ya kuleta barua kwa Spika, alipofika alielezwa na Mlinzi wa Bunge asubiri wafanye mawasiliano kama wanaruhusiwa kupokea barua hiyo kwa kuwa wakati wa Bunge Maafisa wote wa Ofisi ya Dar es Salaam huwa wanakuwa Dodoma. Wakati walinzi wanafanya mawasiliano hayo Afisa huyo wa CHADEMA aliondoka bila kukabidhi barua hiyo. Hii ni baada ya kupata maelezo ya viongozi wa CHADEMA kwa simu kuwa wahusika hawawezi kupokea barua hiyo aondoke na watafanya utaratibu mwingine wa kuituma Dodoma.

Aidha, saa tisa na dakika kumi na tano na sekunde ishirini na nne mchana na saa tisa na dakika kumi na tisa na sekunde arobaini na moja mchana kupitia barua pepe tulipokea barua yenye Kumbukumbu Namba *C/HQ/ADM/PAR/33/37* iliyosainiwa na John J. Mnyika, Katibu Mkuu wa CHADEMA. Pamoja na mambo mengine barua hiyo ilinijulisha kwamba katika kikao chake cha Tarehe 11 Mei, 2022, Baraza Kuu la CHADEMA lilipokea na kujadili rufaa za walioitwa waliokuwa wanachama 19 ambapo walikata rufaa dhidi ya uamuzi wa Kamati kuu wa tarehe 27 Novemba, 2020 na kwamba Baraza Kuu la Chama hicho kwa mujibu wa Ibara ya 7.7.12(f) ya Katiba ya CHADEMA ya mwaka 2006, Toleo la Mwaka 2019 limeazimia kukubaliana na uamuzi wa Kamati kuu ya CHADEMA wa tarehe 17 Novemba, 2020. Hivyo, waliokuwa wanachama wa CHADEMA wameendelea kukosa sifa za kudaiwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini ya Chama hicho

kwamba itaufanyia kazi uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kwa kujibu ya Katiba na Sheria za nchi.

Waheshimiwa Wabunge tarehe 13 Mei, 2022, saa mbili na dakika arobaini na mbili asubuhi barua hiyo hiyo ililetwa kwa mkono ofisi kwangu Dodoma na Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, Ndugu Singo Kigaila. Aidha, tarehe hiyo hiyo 13 Mei, 2022, saa sita na dakika hamsini na tatu mchana, barua hiyo iliwasilishwa tena kwangu kwa njia ya *DHL* kwa mujibu ya Katiba yetu Mamlaka yenye kauli ya mwisho…

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Katiba yetu mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mahakama. Hivyo katika nchi yenye kuongozwa na misingi ya Sheria na kuheshimiana kati ya mhimili mmoja na mwingine Bunge haliwezi kuingilia mchakato wa Mahakama na badala yake inalazimika kusubiri. *(Makofi)*

Narejea tena Bunge haliwezi kuingilia mchakato wa Mahakama na badala yake linalazimika kusubiri hadi hapo Mahakama itakapotoa uamuzi wake kuhusu jambo hilo. *(Makofi)*

Kama nilivyoeleza hapo juu, Wabunge hao 19 walinitaarifu mapema tarehe 12 Mei, 2022, kabla sijapokea taarifa yoyote rasmi kutoka CHADEMA kwamba wamekwenda mahakamani kwa ajili ya kulinda haki zao binafsi kama wanachama halali wa CHADEMA na Wabunge,

pamoja na kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura Namba 343 ambayo iliwafanya wao kwa Wabunge wa Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge lazima tufahamu maelezo haya yanatolewa kwa mujibu wa Katiba yetu, lakini pia sheria tulizozitunga sisi kama Bunge. Hivyo kwa kuzingatia misingi ya Katiba niliyoieleza, nalazimika kutotangaza kwamba nafasi za viti Maalum 19 za CHADEMA zipo wazi hadi hapo Mahakama itakapokamilisha kazi yake ya kutoa uamuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio maelezo yangu kuhusu jambo hili linaloendelea na ikiwa kutakuwa na maswali yoyote msemaji wa jambo hili kuhusu Wabunge hawa ni Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuzungumza hayo sasa tunaendelea na ratiba yetu nimwite Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii aje atusomee mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, natoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa

Majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

(i) Maelezo na uchambuzi kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(ii) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(iii) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yaani Makadirio ya Maduhuli na Matumizi.

(iv) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo

iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati ilipata wasaa wa kukagua Mradi wa Ujenzi na Upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya, Mradi Namba 5411 ulio na miradi mingine midogomidogo mitatu ndani ambayo ni Mradi wa Jengo la Upasuaji, Mradi wa Ukarabati wa Wodi ya Wagonjwa Mahtuti na Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Huduma za Dharura.

Mheshimiwa Spika, baada ya ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilifanya tathmini na kutoa maoni yake kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha na upatikanaji wa dawa usioridhisha. Kamati pia ilitoa maoni kuhusu upungufu wa watumishi, ufinyu wa maeneo na ukosefu wa vifaa tiba katika hospitali hii kama inavyoonekana katika taarifa kubwa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya Wizara kuwasilisha Bajeti yake ya Fungu 52 hapo tarehe 29 Machi, 2022, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara ya mwaka 2021/2022, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo tisa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inapongeza sana Serikali kwa kufanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati iliendelea kuyasisitiza

katika taarifa hii ikiwemo suala la Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na upatikanaji wa dawa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Fungu Namba 52 katika mwaka wa fedha 2021/2022, ilikadiria kukusanya maduhuli ya Shilingi bilioni 507.2, ambapo hadi Mwezi Februari 2022, jumla ya Shilingi bilioni 362.3 zilikuwa zimekusanywa, sawa na asilimia 71.4 ya lengo la makusanyo. Kama ilivyoonekana kwenye kielelezo Na.1.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022; katika bajeti ya mwaka 2021/2022, iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni 2021, Wizara kupitia Fungu Namba 52 iliidhinishiwa Jumla ya Shilingi trilioni 1.03. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 557.3 sawa na asilimia 53.89 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 476.8 sawa na asilimia 46.1 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, kama inavyoonekana katika kielelezo tulichokitoa Na.2.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa, kufikia Februari, 2022, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni 617.7, sawa na asilimia 60 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu Namba 52. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 397.9, sawa na asilimia 64.4 ni za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 219.7 sawa na asilimia 35.7 ya fedha zilizopokelewa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na.3 tulichokitoa.

Mheshimiwa Spika, pia katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2022, Wizara ilipokea Shilingi bilioni 205.01, sawa na asilimia 77.7 ya Shilingi bilioni 263.7 ambayo ni nyongeza ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Fungu 52 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Nyongeza hii inafanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wizara hii kuwa Shilingi trilioni 1.29. Aidha, fedha za nyongeza zilizoidhinishwa zinafanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo kwa Wizara hii kuwa Shilingi bilioni 740.5 sawa na asilimia 57 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa Wizara hii, kama inavyoonekana kwenye Jedwali au kiambatisho Na.4.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nyongeza hiyo, jumla ya fedha zilizopokewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni Shilingi bilioni 424.7. Hivyo, nyongeza ya bajeti inafanya jumla ya fedha zote zilizopokewa hadi Februari, 2022 kuwa Shilingi bilioni 822.7, sawa na asilimia 63.3.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa upokeaji wa jumla wa fedha ulifikia asilimia 60 ambapo, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa kwa asilimia 64.34 na fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zimepokelewa kwa asilimia 35.7 ya fedha zote zilizopokelewa. Kamati inaona kuwa kiwango hiki cha upokeaji wa fedha hakiwiani na wastani uliotarajiwa kutolewa kwa Wizara. Kamati inasisitiza fedha, hasa za miradi ya maendeleo, zitolewe kwa wakati ili miradi iliyopangwa kutekelezwa basi ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya ripoti yangu inasema kuwa Uchambuzi wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Fungu Namba 52 katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni Shilingi bilioni 622.98. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko la Shilingi 115.7 la makadirio ya makusanyo ya matumizi katika mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 18.8 ya Shilingi bilioni 507.2 zilizokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ongezeko hilo linaonekana kwenye vyanzo vya ndani vya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, makusanyo kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa yamepungua kwa asilimia 6.8 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati imeendelea kubaini kushuka kwa makadirio ya mapato kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa miaka miwili mfululizo. Kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. Sita. Kamati ilielezwa sababu za kushuka huko ni kutokana na hospitali hizo kuanza kuandaa bajeti za makusanyo ya ndani kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyao. Ni ushauri wa Kamati kwa Wizara kutenga makusanyo yenye uhalisia. Pia, ilisisitiza Serikali kuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli hayo katika hospitali, Wizara na Taasisi zake ili kuzuia uvujaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati ikachambua Makadirio na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo: - (a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara Fungu Namba 52 kwa ulinganifu wa mwaka 2021/2022 yaani 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa katika randama ya Fungu Namba 52, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Shilingi Trilioni 1.109. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 554.2 sawa na asilimia 49.96 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni 555.1 sawa na asilimia 50.04 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye kielelezo tulichokitoa Namba (7).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Fungu Namba 52 imeongezeka kwa asilimia 7.3 kutoka Shilingi Trilioni 1.03 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi Trilioni 1.109 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la asilimia 7.6 kwenye bajeti ya maendeleo. Pili, kwa upande wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa asilimia 5.7 wakati fedha za nje zikiwa zimeongezeka kwa asilimia 1.9. Kamati ilielezwa sababu ya ongezeko hilo ni kutokana na mahitaji ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ili ianze kutoa huduma. Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda Maalum na Taifa, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba,

na vitendanishi katika ngazi zote za huduma za afya na kuimarisha matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yote muhimu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida imepungua kwa asilimia 0.3. Kamati ilielezwa upungufu wa fedha za matumizi hayo ni kutokana na kutengwa kwa fedha za watarajali *(interns)* katika Bajeti ya Maendeleo ambazo awali zilikuwa zinatengwa katika bajeti ya Matumizi Kawaida yaani *OC*.

Mheshimiwa Spika, kielelezo Namba Tisa na Namba Kumi zinaeleza zaidi juu ya ulinganifu wa makadirio ya Bajeti ya Fungu Namba 52 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023 ambacho ni kipengele B. Uchambuzi huu wa Kamati ulilenga kubaini athari za Bajeti za Mpango wa Maendeleo wa Taifa dhidi ya Bajeti ya Fungu 52. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, wakati Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2022/2023 imeongezeka kwa asilimia 8.1, bajeti ya Fungu Namba 52 ya Wizara hii imeongezeka kwa asilimia 7.3. Pili, wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo ikiwa imeongezeka

kwa asilimia 3.6, bajeti ya Fungu Namba 52 kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia 7.6. Tatu, wakati bajeti ya Taifa ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa asilimia 11, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Fungu Namba 52 imepungua asilimia 0.54.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba, ongezeko la bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa linawiana na ongezeko la bajeti ya Wizara hii Fungu Namba 52 kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Namba 11, 12 na hii inaonesha kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kipaumbele katika tengeo la fedha za bajeti. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ongezeko hilo la tengeo katika sekta hii muhimu inayogusa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye Maoni, Ushauri na Mapaendekezo ya Kamati. Baada ya uchambuzi wa bajeti, kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji wa Kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni uhaba wa dawa nchini. Upatikanaji wa dawa nchini bado ni changamoto. Kamati inafahamu kuwa kuimarika kwa huduma ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini ni pamoja na kipaumbele cha Wizara hii. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa dawa nchini siyo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha Shilingi Bilioni 218.1kiliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya dawa. Hadi kufikia Februari, 2022 ni asilimia 63.1 tu ya fedha ndizo zilikuwa zimepokelewa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, bajeti ya dawa imepungua kwa asilimia 8.29 hadi kufikia Bilioni 200. Maelezo ya Wizara ni kuwa kupungua kwa bajeti hiyo kunatokana na kiasi hicho kutengwa kwenye bajeti ya ufuatiliaji na usimamizi wa bidhaa hizo. Hata hivyo Kamati imeshuhudia upungufu wa dawa katika hospitali mbalimbali nchini na kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo: -

Kwanza, bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utolewaji na usambazaji wa dawa itolewe yote kwa wakati ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa ili kuokoa maisha ya Watanzania wanaopata huduma katika hospitali zetu.

Pili, Serikali itazame upya mifumo ya usambazaji wa dawa inayotumiwa na *MSD* ili kutatua changamoto zinazotokana na usambazaji. Mifumo ya kielektroniki iwekwe katika vituo vya kutolea huduma za afya ili idhibiti upotevu wa dawa.

Mheshimiwa Spika, Tatu, aidha, Kamati inashauri Wizara kuweka mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya kununua dawa pasipo ushauri wa madaktari. Kamati pia inashauri Wizara kuweka utaratibu wa usimamizi

mzuri kwenye maduka yanayouza dawa za binadamu ili kuondoa matumizi ya dawa yasiyo sahihi kwa wananchi.

Nne, ili kupunguza matumizi ya fedha nyingi kwenye ununuzi wa dawa, Kamati inaishauri Serikali kuipitia upya sheria ya manunuzi ambayo imekuwa mkwamo na ikiongeza gharama kwenye manunuzi ya vitu mbalimbali vya Serikali ikiwemo dawa na vifaatiba.

Mwisho sehemu ya Tano, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia makusanyo ya fedha za mauzo ya dawa nchini kwa kuweka mikakati madhubuti wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato yanayotokana na dawa.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ulikuwa ni uimarishaji wa Hospitali za Kitaifa na Rufaa Nchini. Hospitali za Kitaifa pamoja na Hospitali za Rufaa nchini zimekuwa zikiendelea kuboreshwa kwa kiwango cha Kimataifa. Kwa sasa hospitali kama Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete inapokea wagonjwa kutoka mataifa mbalimbali kama vile Burundi, Uganda na Kenya. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ajili ya uboreshaji huu wa miundombinu na huduma katika hospitali hizi za Kitaifa. Hata hivyo, uboreshaji wa hospitali hizi haujafikia kiwango cha kuridhisha. Hivyo basi, katika hili Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iimarishe huduma za afya katika hospitali hizi kwa kuajiri wataalam wabobevu zaidi;

(ii) Serikali iboreshe zaidi upatikanaji wa vifaatiba vitakavyowezesha huduma za magonjwa sugu kama moyo, figo nakadhalika ambayo wananchi wengi wamekuwa wakifuata matibabu yake nje ya nchi;

(iii) Kwa kuwa sasa hospitali hizi zinapokea wagonjwa kutoka nje ya nchi, Serikali itoe msukumo katika kutangaza au utangazaji wa huduma hizi bora katika mataifa mbalimbali ikiwezesha utalii wa kimatibabu *(medical tourism)* kwa ajili ya kuongeza Pato la Taifa na kuhudumia wahitaji wa huduma za afya. Aidha Serikali iweke mikakati mizuri ya kuvutia utalii wa kimatibabu *(medical tourism)*.

Mheshimiwa Spika, jingine ni suala la bima kwa wote. Ni ushauri wa muda mrefu wa Kamati kuimarisha mfumo wa Bima ya Afya nchini ili bima hiyo ya afya itolewe kwa watu wote. Katika kuharakisha hilo kamati ilishauri juu ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na utoaji wa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa majibu ya hoja za Kamati 2021/2022 iliieleza Kamati kuwa tayari Shilingi Milioni 231 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na utoaji wa elimu kwa umma. Kwa kuwa Serikali bado inapokea maoni na

kuboresha mfumo huo Kamati inashauri sasa kuzingatia mambo yafuatayo: -

Moja, wananchi washirikishwe vya kutosha ili kutoa maoni yao katika kuboresha muswada huo;

Pili, Serikali ione namna ya kushirikisha Sekta Binafsi nchini katika kutoa Huduma ya Bima ya Afya;

Tatu, kumekuwepo na malalamiko kwa wateja wa *NHIF* kukosa baadhi ya huduma zikiwemo dawa, Wizara isimamie kuondoa changamoto hii kwa kuiimarisha zaidi *MSD* pamoja *na NHIF*;

Nne, Serikali iiwezeshe *NHIF* katika kuratibu na kutekeleza mpango wa kuanzisha Bima ya Afya kwa wote;

Tano, vifurushi vya Bima ya Afya kwa wote viwe vyenye uhalisia ili kutoruhusu mfuko kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, jingine ni Uhaba wa Rasilimali watu. Rasilimali watu imekuwa ni changamoto katika hospitali na taasisi nyingi za afya nchini. Katika kupunguza changamoto hii Serikali kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 imeahidi kuajiri watumishi 10,285 wa kada mbalimbali za afya watakaopelekwa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati kwenye Serikali za Mitaa na Hospitali za

Kanda yaani Rufaa, Vituo vya Afya na Hospitali zingine za kimkakati kama vile *DDH*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambapo inaamini itaenda kutatua chagamoto hii ya upungufu wa watumishi katika sekta hii muhimu. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ajira hizi zizingatie mgawanyo wa kijiografia na uhitaji wa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, suala linguine ni Taasisi ya Saratani ya Ocean Road. Kamati inaipongeza Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa mashine ya Cyclotrone ambao unatarajia kuanza kutumika rasmi 01Julai,2022. Kamati inaamini mradi huu ukikamilika utasaidia kugundua ugonjwa wa saratani ukiwa katika hatua za awali na hivyo kusaidia kupunguza madhara yanayosababishwa na maradhi ya saratani. Mradi huu ni moja kati ya miradi muhimu na upo katika nchi chache duniani.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ukikamilika utasaidia kuvutia watu kutoka katika Mataifa mbalimbali kuja katika taasisi hii na kuwa sehemu ya utalii wa kimatibabu na hata hivyo kuhudumia watu wengi na kujiongezea Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, jingine tumeshauri Upatikanaji wa Damu Salama na vilevile tumezungumzia na ugonjwa wa virusi vya *Corona,* Serikali iendelee na juhudi inazozifanya na vilevile tumezungumzia kuhusiana na masuala ya magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nichukue fursa hii nihitimishe kwa kusema kwamba, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuongoza vema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu Mbunge, Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel Mbunge, Naibu Waziri kwa ushirikiano wanaonipa katika Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Afya, *Professor* Abel Makubi, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Seif Shekilage na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Aifello Sichalwe pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati nilitamani niwataje wote wa Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapakazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Nawapongeza sana na naomba majina haya yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu Ndugu Nenelwa Mwihambi, *(ndc)* kwa kuiwezesha Kamati

kutekeleza majukumu yake vema. Pamoja nae namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa katika Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Francisca Haule, Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Emmanuel Mdidi na Ndugu Chacha Nyakega pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja, Fungu Namba 52 jumla ya shilingi 1,109,421,722,000.00.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

(v) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(vi) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(vii) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(viii) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata wasaa wa kukagua mradi wa Upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya wenye **Namba ya Mradi 5411** ulio na miradi midogomidogo mitatu ndani yake. Hali ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

*2.1 MRADI WA JENGO LA UPASUAJI*

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu wa Jengo la Upasuaji ambao Kamati iliutembelea mnamo tarehe 18 Machi, 2022 unahusu ujenzi wa jengo maalum litakalotumika kwa ajili ya upasuaji. Katika Mwaka 2021/2022 mradi huu ulitengewa fedha za ujenzi kiasi cha **Shilingi 3,000,000,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Serikali ilitoa jumla ya **Shilingi 870,319,075.62** kwaajili ya kugharamia mradi huu; sawa na **asilimia 29**. Hata hivyo, kiasi hiki ni pungufu ya fedha zilizoidhinishwa ambazo ni **Shilingi 3,000,000,000.00,** na hivyo kuwa na nakisi ya **Shilingi 2,129,680,924.35,** sawa na pungufu ya **asilimia 70.9.** Nakisi hii ikijumlishwa na fedha kwa ajili ya waranti katika mwaka wa pili na gharama za malighafi na uendeshaji wa kuanzia, jumla kuu ya nakisi katika mradi huu ni **Shilingi 2,719,005,000.00,** Sawa na pungufu ya **asilimia 90.6.** Kiasi hiki cha nakisi ndicho kilichofanya Taasisi kuomba fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na Bunge liliiidhinisha, jumla ya **Shilingi 3,000,000,000.00** kwa ajili ya mradi huu[1] Hadi Kamati inatembelea mradi huu, fedha ambazo zilikuwa hazijatolewa kwa ajili ya mradi huu ni **Shilingi 2,719,005,000.00**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni muhimu sana kwa ajili ya kuboresha huduma za afya kwa wananchi na wakazi wa Mkoa wa Mbeya kutokana na ukweli kwamba:-

(i) Utaboresha huduma za Upasuaji katika Hospitali hii ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya kuwa katika kiwango cha kuridhisha;

[1] Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya: Taarifa ya Mradi Namba 5411, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jami.

(ii) Utapunguza rufaa za kwenda katika hospitali za Kanda na Taifa kama vile Muhimbili;

(iii) Utaongeza mapato ya hospitali kwani wagonjwa watalipia huduma za uchunguzi na upasuaji hivyo kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini na pia kuongeza uwezo wa hospitali kugharamia shughuli za uendeshaji.

**Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa Mradi huu na kutenga kiasi cha Shilingi 3,000,000,000. Kamati inashauri fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kutolewa ili ukamilike kwa wakati kama ulivyopangwa na uweze kuwanufaisha wananchi wa Mkoa wa Mbeya na maeneo ya jirani.**

*2.2 MRADI WA UKARABATI WA WODI YA WAGONJWA MAHUTUTI*

**Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya inatekeleza mradi wa ukarabati wa Jengo Wodi ya Wagonjwa Mahututi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza Januari, 2022 na ulitarajiwa kukamilika Mwezi Aprili, 2022. Hospitali imepatiwa fedha kiasi cha **Shilingi milioni 150** kupitia fedha za mpango wa maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Kamati ilijulishwa kuwa mradi huu mpaka kukamilika unatarajia kugharimu kiasi cha **Shilingi milioni 216**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kipindi ambacho Kamati inatembelea na kukagua mradi huu kiasi cha **Shilingi milioni 66** kilikuwa bado hakijatolewa. Aidha hadi kipindi hicho, Kamati ilipata taarifa kuwa utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilima 51**.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza sana juhudi hizi za Serikali kwani kwa hakika uwekezaji uliofanyika na unaoendelea kufanyika ni mkubwa sana na utaendelea kusaidia kuboresha afya za Watanzania, hususan wanaoishi katika Mkoa wa Mbeya pamoja na maeneo ya karibu.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi kubwa ambayo Hospitali hii ya rufaa inafanya, Kamati ilielezwa changamoto ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Hospitali hii ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya zikiwemo[2]:

(i) Kutokuwepo kwa barabara za lami upande wa Kaskazini wa Hospitali na hivyo kusababisha wingi wa vumbi katika mtambo wa kuvunia hewa ya *oxygen*

(ii) Hospitali kutokuwa na eneo la kutosha, hali inayosababisha hospitali kutokuwa na uwezo wa kuongeza majengo ya kutolea huduma za Afya.

[2] Randama ya Wizara iliyowasilishwa kwa Kamati.

(iii) Hospitali haina jengo kwa ajili huduma za mama na mtoto hivyo kukosesha huduma kwa mama na mtoto katika hospitali hii.

*2.3 MRADI WA UJENZI WA JENGO LA HUDUMA ZA DHARURA*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya pia imetekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la huduma za dharura kupitia fedha za ufadhili wa Global Fund. Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 99.9. Kamati inaipongeza hospitali hii ya mbeya kwa kukamilisha ujenzi wa jengo hili la huduma za dharura na inaamini itasaidia kuokoa maisha ya Watanzania wengi.**

*2.4 MATOKEO NA MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO*

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia ukaguzi huo wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa, Kamati imefanya tathmini yake na inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

**(a) Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kamati imebaini kuwa bado hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi si ya kuridhisha. Mpaka Kamati inatembelea miradi hii, kiwango cha utoaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2021/2022 hakikufikia asilimia zilizotarajiwa **(ambazo ni asilimia 66, ambapo kwa Mradi wa jengo la Upasuaji zilizopatikana ni asilimia 29 tu),** ilhali muda uliopangwa kukamilika kwa

miradi ukikaribia kuisha. **Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itatoa fedha hizo kabla mwaka wa fedha kuisha ili miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa na kufikia malengo yaliyopangwa.**

**(b) Hali ya Upatikanaji wa dawa**

Kamati imebaini kuwa upelekaji wa dawa katika hospitali hii ni wa kusuasua ukilinganisha na mahitaji halisi ya matumizi ya dawa. Kamati ilitaarifiwa kuwa hadi ilipotembelea hospitali hii upatikanaji wa dawa kutoka Bohari ya Dawa "*MSD*" ulikuwa ni **asilimia 41.5%** ya mahitaji ya Hospitali.

**(c) Upungufu wa watumishi**

Hospitali hii ina changamoto kubwa ya Watumishi kama inavyoonekana kwenye changamoto zilizoainishwa. Kamati ilibaini kuwa katika Hospitali ya Rufaa Mbeya kuna upungufu wa madaktari bingwa kwa **asilimia 67**. **Kamati inashauri Serikali itoe kibali cha ajira ili hospitali ya Rufaa Mbeya pamoja na Hospitali nyingine za rufaa nchini ziweze kuajiri watumishi wa kutosha watakaoweza kuhudumia wananchi wengi, ikiwa ni pamoja na kukidhi matumizi halisi ya miradi hii iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa na Serikali, na hivyo kuboresha utoaji huduma za afya ulio bora unaoendana na thamani ya miradi iliyojengwa.**

**(d) Ukosefu wa vifaa tiba**

Kamati ilibaini kuwa pamoja na kwamba jengo la upasuaji lilitarajiwa kukamilika ifikapo mwezi April 2022 lakini hakuna bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kununua vifaa tiba vitakavyotumika kwenye jengo hilo. **Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kununua vifaa tiba vitakavyotumika kwenye miradi hii ili kuwezesha kutoa huduma stahiki kwa wananchi.**

**(e) Ufinyu wa eneo**

Kamati ilitaarifiwa kwamba eneo la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya ni dogo ukilinganisha na mahitaji ya miundombinu inayotakiwa kuwekwa kwa ajili ya kukidhi uboreshaji wa Hospitali hii ya Rufaa unaohitajika. **Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutanua eneo hili la hopitali ili kuruhusu uwezekano wa kuweka miundombinu wezeshi, pamoja na miradi mingine itakayohitajika kwa ajili ya hospitali hii kwa miaka ijayo, kama vile ujenzi wa jengo la mama na mtoto.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Wizara kuwasilisha Bajeti yake ya fungu 52 hapo tarehe 29 Machi, 2022, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

### *3.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA 2021/2022*

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo tisa (9). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi Maoni na Ushauri.** Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu Kamati itaendelea kuyasisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

### *3.2 UCHAMBUZI WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022*

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia **Fungu 52 k**atika mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 507,218,152,321.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 81,717,635,624.00** sawa na **asilimia 16.1** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 92,044,336,376.00** sawa na **asilimia 18.1** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 333,456,180,321.00**

sawa na **asilimia 65.7** kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, hadi Mwezi Februari 2022, jumla ya **Shilingi 362,313,471,534.70** zilikuwa zimekusanywa, sawa na **asilimia 71.4** ya lengo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 75,765,859,852.00** sawa na **asilimia 20.9** zilikusanywa kutoka Wizarani, **Shilingi 41,271,031,424** sawa na **asilimia 11.4** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 245,276,580,258.70** sawa na **asilimia 67.7** kutoka Taasisi na Hospitali za Taifa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, makusanyo makubwa ambayo ni **asilimia 71.4** ya lengo yamekusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya Wizara. **Kamati inaipongeza Wizara kwa makusanyo hayo mazuri. Ni imani ya Kamati kuwa, kufikia mwisho wa mwaka fedha Juni 2022 lengo la makusanyo litafikiwa**.

Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2021/2022 ambao ulikuwa ni **asilimia 71** ikilinganishwa na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2020/2021 ambapo ilikuwa ni **asilimia 56.3.**

Pamoja na makusanyo hayo mazuri, Kamati imebaini pia kuwa, Hospitali za Rufaa makusanyo yake ni chini ya

**asilimia 50,** mfano Hospitali za rufaa za mikoa ya Dodoma, Iringa, Bukoba, Morogoro pamoja na Songea. Kamati ilitaka kufahamu sababu za upungufu wa makusanyo hayo katika Hospitali za Rufaa ambapo ilielezwa kuwa, Malengo ya makusanyo hayakufikiwa kwa sababu ya changamoto ya UVIKO-19 iliyopelekea wagonjwa wengi kutokwenda katika vituo vya afya kupata huduma. Vilevile baadhi ya wateja waliotarajiwa kupata huduma katika vituo vya umma kwenda katika vituo binafsi kupatiwa huduma hizo. Kwa kuzingatia changamoto hizo makusanyo yaliyokadiriwa hayatafikiwa kwa asilimia 100.

**Kielelezo Na 1: Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Kipindi cha Mwaka 2021/2022**




***Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 52 (Machi, 2022) na usanifu wa Kamati***

### *3.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA WA 2021/2022*

**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya mwaka 2021/2022 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2021 Wizara kupitia **Fungu 52** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,034,134,295,000.00** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 557,303,059,000.00** sawa na **asilimia 53.89** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 476,830,236,000.00** sawa na **asilimia 46.1** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 2

**Mheshimiwa Spika,** fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa zinajumuisha mishahara ya watumishi **Shilingi 304,779,799,000.00** sawa na **asilimia 66.32** na matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 252,523,260,000.00** sawa na **asilimia 33.68** ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, **asilimia 73.75** ya fedha hizo ambazo ni sawa na Shilingi **351,700,000,000.00** ni fedha za ndani na **asilimia 26.2** ambazo ni **Shilingi 125,130,236,000.00** ni fedha za nje. (Kielelezo Namba 3).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa, kufikia Februari, 2022 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **617,713,875,390.66** sawa na **asilimia 60** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu 52. Kati ya fedha hizo **Shilingi 397,976,618,865.98** ni za matumizi ya kawaida inayojumuisha kiasi cha **Shilingi 204,107,118,044.41** za mishahara, sawa na **asilimia 33.04** ya fedha zilizopokelewa, na **Shilingi 193,869,500,821.57** za matumizi

mengineyo *(OC)* sawa na **asilimia** 31.3 ya fedha zilizopokelewa. Aidha Wizara imepokea **Shilingi 219,737,256,524.68** sawa na **asilimia 35.7** ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zilizopokewa **Shilingi 209,844,630,170** ni fedha za ndani na **9,892,626,354.68** ni fedha za nje.


**Mheshimiwa Spika,** Pia katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2022 Wizara ililipokea **Shilingi 205,018,748,874** sawa na **asilimia 77.7** ya **Shilingi 263,728,066,998.00** ambayo ni nyongeza ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Fungu 52 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Nyongeza hii inafanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wizara hii kuwa **Shilingi 1,297,861,361,998.00.** Aidha, fedha za nyongeza zilizoidhinishwa zinafanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo kwa Wizara hii kuwa **Shilingi 740,558,502,998.00,** sawa na **asilimia 57** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa Wizara hii, na hii ni sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Hivyo, jumla ya fedha zilizopokewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni **Shilingi 424,756,005398.68.** Hivyo, nyongeza ya bajeti inafanya jumla ya fedha zote zilizopokewa hadi Februari, 2022 kuwa **Shilingi 822,732,624,264.88**, sawa na **asilimia 63.3**; na hivyo kufanya ongezeko la **asilimia 3.6** la nyongeza ya Bajeti iliyotokana na programu ya Kutekeleza Mpango wa

Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO[3]

### 3.4 *UCHAMBUZI WA KAMATI*

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa upokeaji wa jumla wa fedha ulifikia **asilimia 60** ambapo, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa kwa **asilimia 64.34**; na fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo imepokelewa kwa **asilimia 35.7** ya fedha zote zilizopokelewa.

**Kielelezo Na 1: MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022**





---

[2]Randama ya Wizara iliyowasilishwa kwa Kamati,

[3] Majibu ya Hoja za Kamati ya Bunge zilizoibuliwa wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 52) kwa Mwaka 2022/2023.


***Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 52 (Machi, 2022) na usanifu wa Kamati***

**Kielelezo Na 2: Ulinganifu wa Makadirio na Upokeaji wa Bajeti Fungu Namba 52 kwa Mwaka 2021/2022**




***Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 52(Machi, 2022) na usanifu wa Kamati***

**Kielelezo Na 3: Uwiano wa Bajeti ya jumla baada ya nyongeza ya kupambana na UVIKO – 19**




***Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 52 (Machi, 2022) na usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilitaka kujua Kiasi cha **asilimia 35.7** kilichopokelewa hadi Februari, 2022 kwa ajili ya utekelezajia wa miradi ya maendeleo kimefikisha asilimia ngapi ya utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo, na kama kiasi kilichobaki kikitolewa kitakamilisha utekelezaji kwa kipindi kichobakia ili kumaliza mwaka wa fedha. Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara ipo katika hatua mbalimbali. Iwapo Wizara itapokea fedha kwa mujibu wa mpango kazi wa utekelezaji, malengo ya utekelezaji wa kila Mradi yatafikiwa kwa kipindi kilichobaki. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi kufikia Februari,

2022 Wizara ilitakiwa kuwa imepokea **asilimia 66** ya fedha za matumizdi ya kawaida. Hata hivyo, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **asilimia 59.7** tu. Kamati inaona kuwa kiwango hiki cha upokeaji wa fedha hakiwiani na wastani uliotarajiwa kutolewa kwa Wizara. Kamati inasisitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa wakati.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa utekelezaji wa majukumu, mapato na matumizi ya kawaida pamoja na ile ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wizara katika mwaka wa fedha 2022/2023 imepangwa kwa kuzingatia mambo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020[4] kama yalivyofafanuliwa na Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli hizo za Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

### *4.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara (**Fungu 52**) katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni jumla ya **Shilingi 622,986,024,980.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 144,260,331,187** sawa na **asilimia 23** zinakadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Wizara, **Shilingi 85,739,668,813** sawa na **asilimia 14** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 392,986,024,980** sawa na **asilimia 63** kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Taifa kama inavyoonekana kwenye ***Kielelezo Na. 5***

**Kielelezo Na 4: Makadirio ya Maduhuli ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023**





***Chanzo: Randama Wizara (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna ongezeko la Shilingi **115,774,862,084** la makadirio ya makusanyo ya maduhuli katika mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la **asilimia 18.8** ya **Shilingi 507,211,162,896.00** zilizokadiriwa kwa mwaka **2021/2022.** Aidha, mlolongo wa ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli kwa miaka miwili iliyopita inaonesha kuwa katika kipindi cha Bajeti ya **2020/2021** hadi bajeti ya mwaka **2022/2023** kumekuwa na ongezeko la **asilimia 27.2,** ambapo bajeti ya mwaka **2020/2021** kwenda bajeti ya mwaka **2021/2022** kulikuwa na ongezeko la **asilimia 8.4.** Kamati imebaini kuwa ongezeko la makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2022/2023 linaonekana kwenye vyanzo vya ndani vya Wizara vyenye ongezeko la **Shilingi 62,542,695,563.00,** sawa na **asilimia 43.35**; pamoja na ongezeko la **Shilingi 59,529,849,659** sawa na **asilimia 15.1 kutoka** taasisi zilizo chini ya Wizara na hospitali ya Taifa. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa yamepungua kwa Shilingi **6,304,667,563,** sawa na pungufu kwa **asilimia 6.8** ya makadirio ya vyanzo hivyo kwa mwaka 2021/2022). Kamati imeendelea kubaini kuwa makadirio ya mapato kutoka Hospitali za Rufaa yameendelea kushuka kwa mwaka wa pili mfululizo, ambapo mwaka 2021/2022 yalishuka kwa **asilimia 11.4 na mwaka 2022/2023** yameendela kushuka kwa **asilimia 6.8** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6. Kamati ilielezwa sababu za kushuka kwa makadirio hayo

ya maduhuri kuwa ni kutokana na Hospitali hizo kuanza kuandaa bajeti za makusanyo ya ndani zenye kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyao. **Kamati inapongeza kwa wizara kutenga makusanyo yenye uhalisia na inasisitiza serikali kusimamia kuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli hayo katika hospitali, Wizara na Taasisi zake ili kuzuia uvujaji wa mapato.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ongezeko la makadirio kwa Taasisi za Wizara na Hospitali ya Taifa Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hilo linatokana na makusanyo ya tozo za upimaji wa Afya Mipakani kupitia Maabara ya Taifa na ada kutoka Vyuo vya Mafunzo ya Afya. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko la maduhuli kwa upande wa Wizara, linatarajiwa kutoka kwenye ukusanyaji wa mapato ya Maabara ya Taifa ambayo awali hayakuwepo.

**Kielelezo Na. 5: Ukusanyaji wa Maduhuli**




***Chanzo: Randama ya Wizara (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati***

## *4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, Bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2022/2023 inalenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa Taifa ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za Ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Bajeti hiyo inapangwa kwaajili ya kutekeleza mipango mbalimbali ya Serikali kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka mmoja pamoja na miongozo mbalimbali.


**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo:-

**(a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 52) kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023**


**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoainishwa katika randama ya fungu 52, ili kuweza kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 52 inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 1,109,421,722,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 554,289,666,000.00** sawa na **asilimia 49.96** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 555,132,056,000.00** sawa na **asilimia 50.04** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 7.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, sura ya Bajeti ya Wizara inajumuisha **Shilingi 331,566,406,000.00** sawa na **asilimia 29.9** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 222,723,260,000.00** sawa na **asilimia 20** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), **Shilingi 410,298,000,000**.00 sawa na **asilimia 37** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na **Shilingi 144,834,056,000.00** sawa na **asilimia 13** fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo[4], kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7

**Kielelezo Na 6: Bajeti 202/2021 (Fungu 52)**



**Kielelezo Na 7: Mgawanyo wa Bajeti (Fungu 52) 2022/2023**




***Chanzo: Randama Wizara (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuishia hapo, ilifanya uchambuzi zaidi na kubaini kuwa, Bajeti ya Fungu 52 imeongezeka kwa **asilimia 7.3** kutoka **Shilingi 1,034,133,295,000.00** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 1,109,421,722,000.00** mwaka 2022/2023.

i. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la **asilimia 7.6** kwenye bajeti ya maendeleo;

ii. Kwa upande wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 5.7** wakati


fedha za nje zikiwa zimeongezeka kwa **asilimia 1.9**[5]. Kamati ilielezwa sababu ya ongezeko hilo ni kutokana na mahitaji ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ili ianze kutoa huduma. Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa; Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba, na vitendanishi katika ngazi zote za huduma za afya na kuimarisha matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yote muhimu katika Wizara hii.**

iii. Aidha Kamati ilibaini kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida imepungua kwa **asilimia 0.3.** Hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa matumizi ya kawaida kwaajili ya mishahara yameongezeka kwa **asilimia tatu (3)** huku matumizi mengineyo (*OC*) yakipungua kwa **asilimia tatu (3);** Kamati ilielezwa upungufu wa fedha za matumizi mengineyo ni kutokana na kutengwa kwa fedha za Watarajali *(interns)* katika bajeti ya Maendeleo ambazo awali zilikuwa zinatengwa katika bajeti ya Matumizi mengineyo *(OC)*.

[5] **Taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 52) kwa Mwaka 2022/2023**

| Kielelezo Na 8: ULINGANISHO WA BAJETI (FUNGU 52) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA 2022/2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2021/2022** | **2022/2023** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **%** |
| MISHAHARA | 304,779,799,000 | 331,566,406,000 | 26,786,607,000 | **3** |
| OC | 252,523,260,000 | 222,723,260,000 | -29,800,000,000 | **-3** |
| MAENDELEO NDANI | 351,700,000,000 | 410,298,000,000 | 58,598,000,000 | **5.7** |
| MAENDELEO NJE | 125,130,236,000 | 144,834,056,000 | 19,703,820,000 | **1.9** |
| **JUMLA** | **1,034,133,295,000** | **1,109,421,722,000** | **134,045,055,000** | **7.3** |

**Kielelezo Na 9: ULINGANISHO WA BAJETI 2021/2022 NA 2022/2023 (FUNGU 52)**




**Chanzo: Randama ya Fungu 52 (Machi, 2022) na Usanifu wa Kamati**

**(a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu wa Kamati ulilenga kubaini athari za Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa dhidi ya Bajeti ya **Fungu 52**. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Wakati Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2022/2023 imeongezeka kwa **asilimia 8.1**, bajeti ya **Fungu 52** imeongezeka kwa **Asilimia 7.3**;

ii) Wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 3.6**, bajeti ya **Fungu 52** kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 7.6;**

iii) Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **asilimia 11,** bajeti ya matumizi ya kawaida ya **Fungu 52** imepungua **asilimia 0.54**

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri tunayopata katika uchambuzi huu ni kuwa, ongezeko la mafungu yote kwa pamoja lililowekwa katika bajeti ya Taifa, linawiana na ongezeko la bajeti ya Wizara hii (Fungu 52). Hii inaonesha kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kipaumbele katika tengeo la fedha za bajeti. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo la tengeo katika sekta hii muhimu inayogusa maisha ya watanzania.

**Kielelezo Na 10: ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 52 DHIDI YABAJETI YA TAIFA 2021/2022 NA 2022/2023 (KWA MILIONI)**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 52 DHIDI YABAJETI YA TAIFA 2021/2022 NA 2022/2023 (KWA MILIONI) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BAJETI KUU YA TAIFA | | | | | BAJETI YA WIZARA 2022/2023 | | ASILIMIA |
| MAELEZO | 2021/2022 | 2022/2023 | TOFAUTI | ASILIMIA | 2021/2022 | 2022/2023 | |
| BAJETI KUU | 37,411,37 | 41,063,91 | 3,652,54 | 8.1 | 1,034,134.1 | 1,109,421. | 7.3 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 0 | 5 | 5 | | | 7 | |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | **23,002,986** | **25,542,600** | **2,539,614** | **11** | **557,303.1** | **554,289.7** | **0.54** |
| **MATUMIZI YA MAENDELEO** | **14,977,615** | **15,521,300** | **543,685** | **3.6** | **476,832.2** | **555,132.1** | **7.6** |

***Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 52) na Usanifu wa Kamati***


**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Bajeti **ya Fungu 52** imeongezeka kutoka **asilimia 2.85** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **asilimia 7.3** mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 12 (a), (b) na (c). **Kamati inaendelea kuipongeza Serikali na kushauri kiasi hiki cha fedha kitolewe chote na kiendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kuendelea kuboresha Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.**

**Kielelezo Na 11 (a): ASILIMIA YA BAJETI YA FUNGU 52 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022**

| MATUMIZI | BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022 | BAJETI FUNGU 52 2021/2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **OC** | 4,189 | 252.5 | 6 |
| **MISHAHARA** | 8,150 | 304.8 | 3.7 |
| **MAENDELEO** | 14,977.8 | 476.8 | 3.2 |
| **MALIPO MADENI** | 10,663.3 | - | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA** | **37,980** | **1,034.1** | **4.3** |


**Kielelezo Na 12 (b):ASILIMIA YA BAJETI YA FUNGU 52 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022 KATIKA BILIONI**




**Kielelezo Na 13(c): ASILIMIA YA BAJETI YA FUNGU 52 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023**

| MATUMIZI | BAJETI KUU YA MPANGO WA TAIFA 2022/2023 | BAJETI FUNGU 52 2022/2023 | % |
|---|---|---|---|
| **OC** | 4,493.5 | 554.00 | 12.3 |
| **MISHAHARA** | 9,740.8 | 554.00 | 5.7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **MAENDELEO** | 15,521.30 | 555.00 | 3.6 |
| **MALIPO MADENI** | 11,308.4 | - | - |
| **JUMLA** | **41,063.9** | **1,109.00** | **2.7** |



## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi:-

### *5.1 UHABA WA DAWA NCHINI*

**Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa Dawa nchini bado ni changamoto. Kamati inafahamu kuwa kuimarika kwa huduma ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini ni moja ya vipaumbele vya Wizara hii. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa dawa nchini siyo wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha **Shilingi 218,100,000,000.00** kiliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Dawa. Hadi kufikia Februari, 2022 ni **asilimia 63.1** tu ya fedha ndizo zilikuwa zimepokelewa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, bajeti ya dawa imepungua kwa **asilimia 8.29** hadi kufikia **Shilingi 200,000,000,000.00**. Maelezo ya Wizara ni kuwa Kupungua kwa bajeti hiyo kunatokana na kiasi hicho kutengwa kwenye bajeti ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa bidhaa hizo. Hata hivyo Kamati imeshuhudia upungufu wa dawa katika hospitali

mbalimbali nchini na kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utolewaji na usambazaji wa dawa itolewe yote na kwa wakati ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa ili kuokoa maisha ya watanzania wanaopata huduma katika hospitali zetu.

(ii) Serikali itazame upya mifumo ya usambazaji wa dawa inayotumiwa na *MSD* ili kutatua changamoto zinazotokana na usambazaji. Mifumo ya kielektroniki iwekwe katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kudhibiti upotevu wa dawa;

(iii) Aidha, Kamati inashauri Wizara kuweka mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya kununua dawa pasipo ushauri wa madaktari. Kamati pia inashauri Wizara kuweka utaratibu wa usimamizi mzuri kwenye maduka yanayouza dawa za binadamu ili kuondoa matumizi ya dawa yasiyo sahihi kwa wananchi;

(iv) Ili kupunguza matumizi ya fedha nyingi kwenye ununuzi wa dawa, Kamati inaishauri Serikali kuipitia upya sheria ya manunuzi ambayo

imekuwa mkwamo na inaongeza gharama kwenye manunuzi ya vitu mbalimbali vya Serikali zikiwemo dawa na vifaa tiba.

(v) Kamati inaishauri Serikali kufuatilia makusanyo ya fedha za mauzo ya dawa nchini kwa kuweka mkakati madhubuti wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato yanayotokana na dawa.

***5.2 UIMARISHAJI WA HOSPITALI ZA KITAIFA NA RUFAA NCHINI***

**Mheshimiwa Spika,** hospital za Kitaifa pamoja na hospital za Rufaa nchini zimekuwa zikiendelea kuboreshwa kwa kiwango cha kimataifa. Kwa sasa hospital kama Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete inapokea wagonjwa kutoka mataifa mbalimbali kama vile Burundi, Uganda na Kenya. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa ajili ya uboreshaji huu wa miundombinu na huduma katika hospitali hizi za Kitaifa. Hata hivyo, uboreshaji wa hospitali hizi haujafikia kiwango cha kuridhisha. Hivyo basi, katika hili Kamati ina ushauri ufuataao:-

i) Serikali iimarishe huduma za afya katika hospital hizi kwa kuajiri wataalam wabobevu zaidi;

ii) Serikali iboreshe zaidi upatikanaji wa vifaa tiba vitakavyowezesha huduma za magonjwa sugu kama

moyo, figo nk. ambayo wananchi wengi wamekuwa wakifuata matibabu yake nje ya nchi;

iii) Kwa kuwa sasa hospital hizi zinapokea wagonjwa kutoka nje ya nchi, Serikali itoe msukumo katika utangazaji wa huduma hizi bora katika Mataifa mbalimbali ili kuwezesha utalii wa kimatibabu *(medical tourism)* kwaajili ya kuongeza pato la Taifa na kuhudumia wahitaji wa huduma za afya. Aidha Serikali iweke mikakati mizuri ya kuvutia utalii wa kimatibabu *(medical tourism);*

### *5.3 BIMA YA AFYA KWA WOTE*

Ni ushauri wa muda mrefu wa kamati kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ili bima hiyo ya afya itolewe kwa watu wote. Katika kuharakisha hilo kamati ilishauri juu ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na utoaji wa elimu kwa Umma. Serikali katika majibu ya hoja za Kamati 2021/2022 iliieleza Kamati kuwa tayari **Shilingi Milioni 231** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na utoaji wa elimu kwa Umma. Kwa kuwa Serikali bado inapokea maoni ya kuboresha mfumo huo Kamati inashauri sasa kuzingatia mambo yafuatayo: -

i) Wananchi washirikishwe vya kutosha ili kutoa maoni yao katika kuboresha muswada huo;

ii) Serikali ione namna ya kushirikisha Sekta Binafsi nchini katika kutoa huduma ya Bima ya Afya;

iii) Kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko kwa wateja wa *NHIF* kukosa baadhi ya huduma zikiwemo dawa, Wizara isimamie kuondoa changamoto hii kwa kuiimarisha *MSD*;

iv) Serikali iiwezeshe *NHIF* katika kuratibu na kutekeleza mpango wa kuanzisha Bima ya Afya kwa wote.

v) Vifurushi vya bima ya afya kwa wote viwe vyenye uhalisia ili kutoruhusu mfuko kushindwa kutekeleza majukumu yake.

### *5.4 UHABA WA RASILIMALI WATU*

**Mheshimiwa Spika,** rasilimali watu imekuwa ni changamoto katika hospitali na Taasisi nyingi za afya nchini. Katika kupunguza changamoto hii Serikali kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeahidi kuajiri watumishi 10,285 wa kada mbalimbali za afya watakaopelekwa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati kwenye Serikali za Mitaa na Hospitali za Kanda, Rufaa, Vituo vya Afya na Hospitali nyingine za Kimkakati kama vile DDH(Desigdnated District Hospitals). **Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambapo inaamini itaenda kutatua chagamoto hii ya upungufu wa watumishi katika sekta hii muhimu. Kamati inaendelea**

**kusisitiza kuwa ajira hizi zizingatie mgawanyo wa kijiografia na uhitaji wa watumishi hao**.

### *5.5 TAASISI YA SARATANI YA OCEAN ROAD*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa mashine ya Cyclotrone ambao unatarajia kuanza kutumika rasmi 01Julai, 2022. Kamati inaamini Mradi huu ukikamilika  utasaidia kugundua ugonjwa wa saratani ukiwa katika hatua za awali, na hivyo kusaidia kupunguza madhara yanayosababishwa na maradhi ya saratani. Mradi huu ni moja kati ya miradi muhimu na upo katika nchi chache duniani. Mradi huu ukikamilika utasaidia kuvutia watu kutoka mataifa mbalimbali ya jirani kuja kutibiwa katika taasisi hii na kuwa sehemu ya utalii wa kimatibabu, na hivyo kuhudumia watu wengi na kujiongezea pato la nchi.

i. Kamati inashauri Serikali kuukamillisha mradi huu kwa haraka ili kuweza kuwasaidia wananchi kutatua changamoto ya saratani ikiwa katika hatua za awali;
ii. Taasisi ijike kwenye kufanya tafiti ili kutambua sababu ya ongezeko la saratani nchini na kushauri wananchi ipasavyo;
iii. Kuwe na mkakati wa kujenga uelewa kwenye jamii juu ya ugonjwa wa saratani ili kuondoa imani potofu dhidi ya ugonjwa huo na kuwasaidia wananchi kuwahi hospitali mara waonapo dalili za

ugonjwa huo ili kuepusha madhara zaidi yanayoweza kujitokeza hapo baadaye;

iv. Mradi huu ukikamilika ujikite kwenye kutoa huduma ambayo ndio msingi wa uanzishwaji wa taasisi hiyo badala ya kuwaza kuongeza kipato pekee;

v. Serikali iweke utaratibu wa kuwatambua na kushirikiana na wataalam wa tiba asili na tiba mbadala katika utoaji wa matibabu ya saratani kwani wamekuwa chachu katika utafutaji wa dawa kwa ajili ya kutibu magonjwa mbalimbali ikiwemo ugonjwa wa saratani;

vi. Wizara iandae wataalam wanaoweza kutunza na kutengeneza mitambo ya kimatibabu inayowekwa katika hospitali zetu, kama vile mtambo wa *PET CT SCAN* na mashine za MRI ili kuepusha kusimama kwa huduma na kutafuta mafundi kutoka nchi za nje pale zinapoharibika, hali ambayo itaongeza gharama na kuyaweka rehani maisha ya Watanzania;

vii. Itengenezwe makala ya hospitali zetu kubwa zote kama Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, MOI na Hospitali ya Benjamin Mkapa zitakazoweza kutangazwa kwenye vyombo vya habari za kimataifa ili kuvutia watu kuja kutibiwa katika hopitali hizo.

### *5.6 KUIMARISHA UPATIKANAJI WA DAMU SALAMA*

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya upungufu wa damu katika hospitali zetu Nchini. Aidha kamati imebaini uhaba wa vifaa vya kuhifadhia na kubebea damu katika hospital zetu. Uhitaji wa damu katika hospital zetu ni mkubwa ukilinganisha na kujitoa kwa watu katika uchangiaji wa damu. Kutokana na hali hiyo kamati inatoa ushauri ufuataao: -

i. Serikali iweke mkakati wa kuhamasisha wananchi kuchangia damu kwa kuweka vituo vya uchangiaji damu kama vile kwenye shule, vyuoni, masokoni, kwenye mahospitali na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu;

ii. Serikali itoe elimu juu ya umuhimu wa kuchangia damu kwa wananchi; Aidha Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali wa afya nchini kuanzisha kampeni maalum ya kuchangia damu nchi nzima;

iii. Serikali ihakikishe inafanya manunuzi ya vifaa vya kukusanyia, kubebea, na kuhifadhia damu kwa wakati ili kuepusha uhaba wa vifaa hivyo ambao unaweza kuathiri maisha ya watu.

### *5.7 UGONJWA WA VIRUSI VYA KORONA - UVIKO(COVID-19)*

**Mheshimiwa Spika,** ugonjwa wa virusi vya Corona umekuwa ni tishio duniani kote. Ugonjwa huu

umechukua maisha ya watu wengi sana duniani, hivyo tunapaswa tusiuchukulie mzaha. Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake zilizowezesha kupatikana fedha kwa **Shilingi 263,728,066,998.00** zilizoongezwa kwa Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa ajili ya kupambana na athari za virusi vya Korona katika nchi yetu. Hili liliwezeshwa na utashi wake wa kuamua kuunda Kamati ya Wataalamu ambao kwa kushirikiana na Taasisi za Afya Duniani na zile za Kikanda za *EAC* na *SADC* waliangalia suala la Korona kwa undani, ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa kina na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua na jinsi ya kuendelea kupambana na maradhi hayo. Kutokana na hayo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i) Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchanja, kuendelee kuchukua tahadhari kwa kufuata miongozo ya kinga ambayo imekuwa ikitolewa nchini;

ii) Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango madhubuti katika kukabiliana na magonjwa haya ya mlipuko.

**Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni hayo ya Kamati kuhusu ugonjwa wa Korona kama sehemu ya magonjwa ya kuambukiza Kamati pia inaushauri ufuatao kuhusu magonjwa mengine ya kuambukizwa:-**

i) Serikali iendelee kuimarisha utoaji wa huduma ya lishe bora kwa wananchi wote walioathirika na UKIMWI;

ii) Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya kula mboga na matunda kwa wingi ili kupunguza maambukizi na athari za ugonjwa huu.

iii) Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kupambana na malaria nchini, hasa mkakati wa kutokomeza mbu na mazalia yake.

*5.8 MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA (NON- COMMUNICABLE DISEASES)*

**Mheshimiwa Spika**, magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa ni tishio kwa afya za Watanzania. Kamati inaendelea kusisitiza ufanyike utafiti juu ya chanzo cha magonjwa haya. Jamii ielimishwe juu ya magonjwa hayo na juu ya mazoezi na lishe ili kuzuia ongezeko la wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza.

*5.9 KUIMARISHA HUDUMA ZA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA*

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko la matumizi ya Tiba asili na Tiba mbadala nchini ambayo imekuwa ikitumika sana na hasa kwa wakati wa wimbi la kwanza na la pili la ugonjwa wa Korona kwa sasa; jambo ambalo ni jema kabisa. Kamati inapongeza wataalam

hawa kwa kuwa wabunifu na kuisaidia jamii yetu. Hata hivyo kumekuwa na utoaji wa huduma hii usiowekewa ubora ili kujua athari hasi zinazotokana na huduma hiyo. Ili kuboresha huduma hizi kwa wananchi Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

i) Serikali iwatambue watoa huduma hizi za tiba asilia kwa kuwapa ithibati *(Accreditation)* ili kuwapa wananchi uhakika *(Assurance)* wakati wa kutumia huduma hizo;

ii) Serikali iweke utaratibu wa usambazaji wa tiba hizi asilia kama sehemu ya matibabu mara baada ya kupata ithibati ya matumizi yake;

iii) Ili kuepuka uwepo wa watoa huduma hawa wasio waaminifu, Kamati inashauri Wizara iwasajili watoa huduma hawa na dawa zao ambao zimethibitika kuwa zinatibu magonjwa mbalimbali;

iv) Aidha, Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya tiba asili na tiba mbadala ambazo hazina madhara kwa watumiaji.

**SEHEMU YA SITA**

**6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha

maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano wanaoipa Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi Naibu Katibu Mkuu Ndg. Dkt. Seif Shekalage na Mganga Mkuu wa Serikali Ndg. Dkt Aifello Sichalwe pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Mheshimiwa Mhe. Aloyce John Kamamba (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kambamba, Mb, - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Eng. Samweli Hhayuma Xaday, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele - Mjumbe

7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. MheKassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Francis Leonard Mtega - Mjumbe
10. Mhe. Latifa Khamis Juwakali, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu- Mjumbe
14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb, - Mjumbe
15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb- Mjumbe
16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb- Mjumbe
17. Mhe. George R. Mwenisongole,Mb- Mjumbe
18. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb- Mjumbe
19. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb- Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb- Mjumbe
25. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb- Mjumbe
26. Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo,- Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema. Pamoja nae namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunawashukuru sana Makatibu

wa Kamati yetu Ndg. Francisca Haule, Ndg. Happiness Ndalu, Ndg. Emmanuel Mdidi na Ndg. Chacha Nyakega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, **Fungu 52** jumla ya **Shilingi 1,109,421,722,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**
16 MEI, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu tunakushukuru kwa kusoma maelezo hayo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia na tutaanza na wachangiaji wafuatao na wachangiaji hawa wanachangia kwa dakika saba. Kwa hivyo, kengele

itagongwa dakika tano halafu unajua zimebaki mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Eric James Shigongo atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili nikiwa mtu wa kwanza kutoa mchango wangu kwa Taifa langu kuhusu idara hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninampongeza sana kwa niaba ya Watanzania kwa uamuzi wa kuongeza mishahara kwa asilimia 23.3. Nchi nzima imejaa shangwe kwa sababu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze kwanza kwa kusema maneno yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 nchi za Afrika zilikutana kule Abuja-Nigeria na wakafikia uamuzi wa kwamba bajeti ya Taifa lolote la Afrika Marehemu Mzee Mkapa alikuwa pale ni lazima asilimia 15 ya bajeti ilielekezwe kwenye huduma za afya. Jambo hili halijaweza kutimia 2019 tulikuwa na asilimia Saba, Mwaka 2020 tulikuwa na asilimia 6.7 na ninavyotazama naona kama tunaendelea kushuka. Sasa mimi nilikuwa

ninaushauri mmoja kabla sijaanza ni kwamba naomba Serikali yangu ifikirie kuongeza bajeti kwenye afya kwa sababu afya ya Mtanzania ni kitu cha muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *preventive medicine,* suala la kuzuia magonjwa yasitokee, tumefanya kazi kubwa sana kama Taifa kutibu watu, tumefanya kazi kubwa sana kuwatibu watu wetu wanapougua lakini hatujawekeza kiasi kikubwa sana kwenye suala la kuzuia magonjwa yasitokee. Katika suala la kuzuia magonjwa yasitokee nitajikita moja kwa moja kwenye chanjo ya homa ya ini na homa ya ini yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 mimi na wenzangu katika Kampuni ya *Global Publisher* tuliamua kufanya kampeni nchi nzima kuwaelimisha watu kuhusiana na ugonjwa wa Homa ya Ini. Kilichotufanya tufanye kampeni ile ilikuwa ni *data* zilizokuwepo za Homa ya Ini zilitushtua, zilitutisha na tukaona kwamba ilikuwa sababu ya mimi na wenzangu kutoa mchango kwa nchi yetu ili kuweza kusaidia watu waweze kupata ufahamu.

Mheshimiwa Spika, wakati huo 2014 katika akina mama waliofanyiwa uchunguzi wa afya wajawazito asilimia tano ya akina mama wote walikuwa wanakutwa na Homa ya Ini. Damu iliyotolewa kwenye benki ya damu hapo Dar es Salaam na sehemu mbalimbali chupa 100 zilizochukuliwa chupa nne zilikutwa na homa ya ini na uwepo wa homa ya ini katika nchi ulikuwa ni asilimia tano *data* zile zilitutisha

tukaanza kampeni ile, tumefanya kampeni kwa muda tu, wakati ule Waziri wa Afya alikuwa Rais wa Zanzibar sasa hivi Mheshimiwa Hussein Ally Mwinyi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alikuwa Mheshimiwa Said Meck Sadiki, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alikuwa Dada yangu Grace Magembe na Meya wa Ilala alikuwa Mdogo wangu Mheshimiwa Jerry Silaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya kampeni ile kwa muda mfupi nikaitwa nikaambiwa Eric kampeni yako ni nzuri lakini tunaomba uiache kwanza inasababisha hofu inaleta taharuki watu wanaogopa, tukakubali kuacha kampeni ile kwa shingo upande. Miaka nane baadaye nikiwa naongea leo naomba nikusomee *data* za homa ya ini nchini Tanzania. Kwa wajawazito 100 wanaopimwa leo kwenye *antenatal clinic* zetu asilimia Saba mpaka Nane wanakutwa na homa ya ini, imeongezeka. Benki ya damu wanapotoa damu watu 100 chupa sita zinakutwa na homa ya ini.

Mheshimiwa Spika, *rate* ya homa ya ini, uwepo wa homa ya ini kwenye Taifa letu sasa hivi ni asilimia mpaka 7.2 katika baadhi ya maeneo. Hii inatisha, hili siyo jambo la kukalia kimya, wala siyo jambo la kuacha kuliongelea.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa leo kuongea nikiamini ya kwamba tuna uwezo wa kuzuia ugonjwa huu, tuna uwezo wa kuokoa maisha ya watu wetu kwa sababu chanjo ipo na mimi nafahamu Waheshimiwa Wabunge humu ndani mnaonisikiliza wengi mmechanjwa kwa sababu chanjo

ililetwa hapa hapa Bungeni, lakini huko nje watu wetu wanashindwa kuimudu hii chanjo, kwa bei ya Serikali ni Shilingi 10,000 kwa chanjo moja mtu anahitaji chanjo tatu na kabla hajachanjwa lazima afanyiwe *rapid test* kuona kama ameambukizwa au hapana Shilingi Elfu Arobaini, Elfu Arobaini ni nyingi kwa mwananchi wa kawaida. Wananchi wanauliza kama chanjo ya *COVID* tumechanjwa bure kwa nini chanjo ya homa ya ini tunaombwa pesa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanakufa, maisha ya watu yanapotea, watu wengi wameambukizwa. Hapa ndani mnaonisikiliza kama haujafiwa, kama humjui mtu aliyekufa basi wewe mwenyewe jipeleleze. Ugonjwa huu unazidi kuenea, kasi ya kuenea ni mara 100 zaidi ya UKIMWI. Tuna sababu ya kuchukua hatua kuokoa maisha ya watu wetu. Tuna kila sababu ya kuchukua hatua kuokoa maisha ya watu wetu, watu wanakufa. Hatuwezi kunyamaza, hatuwezi kujifanya hatuoni, lazima tuchukue hatua tuokoe maisha ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya watu waliotuchagua. Tuko hapa Bungeni kama hatuwezi kutetea maisha ya watu wetu waishi hatuna sababu ya kuwa Wabunge. Najiuliza kila siku kwanini hatuchanji? Kuna mtu akaniambia nchi yetu ni maskini na hatuna uwezo. Nikakataa, nikamwambia ukiniambia nchi ni maskini niletee *report* ya CAG nitakuonesha fedha zinapotelea wapi. Mabilioni ya fedha yanapotea mikononi mwa watu wasiokuwa waaminifu. Tungeokoa fedha zetu

kwenye *report* ya CAG katika nchi hii tungeweza kuwachanja watu wetu wote na chenji ikabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiachana na hilo, naomba niongee jambo moja la msingi sana na bahati nzuri wataalam wako hapa wananisikiliza. Umuhimu wa kumchanja mtu badala ya kumtibu ni jambo la maana mno. Kansa ya Ini, *the Hepatocellular Carcinoma* gharama ya kumtibu hapa Tanzania ni Shilingi Milioni 16 mtu mmoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, sasa kama gharama ya kumtibu mtu mmoja hapa Tanzania ni Shilingi Milioni 15 mwenye Kansa ya Ini inayosababishwa na Homa ya Ini. Ni kwanini tusiwachanje watu kuokoa maisha yao? Fedha zipo, tuwachanjeni watu wetu tuweze kuokoa maisha yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Ahsante sana.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi naweza kuchangia Wizara ya Afya. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge Lake Tukufu. Lakini nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii. Niwapongeze Wizara nzima ya Afya akiwepo Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, Naibu wake kaka yangu Mollel lakini Katibu Mkuu wa Wizara hii na watumishi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu ameendelea kuipa fedha Wizara hii nyeti ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia kwa sababu muda hautoshi kwamba 2021/2022 tulipewa fedha Shilingi Bilioni 129 kwa sababu ya dawa. Nikiongea harakaharaka pia tulipata Shilingi Bilioni 500 hela za UVIKO zilienda Wizara ya Afya. Lakini masikitiko makubwa kwenye hospitali zetu kulikuwa hakuna dawa. Hili ni jambo la kusikitika na ni lazima kama Wabunge tuseme. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri afuatilie fedha zinazotoka kwamba ziende zikafanye kazi iliyoambiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unashangaa Shilingi Bilioni 129 lakini hauoni mrejesho wa dawa ambazo ziko hospitali. Sijui *MSD* kuna tatizo gani au kuna tatizo gani, siwezi kujua lakini naiomba Wizara ifuatilie kwa nini dawa hazikwenda kwenye hospitali zetu. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais alisema

pia fumua *MSD* unasubiri nini? Unasubiri nini fumua *MSD* watu wa-*deliver,* watu wapate fedha zinazokwenda, wananchi wazione, wajue Rais wao anafanya kitu gani. Hauwezi ukapeleka Shilingi Bilioni 129 hospitali hakuna dawa. Nikuombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mkurugenzi mpya wa MSD mpya aliyechaguliwa. Tumuombe akafanye kazi vizuri, yeye ni kijana, tunamjua ni mzooefu, alikuwa anafanya kazi *USAID*. Tunajua ana *exposer* kubwa. Tunakufahamu, tunakuona *comment* zako kwenye mitandao ya kijamii. Tunajua uwezo wako, nenda ukafanye kazi za watanzania. Uhakikishe dawa zinafika kwenye mahospitali. Kufanya kazi vizuri siyo kuweka *program* zako vizuri za kiofisi wakati tukienda hospitali hatukuti dawa, utakuwa haujafanya kazi vizuri. Hakikisha hospitali inapata dawa na safari hii Serikali imetenga Shilingi Bilioni 200 kwa ajili ya dawa peke yake. Shilingi Bilioni 200 kwa ajili ya dawa, tunaimani tutaona dawa kwenye hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuomba sana usiogope, uende ukafanye kazi. Tunajua uweledi wako, tunajua una-*exposer,* tunakujua, tunakufahamu hata wewe kama hutufahamu sisi watu wa mtaani huko tunakujua. Kwa hiyo, nenda kafanye kazi wewe ni kijana, una kesho nyingi, ukiharibu hapo utakuwa umejiharibia mambo yako mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dawa zifike kwa wakati. Unakuta kuna *cycle* dawa zinatakiwa zifike tarehe 15 kwenye Mkoa

wa Tabora, wanakuwa na dawa wanatumia mpaka tarehe 15. 15 inafika dawa hazijafika, zinafika tarehe 22. Watu wakienda pale wanalalamika kwamba hatujapata dawa, kumbe dawa ni uzembe tu wa kuzifikisha kwa wakati. Nimuombe sana Mkurugenzi wa *MSD* aende akafanye kazi yake kwa uweledi kwa kupanga mipango ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwambie pia katika dawa atakazonunua ahakikishe anaweka *package* ya kujifungulia ya mama na mtoto. Hii imekuwa kero sana. Tunasema wakinamama wakijifungua, wakajifungue bure, wakifika pale *package* kama hamna inabidi akanunue, atajifungulia kitu gani haipo hospitali. Kwa hiyo, nimuombe kwenye bajeti zake aweke *package* ya kujifungulia ni kitu cha muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kupekea hii fedha nyingi kwenye hospitali zetu zote za Rufaa za mikoa yetu yote Tanzania nzima, tunampa hongera sana. Nimpongeze tena Rais kwa kuweza kujenga Hospitali ya Mama na Mtoto kwa mara ya kwanza katika Tanzania, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongee, sisi Tabora tumepata fedha nyingi sana, tumepata jengo la *emergency* la kisasa, mambo ya *CT scan* tumepata na kadhalika. Lakini tuna changamoto moja ndogo, nimuombe Mheshimiwa Waziri. Tulikuwa tumepangiwa kujengewa Hospitali ya Kanda kwenye Mkoa

wa Tabora, tukaonesha na eneo, mpaka leo hamna Hospitali ya Kanda. Tatizo ni nini Mheshimiwa Waziri? Naomba ukija hapa utuambie kwa nini Hospitali ya Kanda haijaanza kujengwa kwenye Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hospitali yetu tuliyonayo ya Mkoa imejengwa 1906 ikiwa kama kituo cha kupokelea majeruhi wa kivita wa Mkoloni ndiyo hospitali tuliyonayo. Miundombinu imechakaa, kwa maana miundombinu ya maji na umeme imechakaa kwa kiwango kikubwa sana. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri tunaomba mtujengee Hospitali ya Kanda kama mlivyotuahidi siku zote kwenye Mkoa wa Tabora. Mheshimiwa Ummy akiwa Waziri kipindi kilichopita, ulikuja na ulituahidi Hospitali ya Kanda katika Mkoa wa Tabora itajengwa, tunaomba sana mtujengee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Madaktari, tuna Madaktari Bingwa katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Tabora watatu tu, yupo wa watoto na wanawake. Tunaomba tupate Daktari Bingwa hata wa upasuaji Mheshimiwa Ummy. Masuala ya upasuaji watu wanakufa, hatuna Daktari Bingwa. Hatuna Daktari Bingwa wa dawa za usingizi, mtu akiingia *theater* mara nyingi watu wamefariki, hatuna Madaktari Bingwa. Tunaomba Madaktari Bingwa wawepo hata ikitokea kufariki basi iwe ni bahati mbaya siyo kwa sababu hakuna Madaktari Bingwa. Hata mmoja akiwa wa upasuaji kwenye Mkoa mzima tukimpata itakuwa imewasaidia sana wananchi wa Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Ametoa ajira tunajua kwenye Wizara ya Afya ametoa ajira 10,000. Tunaamini hata Tabora na sisi tutapata watumishi wa Wizara kwa sababu kwa kweli watumishi ni wachache sana na inatokea kuleta malalamiko kwamba labda Wizara ya Afya haifanyi kazi vizuri. Tukienda hospitali Madaktari hawatuhudumii, Manesi lakini Manesi wanachoka.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kulala na mgonjwa kwenye wodi moja ina vitanda 40. Kitanda kimoja watu wawili, watu 80 lakini yuko *Nurse* mmoja anahudumia usiku kucha. Heri ni wewe utamuonea huruma *Nurse,* huyu amemaliza dripu, huyu anatapika, huyu anataka kwenda kujisaidia, halafu wanasema wasilale na ndugu, yuko *Nurse* mmoja. Niliyepata bahati ya kuingia nilikuwa namwambia *Nurse* kamuwekee yule dripu acha nimfutie huyu matapishi, yaani unajisikia kuumia kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Wizara ya Afya pale mnapoona Ma-*nurse* ni wachache, ruhusuni ndugu wa mgonjwa walale hospitali. Tusifate tu kwamba Ulaya hawalali hospitali, wenzetu wana Ma-*nurse* wengi, wanaweza kumuhudumia mgonjwa kwa wakati unaoweza kustahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Ummy Mwalimu. Waziri Ummy tunakujua, tunakufahamu, tumefanya kazi na

wewe muda mrefu. Ni Waziri mahiri, ni mchapakazi, tunaomba uende *MSD* ukafanye kazi *MSD*. Uifumue *MSD* kama ulivyoambiwa na hatimaye tuone matunda kwa kupata dawa kwenye Hospitali zetu za rufaa, zahanati na vituo vya afya, tuombe sana. Lakini tumuombe mtu wa *MSD*, mmeagizwa mnunue dawa kwa *owners* ili dawa ziwe kwa bei rahisi. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba niwaombe Waheshimiwa Wabunge twendeni tukaseme mambo mazuri yanayofanywa na Rais wetu Samia Suluhu Hassan. Tumeona kwenye Wizara fedha alizozitoa, haijawahi kutokea kupeleka Shilingi Bilioni 500 kwenye Wizara ya Afya. Twendeni tukahakikishe Watanzania hawajawahi kumpigia Rais mwanamke kura, 2025 apigiwe kura za heshimiwa kubwa sana kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya, Wizara hii tunaitegemea sana lakini inalinda uhai wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuwapongeza sana Wizara kwa kazi kubwa na kasi nzuri inayoendelea hivi sasa kwa upatikanaji wa madawa. Jambo hili linakwenda vizuri lakini yote haya baada ya mabadiliko yaliyojitokeza hivi karibuni naamini Mheshimiwa Waziri kwa uzoefu wake atatusaidia sana Waheshimiwa Wabunge na kuhakikisha huduma za kinamama zinaendelea kupatikana katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba jambo moja, Wizara hii ambayo anaisimamia Mheshimiwa Ummy. Sisi kwenye Wilaya yetu ya Itima tumejenga hospitali ya wilaya lakini tumejenga kituo cha afya. Lakini vilevile kuna bajeti iliyopitishwa mwaka jana kwa ajili ya kuleta vifaa tiba, mpaka hivi sasa ninavyoongea na mkandarasi ni *MSD*, mpaka hivi sasa kati ya vifaa 51 vimekuja *item* saba tu. Sasa utaona ni namna gani Serikali inavyozidi kuwekeza katika maeneo haya muhimu lakini bado tunakuwa na changamoto hiyo kubwa ambayo na Serikali tayari inaendelea kuleta fedha nyingi katika maeneo hayo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kupongeza tu, Serikali imeendelea kuongeza majengo katika hospitali yetu ya wilaya lakini na katika vituo vyetu vya afya. Changamoto kubwa ni pale ambapo watumishi hawapo wa kutosha. Wilaya yangu ya Itilima ina takribani wakazi 500,000. Watumishi Idara ya Afya ni 171 tu, sasa tuna vituo vya afya vinne na tuna zahanati 31 na tuna hospitali ya wilaya. Utaona

ni adha ipi kubwa ambayo watumishi hawa wachache ambao tunawapata na tunawapa kazi ngumu ya kushindwa kuwahudumia wananchi hawa na matokeo yake mtumishi huyu wa afya anafanya kazi mpaka inazidi uwezo wake na wakati mwingine inafika mahala anajibu tofauti kwa sababu tayari akili yake imeshazidiwa jinsi ya huduma aliyotoa kwa siku hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika kuna vijana ambao wamechukuliwa kwenye baadhi ya halmashauri kuendelea kujitolea. Katika nafasi hizi ambazo zimetolewa basi iwe kipaumbele kuhakikisha kwa sababu wapate hiyo ajira angalau itatutia moyo na vijana wengine ambao wapo mitaani wataendelea kushawishika kuendelea kutoa huduma na kusaidia kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine tuna Kituo chetu cha Afya Zagayu ni cha muda mrefu sana hakina wodi ya wazazi, wodi ya watoto na maabara na kimechakaa sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri basi katika mipango yake akiangalie kile na kubwa zaidi ombi langu kubwa ni kuhakikisha tunaletewa watumishi wa kutosha katika Wilaya yetu ya Itilima na Kituo cha Afya cha Mwanunda ambacho ni kipya kimeshakamilika tunatarajia Juni Mungu akipenda kinaweza kukamilika kikaanza kutoa huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa watumishi tulionao hao wachache haitawezekana. Pongezi nyingi tunaendelea kukupa Mheshimiwa Ummy tunachoamini kwamba na

pongezi hizi tunakuamini ni mchapakazi na nimsikilizaji mzuri kwa Wabunge na kwa wananchi na kwa wataalam wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tungeendelea kukuomba pale ambapo kuna umuhimu basi tia nguvu ili shughuli zinazofanywa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan ziendelee kutimilika kwa vitendo. Tukifanya hivi wananchi wetu na malalamiko haya ambayo tunayazungumza tutakuwa tumeyapunguza kwa asilimia kubwa sana. Changamoto ya afya ni kubwa, kubwa sana lakini tunahitaji sasa kuendelea angalau ku-*balance* uwiano wa watumishi wetu katika maeneo husika ili kazi hii ifanyike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na la mwisho, ombi langu kubwa kwa Mheshimiwa Waziri ninaomba sana watumishi utupatie wa kutosha nakumbuka kwenye *program* ya Mkapa *Foundation* ulikuja kutupatia watumishi pale Itilima na ukaahidi kituo cha afya pale Makao Makuu. Naomba Mheshimiwa Waziri kiwe kipaumbele chako kwa sababu ni maneno uliyazungumza wewe na bahati nzuri Mwenyezi Mungu amekurudisha kwenye Wizara hiyohiyo, sasa naomba sana utekelezaji huo ufanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuatiwa na Meshimiwa Catherine Valentine Magige. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa leo tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa maamuzi yake ya upendo sana kwa kuongeza kima cha chini cha mshahara mpaka asilimia 23.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri, dada yangu Ummy Ally Mwalimu kwa kazi kubwa anayochapa kwenye Wizara hii akiambatana na kaka yangu pale Mheshimiwa  Dkt. Mollel. Kwa kweli katika Wizara ambazo sisi Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii tunakuwa *comfortable* nazo ni pamoja na Wizara ya Afya. Tunawapongeza sana, tunawapongeza sana ongezeni hiyo *spirit* ya kuwajibika kwa ajili ya nchi yetu ili tuweze kutengeneza maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama leo kwa ajili ya jambo moja tu, huduma ya mama na mtoto. Huduma ya mama na mtoto ukisoma Sera ya Afya, ukisoma miongozo yote ya afya inaeleza namna gani Serikali imepanga kuokoa vifo vya

mama na mtoto hasa kwa kuondoa tozo na fedha zote ambazo mama mjamzito na mtoto mchanga wanaweza kugharamia kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, uhalisia ulivyo ni tofauti kabisa na miongozo yetu inavyotolewa. Nimshukuru sana mchangiaji aliyemaliza Mheshimiwa Munde ameligusia na ametoa msisitizo vizuri kwamba hali ilivyo ni tofauti kabisa na miongozo ambayo inawekwa mezani.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano wa baadhi ya maeneo, Kilindi kuna Kata moja inaitwa Kwasunga ipo zaidi ya kilometa 100 kutoka kwenye Kituo cha Afya Mkata. Akina mama wa Kwasunga wanajifungua njiani kuelekea kwenye kituo cha afya. Lakini pamoja na kwamba wanajifungua njiani wakifika hospitalini kwenye Kituo cha Afya Mkata hawana fedha, hawapati huduma. Kama siyo fedha waende na ile *package, gloves* na nini kwa ajili ya kwenda kujifungulia. Lakini ukija kwenye utaratibu wa Sera na Miongozo inasema huduma ya mama na mtoto ni bure.

Mheshimiwa Spika, niliombe Bunge na niiombe Serikali kama kuna sehemu tunataka kufanya siasa siyo kwenye huduma ya mama na mtoto. Huduma ya mama na mtoto ni ustawi wa Taifa letu kwa ujumla, ni eneo ambalo ni nyeti na ndiyo inasababisha kwenye ustawi wa shughuli zetu za maendeleo kama tutakuwa na mama mwenye afya akajifungua mtoto mwenye afya bora. Sasa bila kusimamia kwa dhati kwa sababu Sera zipo, Miongozo ipo lakini

utekelezaji umekuwa mgumu. Bila kusimamia eneo hili la utekelezaji sawasawa bado tutakuwa tunafanya siasa na kifo cha mama na mtoto nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Majengo–Korogwe Hospitali ya Wilaya yameshatokea haya akinamama wameenda kujifungua wameombwa fedha bila fedha na wanapiga simu. Mheshimwia Waziri nataka nikwambie moja ya eneo ambalo nimetangaza vita na watoa huduma ya afya kwenye Mkoa wa Tanga ni hili la afya ya mama na mtoto. Nimewapa namba zangu za simu wale akinamama wakishamuingiza kwenye kumi na nane mtoa huduma anayeoomba fedha, Mheshimiwa Waziri nitamsukumia kwako na ikitokea umechukua muda Mheshimiwa dada yangu Ummy Mwalimu nakupenda sana lakini kwenye eneo hili kama haitapatikana tiba ya dhati ya kuondoa kweli kwa dhati na kwenye utekelezaji ikaonekana kwamba mama na mtoto wanapata huduma bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema naweza kushika Shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Lakini eneo hili ni gumu, eneo hili linatia uchungu akinamama wanapata shida, kipato chao ni kidogo hata hicho ambacho Serikali imeamua kukitengeneza kwa ajili yao na chenyewe hakipatikani. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya *windup* atoe maelekezo ya Serikali ni kwa namna gani wataenda kusimamia *perpendicularly* kwa dhati kabisa mama na mtoto apate huduma bora bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Catherine Valentine Magige atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle. Mheshmiwa Tecla Mohamedi Ungele ajiandae.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Afya inayoongozwa na mwanamke shupavu, jasiri ambaye halali usiku na mchana akihakikisha anamsaidia Mheshimiwa Rais kuboresha huduma za afya na si mwingine bali ni Mheshimiwa Ummy Mwalimu akisaidiana na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mollel nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi katika huduma ya afya ikiwemo afya ya wakinamama wajawazito na watoto. Vilevile tunaona hii *Royal Tour* pia fedha nyingi zitakazopatikana zitaenda katika huduma ya afya na kwenye kuboresha pia afya ya wamama wajawazito na watoto. Wanawake wa Arusha tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali za rufaa za mikoa. Sisi wa Mkoa wa Arusha tunaomba hospitali yetu ya Mkoa ya Mount Meru iboreshwe ili iweze kuwatibu wananchi pamoja na

watalii sambamba na uboreshaji wa hospitali hii tulikuwa tunaomba Madaktari Bingwa katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kufahamu ni kiasi gani cha pesa zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa Hospitali ya *Mount* Meru ya Mkoa wa Arusha? Mkoa wa Arusha katika Jiji la Arusha tulikuwa tuna kiwanda cha dawa lakini kiwanda kile hakifanyi kazi muda mrefu sana. Kiwanda kile kilikuwa chanzo cha ajira kwa wananchi wa Arusha na mikoa iliyo jirani na Mkoa wetu wa Arusha. Vilevile kilikuwa kinaongeza mapato katika Jiji la Arusha. Tunaomba Serikali mliangalie hili, kiwanda hiki cha dawa cha Arusha kiweze kuanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais kwa kupeleka pesa nyingi katika ununuzi wa dawa na vifaatiba. Tumeona mwaka huu zimetolewa Shilingi bilioni 129 *MSD,* lakini cha kushangaza, kama Mheshimiwa Rais kaidhinisha Shilingi bilioni 129 kwenda *MSD,* ni kwa nini kuna upungufu wa dawa? Ina maana pale kuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko *MSD*. Mabadiliko haya yatasaidia sana. Tumeona amemteua Mkurugenzi kijana ambaye tumeambiwa ana uzoefu katika masuala mazima ya dawa. Nina imani kabisa mabadiliko haya yataleta tija katika upatikanaji wa dawa na vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeona mjumbe wa bodi ni mwanamke. Jamani, tunaona mfano, alipo mwanamke haliharibiki neno. Mmeona mama Rais wetu ni mwanamke, mmeona wafanyakazi sasa hivi wanacheka, huyo ni Rais mwanamke. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Bodi kwa sababu ni mwanamke, waziri naye ni mwanamke, najua kabisa mambo yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tunaomba sana mkajipange, Rais ameshatoa mwelekeao, miezi mitatu minne inawatosha kabisa kujipanga kuhakikisha wananchi wanapata dawa. Hatutaki tena kusikia sababu sababu, tunachotaka wananchi wapate dawa na vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna upungufu wa madaktari. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, katoa ajira, wameajiriwa katika Sekta ya Afya wafanyakazi wengi, lakini hawatoshi. Tunaomba atoe ajira zaidi kwa wauguzi na wakunga ili wananchi wasipate changamoto tena. Vilevile tumekuwa tukisikia changamoto katika Hospitali za Serikali juu ya huduma. Wizara ya Afya tunaomba mliangalie hili mhakikishe changamoto hizi zinafikia ukomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, vilevile tunashukuru Wizara nzima ya Afya, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Dkt. Mollel, mnafanya kazi kubwa sana. Tunaomba changamoto hizi ndogo ndogo tunajua haziwashindi. Afya ndiyo kila kitu,

tunawaamini, tunaomba mfanye kazi mwendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ummy Rais amekuamini na hujawahi kumwaibisha Rais. Tunaomba dada yangu Mheshimiwa Ummy ufanye kazi kwa bidii, tuna imani kubwa na nyie, tuna imani kubwa na Naibu Waziri, Katibu Mkuu; Mkurugenzi mpya wa *MSD,* na wewe na Mwenyekiti wa Bodi. Hatutaki tena kusikia changamoto za dawa na vifaatiba.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle atafuatiwa na Mheshimiwa Teclas Mohamed Ungele na Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kunipa uhai mpaka kufika leo. Pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuwafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Afya, sisi Kasulu tumeendelea kulamba asali kama alivyosema Mzee Makamba juzi. Tumepokea chini ya Mheshimiwa Rais Samia zaidi ya Shilingi bilioni 3.1 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kasulu DC. Pia tumepokea Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya Kitanga, tumepokea Shilingi

milioni 500 kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Afya cha Kurugongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepata pia Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba ambazo ziko *MSD*. Hapo nataka nigusie kidogo; Mheshimiwa Ummy yuko hapa; kwanza napongeza maamuzi ya Mheshimiwa Rais kufanya *overhaul* kwenye *MSD* na kupata Mkurugenzi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mkurugenzi mpya na ninaamini kwamba ataenda kufanya marekebisho pale ambapo kulikuwa na changamoto ili kuhakikisha kwamba vifaatiba hivi na dawa vinafika kwa wakati. Nimtie moyo tu kwamba yeye sasa hivi ndio Mkurugenzi wa *MSD,* kwa hiyo, asiogopeogope. Pale ambapo kuna changamoto ambazo zinatakiwa kufanyiwa mabadiliko kisheria, amwambie Waziri atuletee sisi hapa ndio Wabunge tunaotunga sheria, turekebishe kuhakikisha kwamba hatuna changamoto za kisheria ambazo tunaweza kuzipitia.

Mheshimiwa Spika, Kasulu vijijini tunayo changamoto ya watumishi. Mheshimiwa Waziri sisi tuna watumishi 192 peke yake. Tunazo Zahanati 32 Vituo vya Afya sita na Hospitali ya Wilaya moja, lakini wote hao wanahudumiwa na watumishi 192, ambayo ni sawasawa na asilimia 22 tu ya mahitaji yote. Chonde chonde, naomba sana Kasulu Vijijini katika jambo hili tupewe jicho la kipekee sana, kwa sababu watumishi wanafanya kazi sana, wanachoka. Tuna sekta kama upande wa mionzi, tuna mtumishi mmoja tu ambaye anahudumia

halmashauri nzima. Kwa hiyo, naomba sana jambo hilo litazamwe.

Mheshimiwa Spika, suala la wizi wa dawa, kwanza linafanya bima yetu ya afya kubeba mzigo mkubwa sana, kulipa dawa ambazo watu hawajatumia. Pili, inachafua mno Serikali yetu. Majengo mazuri, lakini hayana dawa. Mwananchi haendi pale kwa ajili ya kutazama majengo, anaenda kwa ajili ya kutafuta huduma. Sasa nina ushauri kidogo, huwezi kuzuia wizi wa dawa kwa kufanya tu ziara za kushtukiza hospitali. Utafanya ngapi?

Mheshimiwa Spika, huwezi kuzuia wizi wa madawa kwa kusema kwamba ile sheria ambayo tuliipigia kelele kidogo kwamba maduka ya dawa yajengwe mbali na zahanati au na Kituo cha Afya, Hapana. Kwa sababu yakijengwa hapo hapo au mbali, wizi kama upo, upo tu. Hoja yangu ni kwamba, katika dunia ya leo ambayo teknolojia imekuwa kubwa sana, Mheshimiwa Waziri unayo fursa ya kuja hapa kutuomba hela tukupe fedha za kutosha uweke mifumo thabiti ya *IT* ili kuweza kuondoa wizi wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda huko kwa wenzetu, suala la wizi wa dawa limeshaondoka, siyo kwa sababu ya vitisho wala kauli mbalimbali, Hapana. Ni kwa sababu wameweka njia ambazo ni za kisasa za mifumo ya kiteknolojia kwa ajili ya kulinda dawa. Wewe Mheshimiwa Waziri kipindi ukiwa ofisi kwako huwezi kujua kuwa Kasulu Vijijini kuna kiasi dawa kiasi gani? Siyo mpaka upige simu, uki-*click* tu unaona *track*. Njoo

uombe hela hapa Bungeni, tukupitishie uende ukafanye. Najua ni *investment* kubwa, lakini ukafanye kwa ajili ya maslahi mapana ya Watanzania, *otherwise* naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Teclas Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kujali afya za Watanzania, na wote tunashuhudia miundombinu mbalimbali imejengwa sehemu zote nchini Tanzania kwa ajili ya huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, pia hata bajeti naona inaendelea kuongezeka kidogo kidogo kwenye Fungu Na. 52, lakini naamini Mheshimiwa Rais kwa sababu anajali afya ya Watanzania, ataendelea kuongeza siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza Wizara ya Afya; Mheshimiwa Ummy Mwalimu na timu yake yote mpaka kule vijijini kwenye ngazi ya kaya, watoa huduma za afya wanaendelea kutoa huduma na ushauri nyumba kwa nyumba.

Mheshimiwa Spika, najikita kwenye magonjwa yasiyoambukiza. Magonjwa yasiyoambukizwa ni tatizo kubwa na ni kilio kikubwa nchini Tanzania, pia ni gharama kwenye matibabu na athari yake ni kubwa sana. Wote tunashuhudia, miaka iliyopita hakukuwa na tatizo kubwa la shinikizo la damu, wala moyo wala sukari, lakini sasa hivi kila familia, na kama siyo kila familia hiyo, basi hata jirani yako anakumbwa na tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu za magonjwa yasiyoambukiza, machache ni mtindo wa maisha tunayoishi, vyakula vyetu, kutokufanya mazoezi, utumiaji wa tumbaku, matumizi makubwa ya sukari na kadhalika. Vitu hivi vinaweza vikazulika. Ukubwa wa tatizo, tunaona wakati wa janga la UVIKO lilivyoshamiri wagonjwa katika hospitali moja kule Dar es Salaam ilitoa taarifa kwamba asilimia 86 ya vifo ilitokana na wagonjwa ambao tayari walikuwa na kisukari, lakini asilimia 65 ya vifo vile vya UVIKO 19 tayari wagonjwa wale walishakuwa na shinikizo la damu na asilimia 45 tayari walishakuwa na pumu. Hivyo unaona magonjwa yasiyoambukiza ukiwa nayo, ukipata ugonjwa mwingine hali inakuwa ngumu zaidi,

Mheshimiwa Spika, tunaona pia hata mfuko wetu wa Bima ya Afya unalemewa kutokana na magonjwa yasiyoambukiza. Hata Mkoa wa Lindi kwenye Wilaya ya Nachingwea kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wenye magonjwa yasiyoambukiza kama presha na kisukari.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kifanyike? Ni ushauri wangu kuwa imefikia wakati sasa naomba tume maalum ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza ianzishwe, kama vile tulivyoanzisha *TACAIDS*. Kwa nini nasema hivyo? Tunaona sababu zinazoleta magonjwa yasiyoambukiza nyingi ni za kijamii; mtindo wa maisha, kutokufanya mazoezi, *consumption* ya tumbaku; pia tunaona sababu nyingi ni za kiuchumi. Sehemu nyingi katika nchi yetu, tumbaku ndiyo uchumi, miwa ndiyo uchumi, na pombe ndiyo uchumi. Sasa tunafanye kujikwamua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiachia suala la magonjwa yasiyoambukiza kwenye afya peke yake itakuwa ngumu kama ilivyotuumiza kwenye UKIMWI. Hivyo basi, tuliache jambo hili, afya waendelee kushughulikia matibabu, lakini pia kijamii tuendelee kuwa na mkakati maalum wa kuendelea kushughulikia magonjwa yasiyoambukiza. Tunaona hata wakati wa masuala ya UKIMWI, sasa hivi tayari wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI wana uwezo kabisa wa kutambua kwamba hapa nifanye jitihada za kuzuia ili nisipate maambukizi mapya. Pia wale hawajapata kabisa, jamii inaelewa kwamba tusipate maambukizi mapya.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, naomba hata kwenye magonjwa yasiyoambukiza, suala hili tuliache kwenye jamii, kwa sababu ni suala mtambuka, kila sekta ina husika kwenye masuala haya katika kuhamasisha kuzuia magonjwa yasiyoambukiza. Vinginevyo tutaendelea kugharamika bajeti itaendelea kuwa kubwa na kila familia itaendelea na simanzi

kwa sababu ya athari ya magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham atafuatiwa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo ajiandae**.**

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu. Kwanza pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kusimama na kuweza kuchangia kwenye Wizara ya Afya. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayofanya. Anafanya kazi kubwa sana. Kiukweli tumpongeze, anafanya kazi kubwa, ameweza sana kuwekeza kwenye Wizara ya Afya na ameweka pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Ummy, amejaribu sana kujibu maswali yangu kwenye hotuba yake, lakini naamini kwamba itaenda kufanya kazi vizuri zaidi. Kiukweli Wabunge wengi ambao wakisimama hapa kuchangia hawatakosa kutaja vitu vitatu tu ambavyo vinawaathiri Watanzania kwenye suala la afya. Hatuwezi kujenga Taifa lenye uchumi mkubwa kama watu wetu hawana afya ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila anayesimama hapa, changamoto ya kwanza atakwambia ni dawa, changamoto ya pili atakwambia vifaatiba na changamoto ya tatu atakwambia upungufu wa watumishi. Hatuwezi kukwepa. Mheshimiwa Ummy nikwambie, huwezi kukwepa hilo, unatakiwa uende ukafanye kazi kubwa sana kwa kushirikiana na Naibu wako. Kwa sababu ukitoa mfano kwenye jimbo langu, nina *deficit* ya wafanyakazi wa utumishi wa afya asilimia 67. Mbunge mwenzangu aliyepita hapa amesema anao watumishi asilimia 22, kwa maana maana *deficit* ni asilimia 78. Ukipiga hesabu kwenye nchi nzima, inawezekana *deficit* ikawa asilimia zaidi ya 60 watumishi wa afya hamna. Hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia kwenye suala la vifaatiba, vifaatiba hakuna. Jimboni kwangu kuna *X-Ray* ya miaka 20 na zaidi haifanyi tena kazi, tumehangaika kuitengeneza na Mkurugenzi wangu wa Wilaya zaidi ya mwaka mzima, imeshindikana kabisa. Hakuna taasisi yoyote inayotoa huduma ya mionzi kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatakiwa waende kilometa 75 wilaya nyingine kupata huduma ya mionzi kwa maana ya *X-Ray*. Huyu mwananchi ataweza wapi ku-*afford* hiyo gharama? Gharama ya *X-Ray* ni Shilingi 10,000/=. Nauli Shilingi 10,000/= kwenda, kurudi Shilingi 10,000/=, hajala, huyo mtu hawezi kufanya hivyo vitu. Tunaomba sana Mheshimiwa uende ukalifanyie kazi. Nafikiri kwenye ofisi yako nina maombi

ya *X-Ray* muda mrefu sana. Naomba pia hilo uende ukalifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, hatuna *ambulance* kwenye Jimbo langu. Ukiwauliza Wabunge wengi hapa watakuwa wamenunua vigari kwa ajili ya kusaidia wananchi wao kama *ambulance,* na ndiyo ukweli ulivyo. Ina maana vifaatiba bado havitoshi. Changamoto bado ni kubwa! Hizi changamoto tatu ni lazima ukazifanyie kazi, vinginevyo hatuwezi kujenga Taifa lenye uchumi mkubwa kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lingine lazima niseme, nilileta tena maombi kwenu kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya yangu ya Ulanga. Hospitali hii hali yake ni mbaya sana. Ukienda maabara ya Hospitali ya Wilaya ya Ulanga, unaweza kusema labda hiki ni chumba na sebule ya Manzese. Ni kitu ambacho kinawakwaza sana wananchi. Miaka sita iliyopita tulipata pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa hospitali ile. Hospitali imejengwa enzi ya mkoloni, lakini kila ilipokuwa inaguswa kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati, ilikuwa haiwezekani, inaharibika zaidi. Wakafanya maamuzi ya kujenga majengo mengine. Sasa ardhi imejaa, hospitali imejaa, haiwezekani tena kwenda kuongelea majengo.

Mheshimiwa Spika, sisi ardhi tunayo, tunaomba mtujengee Hospitali yetu ya Wilaya ili tuweze kupata huduma bora. Kiukweli kuendelea kujenga Zahanati na Vituo vya Afya, kama hatuna huduma za kutosha ni sawa sawa

tutakuwa tumejenga magofu, hali ya afya bado ni ngumu. Fanya tathmini ya Wabunge wote wanaochangia hapa ndani, hizi ndiyo changamoto wanazozitaja. Vinginevyo ni kwa sababu tunatakiwa tuendelee kuchangia, lakini vinginevyo changamoto zako ambazo unatakiwa kwenda kuzifanyia kazi Mheshimiwa Waziri zote zinatamkwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto kubwa sana kwenye dawa. Inawezekana kuna tatizo *MSD* na Serikali, sijui ni ipi, lakini inawezekana kuna tatizo. Mwingine amezungumzia suala la wizi. Wizi kweli haukwepeki. Ni lazima tunapotoa hizi fedha tuangalie na mfumo wa udhibiti wa dawa. Ni lazima tuangalie mfumo wa udhibiti, ni mbaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali yangu ya Wilaya mwaka 2010 *population* ya watu ilikuwa 150,000. Ndani ya miaka 10 tu leo tunaenda kuzungumzia watu 200,000, bado hospitali ni ile ile ya mwaka 1970, hatuwezi kufika. Tunaendelea sana kujitahidi na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini tunambebesha tena huu mzigo mwingine, bado huduma ya afya siyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda vijijini ukianza kuzungumzia suala la Bima ya Afya, wanakijiji wanaweza wakakutukana matusi. Hawaelewi suala la huduma ya Bima ya Afya, kwa sababu anabeba kadi yake, akienda hospitalini hapati huduma. Bado utamshawishi huyo mtu akate bima! Ya nini?

Yaani umeenda hospitalini na kadi yako na unaambiwa dawa hamna. Hakuna sababu. Kwa hiyo, wananchi hao pia kuzungumza nao kuhusu kuwashawishi kukata huduma za bima, inakuwa ni vigumu sana kwa sababu ni wagumu pia kuelewa pia kwamba kweli wakienda na hizo kadi wanaweza kupata huduma katika hospitali.

Mheshimiwa Spika, haya niliyozungumza ndiyo changamoto ya Tanzania yetu. Mheshimiwa Waziri naomba uyapokee, uyafanyie kazi. Vile vile napenda sana utembelee kwenye jimbo langu baada ya Mkutano huu kuahirishwa ili ukajionee haya ambayo nimekwambia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA.** Ahsante sana, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, Mheshimiwa Kabula Shitobelo ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya dakika hizi chache niweze kutoa mchango wangu kwenye wizara hii muhimu sana ya ulinzi wa Maisha ya watanzania.

Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Wake pamoja na Katibu Mkuu na Sekretarie nzima ya afya kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia Ilani ya Uchaguzi ambayo

imeelekeza kuhakikisha ya kwamba Watanzania wanapatiwa afya na tiba ambazo zinalinda afya zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu maelekezo yake mengi yamekuwa yakifanyiwa kazi kwa usahihi. Pale Mwanza kwenye Jimbo la Nyamagana ambapo kuna Hospitali ya Mkoa wa Mwanza inayoitwa Seketoure, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu sasa baada ya kupata takribani shilingi bilioni 10 jengo limekamilika zaidi ya asilimia 98. Na hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Waziri, leo narudia tena, niwapongeze sana kwa maamuzi mazuri yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais zile fedha za UVIKO zilipelekwa kwenye maeneo ya afya ili kwenda kutatua changamoto vya vifaa.

Mheshimiwa Spika, Seketoure peke yake ilipata takribani bilioni mbili na milioni mia saba, Mheshimiwa Waziri kwa maelekezo imetumia zaidi ya asilimi 68, bilioni moja na milioni mia nane kununua vifaa vya lile jengo lote ulilolishuhudia pale, lakini asilimia 32 peke yake ndiyo imekwenda kwenye matumizi mengine ikiwemo nyumba ya muuguzi atakayekuwa anakaa pale, *furniture* na vifaa vingine.

Mheshimiwa Spika, sasa haya ni moja kati ya matokeo ambayo tunaamini wizara hii; Mheshimiwa Sekiboko amesema pale juu ya kulinda vifo vya mama na Watoto, na Mheshimiwa Waziri nikuhakikishie baada ya kuimarisha Hospitali ya Seketoure imeendelea kupunguza vifo vya mama na mtoto kutoka 18 mpaka vifo nane leo. Hatuna

shaka ya kwamba vifo hivi vitaendelea kushuka sana kwa sababu ya uimarishaji bora wa huduma hizi za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwa haraka sana kwa sababu ya muda, ni kuhusu ulinzi na uimarishaji wa viwanda vyetu vya ndani vya dawa. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea pale *MSD*. Miongoni mwa mambo aliyoyapongeza ni kuona Kiwanda cha Keko *Pharmaceutical* pamoja na jitihada ndogo zilizokuwepo kimepiga hatua ya kuendelea kuzalisha dawa zinazohitajika ndani.

Mheshimiwa Spika, lakini nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, kiwanda hiki uwezo wake ni asilimia 36 peke yake. Tumekwenda pale na kamati yako ya *PIC* tumejionea shughuli na changamoto nyingi zilizokuwepo pale. Niombe, *MSD,* Keko *Pharmaceutical* wanahitaji bilioni 12 peke yake ili wafikie uwezo wa dawa zote 10 zinatakiwa hapa.

Mheshimiwa Spika, na nimpongeze sana mkurugenzi mpya wa *MSD,* ninaamini Serikali, Waziri Mheshimiwa Ummy na Serikali mmefanya nafasi yenu. Hili wala si la kufumbia macho, popote jicho lako linapokwambia kuna shida inaweza kukwamisha maendeleo ya sekta ya afya chukua maamuzi na amua mara moja ili tuweze kutoa tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunamkurugenzi mpya *MSD,* sina shaka na yeye atakuwa na nafasi yake kwenye maeneo ya

ndani ya utawala wake. Na Mheshimiwa Waziri tukifumbiana macho katika sekta ya afya ambayo ni moja ya sehemu ya ulinzi wa taifa hili hii ni zaidi ya kiwanda cha mabomu. Mheshimiwa Waziri usipolinda sekta ya afya vizuri nataka nikuhakikishie watu wako watakufa kwa magonjwa, watu wako watashindwa kupata tiba na sisi tutakuwa hatuna maana ya kuwepo hapa ndani kwa sababu moja ya jukumu letu ni kuwapa nguvu viongozi mliopewa nafasi ya kusimamia sekta hii; na sisi tunawaunga mkono tunaamini sasa changamoto zote zilizokuwepo *MSD* zitakwisha na hata hiki kiwanda cha Keko.

Mheshimiwa Spika, tumetembelea pale sisi, meneja anayekisimamia na wasaidizi wake wengi wote ni akina mama. Kwa hiyo, tunaamini akina mama katika ile eneo la kusimamia kazi zenu kwa nguvu mkurugenzi atasimamia na atafanya kazi yake vizuri. Tunataka tuione *MSD* kwenye kiwango cha kimataifa. Tupate ithibati ili tuuze dawa mpaka kule kwenye nchi za *SADC* kwa kufanya hivyo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine tunaomba kufahamu, Mikoa ya Kanda ya Ziwa sasa hivi ugonjwa wa kansa umeendelea kuwa mkubwa sana. Mimi niwapongeze, sana mlipoweka nguvu kuhakikisha Hospitali ya Bugando inajenga jengo kwa ajili ya wagonjwa maalumu wa kansa, na sasa hivi jengo hili lipo takribani asilimia 98. Watu wa Bugando wamesimamia vizuri; na nimpongeze sana Mkurugenzi wa Bugando na timu yake nzima. Unajua watumishi wa afya

hawa pamoja na changamoto nyingi tulizonazo lakini hakika wanajitahidi kufanya kazi yao vizuri na wanastahili sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jengo hili la Bugando kukamilika kwake tunahitaji vifaa; kwenye bajeti yako hakikisha kadiri unavyoweza. Niwapongeze kwa sababu mmeshaanza na *Ocean Road*. Mmeweka kiwanda ambacho viwanda vya aina hii katika Afrika vipo vinne peke yake; na sisi dawa zote tunategemea Afrika Kusini. Leo tukiongeza cha kwetu kitakuwa cha tano katika Afrika. Maana yake ni kwamba, sasa ukiongelea lile suala la Mama anaupiga mwingi ulitazame kwenye *angle* hii, ambayo inakwenda kuokoa maisha ya wananchi wengi wa kanda ya ziwa; na kwa kufanya hivyo mtakuwa mmelisaidia sana taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mambo tunayoyasema si mambo mepesi. Wenzangu wameongea hapa juu ya mfumo wa ulinzi wa mapoteo ya pesa za *NHIF*. Leo ukitibiwa Bugando au Seketoure ukapata *referral* kwenda Muhimbili ukifika kule unaenda kuanza upya. Kumbe kungekuwa na mifumo hii ambayo inasomana vizuri ingekuwa ni rahisi daktari aliyepo kule Muhimbili kuona taarifa zako za Bugando na akawa na ulinzi mzuri kwa ile kadi na fedha ambayo mnaitoa ya *NHIF*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, najua kengele imegonga, hasa kwa sababu nilikuwa kwenye moto sijui ni ya pili sijui ni ya kwanza.

**SPIKA:** Ya pili Mheshimiwa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge tumpe ushirikiano wa kutosha Mheshimiwa Waziri tuipe ushirikiano wa kutosha Wizara hii, Katibu na timu yake nzima. *MSD* pia tuipe nguvu ili ifanye kazi vizuri.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabula Shitobelo, Mheshimiwa Cecilia Paresso, ajiandae.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii nyeti, Wizara ya Afya. Kwanza kabisa nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema lakini pia kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nipende kumpongeza Mheshimwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha wananchi wetu wa Tanzania wanakuwa na afya njema ili waweze kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri, Ndugu yetu na rafiki yetu, anafanyakazi kubwa sana kuhakikisha wizara hii inafanyakazi nzuri sana kwa wananchi wa Tanzania waweze kuwa na afya njema lakini niishukuru wizara nzima Naibu Waziri, Katibu Mkuu lakini na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kanda ya Ziwa tumekuwa na tatizo kubwa sana na changamoto kubwa ya kansa ya kizazi kwa sisi wanawake. Nimesimama kwenye Bunge lako kuongea tatizo hili kwasababu tumekuwa na changamoto hii wanawake wengi tumekumbwa sana na tatizo hili la kansa ya kizazi hasa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021 wanawake 36,224 waliofanyiwa uchunguzi wa kansa ya kizazi waliokutwa na dalili za kansa ya kizazi walikuwa ni wanawake 1,597 na wanawake 252 walidhaniwa kuwa na vimelea vya kansa ya kizazi, wanawake 66 walikutwa tayari na ugonjwa wa kansa. Hii inaumiza sana ukizingatia sisi ni wanawake na ukizingatia ndio tunaotegemewa katika nchi yetu na katika majukumu makubwa ya familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kubwa kwa Wizara ya Afya ni kutoa elimu kuanzia kwa mabinti zetu mpaka kwetu sisi akina mama ili kuweza kuelewa ni kwasababu gani tatizo hili limekuwa kubwa sana katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukienda Bugando kuna wagonjwa wengi sana wa kansa ya kizazi. Ukienda *Ocean Road* imejaa wagonjwa wengi sana wanaotoka Kanda ya Ziwa. Hii inaumiza sana, ukizingatia na sisi ni wanawake na Mheshimiwa wetu Waziri wa Afya ni mwanamke mwezetu. Ombi langu ni kuomba sana elimu itolewe kuanzia mashuleni kwa mabinti zetu na hata kwa akina mama ambao watakuwa wanakwenda kliniki hata wanaokwenda hospitali waweze kujua tatizo hili linapatikana vipi lakini pia linatibika vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ni nchi ya nne kwa tatizo kubwa la kansa ya kizazi. Tanzania inaongoza kuwa ni nchi ya nne. Kati ya wanawake 100, wanawake 59 wanakufa na kansa ya kizazi nchini kote; na Tanzania ikiwa ni nchi ya nne, hii inaumiza sana na inaumiza kwasababu ni wanawake wengi wanaopoteza maisha kutokana na tatizo hili kubwa. Niombe sana wizara hii iweze kuangalia kwa jicho la tatu tatizo hili kwa wanawake limekuwa ni sugu na linatuangamiza sana sisi wanawake, elimu itolewe sana kwa mabinti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hili nchi yetu ya Tanzania inaongoza kwa vifo vya kansa ambavyo tuna aina

tano za kansa katika nchi yetu ya Tanzania. Ukiacha kansa ya kizazi ya wanawake tuna kansa za ngozi, mkojo (kansa ya tezi dume), kichwa, shingo, koo na kinywa, pamoja kansa ya matiti. Magonjwa yote haya hayajatolewa elimu ya kutosha, hayafahamiki ni jinsi gani tunaweza kuyaepuka ili tuepukane na hili tatizo. Kwa hiyo, ombi langu kubwa kwa Serikali niombe sana iweze kutoa elimu kuanzia kwa mabinti zetu lakini pia iweze kuwafahamisha ni kwanini tatizo hili limekuwa sugu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vifo hivi vinavyoangamiza wanawake wenzetu na mabinti zetu ni vingi sana. Inavyoonesha tatizo hili ni sugu katika nchi yetu wanawake wanaokufa kwa kansa ya kizazi ni wengi. Kama takwimu zinavyoonyesha, kati ya wanawake 100,000 wanawake 59 wanakufa kwa kansa ya kizazi…*(Makofi)*

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Agnes Marwa.

**T A A R I F A**

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, natoa taarifa kwa muongeaji kwamba kutokana tatizo hili kubwa ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali Maalum ya Taifa kwaajili ya wanawake na watoto ikiwemo suala la hili la kansa kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo.

**FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ninaipokea, lakini ninaomba sana elimu itolewe, na hasa chanjo kwa mabinti zetu zipatikane. Kwasababu tatizo hili ni kubwa nasilakufumbia macho. Vifo vya kansa ya kizazi vimekuwa ni tishio katika nchi yetu hasa kwa upande wa Kanda ya Ziwa. Ni vifo ambavyo vinaangamiza sana wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara iangalie tena kwa jicho la tatu.Tunaliongelea suala hili hapa lakini wengi hawana elimu na hawajui kwasababu gani wanapata matatizo kama haya. Wengi wanapata tatizo hili wanatoka wanakwenda kutibiwa kienyeji, na wengi wanakufa kwa kukosa elimu.

Mheshimiwa Spika, tulipata tatizo la *HIV* katika nchi yetu elimu ilitolewa mpaka mashuleni wakajua nini chanjo cha tatizo la *HIV;* iweje leo wanawake waangamie kwa kukosa elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kubwa ni elimu kwa akina mama na vijana wetu. Chanjo hii kwa vijana inapatikana, kwanini vijana wetu hawapati chanjo? Niombe vijana wetu waweze kupatiwa chanjo hii ya kansa ya kizazi ili

tuweze kuepukana na hii changamoto. Sisi akina mama tukimalizika kwa tatizo kama hili nchi yetu itaendeshwa na watu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache lakini naomba sana, Mheshimiwa Ummy amenielewa Waziri wetu naimani atakwenda kulifanyia kazi kubwa ni mwanamke mwenzetu anawatoto wa kike na anajua changamoto ni kubwa. Hoja yangu ninayomalizia ni elimu itolewe sana kwa vijana wetu…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kabula Shitobela atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, ajiandae.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kutupa amani katika Taifa letu. Pili; napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza na kuiboresha sana Wizara ya

Afya. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya na Makamu wake, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Mollel na watu wote kwa kuongoza vizuri na kwa kuchapa kazi nzuri. Pia ningependa kuwapongeza sana wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali, mwaka 2015 Serikali iliweza kupunguza wastani wa vifo kutoka akina mama 11,000; mpaka kufikia 2020 Serikali iliweza kupunguza vifo 3,000 kwa taifa zima. Nakiangalia takwimu ya Kanda ya Ziwa mwaka 2019 akina mama 448 walipoteza maisha kutokana na uzazi, na mwaka 2020 akina mama 410 walipoteza maisha pia. Mwaka 2021 vifo 374 pia kupoteza maisha mwaka huo, 2020/2021. Hali hii bado si nzuri japo namba zinaonesha kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kuendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa zote zinazotibu magonjwa haya yanayosababisha vifo hivi vya akina mama, kama vile magonjwa ya kifafa cha mimba, chinikizo la damu kutoka damu nyingi kabla na baada ya kujingua na uambukizo wa vimelea kwenye mfumo wa uzazi. Pili; kupeleka madaktari bingwa na waganga wa akina mama, hasa katika hospitali za wilaya na mikoa. Hii itasaidia sana kubaini matatizo mapema na kumaliza kabisa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza Wilaya ya Buchosa Visiwani kuna tatizo kubwa hasa Visiwa vya

Maisome, Migingo, Lubalagazi pamoja na Buzikimba. Visiwa hivi vinachangamoto kubwa ya boti maji au *ambulance* ya kwenye maji. Naiomba sana Serikali itupelekee kule *ambulance* kwasababu akina mama wengi wanafariki dunia kwa kukosa huduma za haraka.

Mheshimiwa Spika, pia katika Visiwa vya Ukerewe kuna upungufu wa asilimia 56 ya watumishi wa afya, Wilaya nzima ya Ukerewe pamoja na kuwa ni visiwani hakuna *x-ray machine;* iliyopo kwa sasa niyakizamani sana imekuwa na tatizo la kuharibika mara kwa mara na inapelekea usumbufu wa wagonjwa kutoka pale Ukerewe wapande boti mpaka Mwanza Mjini ndipo waende kutibiwa. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie sana hasa kwenye miundombinu migumu kama Ukerewe kwasababu hakuna usafiri mwingine zaidi ya kupanda meli au boti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba sana Wizara Ummy Mwalimu, namwamini kabisa, ni dada jemedari, hodari sana, ni jembe. Kwa hiyo naomba sana uangalie, hasa akina mama wenzangu kule Ukerewe na huku Bushosa Visiwani ambako kwakweli shida ni kubwa mno. Akina mama wanajifungulia njiani boti ikiharibika kidogo, mabapo inabidi wasubirie mpaka boti nyingine ifike ndiyo waweze kupata usafiri kuelekea Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiangalia tena katika Wilaya ya Kwimba kijiji cha Nyambiti Kituo cha Afya cha Nyambiti hakina jengo la upasuaji. Wananchi wamenunua vifaa kwa

kuchanga wao wenyewe. Sasa naiomba Serikali iharakishe kutusaidia kutuwekea japo hilo jengo kwasababu wananchi wameshatumia nguvu zao wenyewe kununua vifaa. Kwa hiyo, ninaomba sana, nakuomba sana ndugu yangu mtani wangu Ummy Mwalimu uwaangalie watani zako wa Kijiji cha Nyambiti na uwajengee hilo jengo ikiwezekana hata mwaka huu tutashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kumwongelea mtoto njiti, ndani ya miezi minne watoto 1,000 huwa wanalazwa hospitalini kwa magonjwa ya aina mbalimbali, lakini asilimia 50 ya watoto hao huwa ni watoto njiti na asilimia 25 katika watoto hao kwenye 50 *percent,* asilimia 25 ya vifo hivi ni mtoto njiti kwa sababu hawana kinga mwilini. Ushauri wangu kwa Serikali wawekeze upatikanaji lishe inayotolewa kwa njia ya mpira, upatikanaji wa vifaa vya kutunza joto la mwili *(incubator)* hasa kwenye Vituo vya Afya vya Vijijini kwa sababu sehemu za wilaya nyingi hazina vyumba maalum kwa ajili mtoto njiti. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE.KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu. Muda wetu ukiruhusu Mheshimiwa Francis Leonard Mtenga, atachangia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Afya. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu pamoja na timu yake, kwa kweli wanajitahidi na wanafanya vizuri. Pia Wizara hii imekuwa ikitupa ushirikiano sisi wajumbe wa Kamati kwa kadri inavyowezekana hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo mawili. Hoja ya kwanza ni katika eneo ya magonjwa yasiyoambukiza. Tunapoongelea afya ya Watanzania au magonjwa ambayo mengi yanayowasumbua Watanzania leo, mengi ni magonjwa yasiyoambukiza. Tafiti zinaonyesha asilimia 40 ya vifo nchini vinatokana na magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa haya ni kansa, sukari, *pressure* na kadhalika. Kwa kiwango kikubwa haya magonjwa yasiyoambukiza kwa namna moja ama nyingine kama tukiwa na mikakati ya kutosha kama Serikali lakini kama jamii ikatambua athari ya magonjwa yasiyoambukiza basi tunaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa na badala ya Serikali kufikiria kutibu, kwa sababu tunavyoongelea Hospitali za Rufaa zina upungufu wa dawa na kila kitu ni kwa sababu ya ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza. Sasa tukiweka nguvu huko maana yake tutaweka kinga zaidi badala ya kutibu.

Mheshimiwa Spika, hata leo Serikali wanapoomba bajeti kwenye Wizara hii ya Afya zote zinaenda kutibu siyo kukinga, kwa sababu ya aina ya maisha ya Watanzania ambayo tulikuwa nayo huko nyuma, tumepata magonjwa yasiyoambukizwa kwa wingi. Hivyo tunaweka nguvu kubwa katika kuyatibu. Nashauri Serikali na wadau mbalimbali sasa tuweke pia nguvu kuhakikisha tunaweka kinga kwa magonjwa yasiyoambukiza ili hii asilimia 40 ya vifo inayotokana na magonjwa ya kuambukiza, basi tuweze kuipunguza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo lazima jamii ipewe elimu na kueleweshwa. Kuna mambo mengine kwa mfano mtindo wa maisha tunayoishi, wakati mwingine yanapelekea ndiyo tunapata sukari, tunapata *pressure*, mtu anaona anaishi maisha fulani ndiyo yuko sawasawa kumbe siyo sahihi. Kwa hiyo nadhani Serikali kwa kushirikiana na Wizara nyingine mtambuka pamoja na wadau tuone namna ya kubadilisha maisha ya Watanzania tunayoishi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, leo vijana wetu wa bodaboda wanaendesha bodaboda siku nzima, *ok* wamejiajiri wapate kipato lakini hawa vijana wanakunywa kinywaji maarufu kinachoitwa *energy drink* ambazo ziko za aina mbalimbali. Hawa vijana wanaweza kunywa *energy drink* tatu, nne, tano kwa siku, huyo utegemee baada ya miaka 10 au 20 Serikali tutaanza kumtibu kwa sababu amepata magonjwa yasiyoambukiza. Yeye leo anaona yuko

sawasawa inawezekana hajui madhara na ni kweli kwamba wengi hawajui madhara.

Mheshimiwa Spika, siyo hao tu nimetoa mfano mmoja wa kundi moja la vijana wa bodaboda kwa sababu tunawaona, wako wengine wengi tu wa makundi mbalimbali hata watu ambao wapo maofisini, kwenye sekta binafsi mtu anaona kunywa *energy drink* labda ni *Red Bull* au nini ananunua 3,000 mpaka 4,000 anaona ni ufahari kwa sababu ni kinywaji ambacho angalau kina bei fulani, kumbe ni kinywaji ambacho tunajitengenezea matatizo mwisho wa siku tunapata kansa, tunapata kisukari, sijui wanasema maini yanavimba, mimi sielewi vizuri utaalam. Lakini yote hayo yanapelekea kwenye…

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso ngoja, ngoja twende vizuri kwa sababu hapa Bungeni pamoja na mambo mengine hizo biashara zinazosemwa hapo ni biashara za watu, sijajua kitaalam kama hivyo vinywaji unavyovisema ndivyo vinavyoleta hayo magonjwa unayoyasema. Maana kama Serikali imeruhusu viuzwe halafu vina madhara hayo makubwa unayoyasema itakuwa mtihani. Hapa kuna kimoja ambacho umekitaja mahsusi. Sasa ili usitupeleke kwenye hiyo hoja, hoja yako ni ya msingi lakini usitupeleke kwenye hiyo hoja ya wafanyabiashara fulani kuona wao wanaonewa na Bunge. Hebu hiyo sehemu ya mchango wako rekebisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa maelekezo. Nirekebishe tu kwa kusema

vinywaji vya kuongeza nguvu kwa ujumla wake vinavyoitwa *energy drink* kwa ujumla wake, sasa pamoja na kwamba vinapata kibali vinaingizwa, lakini Serikali ione namna gani ya kutoa maelekezo ya unywaji ulio bora ili tusije tukaingiza Taifa au watu wetu kwenye magonjwa yasiyoambukizwa kwa kuleta madhara kimwili na kiafya. Kwa hiyo hilo ni upande mmoja katika vinywaji hivi vya kuongeza nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la utumiaji usio sahihi wa…

**SPIKA:** *Sasa Mheshimiwa Paresso hapo umeeleza vizuri, hebu sasa ondoa yale maneno yako ya Red Bull.*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naondoa yale maneno niliyotaja ya *Red Bull*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine pia ni utumiaji usiyo sahihi wa viatilifu kwa wakulima. Wakulima wetu wengi wanatumia hayo madawa mashambani kwa namna isiyo sahihi, pamoja na kwamba vinapata vibali, vinaingia, kuna ukaguzi na vitu kama hivyo, lakini hawatumii kwa namna isiyo bora. Kwa hiyo wasipotumia kwa namna isiyo bora tutegemee mwisho wa siku na huko vijijini tunaona. Kwa mfano sisi tunaotoka Karatu kuna bonde moja linalima vitunguu pale.

Mheshimiwa Spika, ukifika wakati wa kupulizia dawa wanapulizia tu ilimradi mtu anachukua bomba anapuliza, hana namna yoyote ya kujikinga. Kule pia kuna shida kubwa

watu wanaanza kuwashwa na wanaanza kupata magonjwa ya ngozi. Huyu mwisho wa siku akiendelea muda mrefu kuna nafasi kubwa sana ya kupata ugonjwa wa kansa. Kwa hiyo iko namna ya kutazama pia kwa wakulima wetu tuwasaidie, kuwepo na mbinu mbadala kwa kushirikiana Wizara husika na Wizara zingine Wizara za Kisekta tuone namna gani pia wakulima wetu watumie kwa usahihi hivi viatilifu ili kuondokana na hatari ya kuingia kwenye magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine pia, suala la kutokufanya mazoezi ni sehemu pia ya namna ambavyo tunajiweka kwenye mazingira hatarishi ya kupata magonjwa yasiyoambukiza. Tunafahamu siku hizi kuna kampeni mbalimbali za kufanya mazoezi, ni kweli lakini ni wachache, Watanzania walio wengi bado hawajui manufaa ya kufanya mazoezi. Mfano mtu anakaa ofisini au yuko nyumbani anafanya hivi, anakula wanga wa kutosha akitoka hapo hafanyi mazoezi hajishuhgulishi hafanyi chochote. Huyu utegemee baada ya miaka 10, 20 anaanza sukari, anaanza *pressure,* Serikali inaanza kuweka nguvu kubwa sasa ya kutibu *pressure* yake na sukari yake, lakini kumbe tungeweza kuweka nguvu kubwa ya kupunguza hiyo *life style* yake au kwa kufanya mazoezi kwa kupunguza hatari kubwa ambayo iko mbele yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe rai kwa Serikali pamoja na wadau tuweke nguvu kubwa ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, tutoe elimu kwa Watanzania kwa

kushirikiana na wadau mbalimbali, Watanzania wajue namna ya ulaji sahihi na kwa wakati, wafanye mazoezi, ili basi tuone kwamba tunapunguza haya yaliyoko mbele yetu ya vifo karibu asilimia 40 vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Spika, suala la pili nizungumzie vifo vinavyotoka na uzazi. Kupitia Hotuba ya Waziri ameeleza vizuri sana angalau vinapungua vifo hivi vinavyotokana na uzazi, lakini bado takwimu zinaonyesha vifo hivi bado ni vingi sana. Pamoja na kwamba kuna jitihada zinazoendelea lakini pia uhudhuriaji wa *clinic* kwa akinamama wajawazito umeeleza na mpango wa kuhakikisha Serikali inatoa elimu kwa akinamama wanaohudhuria *clinic* ni jambo moja zuri, lakini hata pale wanapofika *clinic* wanapokelewaje, hapo pia kuna tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mtu anaweza akaenda tu anapimwa anaondoka zake, yaani samahani kusema haya, baadhi ya manesi utakuta tu maskini anampokea mama mjawazito yeye mwenyewe amenuna kweli kweli. Yaani huwezi jua alikotoka kule ana mazingira gani, inawezekana ugumu wa maisha, inawezekana ndivyo alivyo, lakini tuangalie pia hii *customer care* kwa akinamama wanaofika pale *clinic,* anapokelewaje. Ndiyo atahudhuria, tutawahamasisha kweli wahudhurie na hapa wameonyesha takwimu zinaongezeka kidogo, lakini bado wako wengine wengi ambao hawahudhurii. Akifika pale anapokelewaje, anakaguliwaje, yuko katika hatua gani anapewa maelekezo gani na

maelekezo gani na maangalizo gani ili anapofikia hatua za kujifungua au akiona dalili fulani hatarishi afanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hilo ni muhimu sana, wakaweka ama ni dawati hapo pekee maalum, akishamaliza kwenye vipimo awe na mtu wa kumsemesha. Nikwambie ugumu wa maisha uliyopo leo pia kwa kiasi kikubwa unachangia, mama ametoka huko maskini ana *stress* za maisha huko, *stress* za familia, jamii inayomzunguka akifika pale anatamani apate *comfort* fulani kwa kuongea unajua sijui wataalam wanasema hata ukisema una-*release stress* uliyonayo. Kwa hiyo afike pale kwenye kituo anaenda *clinic* lakini anakutana na mtu ambaye pamoja na atampa ushauri wa hali yake ya ujauzito lakini apate hata haya mengine ya kupumua ili huyu mama mwisho wa siku aweze kujifungua salama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, mchango wangu ni huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ili kutoa mchango wangu mfupi katika Wizara hii ya Afya ambayo kimsingi ni Wizara muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu na *sustainable development* kwa ujumla katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nataka niseme kwamba, imani kubwa ambayo Watanzania wameendelea kuwa nayo kwa Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kiwango kikubwa imani hiyo inachagizwa na mambo makubwa ya msingi yanayotokana na upelekaji wa huduma za msingi kwa wananchi. Jambo ambalo limeendelea kuwafanya Watanzania waendelee kuwa na *trust* na Serikali iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu kubwa mbili. Kwanza kabisa, Rais wetu Mama yetu aliyoko madarakani Mama Samia Suluhu Hassan amefanya juhudi kubwa sana na hatuwezi kuacha kulisema hili. Tumekuwa tukizungumza habari ya *revolution* kubwa iliyofanyika katika kuboresha masuala mazima ya Afya katika Mikoa, Wilaya mpaka Kata. Rais wetu tunampongeza sana na jambo hili mimi nasema kwamba tukiendelea kumpongeza Rais kwa mambo haya anayoyafanya tukaacha kuifanya Serikali na baadhi ya watendaji kuwajibika kwa makosa ambayo yanaweza yakamtia Rais doa tutakuwa hatulitendei haki Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo kwa sababu kubwa mbili. Miezi minne iliyopitia tumemsikia Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipita na kulalamika nchi ikiwa inakumbwa na upungufu mkubwa wa madawa kuanzia kwenye Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Mikoa mpaka Hospitali za Rufaa. Kama hilo

halitoshi, tumemsikia Waziri wa Afya akilalamika upungufu wa madawa kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme na Mheshimiwa Ummy naomba anisikilize kwa makini sana Bunge hili sisi tuko hapa kwa sababu ya *legacy* ya kuhakikisha kwamba wale wananchi waliotuchagua ambao ndiyo walipa kodi tunakuja kuwasemea na kuhakikisha kwamba *welfare* zao zinatekelezwa na Serikali iliyoko madarakani. Kitendo cha wapiga kura wetu ambao ndiyo wananchi tunakwenda kwenye mikutano ya hadhara, tunahutubia mikutano tukimaliza tunaambiwa Mbunge mmetujengea Kituo cha Afya dawa ziko wapi. Jambo hili lazima lifike mahali likome kwenye Taifa letu, watu wanaotuchagua na sisi kama Wabunge ambao tunatokana, kwa mfano kama mimi natokana na Chama Tawala. Chama changu kimepewa ridhaa ya kuongoza Taifa kwa sababu kilikuwa na *election manifesto*, kimeahidi mambo ya kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, jambo la ukosefu wa dawa nakwambia limekuwa kero kubwa kwa wananchi huko mtaani na wananchi wetu wapiga kura wamekuwa hawatuelewi. Jambo la kusikitisha Serikali inatoa fedha, *MSD* inapelekewa pesa, Mheshimiwa Waziri Ummy watuambie jambo gani linatokea dawa haziendi kwa wananchi? Jambo gani linatokea *MSD* huko dawa hazifikiwa kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu analalamika, Waziri analalamika, *what's going on* kule *MSD*. Hili jambo nalisema kwa dhati ya moyo wangu, sisi kama Wabunge na mimi kama Mbunge ninayetokana na chama kilichopo madarakani, tunawapa Wizara muda wa matarajio, tunaomba jambo la ukosefu wa dawa kwenye Taifa hili, tunawapa miezi minne au mitano, tutakuja hapa Bungeni… *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na tatizo kubwa lililotokea *MSD,* naomba Bunge na nimwongezee Mheshimiwa Kingu kwenye taarifa yake, ni vizuri Wizara hii ifanye *special audit MSD* ili ambaye anatuhumiwa, kazi iendelee. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu, unapokea taarifa hiyo.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naipokea kwa sababu mimi nimetumwa na wananchi nije niwe sauti yao kwenye matatizo yao. Wananchi wa jimboni kwangu moja ya changamoto zinazowakumba hakuna madawa, Mama Rais anatoa fedha na Serikali sisi Wabunge tunaidhinisha hapa bajeti, Bunge lako linaidhinisha bajeti zinakwenda kwa nini dawa hazifiki? Hili jambo nataka

niwaambie Wabunge sisi ndiyo tutakaoenda kuulizwa kule, sisi ndiyo tunaounda Serikali, lazima tusimame imara hapa Bungeni kuhakikisha Serikali yetu tunai-*task*, kuhakikisha kwamba dawa zinawafikia wapigakura wetu na walipakodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hilo hilo linaloendana na dawa. Nataka nimshauri Waziri waende wakalete Sheria tuje tuwapitishie. Tuunde kitu kinaitwa *Health Commodity Revolving Fund,* tuweze kuwaundia chombo cha Kisheria. *TANROAD* wana chombo chao cha kuleta fedha kwa ajili ya dawa, maji wana chombo chao. Afya ni jambo muhimu linalohusiana na masuala mazima ya usalama wa Taifa, waende wakalete Sheria tutawaundia Mfuko wa Fedha wa Dawa. Mfuko huo utafutiwe vyanzo vya uhakika vya fedha ili kuwasaidia watu wetu waweze kuhakikisha kwamba wanapata uhakika wa dawa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu tutautafutia vyanzo vya uhakika vya *fund* ili kusudi uweze kuwasaidia watu wetu na tuweze kulisaidia Taifa letu. Nataka niwaambie nipo kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, Makamu wangu Mwenyekiti yuko jirani hapa, hapa kuna wajumbe tuko tayari, Wizara ilete hiyo sheria, tutaichakata, tutaileta Bungeni, tulisaidie Taifa waweze kuwa na *special fund* ya kusaidia mambo ya dawa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu, Madaktari wetu, naomba wanisikilize kwa makini sana Waheshimiwa

Wabunge. Tunapozungumzia jambo la Madaktari kwenye Hospitali za Umma, *public facilities,* Daktari anakwenda pale anakaa dakika 20 anatibu, anakimbia anakwenda hospitali B, anatoka hospitali B anakaa dakika 10 anakimbia, anakwenda hospitali C. wanahangaika kujikimu maskini, Mheshimiwa Ummy dada yangu niwaombe Madaktari hawa kama walivyo watumishi wengine ni watu wamesoma hizi taaluma zao, wanatibu, haya mambo ni mambo ya usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara waende wakahakikishe zile *package* za *percentage* wanazozipata *private,* wawape wanapofanya kazi kwenye hospitali za umma. Waende wakawape Madaktari wetu, hili jambo la Madaktari kukimbia hawataliona, wata-*concentrate* kuwatibu watu katika *public facility*. Jambo hili litaongeza tija ya utendaji na tutakuwa tumewasaidia Watanzania na tutaleta tija na sisi watatturahisishia kazi ya kwenda kuomba kura 2025 kuhakikisha kwamba Mama ambaye huyu ameleta matumaini kwa Taifa na kwa kweli kwenye hili wanawake shikamooni, mmetisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili nasema kwa dhati ya moyo wangu, kwenye hili mimi mwenyewe sasa hivi kwa dhati ya moyo wangu nimeamua kuwa *advocate* wa akinamama. Akinamama mkiaminiwa uwezo wenu wa kufanya kazi na sema kwa dhati ya moyo wangu, wanawake shikamooni, uwezo wenu wa kufanya kazi ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa hata utulivu huu wa Bunge aliyekaa hapo ni mwanamama, ukiangalia hata namna Taifa linavyokwenda, mimi juzi nilikuwa nasoma *statistic,* Afrika nzima Rais wa Tanzania mwanamama amepandisha mishahara Afrika nzima 23 *percent,* nani kama mama? Kwa uwezo huu akina mama, nashawishika kabisa hata kuamini hata baadaye tukileta sheria hapa wanawake tuawaongeze kwenye Uongozi watalisaidia sana Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo langu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu kengele imeshagonga. Ahsante sana.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *Point* zangu zingine nitaziwasilisha kwa maandishi. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walimtunza fedha Mhe. Elibariki Kingu kutokana na mchango wake)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya mchango huo na hili lililojitokeza hapa nadhani kuna umuhimu wa kuweka

utaratibu kwanza wa kodi wa pesa zinazopokelewa namna hii. Tuweke utaratibu mzuri ili ziwe zinalipiwa kodi hizi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Niwataje Wabunge ambao wataanza kuchangia mchana, Mheshimiwa Francis Leonard Mtenga, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Maimuna Mtanda na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Wapo wageni ambao niliwataja kwa makundi ile asubuhi majina yao nilikuwa sijayapata hapa, sasa nimeletewa hayo majina. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Judith Kapinga yuko Askofu Mkuu wa Kanisa la Mennonite, Askofu Kisare, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yuko Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya *BAKWATA* Shekh Hamisi Mataka, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Mhasham wa Baba Askofu wa Jimbo Katoliki Mkoa wa Geita na Makamu wa Rais wa Baraza la Maaskofu *TEC* Askofu Flavian Kasala, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Padri Paul Chobo ambaye ni Mkurugenzi wa Afya, Baraza la Maaskofu *(TEC)*. Karibuni sana Viongozi wetu wa Dini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.15 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay ajiandae.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote ninaipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na viongozi wote waandamizi ngazi ya taifa kwa kuendelea kutoa fedha

nyingi katika miradi mbalimbali ya afya kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Katibu wa Wizara pamoja na Watendaji wote kwa usimamizi wao mahiri na Wizara inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo nitajikita zaidi kuelezea uhaba wa rasilimaliwatu namna unavyoathiri uadilifu na ufanisi katika kazi. Kabla sijaingia kwenye mchango wangu niongelee kidogo kuhusu ajira. Nashukuru na kuipongeza Serikali kwa ajira hizi 10,285 lakini kwenye Kamati yetu tulishauri kwamba ajira hizi zizingatie usawa, haki na kijiografia pia kwa kuona kwamba mchakato mzima wa ajira zenyewe kwa kuwa ni mfumo basi angalau kila sehemu, kanda, iwe na waliochaguliwa. Sisi kama wawakilishi kwa kweli tumekuwa tukipigiwa simu nyingi na waliomba nasi kama sauti zao naomba kusisitiza hili kwamba, kwa kuwa wanaomba kwa mfumo labda Waziri aangalie namna ya kuunda *Posts Selection Committee* ambayo atachagua wataalam baadhi kutoka Wizarani na wengine kutoka hospitali mbalimbali ili kuhakiki kuona kwamba malengo yaliyowekwa yamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi mifumo wakati mwingine inaweza kuwa *tampered,* badala ya kuchagua kama ilivyoainishwa kwenye mpango, idadi na aina za wale

wanaochaguliwa ikawa *tempered* badala yake wakachaguliwa wa sehemu moja au ukanda moja na pengine wengi kupitia kanda moja kuliko nyingine kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili niendelee na mchango wangu kuhusu uhaba wa Rasilimaliwatu. Kwenye Kamati tumeshauri kwamba hawa watumishi wasimamiwe vizuri katika kuziba mapengo yaliyopo katika Idara mbalimbali. Lakini kukiwa na uhaba wa Rasilimaliwatu mara nyingi sana kama tulivyoona michango ya Waheshimiwa waliotangulia kwamba wengi wao kufuatana na maadili yao na viapo vyao siyo walalamishi wanavumilia, anazidiwa kufanyakazi lakini anajituma anaendelea kujitahidi kwa kadri ya uwezo alionao. Tofauti na sekta zingine kama walimu utaona athari zake moja kwa moja, amezidiwa wanafunzi wengi wanapiga kelele, hata akichoka anaweza akawapa *assignment* akaenda kunywa chai, akaenda kupumzika kidogo, lakini huyu wa Idara ya Afya hana nafasi hiyo, atajitahidi mpaka pale atakapotimiza kumaliza wagonjwa wote walio mbele yake.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingi hazihitaji presha, hata kama ni kazi ndogo kiasi gani iwe ya kutafuta mshipa wa damu, kama ana presha ana haraka hiyo kazi badala ya kutumia dakika mbili atatumia nusu saa. Halikadhalika upasuaji mdogo na kadhalika, hivyo tunahitaji rasilimali watu ya kutosha ili wafanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari nyingine ni wale wagonjwa wanaosubiri watahisi kwamba huyu mtu labda hahudumiwi ili apewe rushwa, kumbe yule mtumishi amezidiwa. Sasa wanashawishika kutoa rushwa wakidhani kwamba wanacheleweshwa maksudi lakini kumbe ni uhaba wa rasilimaliwatu.

Mheshimiwa Spika, pia wapo wanaotumia nafasi hiyo kuchukua rushwa, kwamba atajifanya amezidiwa na kazi mpaka ndugu wa mgonjwa aende amuone atoe chochote ndipo amhudumie. Imetokea hospitali fulani ipo barabara sintaitaja hapa, na ni Hospitali ya Mkoa ya Rufaa. Kijana alipelekwa usiku pale anavuja damu, amevunjika mfupa unaonekana, hahudumiwi, ndugu wanaambiwa nendeni barabarani mkatafute *Panadol* na baadaye wale vijana wanashangaa wanaulizwa je, mna fedha zozote mtupatie? Kama hamtoi mgonjwa wenu atafariki, wanaambiwa waziwazi.  Wale ndugu baada ya kushauriana ilibidi wamtoe mgonjwa usiku ule wakaondoka naye kwenda hospitali nyingine ambako walihudumiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda unakwenda mbio, niongelee athari katika upimaji *physical examination*. Pale kuna takiwa wafanyakazi wa kutosha wa jinsi tofauti tofauti kwa sababu kuna hatari kama anayepima ni jinsi nyingine na ni peke yake, akamdhalilisha yule mgonjwa akamfanyia visivyo lakini kumbe wakiwa wengi basi atafanya kwa uhakika na bila matatizo yoyote wala wasiwasi kwa mgonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee Hospitali zetu za Rufaa. Sina shaka ngazi ya Taifa zinafanya vizuri, wabobezi wapo wengi, wanafanya kwa umakini, lakini hizi za Mikoa nina wasiwasi nazo huduma kwa kweli labda zichunguzwe ziitwe Rufaa zile zinazotoa huduma nzuri kabisa. Pamoja na ubobezi walionao lakini kama mtu anavuja damu anaambiwa akanunue *Panadol* halafu inaitwa Hospitali ya Rufaa kwa kweli hii inatia shaka sana. Wale wa Hospitali za Rufaa tulizotembelea kule Muhimbili, Taasisi ya Mifupa *MOI* na Taasisi ya Magonjwa ya Moyo, kwa kweli waliomba kwamba tunaomba tufikiriwe, tunaomba mtupigie kelele tuongezewe angalau tupate fedha zaidi kwa sababu tunajituma na kazi ni kubwa. Nami leo hapa natumia nafasi hii kuomba Wizara i-*top up* kwa kuwa Mkurugenzi kule alituambia kwamba yeye anatoa motisha kulingana na mapato ya ndani. Lakini Serikali, Wizara naomba i-*top up* kwa kweli kuwapongeza wale wanafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia zipo kazi ambazo zinatumia umakini zaidi. Kwa mfano, tulifika *MSD* tukakuta kijana amekaa pale muda wote ana-*check* kidonge kwa kidonge kwenye mizani, kina uzito gani, kina ugumu gani, kiko bora kiasi gani? Lakini tulivyotoka pale wanalalamika kwamba sisi hapa hatuna mgahawa. Sasa motisha ya aina hii kukosekana kwa watu wanaofanya *very tedious work* kwa kweli inakatisha tamaa na hawa wakati mwingine ndiyo wakuibua maovu yanayofanyika pale. Sasa wasipoangaliwa vizuri, wanahudumiwa vizuri hawatatoa taarifa yoyote na ni rahidi

kurubuniwa wakapewa kitu kidogo mambo yakaenda hovyo. Mara nyingi wale wanaotoa siri, waadilifu wanapigwa vita.

Mheshimiwa Spika, tumefika Butimba tukakuta Muuguzi mmoja anasota pale Butimba kwa kosa dogo tu la kukosea kuingiza *data* kwenye mfumo, hasara ya Shilingi 8,000 imemuweka muuguzi yule Butimba, kwa kweli, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa…..

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Shukrani. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mheshimiwa Maimuna Mtanda ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuwa na hali ya uzima na afya, kufika hapa leo katika ukumbi wako huu Tukufu na kwamba hivi sasa naweza kuchangia Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru mwanangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu anafanyakazi vizuri, anaupiga mwingi, usemaji wa vijana anaupiga mwingi Waziri wangu

Ummy Mwalimu, Mwenyezi Mungu akujaalie pamoja na Naibu wako anafanyakazi naye vizuri mpaka anawasaidia na watu wengine ili kupata matibatu katika hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na Mama yangu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ndugu yangu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yeye kwa kuupiga mwingi, kila pembe, kila rika, kila mahali ameingia. Mwenyezi Mungu amjaalie kheri na baraka, ampe uzima, amuondolee nuksi, amuondolee kila dhiki ili ampe uzima aweze kuendelea mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuna baadhi ya Vituo vya Afya vinafanyakazi vizuri sana, lakini kuna baadhi ya Vituo vya Afya ukiingia katika vituo vile kwenda kutafuta huduma wahudumu wanakuwa wanajisikia sijui kama mtanielewa. Wanajisikia sana mtu unamkuta unakwenda una muulie ile hali kukuitikia hawezi. Mheshimiwa Waziri hawa watu wapo, bado juu ya utekelezaji mkubwa wa Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini hawa watu wapo wanajisikia, mtu anaweka miguu juu ya meza anataka ahudumiwe tena kwa kipimo tu cha presha, namuuliza wewe mfanyakazi, ana niambia ndiyo, sasa kwa nini umeweka miguu juu kama hivyo? Wapo watu kama hao leo nasema katika Wizara katika wizara hiyo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu suala la presha, sukari pamoja shinikizo la damu. Hili suala lipo siku nyingi sana

mimi nataka kulingumzia. Walengwa wengine tupo humu humu katika masuala hayo. Nasema haya kwamba shuhuda ninayo, kwamba kuugua ugonjwa wa sukari pamoja na presha unaua na unaumiza na hasa kwa wanyonge wale waliokuwa hawana fedha. Wanakwenda kupima sukari, wanapata maradhi ya sukari, lakini huduma kujihudumia hawana. Ukiingia kwenye masuala la bima, ukienda ukitaka dawa unaambiwa uongeze fedha ili uweze kupata dawa uende ukahudumiwe, hapo mgonjwa mnyonge atapona kweli? Hatapona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, naomba Wizara hii au naomba Wizara yangu ya Afya nchini ifanye kazi kwa wanawake hasa tunaoathirika na masuala ya presha, sukari pamoja na shinikizo la damu. Maana ukiingia kwenye masuala ya sukari na presha kwa wanaume ndiyo yanaumiza nguvu kabisa, kwa wanawake ndiyo wanaleta ugomvi ndani ya nyumba hawawezi kwenye masuala la ndoa. Sukari inaumiza, inaharibu huwezi kulifanya tendo la ndoa wakati wewe binadamu umeumbwa ukae na mwenzio ili uweze kulifanya lile, hamu iko wapi kutokana na sukari? Hamna. Tujitahidi jamani suala la sukari na shinikizo la damu linaumiza na litatuumiza kwa sana hata sisi wanawake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la saratani. Suala la saratani lipo nalo vilevile linaumiza kwa wanawake hasa kwenye kizazi cha wanawake. Hili mimi limenigusa mwenyewe ndani kwangu yupo mgonjwa huyo, lakini

nashukuru Serikali hili suala linaweza kufanya na mtu akapona akawa mzima wala asijue hasa kama mimi nilipata maradhi ya saratani. Kwa hiyo, naomba Wizara hii ichukue jitihada kubwa sana ya kuweza kuwahudumia wagonjwa wa saratani kwa hali na mali ili waweze kufanyakazi vizuri na kuweza kujihudumia. Maana magonjwa ya saratani, kuna mtu katibiwa mzima na kaolewa na mumewe hivi sasa anakwenda na shughuli zake na pilika zake. Kwa hiyo, mimi Wizara hii niishukuru sana na niipongeze sana, inafanyakazi vizuri bila wasiwawasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwenye Wizara hii ya Afya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Enhee nimeyaona makofi mengi sana humu ndani sitawataja waliokuwa wanapiga zaidi ya wengine. Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niungane na wachangiaji wote walio mshukuru Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya. Mimi nichangie tu mchango mdogo sana, la kwanza ni kwenye Bima ya Afya.

Mheshimiwa Waziri Bima ya Afya kwa baadhi ya hospitali imekuwa tatizo kubwa sana. Nadhani ni wakati muafaka wa kufanya tathmini kuongeza idadi ya watu tutakaowataka maoni yao kuhusu suala la Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Bima ya Afya huduma inayotoa Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Dodoma na baadhi ya hospitali hapa nchini inatolewa kwa hatua ya juu sana, lakini katika hospitali nyingi nchini Bima ya Afya inalalamikiwa sana. Nadhani ifike mahali sasa tuone kwamba namna ya Bima ya Afya ni pamoja na kuangalia utoaji wa huduma kwa wanachama wake na jinsi ambavyo kila hospitali nchini inakuwa na dirisha na Afisa anayehudumia pamoja na Daktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Benjamin Mkapa na ukaenda Hospitali ya Rufaa ya Dodoma wanao Madaktari waliopangwa kuhudumia watu wa Bima ya Afya, lakini katika hospitali nyingine wanachama wa Mfuko huu wa Bima ya Afya na Makundi yale mengine ya Bima ya Afya wanalalamika sana. Jukumu letu kubwa ni kusema yale ambayo ni mazuri na yale ambayo kidogo wapokea huduma wanalalamika. Mimi nadhani tuongeze wigo wa mikutano kwa mwaka kama mara mbili kwa wale wapokea huduma ili tujue wanasema nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la utendaji wa *MSD*. Kupitia Bunge hili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *MSD* utendaji wao tumechoka, *MSD* nanunuzi yenyewe

yanachukua miezi Sita, mifano hai *ambulance* tunazosubiri sasa ni miezi sita, lakini pia picha ya wazi ipo kwenye Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Tumeagiza jokofu ni miezi sita sasa, jokofu halijaletwa wananchi wanapata matatizo, tumehangaika vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hebu tuulizane kumbadilisha Mkurugenzi Mkuu inatosha Mheshimiwa Waziri? Kupitia ile ziara ya Waziri Mkuu hadi sasa, kwa nini tusiangalie kurudi kwenye suala la kuangalia upya mfumo mzima wa *MSD* na watendaji wake? Jambo hili linawaumiza watanzania walio wengi, kwa sababu tunaweza tukambadilisha Mkurugenzi Mkuu lakini *MSD* ikabaki na mfumo uleule ambao una matatizo. Nilitegemea baada ya ziara ya Waziri Mkuu, naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa sana Serikali haitachukua hatua. Lakini ni wapi tumepoteza hata ile sura ya kutumbua tumbua, tukatumbue tumbue huko huko *MSD* kwa sababu kuna matatizo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, katika hali ambayo tunafanya hii kazi ya kuwawakilisha wananchi, wananchi wanalamika kule, hiyo *MSD* yenyewe ukizungumza upande mmoja, Mbulu Mji hatuna *ambulance, x-ray, mortuary*. Hivi kweli Watanzania wa Halmashauri ya Mji Mbulu inazungukwa na eneo lote la vijijini, huduma ni pale katikati, vitu vyote hivyo havipo! Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana umefanya kazi kubwa sana ulipokuwa Wizara hii ndiyo maana Mheshimiwa Rais amekuona akakurudisha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli watanzania wa Mji wa Halmashauri ya Mbulu Hospitali ya Mji wa Mbulu inazungukwa na eneo lote la vijijini huduma ni pale katikati vitu vyote hivyo havipo. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana umefanya kazi kubwa sana ulipo Wizara hii ndio maana Mheshimiwa Rais amekuona akakurudisha Wizara hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kama itawezekana tuone utaratibu wa namna gani tunaweza tukatazama. Kama ni sisi tunashindwa kumudu huduma hizi za upatikanaji wa dawa na huduma zingine tukae chini tuangalie, ni utaratibu gani utakaowawezesha Watanzania kupata huduma ya dawa na huduma nyingine za matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ufunguzi wa zahanati. Halmashauri ya Mji wa Mbulu tayari tuna zahanati nne zilizo tayari zimeanzishwa kwa mchakato wa wananchi takribani miaka kama saba, nane, sita sasa hivi ziko tayari kibali tu cha kusajili zahanati hizi imechukua zaidi ya mwaka. Wananchi waliouza mali zao waliotumia nguvu zao wakajenga zahanati hizo wanasubiri huduma lakini huduma haziwafikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani tuharakishe utaratibu huu wa mchakato wa kusajili zahanati na vituo vya afya ili walau, huduma za mwanzo zianze kutolewa tuweze kufanikiwa

namna ambavyo tunaweza tukapata hali halisi ya mafanikio katika utoaji wa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawatuelewi kabisa wanapoona wamemaliza kujenga zahanati mwaka wa kwanza unakwisha mwaka wa pili unakwisha. Ninawaomba sana watu wa Wizara ya Afya na TAMISEMI kaeni pamoja mtufungulie hizo zahanati ili wananchi wapate huduma za mwanzo. Mwananchi analalamika anapotoka kwenye Kijiji kwenda kwenye Hospitali ya Mji kwa gharama pengine ya Shilingi 20,000 kwenda Shilingi 10,000 na kurudi Shilingi 10,000 lakini huko huko dawa anagharamikia nafuu angekuwa anapata hiyo huduma anayofuata pale alipo ili gharama za usafiri zisiwepo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni matumizi ya lugha ambayo hayaridhishi. Yapo matumizi ya lugha kwa baadhi ya watumishi wetu wa sekta ya afya hususani wale ambao tunawaita wakunga, wauguzi pamoja na madaktari. Lugha ya daktari ni sehemu ya tiba anapotumia lugha ambayo mgonjwa akifika anaongezeka ugonjwa ni shida sana. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana katika jambo kama hili tusione haya kuchukua hatua unapofanya ziara. Alikuja Naibu Waziri wa TAMISEMI Afya alikuta madudu kule Mbulu alipewa taarifa ambayo haina uhalisia, alipokwenda kwenye nyaraka inapishana na taarifa ambazo amepewa hadi leo hakuna hatua iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kama Waziri wa TAMISEMI amefanya ziara awasiliane na Waziri wa Afya hatua zichukuliwe mapema ili huduma ibadilike, lakini pia wananchi waone kuna mabadiliko baada ya maagizo ya viongozi wanaokuja. Mwisho niseme tu kwamba ninaomba sana Wizara ya Afya itembelee Hospitali ya Mji wa Mbulu ina matatizo nyinyi kama Wizara chukueni majukumu yaliyo yenu TAMISEMI kama Wizara itachukua majukumu yaliyo yao, ili kuona ni kwa namna gani walau Hospitali ya Mji wa Mbulu inakuwa sehemu ya kimbilio kwa huduma za afya kwa wakati wote katika hali ya kumhudumia mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la *Ambulance* Mheshimiwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Jafo alipokuwa Waziri nimeandika barua hakuna *Ambulance* iliyokwenda, nimeomba *Ambulance* hakuna *Ambulance* iliyokwenda, sasa hivi tena ni mwaka unakwisha. Jamani kama ni namna hii tungeelezwa lugha ya wazi tu kwamba *Ambulance* hizo hazipo, *X-Ray* hiyo haipo lakini pia tungeelezwa kama ambavyo dawa inakosekana. Mimi nilikuwa nashauri kwenye dawa tuna shida gani tusiweke alama kwenye dawa za Serikali kama tatizo ni wizi. Tuna ugumu gani wa kuweka alama ya Serikali kwenye dawa za Serikali ili upotevu wa dawa na wizi wa dawa…

**SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Mtanda atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan kwa kweli anafanyakazi kubwa pamoja na wasaidizi wake wote. Nimshukuru pia Waziri wa Afya kwa wasilisho zuri ambalo amelifanya pamoja na wasaidizi wake wote. Uchumi wa nchi yetu ukuaji wake unakwenda sambamba na masuala ya afya kwa wananchi wake. Kwa hiyo, kama afya haitatiliwa mkazo maana yake hata zile juhudi ambazo tunazifanya za kukuza uchumi wa nchi yetu hazitaleta matunda ambayo tunayatarajia. Kwa hiyo, afya ni kitu muhimu tuwekeze tuisimamie ili tuweze kupata tija ile ambayo Taifa inalitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende sasa kwenye changamoto. Changamoto ya kwanza kama ambavyo wametangulia kusema waliotangulia ni suala la uhaba wa watumishi katika kada za afya. Maeneo mengi hasa ya pembezoni watumishi wa kada hii ni wachache hali ambayo inaleta changamoto katika uletaji wa huduma zenye ufanisi

katika maeneo hayo. Kwa mfano, ukienda kwenye Jimbo la Newala Vijijini tunao watumishi 119 tu ambao ni sawa na asilimia 19 ya mahitaji wa watumishi wa afya wanaohitajika katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala Vijijini. Hii ni hatari kubwa kwa sababu kuna watu wanafanyakazi ambazo hawajasomea. Kutokana na uchache huo utamkuta Nesi anaandika dawa huyo huyo akachome sindano ni hatari, tunahatarisha usalama wa wananchi wa Jimbo la Newala na maeneo mengine ambayo yana shida kama za Newala Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine inaleta uchonganishi kati ya wananchi na Serikali kwa sababu wananchi wanaohudumiwa wanaongea vibaya kwa sababu tu wanakosa huduma stahiki, lakini shida kubwa ipo kwenye uchache wa watumishi waliopo katika maeneo hayo. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu unafanya kazi kubwa sana kazi nzuri inaonekana umepata kibali cha kuajiri watumishi zaidi ya 10,000. Naomba sana angalia sana maeneo yale ambayo yana uhaba mkubwa wa watumishi ili na wao wakaweze kupata huduma kutokana na watumishi ambao watapelekwa katika maeneo yao ikiwemo pia na Newala Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni uchache wa nyumba za watumishi wa kada ya afya. Sawa, watumishi wako wachache lakini hawana maeneo ya kuishi hawana nyumba za kuishi. Ugonjwa hauchagui muda wala dakika sasa kama mtumishi yuko mbali anapatikana mbali, anamuhudumiaje

mwananchi ambaye amepata shida eneo X ambalo ni mbali kutoka pale anapoishi? Lakini hata hivyo hizo nyumba chache zilizopo kwa mfano ukienda kwenye Jimbo la Newala Vijijini, tuna mahitaji ya nyumba 184 lakini tuna upungufu wa nyumba 140. Zipo nyumba 44 katika hizo nyumba 44 ni nyumba nne tu ndizo ambazo zina nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyumba ni chakavu hazistahili kwa kweli kuishi watumishi wale wakati mwingine wanakata tamaa, kwa namna ambavyo wanaishi yale maeneo ambayo wanatoka kwenda kuhudumia wananchi wetu. Nimuombe sana Waziri na timu yake tuangalie miundombinu ya nyumba kwa watumishi wetu wa Idara ya Afya ili na wao waishi sehemu nzuri na salama wapate moyo wa kwenda kutuhudumia, ili kupata ufanisi baadaye wa zile fedha ambazo Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kupeleka huko lakini inakutana na watumishi waliokata tamaa ambao wanashindwa kutoa tiba vizuri kutokana na mazingira ambayo wanaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo haliko Newala Vijijini peke yake liko pia Newala Mjini liko pia na maeneo mengine ya Mtwara. Suala lingine ni mahitaji ya vifaa tiba pamoja na vitenganishi katika Jimbo la Newala Vijijini tunazo zahanati tatu ambazo zimekamilika, tunayo zahanati ya Mpwapwa, tunayo zahanati ya Nakahako, tunayo zahanati ya Hengapano. Zahanati zile tunaishukuru Serikali imesaidia kukamilisha maboma zimekamilika, tunaomba sasa kupatiwa vifaa tiba ili zikaweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. Pia

tunayo majengo ya *OPD* na maabara katika Hospitali ya Wilaya nayo tunayaombea dawa pamoja na vifaa tiba, ili ikaweze kutoa huduma katika maeneo ambayo yanahitajika kutoa huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninalo pia linalohusiana na *MSD* niombe sana *MSD* iwe na dawa wakati wote ili kuondoa mkanganyiko kwa sababu, zahanati pamoja na hospitali zinapoomba dawa basi ikute *MSD* ina dawa kiasi ambacho haitagharimu tena suala la kwenda kutafuta *Alternative Way* ya kupata hizo dawa. Kuchelewa kupatikana kwa dawa kunaigharimu sana maisha ya wananchi wetu kiasi kwamba wengine inawezekana tungeweza kuokoa maisha yao, lakini kwa sababu dawa hazipatikani vituoni kutokana na ukosefu wa dawa kwenye *MSD* inakuwa ni changamoto ambayo wananchi wengi wanakwenda kupata shida jambo ambalo lingeweza kutatuliwa kama *MSD* ingekuwa na dawa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuomba katika Kituo chetu cha Mkwedu ambacho kipo katika Jimbo la Newala Vijijini, tunayo *Ultrasound* iko pale lakini haina mfanyakazi/mtaalam tulishaomba muda mrefu. Pia Makamu wa Rais alishatoa maagizo mtaalam apelekwe pale mpaka leo tunavyoongea mtaalam hajapelekwa kile kifaa kimekaa pale kama mapambo hakifanyi kazi, wakati uhitaji wa wananchi wa kutumia kifaa hicho ni mkubwa sana sasa inasababisha kero na inawezekana pia kikaenda kuharibika kwa sababu hakitumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi pia nishukuru kwa ajili ya juhudi kubwa za Wizara ya Afya na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anaendelea kuimarisha afya katika Taifa letu. Nawashukuru kwa ajili ya Kituo cha Afya Mkimbizi ambapo mmetupatia Shilingi milioni 250 na baadaye mmeongeza tena Shilingi milioni 250 nawashukuru sana, kwa ajili ya Wodi zinazojengwa katika Hospitali ya Frelimo ya Wilaya pale mawili na *ICU* pamoja na Mochuari. Nawashukuru pia kwa utanuzi unaoendelea wa Hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa ingawa tuna changamoto kubwa ya upungufu wa watumishi, maana tunahitaji kuwa na watumishi karibu 466 na tuna watumishi 266 tu na nyinyi mmeipangia ile kwa ajili ya huduma ichangie zaidi ya Shilingi Bilioni 5.8 kwa hiyo tunaomba tuongezewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba leo niongelee hoja ya afya ya akili. Mheshimiwa Waziri nimesoma katika mambo yako sijaona sana unaongelea suala la afya ya akili, lakini afya ya akili ni kitu cha muhimu sana na ni

lazima kama nchi tuhakikishe kwamba tunakichukulia uzito mkubwa na kukiwekea mipango. Kwa sababu, suala la afya ya akili tunaposema mtu awe na afya ya akili maana yake kwanza awe na uwezo wa kujitambua. Mtu anaonesha ana uwezo wa kutatua changamoto zake, mtu anaweza kufanya kazi na kuzalisha lakini mtu huyo anaweza akatoa mchango kwenye jamii yake. Sasa ukitaka kujua mpo kiwango gani cha afya ya akili kama wananchi lazima mjielekeze kuangalia hoja hizo. Kwanza kabisa tukienda namna gani labda kama Watanzania tunachangia ukiona mara nyingi raia wanajiuliza, Serikali inatufanyia nini na sio wao wanataka kusema sisi tunaifanyia nini Serikali ujue kuna tatizo kubwa kwenye afya yao ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wote wenye afya za akili wanajiuliza mimi nitaifanyia nini Tanzania na sio Tanzania itanifanyia nini. Sasa sisi mara nyingi tunatumia *Technic* ya walevi au ya watu wanaopenda kunywa mara nyingi wako baadhi yao, wakiwa na tatizo anaahirisha tatizo kwa kulewa halafu kesho anajua akiamka mambo yatakuwa safi. Lakini kiuhalisia haiwi hivyo kwa sababu akiamka kesho fedha ile, ambayo anatakiwa aanze kutatulia changamoto ameitumia yote imekwisha. Suala hili lipo kwetu inapotokea changamoto mara nyingi tunakimbilia kutaka Serikali ifanye jambo bila kuangalia sisi wenyewe tunakwendaje kutatua lile jambo. Uwezo wetu wa kutatua changamoto kama wananchi/viongozi inaonekana umeshinda na hiyo ndio *ina-comprise* afya ya akili mna afya ya aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi ikishuka bei ya mazao tunataka Serikali iweke ruzuku ikishuka bei ya mbolea tunataka Serikali iweke ruzuku imepanda bei ya mafuta tunataka Serikali iweke ruzuku. Sasa mimi najiuliza ni kwa nini hatufikirii kutatua changamoto na siku nyingine kutumia akili walizotumia wazee wetu, yamkini akili zao zilikuwa zina afya wakasema tunapita kwenye kipindi cha vita ni wakati wa kujifunga mikanda tuhakikishe tunapambana ili tujenge uchumi. Mimi leo najiuliza ile Shilingi Bilioni 100 tunayoiweka huku haijatoka kwenye *TARURA* kweli hatutaanza kutembea kwenye barabara zina makorongo, hatutaanza kukosa dawa? Sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya tuangalie sana kwenye suala la afya ya akili, unatusaidia vipi tuweze kutatua changamoto zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kujitambua ni ukweli usiopingika Taifa lolote linalotegemea kuendelea kuwa na nguvu, linafanya uwekezaji mkubwa kwa vijana wake na tunaposema vijana hapa ni miaka 15 mpaka 35. Sasa tuangalie kama Taifa tunawekezaje kwa vijana wetu unapofika mahali unaona vijana wa miaka 35 hawapewi *priority* wakati nchi nyingine sasa hivi zinahama zinaelekea hata kumpa kijana mwenye miaka 27 kuwa Rais wa nchi. Lakini sisi kwenye nafasi tu za Umeneja kwenye nafasi tu za Uenyekiti wa Bodi, tunajaa wazee na tunakaa sisi tu wakina bibi hili Taifa ni Taifa ambalo litafika mwisho. Kwa sababu, kama unaendelea kuwekeza kwa wazee unaendelea kila siku kuhuisha mikataba watu wamestaafu unakazi ya kuhuisha mikataba wazee waendelee wazee waendelee, maana yake ni kwamba

vijana wako utawatumia lini? Utawapa *practice* lini maana huo ndio udumavu wa akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu udumavu wa akili ni kama unashindwa kuwa na *adequate simulation* ile *Sy social simulation* ukishindwa kuwa nayo ile ina maana unashindwa kuwandaa vijana wako wajipange. Kwa nini kwenye hizi nafasi kama Profesa ni bibi basi msaidizi wa Profesa awe kijana mdogo ili kumuandaa. Kwenye nafasi kubwa tunashika sawa wewe umeshika nafasi kubwa ni mtu *aged* kwa nini hufanyi *succession plan* ya kumuandaa kijana. Sasa Taifa letu litakuwa halina nguvu kama siku zote tutaendelea kufikiri kwamba wanaoweza kushika nafasi kubwa, ni watu wenye umri mkubwa na kusahau vijana na hilo ni tatizo la afya ya akili. Kutotambua kwamba wewe ni mzee utaondoka nchi unatakiwa umuachie kijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri afya ya akili tunaiangalia sehemu nyingine sisi tunaweza tukaleta hoja kutoka huku chini lakini wenzetu mkikaa huko Wizarani mnatuona sisi kama... sisi tuko juu ndio wenyewe. Unaona sisi tuliwaambia ile Hospitali ya Mkoa wa Iringa mmeng'ang'ania kuitanua pale kwenye *car seater* pamejaa hata hapatanuliki mmebanwa na Magereza mmebanwa na Mahakama, pelekeni kwenye heka 35 kule mkaitanue vizuri nyinyi wenzetu mmekataa mmetuona sisi hatuna afya ya akili lakini kimsingi nyinyi ndio hamna afya ya akili. Kwa sababu, wewe unaweza kubadilisha Magereza iwe *ICU* kwa kuwaondoa Magereza

pale? Nyinyi ndio hamna afya kwa hiyo sisi tunaomba muangalie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Ummy hilo lisikupe taabu unafanya kazi vizuri mimi ninachoomba niletee Hospitali ya Wilaya ya Iringa, hujaiingiza hapa na uliniahidi kwamba basi tutakujengea Hospitali ya Wilaya lakini kwenye bajeti haipo mama yangu. Naomba kwa sababu sisi ile hospitali hatutibu watu wa Iringa tu na Majimbo yote yanayotuzunguka wanakuja pale, Isimani wanakuja, Kilolo wanakuja, kule kwa Kiswaga wanakuja, Kalenga na Mafinga wanakuja pale katikati tunaomba mtujengee hiyo hospitali yetu ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea afya ya akili angalia hali halisi ya *performance* ya Watanzania wetu. Leo hii unaweza kumuona mama amebeba begi zuri ukafikiri labda ndani ya begi mule sijui kuna nini lakini ukiangalia kuna maji ambayo amepewa sijui kwa Nabii gani yamletee magari, yamletee nyumba, yamletee utajiri, ana tango ameombewa sijui la kuimarisha ndoa, ana chumvi sijui ya kumwaga avute wateja, ana vitu kibao yaani vitu vinavyoonesha watu hawana afya ya akili. Wanadanganywa kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Afya hiki ni kitu cha msingi, tunaomba ukiweke kwenye bajeti yako utatusaidiaje Watanzania hawa wawe na afya wasidanganyike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna namna hata Mungu mwenyewe anasema nitabariki kazi ya mikono yako sio kwa

kutembea na maji yaliyochotwa *Jordan* au maji yamechotwa Mto Meru sasa hili ni tatizo la afya ya akili. Hebu tuangalie afya za akili zetu wanasema afya ya akili ni kujitambua. Leo hii tuna vijana wengi wanaogopa kuoa wanaogopa kuolewa ukimuuliza wewe kwa nini huolewi anasema nipo nipo kwanza umri unakwenda, wewe kwa nini huoi nipo nipo kwanza. *(Makofi)*

Kosa la afya ya akili. Akili yake hai-*reason* sawasawa. Umri umefika, bado hajitambui. Sasa hiki kitu ni cha muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii afya ya akili tusipoishughulikia, ina tabia ya kuleta umasikini kwenye nchi, kwa sababu uwezo wa watu kuzalisha unapungua kwa sababu hawafikirii. Umenielewa? Leo nimekuja nikasema hapa jamani, wanaume hawa wanapendwa wakiwa na kitu (fedha), lakini kuna mwanaume mmoja anaitwa Heche, amelalamika kwa nini nimesema wanaume, sio warembo? Hilo ni tatizo la afya ya akili. Mimi siamini kama kuna mwanaume hapa atataka kuitwa mrembo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, afya za akili za watu haziko sawasawa, mtusaidie. Watu wanalalamika ndoa zinavunjika kwa sababu ya suala la afya ya akili. Tumepeleka mikopo akina mama wakope, leo anakopa *FINCA,* anaenda *PRIDE,* anaenda huku anaenda huku. Ndoa nyingi zinavunjika kwa kuwa watu wanakimbia kwa sababu ya mikopo. Hajui namna

ya kuzalisha. Unaona! Kwa hiyo, anakosa afya ya akili nini? Ya akili! Kwa hiyo, inatuletea matatizo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca dakika zako zimeisha, lakini nakuongezea dakika moja, malizia mchango wako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naendelea. Kama tunafikiri kwamba umasikini wa nchi hii utaisha kwa sababu ya kutoza kodi, mama aliongea *categorically,* Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatutaki kodi zenye dhuluma. Tunataka kodi kwa haki. Kama kuna kiongozi, bosi amekaa kwenye Ofisi ya *TRA,* anajua kabisa huyu mfanyabiashara uwezo wa kulipa hii kodi hana, halafu yeye anambambika kodi na kumtoza kodi kubwa, ni afya ya akili hana. Yeye mwenyewe analipwa kwa hiyo biashara, halafu anachagiza kuiua hiyo biashara. Ina maana mtu huyo hana afya ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapokwenda na nguvu kufunga biashara, badala ya kumwelimisha mtu kwamba hii biashara fanya hivi na hivi, au nipe mpango wako wa kulipa kodi; wewe kazi yako ni kufunga biashara na wakati umetumwa ukalate na kuongeza mapato ya Taifa hili, afya yako ya akili ina mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana na viongozi wetu, tupo kwenye idara na kwenye Serikali, bado tunaona kuna vitengo. Mimi niko Kamati ya Nishati, nashukuru sana. Sisi tuna Kitengo cha *Geothermal. Geothermal* ni umeme wa jotoardhi, wamejipanga vizuri kupitia Waziri wetu anawasimamia, yule mzee tumefika anatusomea taarifa kwamba mimi nastaafu, lakini nimemwandaa kijana huyu hapa, anakuja kuchukua hii nafasi. Zipo Wizara na wapo mabosi wengine wa Wizara hapa, bado wanafikiri kuendelea ku-*renew* mikataba kwa wazee na wamesha-*renew* mikataba mara sita, mara saba. Wakati una-*renew* mkataba mara tatu mara nne, tayari tuna *workforce* ambayo ni vijana wamesoma hatuwaandai, ni kutokuwa na afya ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami naomba Mheshimiwa Ummy unapokuja hapa, useme hiyo afya ya akili unaiwekaje tupone?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pauline Daniel Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, ajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya Afya. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mungu kwa kunipatia nafasi nami kuweza kuchangia katika

Wizara hii ya Afya. Napenda sana kumshukuru Rais wetu kwa ajili ya kumwamini Mheshimiwa Ummy Mwalimu kuwa Waziri katika Wizara hii ya Afya pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mollel. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pasi na shaka Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni mchapa kazi, Rais hajakosea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya mchango kuhusu afya ya akili, sasa huyu ni mtaalamu wa afya ya akili. Kwa hiyo, tumsikilize mtaalamu wa afya ya akili akichangia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba muda wangu dakika moja uweze kuniongezea. Nampongeza mchangiaji aliyechangia katika masuala ya afya ya akili. Aliloliongea nami nataka kuliongezea hapo hapo.

Mheshimiwa Spika, suala la afya ya akili na magonjwa mengine kwa kweli ni changamoto. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2020, ukurasa wa 138 (w), lengo la chama chetu wakati tunainadi ilikuwa inasema hivi, nanukuu: "*kutoa elimu na uhamasishaji kwa wananchi kuhusu kinga, udhibiti na kuzuia magonjwa yasiyoambikiza ikiwepo afya ya akili.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika takwimu za Shirika la Afya Duniani *(WHO)* ya mwaka 2021 inaonesha kwamba, watu

takribani milioni 38 hupoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambikiza ikiwepo afya ya akili. Hawa watu ni wa umri kati ya miaka 30 mpaka 69 hasa katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa ni changamoto katika nchi yetu na magonjwa haya Waheshimiwa wengi waliochangia hapa wameyaelezea. Ukiangalia hata matatizo yote ya kijamii ni kutokana na magonjwa ambayo siyo ya kuambukiza ikiwemo hiyo ya afya ya akili. Magonjwa hayo ni kama shinikizo la damu, moyo, kisukari, saratani na mengine kama ya afya ya akili, kupooza, hata kutokuona vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magonjwa haya, kama alivyotangulia kusema aliyechangia, ni ya maisha na hivyo basi tiba yake ni ghali sana. Hupoteza nguvukazi ya watu, watu hubaki na umasikini, mahusiano huvunjika na mwisho watu kuchanganyikiwa na hivyo basi, nchi kuendelea kuwa masikini.

Mheshimiwa Spika, haya magonjwa yasiyo ya kuambikiza ni ghali kwa sababu magonjwa mengi matibabu yake ni ya maisha. Yaani mtu akishagunduliwa kwamba ana matatizo ya akili itachukua muda kumtibu huyu mtu mpaka apone kabisa. Mtu akigundulika ana magonjwa ya kisukari, mtu akigundulika ana shinikizo la damu, matibabu yake ni ya maisha, lazima awe anakwenda katika vituo vya afya mara

kwa mara. Pia dawa za kutibu haya magonjwa ni ghali sana na hivyo huigharimu Serikali pesa nyingi kuyatibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, visababishi vya magonjwa haya ni maisha ya kawaida ikiwepo na kutumia vitu kama tumbaku, pombe za kuzidi kiasi, vitu kama lishe isiyozingatia misingi ya afya, kwa mfano, kutumia sukari nyingi, mafuta mengi au chumvi nyingi. Vilevile kutoshughulisha mwili, kwa mfano kutokufanya kazi za kutumia misuli na vile vile kutokufanya mazoezi. Kuna sababu nyingine kwa mfano za uzee au za kurithi zinazosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza, lakini haya hatuwezi kuyazuia.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali ikatilia mkazo masuala ya magonjwa yasiyo ya kuambikiza. Moja katika sera yetu ni kutoa elimu. Hivyo basi, naishauri Serikali itilie mkazo elimu ya afya ya jamii katika jamii yetu ili tuweze kuzuia magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza ili wananchi wetu waweze kubaki salama. Naishauri Serikali kuimarisha kitengo hiki cha afya ya jamii katika Wizara. Hii itapunguza magonjwa mengi na hivyo kuipunguzia Serikali gharama kubwa ya kutibu magonjwa haya yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, itabidi sasa Serikali chini ya Waziri wetu mwenye dhamana ya afya kuangalia ni jinsi gani anaweza akatumia mbinu, *interventions,* katika kuhakikisha kwamba afya ya jamii inaenda mpaka ngazi za chini kabisa katika *family level* ili kuweza kugundua magonjwa haya na kuweza kuwaelimisha hawa wananchi

kujua ni njia gani au ni visababishi gani vya magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza yakiwemo ya akili. Hivyo basi, naishauri Serikali kuimarisha kitengo badala ya kuimarisha zaidi tiba, iweze kuweka *balance* kati ya tiba na kuzuia. Pawepo na uwiano ulio sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata kama pesa nyingi zitawekezwa kwenye tiba, dawa na *MSD,* lakini vilevile katika kuzuia, pawe na uzito ule ule. Vijijini, wataalm wasambazwe huko; shuleni kuanzia msingi watoto wafundishwe kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiuza ili watakapofika miaka 30 wajue wanafanyaje? Wajue kufanya mazoezi, wajue kula lishe bora ili hizo ndoa ambazo zimeshasemwa na wachangiaji ziimarike. Lishe bora iwekwe katika familia, watu wajue wanafanyaje katika kuzuia ili wasipate kisukari? Wanafanyaje kuzuia wasipate *pressure?* Wafanyaje ili wazuie kutokupata magonjwa ya akili kama yalivyosemwa na kushangiliwa hapa?

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, katika mchango wangu niseme tu, kinga ni bora kuliko tiba. Hilo halipingiki. Tuhakikishe kwamba sasa Wizara iweke kipaumbele pia katika kinga. Simaanishi kwamba tiba isiwepo, kwa wale ambao tayari wameshapata magonjwa haya, tiba iwepo, lakini tuzuie mafuriko kabla hayajaingia yatudhuru zaidi. Tuwekeze zaidi katika kinga. Sawa, haitachukua muda mfupi kama tunavyofikiria, lakini tuzuie ili ile *generation* inayokuja juu isiweze kupatwa na magonjwa hayo. Hata kama ikipatwa,

basi iweze kujua namna ya kuishi nayo na namna ya kujua dalili za awali kabisa na kupata tiba mapema.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nami pia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hasa tunaobeba pochi, pale maaskari wameshapewa maagizo maalum, pochi zinazoingia humu ndani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Kyombo na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani. Nami nianze kwa kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri anayoifanya; pili, kwa Naibu wake Mheshimiwa Dkt.  Mollel kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Mawaziri hao kwa kweli ni wasikivu na ni miongoni mwa Mawaziri ambao wanapokea simu hadi saa 8:00 za usiku, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii, Mheshimiwa Prof. Makubi, Naibu Katibu Mkuu Dkt.  Shekilage na Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt.  Sichwale. Watendaji hawa wanafanya kazi vizuri na tunaona muda

mwingi wanahangaika kutatua kero katika sekta yetu ya afya. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa leo, watu wengi wanachangia sana kwenye suala la dawa na utumishi kwa sababu ndiyo maeneo makuu ambayo yatasaidia kuboresha sekta yetu ya afya. Nami nitatumia muda huu kujikita kuhusu suala la upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeze Waziri, kwenye kitabu chake ukurasa wa 44 amekuja na takwimu za uhalisia. Huko nyuma tulikuwa tunapewa takwimu ambazo siyo za uhalisia kwamba kuna upatikanaji wa dawa asilimia 90, au asilimia 80. Nampongeza Waziri na hata kwenye kamati yetu alikuja akasema takwimu nyingine za dawa siyo sahihi. Hapa katika ukurasa wa 44 ameonesha uhalisia kwamba kwenye *MSD* upatikanaji wa dawa ni asilimia 51, hakutaka kuficha. Nakupongeza sana Waziri, na unachokifanya Mwenyezi Mungu atakulipa. Badala ya kuwadanyanya Watanzania unaamua kusema ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa maagizo yake aliyotoa kuhusu *MSD* na kipekee nimpongeze Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyoifanya *MSD*. Nakuomba dada yangu sasa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais ameshatekeleza kwa upande wake, kuna kazi sasa ambazo Waziri, Katibu Mkuu na Mtendaji Mkuu lazima mzifanye. Mafanikio ya taasisi hayaletwi na *management* peke yake,

kuna wafanyakazi wa kati na wafanyakazi wa chini. *MSD* ifumuliwe ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa kati wanaweza kumkwamisha *CEO* wa taasisi. Madereva wanaweza kumkwamisha mpaka *CEO* wa taasisi. *MSD* wanasambaza dawa, tukiwa na timu ya madereva ambao wanataka kufanya *sabotage,* wanaweza kumwambia Afisa Utumishi kwamba, mimi ni *CEO* wa nane hapa kwenye taasisi, hamnibabaishi, na akashindwa kupeleka dawa kwa wakati. Kwa hiyo, *overhaul* ya *MSD* isiwe kwa *CEO* na bodi tu, twende mpaka kwa madereva, watumishi wa kati na watumishi wengine ili *MSD* sasa tuipe muda iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kuna upotevu wa dawa. Hili nalo lazima lidhibitiwe. Sehemu kubwa kuna mgongo ambao watu wanajificha kwamba kuna suala la msamaha. Hili nalo liangaliwe. Hii fedha ya dawa ambayo tunasema kwamba inaingia kwenye msamaha: Je, ni kweli zimeenda kwenye msamaha? Kwa sababu tulitarajia kwamba fedha tunazopeleka kwenye dawa iwe *revolving fund,* tunapeleka kila mwaka, na kule dawa hazitolewi bure, zinauzwa. Kwa hiyo, lazima zile fedha zizunguke. *Otherwise* kila mwaka tutakuwa tunapeleka fedha na matokeo hatuyaoni. Kwa hiyo, lazima tufuatilie zile fedha ambazo zinapatikana kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu bajeti ya *MSD*. Lazima hawa tuwaongeze fedha. Baada ya kufanya *overhaul* tuwaongeze fedha sasa. Pia tumefanya mabadiliko kuhusu Sheria ya *MSD* kwamba sasa wanaruhusiwa hata kujenga viwanda kutengeneza dawa. Wana mradi wao pale Keko na wana kiwanda chao pale *Keko Pharmaceutical,* tuwaongezee mtaji ili waweze kuzalisha dawa zenye ubora ili tuweze hata kuuza nchi majirani. Kwa hiyo, naomba tuwaongezee mtaji ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ni kuhusu upungufu wa watumishi. Mheshimiwa Waziri amesema kinagaubaga kabisa katika ukurasa ule wa 75 kwamba watumishi waliopo kwenye sekta ya afya ni asilimia 47 ya mahitaji yao na asilimia 55 ni upungufu. Kwa hiyo, hapo utaona wazi kwamba lazima tuwe na jitihada za makusudi za kuajiri watumishi wa afya ili kupunguza hii nafasi iliyopo. Ndiyo maana kila Mbunge hapa akisimama anazungumzia upungufu wa watumishi wa sekta ya afya. Kwa hiyo, naomba kibali maalum kitolewe ili kupunguza changamoto hiyo. changamoto hii ni kubwa sana tunapokwenda kwenye maeneo ya vijijini. Kwa mfano kwenye Jimbo langu mimi la Nanyamba tuna upungufu wa asilimia 79. Mahitaji ya watumishi wa sekta ya afya ni 425, waliopo ni 106 tu. Kwa hiyo, utaona hapo tuna upungufu wa asilimia 79. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tutoe kibali maalum, kwa sababu kuna vituo vingine vya afya kama Kiromba na Majengo, hakuna madaktari, ni wauguzi tu

wanaendesha vile vituo. Sasa hii ina madhara makubwa sana. Tutoe kibali maalum, watumishi waajiriwe ili wakatoe huduma kule ambako tumeshafanya uwekezaji mkubwa kwa kujenga vituo vya afya, hospitali za Halmashauri na zahanati zetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kuhusu suala la hospitali yetu ya Kanda ya Kusini Mtwara. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa fedha nyingi za kumalizia ujenzi kwa *phase one* hospitali yetu ya kanda ya Kusini inayojengwa pale Mikindani, Mtwara, tunawashukuru sana. Isipokuwa sasa hivi tuna changamoto ya watumishi kama nilivyosema hapo awali. Ilipofunguliwa ile hospitali ya kanda walitolewa watumishi kutoka katika maeneo mbalimbali wakapelekwa pale watumishi 42. Sasa hivi idara inayofanya kazi ni moja tu ya *OPD*. Naomba Mheshimiwa Ummy na timu yako muongeze idadi ya watumishi ili mtumishi akienda kwenye hospitali ya rufaa apate zile huduma za kibingwa ambazo anazitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kutenga fedha, Shilingi bilioni saba kwa ajili ya kununua, vifaa muhimu; *CT-Scan* na *MRI.* Naomba sasa vifaa hivyo msambazaji avilete kwa wakati ili tuweze kutoa huduma iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa na Mheshimiwa Dorothy Kilave ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuweza kuchangia katika bajeti yetu ya Wizara ya Afya. Niungane na wachangiaji wengine kumpongeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya kuhakikisha maendeleo ndani ya nchi yetu yanasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimahsusi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa mabadiliko makubwa anayoyafanya ndani ya Wizara ya Afya na mahsusi zaidi ndani ya Taasisi yetu ya MSD tulishauri hapa Bungeni na kupitia Wizara yetu chini ya Mheshimiwa Ummy Mwalimu na msaidizi wake Dkt Mollel na wasaidizi wao na Mheshimiwa Rais akaitikia wito akabadilisha uongozi ndani ya taasisi yetu ya MSD na kuweka viongozi ambao ni wataaluma wa dawa, naamini tukiboresha mazingira ndani ya taasisi hiyo tutaona mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mageuzi hayo ya kiutawala lakini bado niendelee kuiomba Serikali. Viongozi hao tumewaweka katika kazi mahsusi. Tusipoweka mazingira

ambayo ni wezeshi mazingira ambayo ni rafiki inawezekana tukawakwamisha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe, katika eneo hilo la *MSD* zipo changamoto mbalimbali ambazo tunahitaji kuzifanyia kazi; zingine ni za kikanuni, na zingine ni za kisheria. Mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni msikivu na ni mtenda kazi anayeamini katika taaluma, hivyo uwape nafasi uliowateua kukusaidia kazi waweze kuleta yale mahitaji na muyafanyie kazi yaweze kufanyika na dawa ziweze kufika katika vituo vyetu na wananchi wapate dawa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo kwa uchache tunaona kwamba kazi ya *clearance* ya dawa kwa Sheria ni kweli imepewa *GPSA,* lakini bidhaa za dawa vifaa tiba na vitendanishi ni bidhaa ambazo ziko *sensitive* sana. Unakuta katika *process* ya manunuzi kuanzia kununua mpaka kusafirisha mpaka kuzi-*clear* pale bandarini hata ule muda wa matumizi unakuwa umepungua. Hatimaye hizi bidhaa zinaingia mtaani zikienda kusambazwa kwa walaji muda wa matumizi unakuwa umekaribia kuisha. Kwa hiyo saidia, najua ni sheria zipo na GPSA wanafanyakazi kwa mujibu wa sheria lakini bado Bunge Tukufu linaweza likafanya mabadiliko kwa ajili ya kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine ningependa kutoa mchango wangu mdogo katika jukumu la udhibiti wa chakula na vipodozi. Mwaka 2019 suala la chakula na vipodozi lilihamishwa kutoka Wizara ya Afya likapelekwa

katika Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara chini ya *TBS*. Katika utaratibu wa kidunia tukiangalia *basic practice* duniani kote kwa kweli kidogo katika eneo hilo mpaka leo Tanzania bado watatushangaa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue historia kidogo. Tukiangalia kuanzia mwaka 1946 tulikuwa na sheria ya *The Food and Brad Ordnance Cap.* 93. Hii tangu tunatawaliwa na wakoloni mpaka Mwalimu Nyerere mwenyewe alivyokuja hizi bidhaa zilikuwa zinadhibitiwa chini ya Wizara ya Afya. Ilipofika mwaka 1978 Serikali ikaona iboreshe kwa kutenganisha bidhaa hizi kwa kutunga sheria zingine mbili. Ikatunga sheria ya kwanza ya *The Pharmacy and Poison Act*. ya Mwaka 1978, ikatunga *The Food Control Quality* ya mwaka 1978. Nia ilikuwa ni kuboresha bidhaa hizi kwa sababu zina linda afya ni kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu. Na Serikali katika taasisi hizi chini ya sheria hizi ikawezesha miundombinu na wataalamu, kazi zikaanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mabadiliko ya kidunia ilipofika mwaka 2003 kuangalia na mwenendo wa dunia nzima Serikali ikaamua kuziunganisha tena bidhaa hizi na kuvunja sheria hizo mbili na kuunda sheria moja; Sheria ya Chakula Dawa na Vipodozi na Vifaa Tiba Na. 1 ya Mwaka 2003. Katika eneo hili taasisi ambazo zilipewa dhamana ya kusimamia hivi chini ya Wizara ya Afya zimefanya kazi kubwa. Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika eneo hili. Imeweka miundombinu ya kutosha mpaka nchi yetu ikapata vigezo vya kimataifa mpaka tukawa na maabara

inayotambulika kimataifa tukapata *WHO* pre-*qualified laboratory* ambayo unaweza ukapima bidhaa zote ndani ya nchi na nje ya nchi. Haikuishia hapa, tukapata ithibati kutoka *WHO* ambayo ilikuwa inaonyesha kwamba mifumo ya udhibiti imehakikiwa na inakidhi vigezo vya kimataifa

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019, kama nilivyotangulia kusema, mabadiliko yakafanyika; inawezekana yalikuwa na nia njema. Hata hivyo, hata hivyo bidhaa hizi zikaenda kurushwa sehemu ambayo ukiangalia kwenye *Blue Print* ya Taifa letu si majukumu yake. Kwa hiyo kupelekwa *TBS* ambayo yenyewe inadhibiti viwango na ukaipelekea udhibiti tunaenda kuhatarisha afya ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bidhaa hizo madhara yake ni makubwa sana, na taarifa za takwimu za *WHO* ukiangalia katika dunia nzima magonjwa zaidi ya 200 yanatokana na ulaji wa vyakula ambavyo si salama. Lakini ukiangalia watu milioni 600 katika uwiano wa mtu mmoja katika watu 10 wote hao wanapata madhara wanapokula vyakula ambavyo si salama. Lakini tukiangalia watu 420,000 hufa kila mwaka kwa kula vyakula ambavyo si salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia fedha zinazotumika duniani dola za kimarekani bilioni 110 zinatumika katika kutibu magonjwa yanayotokana na vyakula hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niombe sana katika eneo hili. Serikali inakuwa inafanyakazi nzuri kuhakikisha kwamba itapata matokeo mazuri lakini katika eneo hili matokeo siyo mazuri na mimi nishauri na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba Mheshimiwa Ummy Mwalimu, nafikiri Mwenyezi Mungu ana makusudi yake. Wakati suala hili linafanyika najua ulipambana sana kulizuia katika Wizara yako, na kipindi hicho nilikuwa sijajua kama nitakuwa Mbunge; lakini halikufanikiwa na leo Mwenyezi Mungu amekurudisha humo humo katika Wizara hiyo hiyo na leo sasa na mimi naliongelea.

Mheshimiwa Spika Mheshimiwa Waziri na msaidizi wako suala hili; na inawezekana kwa kiasi kikubwa mlishaanza kuifanyia kazi. Okoa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, vipodozi hivi vinaleta kansa ambazo nimesikia Waheshimiwa Wabunge wanasema. Hakuna mchawi, ni kwamba sisi tumeamua kuweka vipodozi watu watumie wanavyotaka. Unalala asubuhi unakuta mtu *shape* iko hivi, baada ya muda mfupi madhara yake ni yeye na hospitali, hospitali na yeye; kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba tunatafuta mchawi ilhali hapa tumeongelea saratani na hivyo vipodozi ambavyo havijadhibitiwa vimekaa mtaani. Sisi tuna uchungu na wananchi, na Bunge lako Tukufu limepewa dhamana hii kushauri Serikali kuhakikisha kwamba inafanyia kazi maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunaona matatizo ya figo pamoja na matatizo ya ini yataendelea kuongezeka.

Nasimama hapa, nasema, tukiangalia miaka miwili ijayo mbele inawezekana tukawa na madhara ya magonjwa mengi kwa ajili ya kuziacha hizi bidhaa mtaani zikiwa hazina udhibiti na zikiachiwa taasisi ambayo si jukumu lake. Kwa hiyo niombe sana niombe sasa Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yetu ya Afya basi ifanye utaratibu mapema ili bidhaa hizi ziende katika eneo linalokubalika, ambalo ni Wizara ya Afya chini ya mamlaka ya Chakula na Dawa na vipodozi au yoyote itakavyoitwa….*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kusema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO: …**nikushukuru, naunga mkono hoja, ahsante sana, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana sasa Mheshimiwa Kyombo umetuweka wakati mgumu sana sisi wenye *shape* humu ndani. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa atafatiwa na Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Kwanza kabisa nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Ummy kwa kurudishwa katika Wizara hii yeye pamoja na Naibu wake, kwa kweli naamini kabisa sasa mambo yatakaa sawa. Ambaye hamjui Mheshimiwa Ummy akaiulize Covid Ummy ni nani ndiyo mtamfahamu kwamba Ummy ni nani. Hata Covid ikimsikia Ummy inakimbia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa hiki kitendo alichokifanya cha mabadiliko *MSD,* kwa kweli amefanya kitendo kizuri sana na kuwafariji Watanzania ambao wengi sana walipata maumivu makali sana ya mambo mengi maovu ambayo yalikuwa yakitokea. Na bahati nzuri amemchagua Mkurugenzi ambaye ni jembe ambaye naamini kabisa, timu yao kwa kushirikiana na Mheshimiwa Ummy na Naibu Waziri, sasa mambo yatakaa vizuri. Kwa hiyo mimi niseme nawaombea Mwenyezi Mungu ili watufikishe salama.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba Mheshimiwa Waziri aangalie, kuna mambo ambayo ni ya muhimu sana naomba ayatupie jicho la tatu, yeye pamoja na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, kuna hizi gharama za kufungua faili na kumuona daktari, naziona hapa; kwa kweli hizi gharama zimepanda sana kutoka shilingi 3,000 zimefika 7,000 hadi 10,000. Kwa Mtanzania wa kawaida na haswa mwanamke ni ngumu sana ku-*afford* gharama hizi kutokana na hali halisi ya maisha ya Kitanzania. Kama mnavyojua, kwa mfano ukiangalia kule kwetu, vijijini, kama vile Mkoani Mara, kule

shughuli zetu ni ndogo ndogo ambazo zinakuwa kidogo ni ngumu sana, na haswa mama anapouguliwa na mtoto au yeye mwenyewe anapouguliwa; na ukizingatia sisi wanawake wa Mkoa wa Mara wengi ndio sisi viongozi wa familia au tunao hudumia familia kwa ujumla. Naishauri Serikali iziangalie gharama hizi kwa jicho la pili ili kuangalia namna ya kumpunguzia mwananchi gharama hizi ili aweze sasa kwenda kutibiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niongelee hili suala la dawa hospitalini. Kwa kweli hali ya dawa hospitalini hairidhishi kabisa. Zile dawa muhimu sana pale wanapoenda kutibiwa wagonjwa hospitalini na hasa wale wagonjwa wanaoenda wengine wakiwa wana bima, wanapoenda kutibiwa hospitalini wanaambiwa waende wakanunue nje ya geti la Hospitali, Zahanati na kwenye vituo vya afya. Jambo hili si zuri sana kwa kweli, hili ni tatizo, na waathirika wakubwa ni akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, isitoshe Mheshimiwa Rais ametoa pesa bilioni 129 kwa ajili ya kununua madawa. Sasa je, hawa ambao wanachelewesha chelewesha au kubana bana hizi fedha hawaoni kama wanamchonganisha Mheshimiwa Rais na wananchi?

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe kama mtoto wa Chifu Hangaya, msimuangushe mama yetu, amefanya kazi kubwa sana. Fedha aliyowapa fanyieni kazi, *otherwise* kila siku mtakuwa mnatumbuliwa na mnalalamika. Naamini

kabisa, kwa huu uteuzi wa sasa wa Mheshimiwa Ummy pamoja na Mkurugenzi mpya na ofisi yake, naamini kabisa sasa mambo yatakaa vizuri. Mheshimiwa Ummy usituangushe. Waheshimiwa Wabunge tunakuamini sana, tunaamini mambo yatakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kweli kipekee nimpongeze sana kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kutuendelezea hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Mkoani Mara. Mama ametoa fedha ambazo zimeendeleza hospitali hiyo. Sasa, mimi niwaombe watendaji kuwa fedha hiyo itoke ili hospitali hiyo imalizike. Pia niombe, kuna suala la wauguzi, tunaomba pia tupate madaktari bingwa ili kudumisha ile huduma ya afya zaidi. Kipekee zaidi nimpongeze pia mama yetu kwa kazi nzuri sana aliyoifanya ya kuongeza ajira kwa Watanzania. Ajira Mheshimiwa Rais alizozitoa zimeleta faraja kubwa kwa baadhi ya Watanzania, kwa kweli tunamshukuru sana na kumpongeza Mungu ambariki.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali lakini pia nimuombe mama. Mama hapa ulipokaa basi tunakuomba uongeze ajira mama kwa kuwa hazitoshi, ajira bado watu wengi wana vyeti ambavyo viko kwenye mifuko yao na wengine wameviweka chini ya kitanda. Mama tunakuomba ongeza ajira kidogo, wapo watu wengi ambao hawana ajira. Kwa hiyo mimi niseme tu nashukuru sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia zaidi nampongeza sana mama kwa kitendo alichokifanya juzi cha kuwajali Watanzania wafanyakazi kwa kuwaongezea mishahara, Mungu akubariki sana mama, tunaamini mama unaupiga mwingi, haulali usingizi unatuhangaikia Watanzania, tunasema tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais. Jamani Waheshimiwa Wabunge akina mama na akina baba pigeni vigelegele jamani kwa Chifu Hangaya wakeeee!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave atafatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Ally Makoa ajiandae.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na mimi. La kwanza niweze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameweza kunisimamisha mahali hapa ili nami niweze kuongea kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Temeke. Nimshukuru sana Rais wangu Mama Samia Suluhu kwa kazi nzuri anayoifanyia nchi yetu ya Tanzania na hata sasa sisi wanawake tunajiona fahari kwa sababu tunaye kiongozi mwanamke ambaye hakika anaupiga mwingi.

Mheshimiwa Spika, nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Ummy pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa nzuri mnayoifanya, na tunaamini sana kwamba kwa sasa kazi

hii itakwenda kufanyika vizuri na Watanzania tunawaamini sana. Lakini si ninyi tu, ni pamoja na timu yenu nzima ya Wizara ya Afya kwa kazi kubwa ambayo mnakwenda kuwafanyia Watanzania. Mimi pamoja na yote najua na ninaamini kabisa kwamba madaktari wapo, wauguzi wapo katika hospitali zetu; lakini nasema ni wachache. Kwa kuwa mmepata nafasi ambayo Rais amewaongezea muweze kuajiri basi tuombe muajiri kwa haraka sana ili hawa watumishi waweze kuwepo katika hospitali zetu nyingi na zahanati ambazo zimeongezwa na Rais wetu mama Samia Suluhu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nijikite sana katika Jimbo langu la Temeke. Kwanza hospitali yetu ile ya Temeke imechukuliwa na imefanywa ni ya Rufaa ya Kimkoa. Lakini Serikali hamkutuacha hivyo Jimbo la Temeke mkatujengea hospitali nzuri sana ambayo iko Yombo Vituka, na ni hospitali ya kisasa na ni ya ghorofa. Kwa kweli tunawashukuru sana wana Temeke. Lakini pamoja na uzuri wa hospitali ile viko vifaa baadhi vimeshaingia, kwenye wodi zile viko vitanda na kadhalika ambavyo vimeingia.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna tatizo moja kubwa sana. Ni kwamba, ile hospitali ya mwanzo chumba cha operesheni kiko chini, na ni kidogo, kina kitanda kimoja tu. Ikitikea kama wagonjwa wako wamezidiwa operesheni inafanyika kwa mtu mmoja tu. Kwa hiyo niombe sana juu kule tulikojengewa lile jengo la ghorofa kuna chumba kikubwa sana cha operesheni lakini vifaa havijafika na fedha mnazo *MSD*. Tumetoa karibu

mwaka mmoja na nusu sasa lakini hatuwezi kufanyiwa operesheni kule kwenye chumba cha juu. Na kikubwa zaidi kinachoharibu ni kwamba, hospitali ile mmeiwekea *lift* lakini yule mkandarasi ambaye aliweka ile *lift* ameifungia; takriban mwaka mmoja na nusu sasa hatuwezi kuitumia kwa sababu anasema anatudai Serikali.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, niwaombe sana, mdogo wangu Ummy mwende, sasa mkaangalie jinsi gani Serikali inaweza kulipa lile deni la mkandarasi ili sasa hata *MSD* waweze kuweka vile vifaa kwenye chumba kile cha operesheni kule juu ili watu wetu waweze kufanyiwa operesheni wakiwa juu; kama bado mtakuwa mnahitilafiana kwenye kulipana deni la ile *lift*.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania, hasa wana Temeke, naamini tunaipenda Serikali yetu, hivyo hatutaki kusema maneno mabaya kwa ajili ya Serikali. Tunajua ni kati ya ninyi pamoja na mkandarasi. Serikali tayari ninaamini wanatamani kuona sisi tunakwenda kwa *lift* ile.

Mheshimiwa Spika, na wahudumu ni wachache; pale wanapokuwa kwamba amefanyiwa operesheni chini inabidi wamsukume kwa *stretcher* kupandisha juu. Hali ni ngumu sana, na wauguzi wale ni wachache sana, kama nilivyosema. Kwa hiyo niombe sana ndugu zangu, *lift* ile ikafanye kazi. Lakin, pamoja na *lift* ile, vifaa vile kule juu viwekwe ili kile chumba kisikae bure.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wana Temeke tunajivunia pale kwa sababu tukizidiwa sana inabidi waende Temeke, na Temeke ni ya Rufaa sasa hivi, kupokelewa ni shida. Kwa hiyo naomba sana ndugu zangu, ninakuomba sana hawa wawe wasikivu, na ninaamini Serikali yetu ni Sikivu, kwamba watafanyia kazi hili jambo kwa sababu tayari mlete fedha zingine. Kilakala mnatujengea hospitali nyingine; lakini hii kama haijaisha kule Kilakala kweli itakwisha na kuletewa vifaa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana, najua Mama Samia ni msikivu sana; tunapokwenda kuomba, kama kuna hitilafu ya fedha kidogo tukiomba naamini tunapewa fedha hizi. Ninamshukuru sana kwa sababu hata ile hospitali juzi tumeweza kuiangalia na mwenge ni hospitali nzuri ambayo tunakwenda kuikamilisha kipindi si kirefu, ile ya Kilakala.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu, *lift* hii ya pale Yombo Vituka wananchi wanafanyiwa operesheni, yaani ni kama foleni ambayo hata mimi wakati mwingine madaktari wanaponiita naona huruma. kwa kweli najisikia vibaya sana. Niombe sana *lift* hii ifanyiwe kazi, *MSD* msikie kilio chetu, kwamba vile vifaa vya chumba kile, hizo taa, sijui za kufanyia operesheni, vitanda hakuna ilhali fedha mnazo. Niombe sana Serikali sikivu iweze kutusikia sisi wana Temeke na kituo kile kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe atafatiwa na Mheshimiwa Ally Makoa, Mheshimiwa Khadija Taya ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na naunga mkono hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Pia nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote tuendelee kumwombea Mheshimiwa Rais wetu ili Mungu amwezeshe kumpa maono, maarifa, busara na hekima ili ajue namna bora na ambayo inastahili katika kuwaongoza Watanzania. Kwa sababu kama Mwenyezi Mungu anaweza kutupa fumbo tusiweze kuijua kesho yetu tunapolala, ni imani yangu Mwenyezi Mungu naweza kumsaidia kumpa maono yaliyo matakatifu na maono mazuri Mheshimiwa Rais ya namna ya kuwaongoza Watanzania kuwafikisha pale wanapopataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa ajili ya hatua ya kwanza ya ujenzi wa hospitali yetu ya wilaya lakini Kituo cha Afya Msangano pamoja na KLituo cha Afya cha Nkulu. Naomba nijielekeze kwenye hoja yangu ya leo, kutoa changamoto zangu ambazo zinawakumba wananchi wa Jimbo la Momba, kupitia Bunge lako Tukufu naomba niseme

kwamba huduma ya afya kwa wananchi wa Jimbo la Momba kiukweli hairidhishi na ni hafifu.

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto nyingi sana ambazo zinatukumba ndani ya Jimbo la Momba. Cha kwanza ni upungufu wa dawa kwenye zahanati zetu na kwenye vituo vya afya. Ukiangalia hatuna hospitali ya wilaya lakini hata Hospitali ya Mkoa ambayo tunaitegemea labda tunaweza tukaitumia kwa ajili ya rufaa iweze kutusaidia, bado pia ina changamoto.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni vifaa tib ana vile vile ukosefu wa watumishi, watumishi kuwa wachache, imepelekea hata mtumishi anapopata likizo yake ambayo ni stahili yake, analazimika kufunga zahanati ili aende kwenye likizo yake na wananchi wanakosa huduma na wakati mwingine inaleta ugomvi na wananchi kuona kwamba walistahili kuendelea kuhudumiwa, lakini mtumishi hayupo ili hali huyu mtumishi ilikuwa ni haki yake kwenda likizo.

Mheshimiwa Spika, pia changamoto hizi ambazo zimeendelea kutupata zimepelekea hata wakati mwingine kuwepo na mchafuko kuzidi kwa imani za kishirikina kwenye jamii zetu, kwa sababu wananchi wanapokosa dawa kwenye zahanati kwenye kituo cha afya na ukiangalia sisi wengine majimbo yetu ni ya vijijini mtu atoke Siliwiti, Mkomba kuja kufuata huduma kwenye Kituo cha Afya cha Kamsamba, pikipiki tu inabidi atumie Sh.40,000.

Mheshimiwa Spika, mwananchi kutoka Kamsamba kwenda Vwawa inabidi atumie nauli zaidi ya Sh.15,000 na wakati mwingine ni kipindi cha mvua barabara hazipitiki. Kwa hiyo kutokana na kwamba mwananchi anaona suala la afya halina mbadala anaona atumie njia yoyote ile kwa ajili ya kutafuta afya. Ninao mfano mzuri wa Katibu wetu wa Chama Cha Mapinduzi, alipata ajali pamoja na Mwenezi mwaka jana mwezi Mei, wakavunjika miguu mara mbili, lakini kutokana na kwamba kwenye Kituo cha Afya cha Kamsamba hakuna hata *x-ray* ambayo angeweza kupimwa kuona inabidi apate huduma ipi akalazimika kwenda kwa waganga wa jadi na mpaka sasa hivi Katibu huyu hajapona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa swali kama huyu tu ndio kiongozi ambaye wananchi wanamwona, kwa hiyo unaweza ukaona namna gani ambavyo kutokuwepo na vifaa tiba na dawa kwenye zahanati zetu na kwenye vituo vyetu vya afya, vinawafanya wananchi waendelee kutafuta njia nyingine mbadala ya kutafuta afya zao. Ombi langu kwa Serikali, tunaomba sana zahanati zetu ambazo zipo katika Jimbo la Momba, zipate dawa za kutosha, vifaa tiba tuweze kuvipata, *whether* tutapata kutoka kwenye Wizara ya Afya au Wizara Afya wataongea na TAMISEMI vyovyote vile itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba, wananchi wa Jimbo la Momba watapata afya stahiki ili

tuweze kupambana, kuendelea kujenga Jimbo letu. Pamoja na kukosekana dawa pamoja na vifaa tiba kwenye zahanati zetu na vituo vya afya, bado hata kwenye Hospitali yetu ya Mkoa wa Songwe ambayo ndio tunaitegemea kama hospitali ya rufaa kwa ajili ya kutusaidia, huduma zipo lakini haziwezi kufanyika kwa ufanisi kama inavyotakiwa, hakuna vifaa tiba kwenye suala la mifupa, hakuna Madaktari Bingwa wa watoto, hakuna Daktari Bingwa wa upasuaji, hakuna Madaktari Bingwa wa magonjwa ya ndani, hakuna Wauguzi wa kutosha, lakini hata vifaa ambavyo vinabidi viwasaidie watu ambao wana changamoto ya mifupa hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye zahanati zetu unaweza ukakuta mgonjwa anakwenda hakuna hata kipimo cha kumpima *BP* imepelekea wananchi hawa wanapata *BP* mpaka wana-*paralyze,* wazee wako wengi kule kila wakati kushinda kwa waganga wa jadi wakifikiri wamelogwa, lambalamba wanatusumbua kila wakati kwa sababu kila mtu anasema huyu kaniloga, huyu kaniloga, lakini kama dawa zingekuwepo za kutosha, watumishi wapo wa kutosha, wakawahudumia wananchi hawa inavyotakiwa sidhani kama kuna mtu yeyote angeenda kutafuta njia mbadala huko mahali pengine ambapo hapafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa watu wa Wizara ya Afya, kipo kitengo kwenye Wizara ya Afya ambacho kinawatambua hawa watu wa Tiba Asili. Tunawaomba wale watu walioko kule ambao wanatoa hizi tiba asili Mheshimiwa Waziri, watoe wito wa namna ya kuwasajili ili tuwajue ambao

Serikali imewaona ndio wanafaa, wanatambulika na watu na *NIMR* ambao wao wanafanya utafiti kwamba hizi tiba asili ndizo zinafaa, huko mitaani ni ugomvi kila mtu kaniloga, kila mtu kaniloga, watu wanauwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ni nani atajua huyu kaniloga halafu nimwache, umeona, mtu anajua fulani kamloga na yeye anaona mimi siwezi kumloga anaenda kumkata mapanga usiku. Kwa hiyo kutokana na huduma mbovu za afya ambazo zipo kwenye jamii zetu zinafanya hivyo vitendo viendee kushamiri, lakini huduma za afya zikiboreshwa na zikiwa nzuri, mtu akaenda hospitali amevunjika mguu, akapata huduma, sidhani kama atawaza kwenda kumtafuta mganga wa jadi, mganga wa jadi atakuwa wa nini? Unaweza Mbunge ukaenda kufanya mkutano wa hadhara, lambalamba akapata wafuasi kuliko hata wewe kiongozi ambaye unaenda kuwaambia mambo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lambalamba amejaza watu kwa sababu gani? Kwa sababu anatoa matunguli, wewe hapo unaumwa mguu kwa sababu huyu alikuloga, wewe hapa ulivunjika mguu hauponi kwa sababu hivi. Sasa huyu ataponaje wala hata hajapimwa, usikute hata mfupa umeoza. Sasa hivi kwenye Hospitali yetu ya Mkoa wa Songwe tunaye mwananchi ambaye amekaa zaidi ya miezi sita, alivunjika mguu ameenda kwa waganga wa jadi, amekaa huko hajapona, mfupa sasa hivi unaoza, lakini kungekuwa na *x-ray* kwenye vituo vyetu vya afyam akapata

huduma inayostahili, kusingekuwa na hii migongano kwa ajili ya kuendelea kufanya jamii zetu ziende…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Kengele ya pili ilishagongwa.

Mheshimiwa Ally Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Taya na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Afya. Nianze kwa kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa inayofanyika, lakini niwapongeze Wizara ya Afya kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache; jambo la kwanza, nimpongeze Dkt. Chandika ambaye ni Mkurugenzi wa Benjamini Mkapa, Hospitali yetu ambayo ipo hapa Mkoani, kwa kazi kubwa anazozifanya. Ombi langu kwa Wizara ni kwamba Hospitali yetu ya Benjamini Mkapa watu wote sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kutoka maeneo mbalimbali tunakwenda kupata huduma ya afya pale, kwa hiyo wajitahidi kama Wizara kuhakikisha hospitali ya Benjamini Mkapa inatoa huduma kwa kiwango

kama vile Muhimbili ama zaidi ya hapo. Wapatiwe vifaa vya kutosha na vyenye sifa na hadhi kwa sababu Benjamini Mkapa sasa Serikali ndio ipo hapa na mikoa mingi ya jirani tunategemea kwenda huko kwa sababu ni karibu kuliko Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunaomba Serikali basi iiangalie hii hospitali kwa sababu sasa inatuhudumia wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naishukuru Serikali unakumbuka Bunge la Bajeti lililopita tuliongelea kesi za akinamama ambao walikuwa wanakufa kwa kukosa huduma za hospitali hasa kwenye Kata ya Suruke. Nilikwenda kwa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye alikuwa Waziri wa TAMISEMI kumweleza ile hali mbaya ya akinamama ambao walikuwa wanakosa huduma kwa sababu wako kisiwani.

Mheshimiwa Spika, leo hii ninapoongea Serikali imekwishajenga kituo cha afya kikubwa cha kisasa na tayari kinakwenda kukamilika. Ombi langu sasa kwa Serikali, katika nia ile ile njema ya kuwasaidia akinamama wale, sasa tunaomba katika mgao huu wa ajira basi tupatiwe madaktari japo watano ili waweze kwenda kukihudumia kituo hicho cha afya, wale akinamama ambao walikosa huduma nzuri ya uzazi wakawa wanapoteza maisha na watoto wao, basi waweze kupata huduma. Kwa sababu Serikali imekwishawekeza fedha nyingi na kituo kilikwishakamilika, ni vema sasa basi Waziri, Mheshimiwa Ummy atupelekee Madaktari ili msimu huu wa mvua unapoanza wale

akinamama ambao wanajifungua kipindi hicho wasipate tena shida ya kuzuiwa na mto, ukizingatia daraja la mto bubu linapelekwa litajengwa mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tuna kituo cha afya kilijengwa Awamu ya Tano. Kituo kile cha afya kinaitwa kituo cha afya lakini hakijakamilika majengo, tunahitaji kupata jengo la *OPD,* chumba cha *x-ray,* pamoja na wodi ya akinamama na akinababa. Kwa hiyo ili kikamilike kile kituo cha afya na kiwe na sifa ya kituo cha afya, basi tunaomba yale majengo yakamilike.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri au bahati mbaya katika bajeti hii sikuona kama nimepata kituo cha afya, lakini sasa kama watatusaidia tukakikamilisha kile kituo cha afya ambacho kilijengwa Awamu ya Tano nab ado hakijakamilika, watakuwa wamefanya jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tuna vituo vya afya, tuna hospitali zetu, tunamwomba Mheshimiwa Ummy hospitali hizi ziweze kupatiwa vifaa pamoja na watumishi ili wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nashukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Taya, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex ajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii tena katika Wizara ya Afya kuchangia mambo mbalimbali. Kwanza naomba nikupongeze sana dada Ummy, Mheshimiwa Ummy anafanya kazi kubwa sana ndio maana leo hii Mheshimiwa Rais amemrudisha hapo, ameona kazi ambayo ameifanya. Leo hii anawasikia Wabunge wengi wakiomba vifaa tiba kwa sababu tayari kuna majengo, kwa hiyo Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri wamefanya kazi kubwa sana kuleta fedha za UVIKO kujenga vituo vya afya vingi na ndio maana leo hii tunaomba vifaa tiba kwa sababu tunayo tayari majengo ambayo yanaenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo sana wa fadhila leo hii kama sitomshukuru Mheshimiwa Rais, kwa sababu Mheshimiwa Rais ni msikivu mno, mwaka jana nilisimama hapa ndani nilizungumza sana kuhusu masuala ya mafuta kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Leo hii nasimama hapa kwa kujidai kwamba Mheshimiwa Rais amesikia kile kilio chetu. Aliwaita watu wenye ulemavu Ikulu na akaelekeza Wizara ya Mheshimiwa Ndalichako kwa ajili ya kutenga bajeti ya watu wenye ulemavu, ya kununua mafuta Sh.60,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini hii bajeti ya Sh.60,000,000 kwa mwaka 2022/2023, itaongezeka kutokana na idadi tutakayopata kutokana na sensa. Tukishafanya sensa tutajua idadi kamili ya watu wenye ulemavu wa ngozi ili

tuweze kupata mafuta yanayotosheleza kabisa, lakini kwa kianzio tumeanza vizuri, Sh.60,000,000 imetengwa na utaratibu mzuri sana utafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kufanya mabadiliko ya *MSD*. *MSD* leo hii tumepata kiongozi mwingine mpya na leo hii kila mtu anasifia *MSD,* lakini naomba niwaambie *MSD* jambo moja, wasijisahau na hizi sifa. Hawa hawa watu leo hii wanaowasifia kesho watawasema humu ndani mtawashangaa. Kwa hiyo, kwa makosa ya huko nyuma waangalie kitu gani wenzao walikosea na wao wajitengeneze kwa namna gani ili waweze kuboresha. Tunawaamini sana *MSD* na sisi, wao ni kimbilio letu kwa sababu sisi tunawawakilisha wananchi, kwa hiyo wao ni kimbilio letu sisi. Kwa hiyo, tunawaomba sana sana katika jambo hili waangalie sana maslahi ya wananchi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii pia nina maombi kadhaa kwa Wizara hii ya Afya; leo namwomba Mheshimiwa Ummy, kuna jambo hili la mashine kwa ajili ya kuzuia kansa. Wanasema kinga ni bora kuliko tiba. Nawaambia kweli humu ndani Wabunge hawajawahi kuona mgonjwa wa kansa mtu mwenye ulemavu wa ngozi au mtu mwenye ualbino na kama wakitoka hapa wakaenda *ocean road* wakaona wagonjwa wa kansa watanielewa kwa nini kila siku nikisimama hapa nazungumzia suala la kansa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, basi naomba hizi mashine zilizopo ziongezwe zipo kwenye mikoa saba, basi tuone namna gani ya kuongeza hizi mashine ili kila mkoa wapate hizi mashine, wasiweze kusafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa ajili ya kuzuia saratani ya ngozi. Pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Ummy amefanya kazi nzuri sana. Leo hii nimefurahi mno, nimefurahi sana sana kwa kuona kwamba kitengo cha mionzi kinahamia Dodoma. Kwa hiyo sasa Dar es Salaam pale *ocean road* kipo kitengo cha mionzi, lakini pia Mwanza pale kipo na sasa hivi Dodoma kipo, ina maana itawasaidia watu wanaotoka Singida, Manyara, Arusha hawatoenda mbali sasa hivi watakuja hapa Dodoma kwa ajili ya kupata mionzi kwa ajili ya saratani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe pia jambo lingine Mheshimiwa Ummy, namwomba sana kitengo cha afya, huduma za afya kwa watu wenye ulemavu namwomba sana, leo hii tunazungumza kuhusu suala la afya ya akili, sisi walemavu mimi mwenyewe nawezakana sina afya ya akili, kwa sababu tukiudhiwa tunakasirika haraka sana, tuna mambo mengi sana ambayo yametuzonga, hiki kitengo kitatusaidia sana kwa huduma zake kwa ajili ya kushauri. Kwa hiyo naomba huduma ya utengemao ili iweze kutusaidia sisi tuweze kufanya majukumu yetu vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kuliletea maendeleo Taifa letu la Tanzania ikiwemo kwenye sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri. Niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri alipokuwa ametoka kwenye Wizara hii kwa kweli tulimkumbuka sana, amerudi mambo mengi yanakwenda vizuri kama yalivyokuwa wakati ule alipokuwepo, wakati ule wa mwanzo. Pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Mollel kwa kazi nzuri na namna ambavyo anachapa kazi katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo katika kupongeza katika kuthibitisha mambo yanavyokwenda vizuri, napenda niseme katika Wilaya yetu ya Kilwa yenye Kata 23 tumepata fedha nyingi ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu uliopita. Jumla ya zaidi ya shilingi Bilioni 1.5 zimewekezwa kwenye miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa wodi maalum Sh.300,000,000 katika Hospitali ya Kilwa Kivinje ya Kinyonga. Pia tumepewa fedha Sh.500,000,000 kwa ajili ya kujenga Kituo

cha Afya pale Mandawa na vile vile tumepewa fedha Sh.250,000,000 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya pale Kipindimbi, Kata ya Njinjo na pia tumepewa zaidi ya Sh.400,000,000 kwa ajili ya umaliziaji wa Zahanati katika Vijiji nane vya Miumbu, Mtepela, Nakindu, Pungutini, Kisongo Namakongoro, Kiswele pamoja na Songomnara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilifanya kazi nzuri na wadau wa maendeleo wa *PAN AFRICA* na wametuwezesha kushirikiana nao na kujenga Vituo vitatu vya Afya, Chumo, Somanga pamoja na Songosongo na pia Zahanati moja imejengwa kwa kushirikiana na hao wadau wa *PAN AFRICA* pale katika Kijiji cha Nahama na Mayunu. Pamoja na mafanikio hayo, bado kumekuwa na changamoto zinaendelea. Changamoto ya kwanza ni kutokuwepo kwa *ambulance*, *ambulances* zetu nyingi zililetwa zaidi ya miaka 10 iliyopita katika Wilaya ya Kilwa na hivyo sasa hivi haziwezi kufanya kazi ya kuweza kubeba wagonjwa na kuwaharakisha kwenda hospitali.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali imekuja na mpango wa kuleta katika kila Halmashauri angalau *ambulance* moja, lakini sisi Kilwa tuna majimbo mawili kwa hiyo itapendeza kama Mheshimiwa Waziri atatuletea *ambulance* mbili, moja ikaenda Kilwa Kaskazini na nyingine ikaenda Kilwa Kusini. Vile vile tuna changamoto ya vifaa tiba, kutokana na ujenzi wa vituo vingi vya Afya na Zahanati vifaa tiba vimekuwa adimu au vichache. kwa hiyo, tungeomba Serikali itusaidie vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna changamoto kubwa ya watalaam au watumishi katika Wilaya yetu ya Kilwa tunauhitaji wa watumishi 1,315 waliopo ni 357 tu. Kwa hiyo, tuna uhaba wa watumishi 958 sawa na asilimia 76 ya uhitaji. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali kupitia zile ajira ambazo zimetangazwa hivi karibuni basi watupunguzie huu uhaba ili shughuli ziweze kwenda tiba iweze kutolewa kama ambavyo inatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hospitali yetu ya Wilaya ya Kinyonga pale Kilwa Kivinje ni ya zamani sana imejengwa tangu wakati wa ukoloni wa Waingereza imechakaa sana inahitaji ukarabati mkubwa ningeomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya ukarabati wa ile hospitali ya Wilaya ya Kilwa ya Kinyonga pale Kivinje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna shida katika baadhi ya vijiji vyetu kuna vijiji kama Tisa Jimbo langu peke yake bado havina zahanati. Kwa hiyo, wanalazimika wananchi kutembea umbali mrefu kwenda kusaka tiba katika zahanati za vijiji vya jirani au Vituo vya Afya ambavyo vipo mbali. Kuna kijiji cha Kinywanyu, Ingerito, Namayuni, Namakoro, Ngorongoro, Bugo, Nambondo na Naipuli havina zahanati, pia kati ya Kata 23 za Wilaya ya Kilwa tuna vituo vya afya Saba tu, Kata 16 hazina Vituo vya Afya. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali itenge fedha za kutosha ili kupunguza uhaba wa Vituo

vya Afya na Zahanati katika Wilaya yetu ya Kilwa ili wananchi waweze kupata huduma katika maeneo ya jirani huduma ambayo ipo bora. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema naishukuru Wizara, narudia kusema naishukuru Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ikupa Stella Alex atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ya kuniwezesha na mimi kutoa mchango mdogo katika Wizara hii ya Afya. Kabla sijaendelea ninaomba niunge mkono hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameweza kumpongeza kwa kuongeza mishahara ya Watumishi wa Umma jambo ambalo linaenda kupelekea ongezeko la mzunguko wa fedha ndani ya nchi yetu. Pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anaendelea kuipa kipaumbele sekta hii ya afya na hasa kibajeti. Tunaona bajeti ya afya jinsi ambavyo

Mheshimiwa Waziri amei-*present* imekuwa na mambo mengi ambayo yanatoa tumaini la sekta hii kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimwia Waziri Ummy Mwalimu Dada yangu kwa jinsi ambavyo anaendelea kuchapa kazi yeye pamoja na timu yake ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 12 mwezi wa Nne mwaka huu niliweza kuuliza swali lakini pia Januari mwaka huu niliweza kuuliza swali nikitaka kufahamu mpango wa Serikali ni jinsi imejipanga kuona kwamba inaandaa vyumba maalum vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu. Ninaishukuru Serikali kwa jibu ambalo lilitolewa lakini mpango ambao ulitolewa ni mpango wa muda mrefu kutokana na umuhimu na unyeti wa jambo hili niiombe Serikali iliangalie jambo hili kwa jicho la tatu, kwa kuja na mpango wa muda mfupi ambao utawezesha upatikanaji wa vyumba hivi vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu kwa haraka, tofauti na ambavyo sasa kwenye jibu lile ilisema kwamba wameandaa ramani ambazo zimeandaliwa sasa hivi kwa maana ya vituo vya afya ama hospitali ambazo zitajengwa basi zitazingatia jambo hili, ninaiomba sana Serikali iliangalie jambo hili kwa jicho la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa *CCBRT* Ndugu Brenda Msangi jambo hili aliposikia tu nilipouliza kazi swali yeye alilifanyia kazi kwa

haraka sana na hivyo pale *CCBRT* sasa hivi wanawake wenye ulemavu wanajifungua vizuri na wanafurahia kuleta viumbe duniani kama wanawake wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nichangie kwenye eneo la wagonjwa wa akili lakini mimi nipo tofauti kidogo na wachangiaji ambao wamepita. Kwa kadri ambavyo nilikutana na kundi hili ambalo pia ni kundi ambalo ninaliwakilisha, waliweza kuzungumzia changamoto ya upatikanaji wa dawa za wagonjwa wa akili. Dawa hizi kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wake lakini hata zinapopatikana zinapatikana kwa gharama kubwa, hivyo niiombe sana Serikali iweze kuangalia kwamba dawa hizi ziweze kupatikana kwa gharama nafuu lakini pia ziweze kupatikana kwa wingi kwa kadri ambavyo wamekuwa wakizihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la mwisho ambalo ninaomba nilichangie ni kuhusiana na upatikanaji wa matitabu kwa watu wenye ulemavu. Hata mwaka jana kwenye bajeti niliweza kuchangia lakini pia Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha bajeti yake mwaka jana aliweza kuongelea mpango mzuri ambao umeandaliwa kwa wazee na mimi nikatumia nafasi hiyohiyo kwamba Serikali sasa inaonaje kwenye ule mpango mzuri wa wazee, alisema zimeandaliwa *t-shirt* wazee kwanza, nikasema kwa nini Serikali sasa isiongeze neno ikawa kwamba wazee na watu wenye ulemavu kwanza ili kuweza kuleta huduma hii ya matibabu kiurahisi kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ufahamu mpango mzuri ambao unaandaliwa na Serikali, Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanakuwa na Bima za Afya hili ninalitambua lakini kwakuwa bado tupo kwenye mchakato katika kipindi hiki cha mpito basi Serikali iweze kuona utaratibu mzuri wa kundi hili kuweza kupatiwa matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa hongera sana Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Afya. Pia hongera kwa Mheshimiwa Rais Mama Samia kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya katika nchi yetu kwa muda nfupi.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri katika eneo la upatikanaji wa dawa, ufanyike ukaguzi wa kushtukiza katika vituo vya afya mara kwa mara ili Wizara iweze kujua ukubwa wa tatizo na kuwabaini wanaofanya ubadhirifu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, miongozo ya Wizara ya utoaji dawa katika vituo vya afya ipitiwe upya na kuangalia ile inayogongana na ya *NHIF* na kuiweka sawa ili kuondoa usumbufu wakati wa madai ya fedha ya vituo vya afya na *NHIF*.

Kuhusu huduma bure kwa akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano itolewe maelezo ya kubainisha hiyo bure inahusisha vitu vipi au gharama zipi ili ieleweke wazi kwamba Serikali inahusika katika maeneo yapi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb) na Naibu wake Dkt. Godwin Mollel (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Naibu wake na timu nzima ya watendaji wa Wizara pamoja na wadau wote wa maendeleo ya afya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo nina ushauri ufuatao; kumekuwa hali isiyo ya kawaida baadhi ya vituo kukosa *ARVs* na kulazimika kutoa dawa zilizoisha muda wake katika Wilaya ya Nyasa; uangaliwe utaratibu wa kununua dawa kwa kuwa baadhi zinanunuliwa nyingi na kupitisha muda wake wakati nyingine hazipatikani kabisa; kuna upungufu mkubwa wa vitanda na vifaa tiba muhimu katika Wilaya ya Nyasa; ni lini Wizara italeta vifaa vya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Kihagara? Pia hali ya watumishi wa

afya, madaktari na wauguzi ni wachache sana. Ni 228/800 na pia tunaomba magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Afya Ndugu Ummy Mwalimu na Naibu wake Dkt. Godwin Mollel na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kuhusu changamoto zifuatazo nikianza na changamoto ya matibabu kwa wazee wenye ugonjwa wa kisukari na kuishia kukatwa viungo kama miguu. Pia sheria inayokataza uwepo wa maduka ya dawa mita 500 kuzunguka Hospitali za Serikali

Mheshimiwa Spika, wazee wanaougua ugonjwa wa kisukari na kukatwa miguu hupitia changamoto kubwa ya gharama kwa kutakiwa kulipia fedha nyingi kununua miguu ya bandia. Gharama za miguu miwili ni kubwa. Kuna mgonjwa amenilalamikia kuwa mwaka wa 2019 alinunua miguu bandia kwa thamani ya shilingi milioni tano ikiwa na *silicone liner.* Mgonjwa huyu huyu mwenye umri wa miaka 68 ameniambia kuwa mwaka huu wa 2022 anatakiwa alipe shilingi milioni tatu kuikarabati.

Mheshimiwa Spika, wazee waliokumbwa na ugonjwa huu na kukatwa miguu wanakuwa hawana uwezo wa kushiriki tena katika shughuli za uzalishaji na kujipatia kipato.

Kwa gharama hizi, huu ni mzigo mkubwa kwa wagonjwa wa kisukari na wanaoshindwa kulipia huishia kufa kwa mateso.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria inayokataza uwepo wa maduka ya dawa mita 500 kuzunguka hospitali za Serikali. Uwepo wa sheria iliyo kwenye GN 269 ya Aprili, 2020 ulitoa kipindi cha mpito cha miaka miwili kuitekeleza, na sasa iko kwenye hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inayokataza uwepo wa maduka ya dawa mita 500 kuzunguka hospitali za Serikali kwa hisia kwamba baadhi ya wataalamu wa Wizara ya Afya wanaihujumu Serikali kwa kuiba dawa na kuziuza maduka ya karibu au huwa na maduka karibu na hospitali za Serikali na huishia kuyakuza maduka yao.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu alitoa agizo la kuondolewa kwa maduka yote ya dawa ambayo yapo mita 500 ndani ya eneo la hospitali za Serikali kwa kile kinachodaiwa kuhujumu upatikanaji wa dawa katika hospitali hizo. Tangazo hili lilisababisha taharuki kubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu, sheria hii ilipotungwa haikuzingatia maslahi ya wagonjwa wa Kitanzania na wamiliki wa maduka binafsi ya dawa yaliyo karibu na hospitali. Maduka haya yapo kusaidia upatikanaji wa dawa na vifaa vya tiba kwani Serikali yenyewe bado

haina uwezo wa kusambaza dawa zote na vifaa tiba kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, hii sheria ina mapungufu, mimi naona hakuna mwananchi anayependa kwenda nje ya hospitali kutafuta dawa au vifaa tiba bali changamoto za uhaba wa dawa na vifaa tiba zilizopo ndani ya hizo hospitali ndio zinafanya waende nje.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzisha sheria hii yanakinzana kabisa na uhalisia uliopo. Tatizo kubwa lililopo Wizara ya Afya ni katika mfumo mzima wa ugavi, usambazaji na usimamizi wa dawa na si uwepo wa maduka ya watu binafsi ya dawa karibu na hospitali za Serikali. Watumishi wasio waaminifu wakiiba na kutoa dawa nje ya hospitali, dawa inaweza kwenda popote nje ya hospitali na hata mikoa ya mbali kwa haraka kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo bodaboda. Ninachokiona si kweli kwamba maduka yaliyo karibu na hospitali ndio wateja wa wizi wa dawa kutoka hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu, napenda kuishauri Serikali yafuatayo; Serikali igharamie viungo bandia (kama miguu bandia) pamoja na ukarabati wake kwa wahanga wa kisukari waliokatwa miguu hususan wazee; gharama za viungo bandia kwa wagonjwa wa kisukari viingizwe kwenye bima ya afya; na Waziri wa Afya kwa kushauriana na Waziri wa Katiba na Sheria wafute sheria

inayokataza uwepo wa maduka ya dawa mita 500 kuzunguka hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo tutawapunguzia wananchi adha ya kutafuta dawa na vifaa tiba wanazoandikiwa kwenda kununua nje ya hospitali za Serikali; Wizara ya Afya itambue kwamba ilitoa vibali mbalimbali vya kuanzisha maduka ya dawa. Kufunga biashara zao kutasababisha hasara kubwa kwa hawa wawekezaji wazalendo na kuikosesha Serikali mapato; maduka ya watu binafsi ya dawa hasa yale yaliyo karibu na hospitali husaidia upatikanaji wa dawa kirahisi kwani Serikali yetu yenyewe bado haina uwezo wa kutoa dawa zote na vifaa tiba; na kufuta hii sheria kutaonesha hawajali wafanyabiashara na wawekezaji wa biashara ya dawa na vifaa tiba hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, nami namshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara ya Afya. Nimshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi za makusudi anazofanya kwa ajili ya kuimarisha huduma ya afya hasa afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye amekuwa mwalimu kama jina lake lilivyo hasa kwa masuala ya afya, tunakuamini endelea kumsaidia Mheshimiwa Rais. Pia nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa jinsi anamsaidia pamoja na wataalam wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, niombe sasa nijikite kwenye mchango wangu katika Kiwanda cha Viuadudu kilichopo Kibaha, Pwani. Suala kubwa katika kiwanda hicho ni soko na mnunuzi mkuu ni Wizara ya Afya. Kwa msingi huo naomba kushauri yafuatayo; Wizara ya Afya na TAMISEMI wasukumwe kusaini mikataba wa manunuzi; ili mkataba utekelezwe Wizara ya Afya itenge bajeti kuendana na mahitaji na Wizara ya Fedha itoe fedha kwa mchanganuo utakaoianishwa kwa manunuzi ya kila mwezi; na fedha ya ithibati itolewe ili kiwanda hiki kiweze kupata soko la nje;

Mheshimiwa Spika, haya yakifanyika lengo la kiwanda hiki na nia ya kujengwa itaonekana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kadha wa kadha anazofanya kwa mustakabali wa Taifa letu. Napenda kumpongeza kwa

jitihada za hivi karibuni za kuendelea kujali utumishi wa umma ambapo amegusa sekta zote ikiwemo sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa maadhimisho ya sherehe za kitaifa za Mei Mosi, Mheshimiwa Rais alisema, mafanikio ya Taifa lolote hutokana na juhudi za wafanyakazi wake, yaani *every nation owes its success to its labourers.* Mheshimiwa Rais amedhihirisha maneno yake kwa matendo kwa kuwa mwaka jana alipunguza kodi ya mshahara kwa watumishi wa kima cha chini kutoka asilimia tisa hadi asilimia nane na kama haitoshi mwaka huu amewaongeza mshahara wa asilimia 23.3 pamoja na kada zingine za mshahara. Mheshimiwa Rais kwa mtindo huu anaendelea kuupiga mwingi kweli kweli na kwa kweli Watanzania watarajie makubwa zaidi kutoka kwa Rais wetu anayewapenda sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Moyo wake wa dhati wa kuboresha sekta ya afya haujaanza leo. Tumeona jitihada zake nyingi za kuboresha sekta ya afya tangu alipoaminiwa kwa mara ya kwanza katika sekta hii. Mara zote amesimama kidete kupambania afya za Watanzania. Namuombea Mheshimiwa Waziri afya njema ili maono aliyonayo kwa sekta ya afya yatimie kwa mstakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uviaji wa mimba ama utoaji wa mimba usio salama umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la vifo vya kinamama wajawazito. Uviaji wa mimba ni utokaji

wa mimba kabla ya wiki ya 28 ya ujauzito. Utokaji wa mimba unaweza kusababishwa na sababu ambazo sio za kukusudia ila kwa kiasi kikubwa ni kwa sababu zinazotokana na mimba zisizotarajiwa na hivyo kupelekea wengi kutoa mimba kwa watu wasio na ujuzi wa kitabibu na katika maeneo yasiyo salama kabisa.

Mheshimiwa Spika, duniani kote, utoaji wa mimba upo kwa kiasi cha milioni 56 kila mwaka ambapo katika utoaji huo, takribani wanawake milioni 25 wanafanya utoaji wa mimba usio salama. Kila mwaka kati ya wanawake hao wanaotoa mimba kwa njia zisizo salama asilimia 98 hutokea katika nchi zinazoendelea ambapo takribani milioni tatu ni watoto wa kike kati ya umri wa miaka 15 hadi 19 na takribani wanawake 47,000 wanafariki kila mwaka kutokana na utoaji huo wa mimba usio salama.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu Tanzania, takribani wanawake 405,000 wanatoa mimba kwa njia zisizo salama na asilimia 40 ya wanawake hupata madhara mbalimbali yanayotokana na utoaji wa mimba usio salama. Asilimia 18 ya wanawake hawa wanatoa mimba kwa madaktari walio na ujuzi stahiki, asilimia 31 wanatolewa na wauguzi ambao hawana ujuzi stahiki na asilimia 51 wanatoa kwa njia za kienyeji ikiwemo kunywa dawa kiholela kwa kushauriwa na wafamasia au kwa njia nyingine ambazo sio za kitabibu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa tatizo hili limepelekea matatizo mbalimbali ya uzazi kwa wanawake ikiwemo

ugumba na matatizo mengine sugu ya uzazi ningependa kushauri, elimu zaidi inahitajika juu ya utoaji wa mimba usio salama. Pamoja na elimu, uboreshwaji wa vitendea kazi na dawa stahiki zinahitajika katika vituo vya afya ili kusaidia madhara yanayotokana na utoaji wa mimba usio salama kwa sababu hatuwezi kusema tuache waathirike na matatizo hayo kisa tu ni jambo lisilo la kimaadili. Tuendelee kuwahimiza kuachana na utoaji mimba usio salama na uzazi salama lakini madhara yanapotokea tuwasaidie kwa kuweka dawa stahiki na vitendea kazi kwa sababu pamoja na yote wapo pia ambao wanapata matatizo ya kutoka kwa mimba bila kukusudi na wanahitaji kusafishwa ila sasa ili huduma zipatikane kwa urahisi ni vyema kuweka dawa na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo naomba suala la Muswada wa Bima ya Afya kwa kadri Mheshimiwa Waziri alivyoeleza lifanyiwe kazi mapema ili Watanzania wengi wanufaike na huduma bora za afya.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, ubora wa vituo vya afya vya Chikobe na Bukoli Jimboni Busanda vinahitaji Wizara ya Afya isimamie huduma *(qualify of service)* na uboreshaji wa miundombinu ili wananchi wahudumiwe vyema.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana kwa kazi nzuri, hii inathibitisha kuwa mnafanya kazi kama timu.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri na mawazo machache; kwanza ni kuhusu udhibiti wa Malaria; nafahamu kuhusu Kiwanda cha Kibaha ambacho ni ubia kati ya Serikali yetu na Serikali ya Cuba, nafahamu kiwanda hiki ni muhimu sana, ikiwa tutaamua kwa dhati kutumia dawa inayozalishwa ili kutokomeza mazalia ya mbu, tutapiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri, jipeni muda kujua uhalisia na mwenendo wa Kiwanda hiki, nani anakisimamia na kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu damu salama, napongeza hatua ya Wizara kugawa mifuko ya kukusanyia damu kwa Halmashauri zote, hata hivyo nashauri suala la hamasa ya wananchi kuchangia damu iongezeke, kwa namna gani. Nashauri namna bora ni kutoa *kits* kama *point* ambazo hizo zinaweza kumpa unafuu katika kupata huduma mbalimbali, kwa mfano tunaweza kusema kuwa wanafunzi wakiomba mkopo wa elimu ya juu, ambaye amewahi kuchangia damu anakuwa na *better chance* ya kupata mkopo kwa asilimia fulani zaidi kuliko mwingine.

Mheshimiwa Spika, nimetoa kama mfano lakini wataalam wetu wanaweza kutusaidia *best practice* ambayo italeta hamasa kuchangia damu, kwa mfano baadhi ya nchi mwenye *point* nyingi anakuwa *considered* katika nafasi kama za ajira, za jeshi na kadhalika. Hii itasaidia sana kukuza

hamasa ya watu au makundi katika jamii kama vile wanafunzi kuchangia damu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa wanaojitolea hasa pale Benjamin Mkapa, nilikuwa na mgonjwa Hospitali ya Benjamin Mkapa, mzazi. Ndugu zangu wiki mbili ambazo nimekaa pale hospitali na mzazi ambaye alijifungua wiki tatu Kayla na hivyo kulazimika kukaa kwa muda hospitali, nimeshuhudia ambavyo kwanza madaktari na wauguzi wakifanya kazi kwa bidii na moyo wa kujituma. Kwa kweli nimeona pia nilivoenda kuwaona wagonjwa ndugu zangu kwa kweli watu wanafanya kazi sana.

Ushauri wangu kuhusu ajira kwa wanaojitolea, Mheshimiwa Waziri nafahamu kwamba zipo taratibu za kiutumishi lakini zipo *exceptional cases,* pale Benjamin Mkapa wauguzi wa kike kwa kiume wanakesha na wale watoto waliozaliwa wakiwa na matatizo kama vile kuzaliwa kabla ya siku, wanafanya kazi, wanawabembeleza kwa moyo tena kuna wakati unakuta hata mama mzazi hawezi kumhudumia mtoto wa aina hiyo kwa kiwango cha hawa wauguzi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba watizamwe kwa jicho la kipekee. Suala hili nimeshauri hata katika mchango wangu kwa Wizara ya Utumishi.

Kuhusu *Mafinga Hospital;* kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy wakati ule kabla hajahamishiwa TAMISEMI, lakini pia Katibu Mkuu alipita Mafinga. Nafahamu

kuwa hospitali hii iko chini ya TAMISEMI, hata hivyo ninaomba kama ambavyo Serikali imefanyia ukarabati shule kongwe, ione uwezekano wa kuzifanyia ukarabati mkubwa hospitali kongwe kama ya Mafinga ambayo inahudumia zaidi ya Halmashauri tano. Tunashukuru kupitia fedha za UVIKO tunajenga jengo la dharura, hata hivyo kwa kuwa iko kando ya *highway* inazidiwa sana kwa huduma. Kwa mfano katika suala la watumishi, bado nasisitiza pamoja na kuwa ni suala la TAMISEMI, Mafinga itizamwe kwa macho mawili kwa sababu ya *location*. Kwa mfano Mafinga inahudumia wagonjwa kutoka Ihalimba - Mkoa wa Morogoro, Mbalari - Mkoa wa Mbeya, Nyigo - Mkoa wa Njombe na pia *Mufindi DC* na *Iringa DC*. Hivyo kwa namna ambayo itawapendeza na kwa fursa zitakazojitokeza kuitizama kwa macho mawili.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimae kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na upungufu wa dawa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya upungufu wa dawa katika nchi yetu ni ya kusikitisha sana. Tatizo hili ni kubwa na linakera sana. Serikali inajitahidi sana kutoa pesa kwa madhumuni ya ununuzi wa dawa lakini bado ufumbuzi wa suala hili ni kubwa. Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuweka mikakati madhubuti ya kuwadhibiti maafisa wetu wanaohusika na manunuzi ya dawa ili kuwachulia hatua za kinidhamu na kisheria ili kukomesha kabisa suala hili.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu chanjo; naipongeza Serikali yetu kwa kuendelea kuratibu upatikanaji wa chanjo pamoja na kuhakikisha chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana katika mikoa yetu yote. Hili ni jambo zuri sana katika nchi yetu. Naomba Serikali yetu iendeleze suali hili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kueneza elimu ya faida ya chanjo hizi katika jamii hasa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, tatu ni upungufu wa wafanyakazi katika vitu vyetu vya afya. Napenda kuipongeza Serikali yetu kwa jitihada kubwa inayochukua kwa kueneza huduma za afya nchini kwa kujenga vituo vya afya maeneo yote nchini. Hudumu ya afya ni miongoni mwa huduma muhimu sana kwa binadamu. Vituo vingi vimejengwa lakini bado

inaonekana kuna upungufu wa wafanyakzi katika maeneo kadhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni ujenzi wa vituo hivi ni vema ukaenda sambamba na kuongeza wafanyakazi ili kuboresha huduma hii. Wafanyakazi wa sehemu zote (idara) pamoja na madaktari ni vyema wakawa wa kutosha kabisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mchango wa maandishi katika Wizara ya Afya na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, pia nakupongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na uongozi wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnazoendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia kwa umahiri suala zima la afya, nampongeza pia Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Wizara ya Afya kwa kumshauri vyema Rais katika kusimamia suala zima la upatikanaji wa dawa nchini. Nampongeza Mama Samia Suluhu kwa ziara yake ya Uganda ambayo imeleta unafuu kwa waathirika wa virusi vya UKIMWI kupata dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI hapa nchi jirani ya

Uganda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni jambo kubwa na zuri limefanyika hivyo tunaipongeza Wizara na wataalamu wake wote kumshauri vyema Rais.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa dawa, bado tunaendelea kuishauri Serikali kama nilivyochangia katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba Serikali ione sasa namna bora ya kuongeza uwezo wa upatikanaji wa dawa kwa kuingia ubia kwa kufufua kilichokuwa kiwanda chetu cha dawa cha Mkoani Arusha (*Tanzania Pharmaceutical Industry- TPI)* hivyo Serikali kupitia *MSD* itachukua 60% ya hisa za uwekezaji wa kiwanda kile ambazo zilikuwa ni za mwekezaji binafsi na hisa 40% zitabakia kwa Msajili wa Hazina kama ilivyokuwa toka mwanzo. Kwa hiyo Serikali itakuwa na 100% ya hisa ili kufufua kiwanda chetu cha Arusha. Tunaamini kwa usimamizi mzuri wa *MSD* tutakuwa na uwezo mzuri wa kuzalisha dawa za kutosha kwa ajili ya wananchi wetu na pia tunaweza kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia kwa dhati na kwa moyo wa kizalendo na kwa kujitoa muhanga katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda ikiwa ni pamoja na viwanda vya kutengeneza dawa ili kuelekea katika kutimiza malengo endelevu ya milenia.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mwakilishi wa wafanyakazi wa Tanzania Bara Bungeni, napongeza kitendo

cha Mheshimiwa Rais na Serikali yake kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi na kuongeza mshahara kwa asilimia 23.3 jambo ambalo halijawahi kutokea katika Serikali yetu na suala la ongezeko la mshahara limekuwa ni kilio cha wafanyakazi kwa miaka isiyopungua sita.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kuliomba Bunge kuazimia kumshukuru na kumpongeza Rais na Serikali yake kwa niaba ya wafanyakazi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika hayo naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nimpongeze Waziri wa Afya pamoja na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Rais wetu kwa kutupa fedha kwa ajili ya kujenga jengo la mama na mtoto katika hospitali ya Wilaya ya Lushoto na pia tumepata shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya kujenga vituo vya afya kama ifuatavyo; Kituo cha Afya Mlola shilingi 700,000,000; Kituo cha Afya Ngwelo shilingi 250,000,000 na Kituo cha Afya Kwekanga shilingi 250,000,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali, bado kuna changamoto ya kujenga vituo vya afya katika maeneo yafuatayo; Kituo cha Afya gare; Kituo cha Afya Kwai

Kwemakame na Kituo cha Afya Mdando Kata ya Makanya. Vituo vyote hivi nilivyotaja hapo juu wananchi wameshaanza kujenga na majengo yapo kwenye hatua mbalimbali. Kwa hiyo niiombe Serikali itenge fedha katika awamu hii ili kuunga juhudi za wananchi walizokwisha kuzianza.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya upatikanaji wa dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zetu. Changamoto hii imekuwa ikiathiri sana wananchi wetu hasa kinamama wajawazito pamoja na Watoto. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue hatua za haraka ili kunusuru wananchi wetu wasiendelee kupoteza Maisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa Serikali, kwa kuwa nchi yetu imejaaliwa na rasilimali ya miti ya dawa pamoja na mimea dawa, na katika nchi hii kuna Watanzania waliojaaliwa vipaji vya kujua miti dawa na mimea dawa, na kupitia miti hiyo wakajaaliwa kutibu magonjwa mengi ni yale yasioambukiza, na utafiti umeshafanyika na kubaini ya kuwa matabibu hao wana uwezo wa kutibu magonjwa yafuatayo; ugonjwa wa kisukari, *pressure,* vidonda vya tumbo, bawasili, figo *stage* zote, kansa *stage* zote, tezi dume *stage* zote na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yote niliyoorodhesha hapa tumeyathibitisha kwa kuwatibu wagonjwa na mpaka sasa hivi wagonjwa wote wanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali kwa nini Serikali isitume wataalam wake kuwafuata matabibu hawa ili nao wajiridhishe ili Serikali ikijiridhisha iwasaidie matabibu hawa, kuwapa vitendea kazi vyote vinavyohitajika ili waweze kuzalisha dawa nyingi na ili Serikali ipunguze kuagiza dawa nyingi nje. Pia Serikali itaokoa fedha nyingi kuagiza dawa nje. Lakini pia kwa kuwa dawa zetu ni za miti yetu ya asili, kwa hiyo dawa zetu zitakuwa ni *organic* ambazo hazitakuwa na madhara yoyote kwenye mwili wa mwanadamu, na hii wazungu wakija kugundua ya kuwa dawa zetu ni *organic*, ni imani yetu kuwa Serikali yetu itaingiza fedha za kigeni, na pia dawa zetu zitakuwa zinachangia pato la Taifa. Sambamba na hayo wataalam wetu waziruhusu au wazisambaze katika hosptali zetu pamoja na kuzitangaza.

Mheshimiwa Spika, hili sio la kupuuzwa, ikiwezekana wataalam wetu wafanye ufuatiliaji wa haraka ili tiba asili iweze kuwa miongoni mwa sekta inayochangia pato la nchi yetu na sisi matabibu tumejipanga kutoa ushirikiano wa hali ya juu popote pale tutakapo hitajika hatutasita kutoa ushauri wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Afya, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Afya, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa sera ya afya ikienda sambamba na ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa Kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Sita, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya afya. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kwa kushirikiana na TAMISEMI, imeendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya Hospitali ya Wilaya na vituo vitano vya afya vya kata za Ikukwa, Ilembo, Santilya, Ilungu na Swaya. Vituo vyote vitano vinaendelea kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa hasa huduma ya watoto na

wakina mama. Hospitali ya Wilaya pamoja na vituo vya afya vimekamilika na maandalizi ya vifaa tiba yapo katika hatua za mwisho ili vianze kutoa huduma kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na janga la *corona virus (Covid-19),* tumejifunza umuhimu wa utayari wa huduma ya afya hasa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali na hivyo Serikali iongeze msukumo wa kupeleka vifaa tiba na kumalizia vituo vya afya na zahanati zilizojengwa kwa nguvu za wananchi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wananchi wa kata za Igoma na Isuto wamejenga vituo vya afya na kuna maendeleo mazuri ya kukamilisha, na pia Mji Mdogo wa Mbalizi wenye wakazi zaidi ya 150,000 hawana kituo cha afya, hivyo napendekeza Serikali kutoa kipaumbele katika bajeti hii kwa vituo vya afya hivi ili vianze kutoa huduma. Pamoja na vituo vya afya vya Ilungu, Igoma, Isuto na Mbalizi, napendekeza kukamilisha zahanati zote ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho ya miundombinu ya hospitali na vituo vya afya, Serikali ihakikishe bajeti ya mwaka huu inajielekeza zaidi ajira ya madaktari na watumishi wa afya kwa ujumla. Pamoja na maboresho hayo ya miundombinu, vifaa tiba na ajira kwa watumishi, napendekeza Serikali ikamilishe mpango kabambe wa Bima ya Afya kwa Wote na hasa kwa wazee na wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika kwa ajili ya kuiboresha afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kujitoa kwake kwa Watanzania kufanya kazi nzuri na nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara ya Afya wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi na kazi nzuri inayoendelea kufanyika, naomba nijikite katika Jimbo la Temeke.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Temeke iliyoko ndani ya Jimbo la Temeke imepandishwa hadhi na kuwa ya rufaa ya kimkoa lakini Serikali ilichukua hatua ya kutujengea Kituo cha Afya kilichopo Yombo Vituka kiitwachwo Malawi. Tunashukuru sana na majengo mazuri na ni ya kisasa ni ya ghorofa lakini lifti iliyoko pale ni nzima ila mkandarasi ameifunga isifanye kazi kwani hajalipwa pesa ya kuiweka pale na sasa ni zaidi ya mwaka na wahudumu wanapata taabu.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa anazofanya katika kuhakikisha Taifa hili linapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto zinazohusiana

na masuala ya afya. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasiyoambukiza yanashika kasi kwa ongezeko na hata idadi ya vifo. Kwa Tanzania magonjwa ya moyo yakiongoza na pili ni magonjwa ya saratani.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la ugonjwa wa saratani kwa sasa ni zaidi ya wagonjwa wapya 40,000 kwa mwaka na kusababisha vifo takribani 30,000 kwa mwaka huku tukiwa na wagonjwa zaidi ya 73,000 ambao wapo kwenye matibabu.

Mheshimiwa Spika, wahanga wakubwa wa ugonjwa wa saratani ni wanawake, na kundi hili la wanawake wanaopata ugonjwa huu wa saratani hasa ya shingo ya kizazi na saratani ya matiti wanakumbana na changamoto nyingi sana katika jamii mfano kuathirika kisaikolojia, kuathirika kiuchumi, mahitaji ya kijamii na kimwili na mapokeo kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi na nyingine nyingi zimekuwa miongoni mwa wanawake wengi wanaopata ugonjwa huu kukata tamaa na hata kutozingatia matibabu ya kitaalam ambapo wapo ambao wameishia kujaribu tiba asili, imani za kishirikina na maombi pekee.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kuhakikisha inaongeza nguvu katika kuhakikisha kunakuwa

na nguvu kubwa katika kupambana na changamoto za wanawake wanaoathirika na magonjwa ya saratani.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara ije na mpango mkakati kuhakikisha tatizo hili la saratani linapewa kipaumbele ili kujenga uelewa mpana kwa jamii kuhusu haya magonjwa ya saratani kwani huku kwenye jamii hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri wa Afya na Naibu wake kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu naomba niiombe Wizara iangalie kwa jicho la umakini zaidi katika maeneo yafuatayo; kwanza kumekuwepo na wizi mkubwa wa dawa katika vituo vya afya nchini, baadhi ya watumishi wasio waaminifu wanachukua dawa kutoka kwenye vituo vya afya na kwenda kuuza kwenye maduka ya watu binafsi. Wizara iweke nguvu kubwa kwenye udhibiti wa vifaa tiba na dawa.

Pili, afya kwa wanadamu ni muhimu sana, hivyo tuwekeze nguvu pia kwenye uzalishaji wa wahudumu wa afya wenye sifa na ujuzi usiotiliwa shaka. Hivyo, tupitie upya

sifa zinazohitajika kwa ajili ya kuwadahili wanafunzi watarajali kwenye vyuo vya afya.

Mheshimiwa Spika, ombi, ninaomba vifaa tiba na dawa na vitendanishi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ngorongoro na Kituo cha Afya Samunge kilichojengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika afya ya mama mjamzito na mtoto. Pamoja na jitihada za Serikali iliweza kupunguza vifo vya uzazi kwa kina mama kwa wastani kutoka 11,000 mwaka 2015 mpaka kufikia 2020 iliweza kupunguza wastani wa vifo 3000 kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Kanda ya Ziwa zinaonyesha kuwa mwaka 2019 wakinamama 448 walipoteza maisha; mwaka 2020 wakinamama 410 walipoteza maisha na mwaka 2021 wakinamama 374 walipoteza maisha pia. Ukiangalia takwimu hizi utaona vifo vinapungua lakini bado hali sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kuendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa zote za magonjwa sababishi ya vifo hivi ambayo ni kifafa cha mimba; kutoka damu nyingi kabla na baada ya kujifungua na uambukizi wa vimelea kwenye mfumo wa uzazi.

Ushauri wangu mwingine ni kupeleka madaktari bingwa wa kinamama hasa katika hospitali za Wilaya na Mikoa kwani watabaini matatizo mapema na kuweza kuyapatia ufumbuzi mapema.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia kuhusu ugonjwa wa saratani. Shirika ia Saratani Duniani *(International Agency for Research on Cancer - IARC)* takwimu zinaonesha kwa mwaka kuna visa vipya vya saratani 40,500 hapa Tanzania. Wagonjwa wengi wanatoka Kanda ya Ziwa na wanahudumiwa na Hospitali ya Rufaa Bugando. Wagonjwa wanaofika Bugando wanaongezeka kwa kasi sana kwa siku wanaohitaji huduma ya mionzi ni 180 lakini hospitali ya Bugando ina uwezo wa kutibu watu 80 tu kwa siku hali inayosababisha ucheleweshaji wa matibabu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe uletaji wa mashine mpya za kisasa na kuongeza wataalamu ili kuboresha huduma hizi.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa maandishi na kwa kifupi kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu naomba nianze kwa kumpongeza Waziri Ummy na Naibu wake Dkt. Godwin Mollel, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani kwa kazi nzuri sana wanayofanya. Lakini kipekee naomba kwa

dhati kabisa, nimshukuru na kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri na jinsi anavyotubeba Watanzania kama vile mama anavyobeba familia yake. Ni kwa sababu ya uongozi wake mahiri Mawaziri wanatekeleza majukumu yao kwa umakini . Pamoja na salamu zangu za pongezi naomba kuweka mezani changamoto zifuatazo kwenye Jimbo la Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Kwanza kuna upungufu mkubwa wa vituo vya afya jimboni na hata vile vilivyopo havikidhi viwango na mfano mzuri ni Kituo cha Afya Makiba ambacho Naibu Waziri alikitembelea.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya miundombinu imechakaa inahitaji ukarabati mkubwa. Mwaka jana tuliletewa shilingi 500,000,000 ambazo zilirudishwa Serikalini kabla ya kutekeleza kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko la mabubu na viziwi kila mwaka, mwaka wa fedha 2018/2019 kulikuwa na mabubu na viziwi 6,103; mwaka 2019/2020 walikuwa 6967; mwaka 2020/2021 idadi ya mabubu na viziwi walikuwa 7246 na mwaka 2021/2022 walikuwa 8508. Ongezeko hilo kila mwaka lina *based implication* watoto hao wanapokuwa mashuleni

Serikali inatoa ruzuku kwa chakula kwenye shule za vitengo maalum.

Mheshimiwa Spika, tuna shule 213 na vitengo 10 vinavyofundisha mabubu na viziwi. Serikali imetumia bilioni 3.4 kwa shule ya mabubu na viziwi mwaka wa fedha 2018/2019; mwaka 2019/2020 bilioni 3.9; mwaka 2020/2021 bilioni nne na mwaka wa fedha 2021/2022 bilioni 6.3.

Mheshimiwa Spika, gharama ya walimu wanaolipwa kuwafundisha wanafunzi hao, na hata uhitaji wa wataalamu wa kuzungumza kwa alama ni mzigo mkubwa kwa Taifa ambao tunaweza kuuepuka. Hata hivyo ustawi wa rasilimali watu unapungua na *well being* ya mtu husika inaharibika na familia nyingi zinataabika. Kwa kuwa gharama za matibabu na hata vifaa vya mabubu na viziwi ni gharama kubwa. Serikali imeshapeleka nje watoto wengi kupandikizwa vifaa vya usikivu. Gharama ni kubwa upasuaji na *machine* ni dola 35000. Serikali imesema katika hotuba ya Waziri kuwa wamepandikiza usikivu kwa watoto 14 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mara ya kwanza wakati wa awamu ya kwanza ya Waziri Ummy upasuaji umefanyika hapa nchini na bado Serikali haingalii chanzo cha yote hayo.

Mheshimiwa Spika, ushauri au mapendekezo yangu kwa Serikali; waweke *audiometer* katika Hospitali za Wilaya, *audiometer* ni kipimo cha kujua usikivu wa mtoto. Audiometer

bei yake ni kati ya shilingi milioni sita had inane, na iwe ni lazima mtoto akizaliwa apimwe usikivu. Pia *ABR* iko muhimbili peke yake, Serikali iongeze *ABR* kwenye hospitali za rufaa nchini ili kubaini watoto wakiwa wadogo na kupunguza idadi ya mabubu na viziwi; matibabu hayo yaingizwe kwenye matibabu yanayohudumiwa na Bima ya Afya na pia Serikali iweke bei elekezi ya vifaa tiba kama hakuna sheria ya bei elekezi basi, Serikali ilete muswada, tutengeneze sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke vitengo vya *speech therapy* kila hospitali ya rufaa na hospitali za Wilaya ili kuwasaidia watoto wa-*develop speech,* lakini watafute namna ya kuongeza wataalam wa *speech therapy* kwa sababu hawapo nchini na ni wachache mno. Watu wanapoteza usikivu kwenye migodi lakini vifaa ni ghali sana na hata wanaopata *stroke* wanahitaji mazoezi ya *speech,* vitengo vya *speech* na wataalamu waongezwe nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Afya. Namshukuru Mungu kwa kunijalia zawadi ya uhai na afya njema. Pia nampongeza sana Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Mollel na Katibu Mkuu Dkt. Abel Makubi na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri ya kuhakikisha wanapata huduma bora za afya, nawapongeza sana, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika*, n*ieleze kwa masikitiko makubwa juu ya kusuasua kwa ujenzi wa hospitali yangu ya rufaa ya mkoa ambao ujenzi wake umekuwa ni wa muda mrefu kwa zaidi ya miaka13 hadi sasa hospitali hii haijakamilika.

Mheshimiwa Spika*,* majengo haya ambayo yalijengwa miaka iliyopita yameshaanza kuchakaa na yatahitaji bajeti nyingine kwa ajili ya ukarabati hivyo kutokuwa na thamani ya ujenzi wa hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika*,* naishukuru Serikali kwa kuendelea kututengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali yetu ya rufaa lakini fedha hizi zimekuwa hazitoshi. Ninaiomba Serikali itutengee fedha za kutosha ili hospitali hii ya rufaa iweze kukamilika, endapo hospitali hii itakamilika itakuwa ni msaada mkubwa sana kwa wananchi ambao wengi hawamudu gharama za matibabu kwenye hospitali za rufaa za mikoa ya jirani hususani wanawake waishio pembezoni. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Ummy atapokuja ku-*wind* unipe *commitment* ya Serikali ni lini hospitali hii ya rufaa ya Singida ni lini itakamilika?

Mheshimiwa Spika*,* pia hospitali hii ya rufaa ya mkoa inakabiliwa na uhaba mkubwa wa vifaa tiba, watumishi wakiwemo madaktari bingwa, tuna madaktari bingwa sita tu na miongoni mwa hao wapo masomoni. Ninaiomba Serikali ituletee madaktari bingwa wa kutosha akiwemo daktari

bingwa wa watoto ili wananchi wetu waweze kupata huduma za kibingwa ndani ya mkoa wao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kutujengea hospitali za Wilaya ya Mkalama, *Singida DC* na Ikungi, lakini hospitali hizi hazina vifaa tiba, watumishi na dawa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa majengo haya mazuri bila ya vifaa tiba na wataalam ni kazi bure, mfano hospitali ya Wilaya ya Mkalama, kwa mwaka wa fedha ulioisha 2021/2022 tulitengewa fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ununuzi wa vifaa tiba, lakini ni vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 77 tu ndivyo vilivyoletwa katika hospitali hii, jambo hili linasikitisha sana, fedha ipo lakini ni kwa nini *MSD* hawaleti vifaa tiba? Wilaya hii pia ina uhaba mkubwa wa watumishi 607. Naomba tuletewee vifaa tiba, watumishi na dawa za kutosha katika hospitali zetu za Wilaya, vituo vya afya na zahanati za Mkoa wa Singida ili malengo mazuri ya Serikali yaweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel atafuatiwa na Mtoja Hoja. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya endelea.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini kwa kutusimamia kwenye hiki kipindi kigumu kidogo naanza kuona

matumaini tumekaribia na mwisho, lakini tumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye siyo tu kwamba amekuwa kiongozi wetu lakini amekuwa *mentor* wetu. Wabunge ni mashahidi akija Majimboni kwetu anatuita Wabunge wenzangu nasi anatuita Mawaziri wenzangu wakati mwingine tunaenda kwa Waziri Mkuu tunaongea tunajisahau tupo na Waziri Mkuu baadaye tukitoka sisi tunajiuliza hivi pale tuliharibu lakini anakuwa ametuvumilia, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru ninyi Wabunge wenzangu mmetuchanganya Mheshimiwa Ummy Mwalimu alikuwa ananiambia haya madeni tutayalipaje, lakini mmetuheshimisha na wakati mwingine tunawaza sasa je, tutaitunzaje, shida siyo kuambiwa mmefanya vizuri shida nitutatunzaje hiki mlichokiaminisha kwetu. Lakini mimi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Ndugu yetu Makubi tulikuwa tunashangaa tukiwa nje kwamba ule umahiri wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambao tunauona sisi na ninyi mnauona tunasema ahsanteni sana Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Kingu na wenzangu ambao tulikuwepo Bunge lililopita, nilipokwenda kwenye uchaguzi 2020 tulikuwa tukipigiwa kura na tukizungumzia *performance* zilizofanywa kwenye Wizara ya Afya, aliyetusaidia tukafika hapo ni huyu Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye tunae leo. Niseme tu alipokuja Wizara ya Afya akasema sisi tunaanzia *strategy*

inayoitwa Samia Suluhu Hassan *strategy* ya 1.3 Trilioni ambayo imekuja yote ikaelekea kwa wananchi akatwambia tukae chini, akaita watu wanaosimamia mradi wa *investing to people* akakaa nao bila kuwagombeza akapunguza kwenye posho, akapunguza kwenye semina, akapunguza kwenye nini, leo tunazo Bilioni 10 tunaenda kujenga hospitali ya akina Mama Dodoma huyo ndiyo Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

Mheshimiwa Spika, hata siyo muda na ninafiriki mtaona kwenye Majimbo kama 100 fedha zinakuja Bilioni 7.8 ambazo hazikuwa kwenye bajeti kabisa, ni katika kukaa kupunguza kwenye posho, kupunguza kwenye nini zikapatikana Bilioni 7.8 na ndani ya wiki zilizopita zimepelekwa TAMISEMI kwa ajili ya kuja kwenye Majimbo yenu, huyo ndiyo Ummy Mwalimu ambaye mmesema hapa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuja tulikuwa tumepanga ilipangwa kwenye bajeti ya kawaida na kwenye utaratibu wa kawaida ilipangwa kwamba tununue *ambulance* 503 akasema hebu niachieni niwapigie *UNICEF* alipowapigia *UNICEF* makubaliano yaliyofanyika kule *ambulance* 503 tukajikuta kwa kununua kupitia *UNICEF* tunanunua *ambulance* 663 maana yake zimeongezeka *ambulance* 160. Maana yake nini Waheshimiwa Wabunge tunapozungumzia sasa hivi suala la *ambulance* kila Jimbo linaenda kupata *ambulance* mbili. Jana alikuwa anatuambia tuhangaike kwenye *Global Fund* tutafute nyingine 150 Mungu akisaidia inawezekana zikaendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Dada yangu Msambatavangu Jesca amezungumizia suala la tiba ya akili, jana tulikaa vilevile Mheshimiwa Waziri akawa anasema hebu tuitishe Kongamano la Afya ya Akili. Tena nilikuwa namwambia hapa lile kongamano unaweza nimuombe akubali awe ni Balozi kuhakikisha kwamba tunapigania suala la Afya ya Tiba ya Akili. Niwaambie tu, shida moja afya tumekuwa tukiliangalia kwamba tatizo la maendeleo ya jamii tu, lakini tiba vilevile ni suala la uchumi. *COVID* ilivyokuja tulizungumzia *COVID* kama ugonjwa lakini tukazungumzia kama suala la kiuchumi, lakini leo ukizungumia kuanzia mtoto anapozaliwa inavyobebwa mimba unapompa lishe na mambo mengine yanakuja kutokea hayo ambayo anayasema Mheshimiwa Mbunge pale na kwamba hata tunapotoa fedha nyingi kwa wanawake kule vijijini, kwa vijana halafu *outcome* ya fedha tunayo *dish* kule kwa ajili ya kukuza uchumi na kufanya mambo mengine, inapokuwa haitokei ina mahusiano makubwa sana na lishe na namna gani tunavyofanya lishe kuanzia watu wanapokuwa wadogo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile wenzetu sasa hivi mashindano tunakwenda dunia ambayo tunaizungumzia dunia ya *artificial intelligent,* wafanyakazi watakaotakiwa kesho kutwa siyo wafanyakazi wenye uwezo wa kufanya kazi ni wafanyakazi wenyewe uwezo wa kufikiri nakuja na mawazo mapya. Kama hujaboresha lishe, kama hujaboresha tiba ya afya ya akili huwezi kupata hiyo kaliba ya watu ambao ni *innovative* na wenye uwezo wa kufanya mambo hayo. Ndiyo

maana nasema Mheshimiwa Waziri amesema hapa hilo kongamano akilitayarisha ni muhimu Wabunge wote tushirikiane.

Mheshimiwa Spika, tumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kipindi kidogo cha mwaka huu mmoja, kwenye hospitali yetu ya *Ocean Road* tumekwenda kwenye Afrika nzima kuna nchi nne tu ambazo zinazalisha mionzi tiba zinaviwanda za mionzi tiba. Leo tunaenda kuingia kwenye historia ya Afrika kuwa nchi ya tano kwa Afrika kuzalisha mionzi tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa tunazungumzia mgonjwa wa Mheshimiwa Saashisha ambaye amechelewa pale tukigojea mionzi tiba itoke kwa ndege siku ya Jumatano kutoka Afrika Kusini. Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kiwanda kimefikia asilimia 95 na sasa ndani ya miezi mitatu tunaenda kuzalisha hapa, na watu wetu watatibiwa hapa na nchi zinazotuzunguka zitaanza kuja hapa kwetu. Ukizungumzia hospitali yetu ya *Ocean Road* kwa maana ya uboreshaji uliofanyika pale utakwenda pale nchi 16 zinakuja pale kuchukua ujuzi wa namna gani unaweza kufanya mionzi tiba, ukienda *JKCI* mpaka kuna watu wametoka nchi zingine za Ulaya wanakuja kutibiwa pale, siyo tu kwa sababu moja kwamba kule wanatoa *standard* ya Ulaya lakini kwa bei rahisi zaidi. Kwa maana hiyo tunapozungumzia Wabunge suala la *medical tourism* Serikali yetu imejipanga na Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan amejipanga vizuri kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amesema waziri hapa suala la upandikizaji wa Uroto na amesema Waziri hapa kwamba kwa Afrika kwa Mashariki na Kati sisi wenyewe ndiyo tunafanya, lakini Waheshimiwa Wabunge muelewe kitu walichofanya Rais wetu kwa kipindi hiki kidogo cha mwaka mmoja, kufanya Uloto kwa mgonjwa mmoja alikuwa anapelekwa India kwa thamani ya Milioni 250 kwa mgonjwa mmoja, leo hapa Tanzania baada ya Rais wetu kununua vifaa na vipo Muhimbili inafanyika kwa Shilingi Milioni 70 na anafanyiwa mgonjwa bure, maana yake tunaokoa Milioni 180 zinakwenda kufanya shughuli zingine za maendeleo. Hayo ndiyo mambo tukisema Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan anaupiga mwingi hiyo ndiyo maana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala zima la ubora wa huduma. Kwa kweli ukizungumzia ubora wa huduma utazungumzia suala la dawa, utazungumzia suala watumishi, utazungumzia masuala mengine yote na upatikanaji, vilevile kwenye ubora wa huduma utazungumzia suala la ujenzi, majengo ambayo yanajengwa na mmeona wenyewe kwamba yamejengwa tunaenda kujenga *EMD's* kwenye Wilaya zetu, tunaenda kujenga *ICU's* na kuweka vifaa, lakini utazungumzia kusomesha wataalamu.

Mheshimiwa Spika, leo kama Tanzania watu wanatoka nchi zilizotuzunguka kuja kujifunza kwa wataalam wetu kuzungumzia nayo ubora wa huduma unazungumzia teknolojia nayo, kwamba tuwe na *high standard* ya

teknolojia ambayo wakati mwingine tunaweza tukawa na mtaalam hapa lakini kama hatuna teknolojia inabidi mtu wetu aende kufuata kule, tukinunua teknolojia hapa ni gharama rahisi zaidi kumleta mtaalam kutoka nje akaja kutusaidia kwenye teknolojia iliyopo hapa na ikawa gharama zaidi na akawatibu wagonjwa wengi zaidi kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu. Kwa hiyo hayo yote yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmezungumzia suala la *incentive,* kwamba Madaktari wetu waache kukimbiakimbia kwenda sehemu tunafanya nini. Tunachowaambia tunampongeza sana *Professor* Mohamed Janabi wa Hospitali ya Jakaya Kikwete, amefanya kazi kubwa sana nzuri, Madaktari wake wanabaki pale pale na wanafanya na hawakimbiikimbii na Mount Meru hospitali wamefanya hivyo. Tutachukua *model* ya *JKCI* na *model* ya Mount Meru *Hospital* ambayo imeboreshwa pale halafu tuone ni namna gani tuna *roll out* kwenye nchi nzima ili iweze kufanyika namna hilo na lile ambalo mmeshauri Wabunge hapa liweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la damu salama kwa kweli damu hainunuliwi, damu hakuna sehemu damu wametembea nayo watu, tunaendelelea kuboresha Mheshimiwa Waziri ameitisha kikao na hii ilikuwa ni kuhakikisha kuboresha kwamba wataalam wetu wanapelekwa.

Mheshimiwa Spika, unajua wakati mwingine unaweza ukampeleka Mkurugenzi wa kukusaidia masuala ya damu

kwenye Kanda lakini huyo mtu hata hawezi kuitisha kikao tu cha ukoo wake, unataka aitishe watu wakubali kutoa damu. Tunataka kuwaweka watu sasa ambao wana uwezo wa ku-*mobilize* kutumia mbinu mbalimbali kuhakikisha watu wanakuwa tayari kutoa damu.

Mheshimiwa Spika, mmezungumzia suala la tiba asili nakwenda haraka haraka, kama tulivyokwisha kusema tayari Rais wetu ametoa Shilingi Bilioni 2.8 zinakwenda kufanya utafiti pale *NIMR* kuhusu tiba asili mbalimbali. Pia kuna muda ambao Waziri wetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu hivi karibuni ataenda kufungua hospitali ya tiba asili iliyopo kule Meru. Ni hospitali ambayo inatumia miti shamba kutoka Mlima Meru kutoka kule Umasaini lakini mengine kutoka Ulaya. Unaingiza kwenye maabara ya kawaida ya kisasa, inaingizwa kwenye vipimo vya kawaida vya kisasa lakini ukifika duka la dawa unapewa dawa za tiba asili.

Mheshimiwa Spika, wanaotibu ni Madaktari wazalendo lakini *supervisors* ni Wazungu wawili kutoka Australia, kwa namna hiyo tutachanganya ujuzi wa mwenzetu kutoka nje na sisi wenyewe tukimaliza tunaweza tukaboresha tibaasili zetu na kama ambavyo Mheshimiwa umesema tutatembelea Momba tutakuja Momba na tuangalie namna ya kufanya na kuhakikisha kwamba na wenzetu wa tibaasili kuhakikisha wanaweka hayo mambo sawa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Imeshagonga, nakushukuru mimi natoa hoja ili la *TMDA* na *TBS* mimi nafikiri tutaendelea kuwasilishiana kwenye Serikali na Waziri amelichukua litaenda kufanyiwa kazi kwa sababu ni kweli chakula ni sehemu muhimu sana lakini chakula usipo *control* tutapata matatizo ya figo, kansa na mambo mengi. Waziri amelichukua kwa uzito.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamuita Mtoa Hoja, wapo wageni ambao wapo hapa Bungeni.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni Kaka yake na Mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. Tunay mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani ambaye ni Katibu wa CCM Kata ya Kijota kutoka Singida Kaskazini Ndugu Amos. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambaye ni Ndugu yake kutoka Kitunda Jijini Dar es Salaam Airine Mwanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu Waziri wa Afya aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii hili niweze kuhitimisha hoja yangu na nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri wenu ambao mmetupatia ili tuweze kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa watanzania. Kipekee tushukuru sana maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya mwenyekiti wetu Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kwa kweli wanatupa ushirikiano mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba maoni na ushauri wa Wabunge tumeuchukuwa na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kwa kweli niwashukuru niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi ambazo mmetupatia, mmetutia moyo mmetupa ari mmetupa nguvu ya kuendelea kusimamia Sekta ya Afya nchini na ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tuna deni kubwa sana kwenu Waheshimiwa Wabunge tuna deni kubwa sana kwa watanzania na tuna deni kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, tunatambua dhamana kubwa tuliyonayo katika wizara hii, afya ni jambo kubwa afya ni jambo linalomgusa kila mtanzania awe tajiri awe maskini. Kwa hiyo, tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutasimamia vyema Sekta ya Afya nchini kuhakikisha watanzania wanapata huduma za afya afya ni mali afya ni mtaji afya ni uchumi.

Mheshimiwa Spika, kipekee nishukuru Wabunge ambao wamechangia tumepata wachangiaji 31 nikiongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Mwenyekiti wa Kamati lakini pia kuna Wabunge kumi wamechangia kwa maandishi na Wabunge saba walichangia wizara yangu wakati wa mjadala wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tuseme kwamba yote ambayo Wabunge wamechangia tutayafanyia kazi na kubwa tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake, kwa utashi wake, kwa dhamira yake ya kutaka kuona watanzania wanapata huduma bora za afya, hususan afya ya uzazi mama na mtoto. Kama mtakumbuka Wabunge ambao mlikuwa katika Bunge la kumi na moja, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais alijifanyisha kazi usiku na mchana ni kama vile alikuwa ndiye namsaidia kuhusu Sekta hii ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuwa anafuatilia huduma za Afya alianzisha kampeni ya jiongeze tuwavushe salama ili tuweze kuokoa wanawake wajawazito Rais Samia huyu ndiye aliweza kuzindua chanjo ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi, ndio alitusukuma tukapata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa mara ya kwanza kujenga Vituo vya Afya vitakavyofanya upasuaji wa dharula ikiwemo kumtoa mtoto tumboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa pia ni maono ya Rais Samia Suluhu Hassan alituwezesha kuzindua pia kampeni ya usichukulie poa nyumba ni choo ambapo pia tunaona sasa kaya za watanzania zina vyoo. Kwa hiyo, suala la afya kwetu sisi tunafahamu kwamba linamgusa kwa karibu sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan. Pia ameingia madarakani tumeona fedha nyingi zinaenda kwenye miundombinu kwenye *ambulance* kwenye watumishi.

Mheshimiwa Spika, kipee pia nimshukuru Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.Mheshimiwa Waziri Mkuu kwetu sisi ni mlezi, mwongozaji, ni mwongoza njia amekuwa akituelekeza usiku na mchana kufanyia kazi changamoto mbalimbali za Sekta ya Afya, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushuru sana kwa usimamizi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi lakini naomba niongee kwa sababu ya muda hoja kama tano au sita ya kwanza ambayo imeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala la upatikanaji wa dawa na vifaatiba katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi ni kwamba hoja hii sisi tutaenda kuifanyia kazi zaidi tumegawanya katika maeneo makubwa matatu eneo la kwanza ni ngazi ya wizara, tutahakikisha tunakata maoteo sahihi ya mahitaji ya dawa na vifaatiba. Kama Jiji langu la Tanga linasema litatumia kwa

mwaka kopo za *paracetamol* 100 kwa hiyo, lazima tutaangalia je wamepata kopo 100 katika kipindi hiki na hii ndio hoja ambayo pia imeangaliwa imesemwa na Waheshimiwa Wabunge kutumia *TEHAMA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TEHEMA* itatusaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya lakini pia sambamba na maoteo tutasimamia miongozo ya kamati za dawa *therapeutic committee* mwongozo wa *standard treatment guideline* wa matibabu ya kitaifa na miongozo mingine. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Kingu kwa kuleta hoja ya kuanzisha *drug revolving fund* kwa kweli hili jambo litasaidia uwepo wa upatikanaji wa dawa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tutafanya *audit* ngazi ya pili ni bohari ya dawa *MSD* kwanza nimeshawaelekeza *MSD* tutawapima kwa upatikanaji wa dawa za miezi minne na sio mwezi mmoja hili tumewaambia tunataka dawa zote 290 pamoja na vifaatiba vipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili pia tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa maagizo yake tumeshaanza kuyafanyia kazi sambamba na Mheshimiwa Rais kubadilisha uongozi Mtendaji Mkuu wa *MSD* pamoja na kumteuwa Mwenyekiti wa Bodi tunawaondoa Wakurugenzi watano wa *MSD* (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Fedha *MSD* anaondoka, Mkurugenzi wa Manunuzi *MSD* anaondoka,

Mkurugenzi wa *Logistic* wa *MSD* anaondoka, Mkurugenzi wa Sheria wa *MSD* anaondoka, na Mkurugenzi wa Utawala wa *MSD* wanaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tumeshauriwa pia tutaenda kuwaangalia na mifumo *supply chain system* mifumo ya usambazaji wa dawa ndani ya *MSD* lakini kubwa tutaendelea kuitaka *MSD* kununua dawa na vifaatiba kutoka viwandani, kwa kuzingatia mikataba ya muda mrefu. Lakini Waheshimiwa Wabunge naomba niseme jambo moja nimepewa dhamana ya kusimamia sekta ya afya hatuta-*compromise* ubora wa dawa na vifaatiba kwa sababu tusije tukaenda kuwapa matatizo watanzania kwa kutoangalia ubora wa dawa na vifaatiba kwa hiyo, jambo hili tutalisimamia kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nimpe pole Mkurugenzi mpya wa *MSD* umepewa hongera lakini jana nilimwambia una kazi kubwa sana kwa sababu matumaini ya Mheshimiwa Rais ya Wabunge na mimi mwenyewe kwake ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusema Tukai Mavele alikuwa ndiye mshauri wa Serikali kuhusu masuala mazima ya dawa akiwa upande wa ubalozi wa Marekani Mwenyekiti wa Bodi Rosemary William Slaa alikuwa ndio mshauri wa Serikali kwa upande wa *Global Fund* ambao wanatupa dawa za UKIMWI *TB* na Malaria. Kwa hiyo, juzi nilikuwa namwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sawa Rais amewaambia nyie si

mnatukosoa nyie si mnashauri haya sasa nendeni mkafanya hayo ambayo mlikuwa mnayaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *DG MSD* una kazi kubwa na Waheshimiwa Wabunge nataka kusema tumemwambia tunataka ndani ya miezi mitatu dawa zifike katika vituo na hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika eneo hili la dawa ni suala la matumizi ya dawa katika ngazi ya hospitali na vituo, *MSD* anaweza akapeleka dawa lakini je madaktari wetu na wataalam wetu wanazingatia miongozo ya matibabu ya Kitaifa? Kwa sababu ziko taarifa tumezipata dawa ambazo zipo katika hospitali zilizonunuliwa na Mfamasia zilizoagizwa na Mfamasia daktari anaandika dawa zake mwenyewe ambazo ni kinyume na *standard treatment guideline* kwa hiyo hili tutalisimamia kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Waheshimiwa Wabunge mtusaidie mnapokaa kwenye mabaraza ya Madiwani ni lazima tuhoji kamati za afya za kusimamia vituo je zinafanya kazi je zinafuatilia upatikanaji wa dawa. Lakini kubwa kwenye eneo la dawa ni *TEHAMA* mifumo ya *TEHAMA* itatusaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha mnyororo mzima wa dawa. Lakini kamati pia imetoa maoni kuhusu matumizi holela ya dawa tutaendelea kuyafanyia kazi eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo pia la mwisho katika dawa tutafufua au kuimarisha uzalishaji wa ndani wa dawa

kiwanda cha Keko tutapata fedha tuweze kuwekeza kununua mashine za kisasa na kiwanda kile cha *TPI* Arusha ambacho pia kimeelezwa na Mheshimiwa Catherine Magige tutahakikisha pia tunapata wawekezaji tayari kesi imemalizika mahakamani *TR* anafanya mawasiliano tunatafuta wawekezaji waweze kufufua kiwanda kile cha *TPI* ambacho kipo Arusha pamoja na kuendeleza viwanda vingine vya Keko na Idodi.

Mheshimiwa Spika, suala la Bima ya Afya hili niseme tutaendelea kutoa elimu kuwahamasisha watanzania kuona umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya ili waweze kupata huduma za matibabu kabla ya kuugua. Lakini pia tutakamilisha haraka Muswada ule wa sheria wa *Universal Health Insurance*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za kinga Mheshimiwa Shigongo amesema jambo zuri pamoja na Dkt. Paulina pamoja na Mheshimiwa Cecilia Paresso ni kweli ukiangalia hii bajeti tunazungumzia tu tiba tunatakiwa pia ku-*foccus* kwenye *preventive Intervention*.

Mheshimiwa Spika, na mimi ndio maana ukiniuliza waziri chagua kipaumbele chako cha kwanza sina hela nitafanya chanjo za watoto kwa sababu ile ni moja ya njia ya kuwakinga Watoto. Lakini Mheshimiwa Shigongo kuhusu homa ini tunakubaliana na wewe kwamba nalo ni janga kwa sababu *prevalence* ni asilimia 4 kwa hiyo tayari nimeshamwelekeza Katibu Mkuu ule mpango wa Taifa wa

kupambana na UKIMWI tunaenda kuubadilisha utakuwa ni Mpango wa Taifa wa kupambana na UKIMWI pamoja na homa ya ini. Kwa hiyo, tunakuwa na *integrated programme* tutaamasisha wananchi wapime na wapate chanjo ikiwemo kuhakikisha wanapata chanjo kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Furaha Matondo umezungumza saratani ya mlango wa kizazi kwa uchungu mkubwa. Ni kweli ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge katika mikutano yetu saratani zinazoongoza kuwakumba watanzania ni saratani ya matiti na saratani ya mlango wa kizazi kwa hiyo, naomba pia tuendelee kuwaambia wazazi na walezi wawapeleke watoto wetu hasa wa kike kupata chanjo ya kuwakinga na maambukizi ya saratani ya mlango wa kizazi.

Mheshimiwa Spika, suala la kinga pia Mheshimiwa Dkt. Paulina tutaweka nguvu katika *environmental health* katika usafi na afya ya mazingira hivi kwa nini vijiji vyetu na miji yetu ni michafu, kwa nini kuna mabwana kwa nini hatufyeki nyasi kwa nini hatuwekezi katika kuhakikisha pia tunazingatia kanuni za usafi na afya bora kwa hiyo, ni eneo ambalo tutalipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la kinga amezungumza Muuguzi mzuri Mheshimiwa Tecla *NCD (non-communicable disease)* ni jambo ambalo linaongezeka kila siku na hela hii ya bajeti Waheshimiwa Wabunge haitatosha

hata siku moja kama hatutadhibiti magonjwa yasiyoyambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sambamba na kutoa elimu ya watu kuzingatia ulajji wa vyakula kuwekeza kwenye kupima kuepuka unywaji wa pombe kupita kiasi kuvuta sigara lakini pia tunataka kuhakikisha kwenye zahanati wananchi wanapata huduma za kupima au kufanya uchunguzi ili tuweze kugundua mapema magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukisubiri saratani imefika hatua ya nne hatua ya tatu inakuwa ni matibabu yanakuwa kidogo ni ghali lakini pia hatupati matokeo mazuri. Suala la afya ya uzazi mama na mtoto mdogo wangu Mheshimiwa Husna ameongea kwa uchungu lakini pia mtani wangu Mheshimiwa Kabula pamoja na Mheshimiwa Mabula. Kwanza nataka kusema hatujabadilisha sera ya afya sera ya afya inasema huduma kwa akina mama wajawazito na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano ni bure.

Mheshimiwa Spika, nimefundishwa kusema ukweli hiyo sera inatamkwa ni bure kihalisia ni kweli wanawake wengi hawapati huduma za bure kwa ajili ya akinamama na Watoto. Kwa hiyo, hili tunalichukuwa tunafanya *calculations* kwa mfano mwanamke anapoenda *clinic* anapoenda kuhudhuria uzurio la kwanza na la pili na tatu na la nne anatakiwa kuangalia wingi wa damu anatakiwa kupimwa

*urine* ili tuangalie kama kuna maambukizi yeyote katika mkojo ili kuhepusha kifafa cha mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia shinikizo la damu afanyiwe pia na *ultra sound* kwa hiyo, tunafanya *calculation* tuone ni gharama zipi ambazo tunaweza kuzibeba kama Serikali na wananchi tuone ni gharama zipi lakini Bima ya Afya tunaamini ndio itakuwa ndio mwarobaini wa sera hii ya bure au ya msamaha kwa wagonjwa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwa upande wa mama na mtoto ni suala la ubora wa huduma tunakubaliana nanyi Waheshimiwa Wabunge amesema pia Mheshimiwa Paresso kama asilimia 99 ya wanawake wanaenda *clinic* je wanapata huduma bora na Waheshimiwa Wabunge mimi sina ajenda nyingine nilivyorudi Wizara ya Afya ajenda yangu ni ubora wa huduma na sio bora huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka watanzania wapate huduma bora za afya akifika pale achunguzwe vizuri apate vipimo vyote apate dawa anazohitajika mmesema vizuri Waheshimiwa Wabunge hata ile lugha tu mgonjwa pale tayari ni mgonjwa, anapoenda pale anafokewa ananyanyaswa anasemwa tayari unamwongezea magonjwa kwa hiyo, hili ni eneo ambalo tutalipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwenye hii huduma za afya mama na mtoto Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Naibu Waziri tunawabana wizarani tuna fedha nyingi nataka kukiri

sisi Wizara ya Afya tuna fedha nyingi za wadau lakini hatuoni matokeo ya fedha hizo ambazo hizi zinawekezwa tumefumuafumua tumepata *NICU (Neonatal Intensive Care Unit)* vyumba vya watato wachanga mahututi 100 tunaenda kujenga katika Hospitali za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumepata fedha kwa upande wa Benjamin Mkapa tunakwenda kuanza kujenga Hospitali ya Taifa ya mama na mtoto lakini pia tutajenga hospitali ya saratani, kwa hiyo hili ni eneo ambalo tutalipa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la afya ya akili Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ameongea hapa kama kiutani lakini ni jambo kubwa sana na mimi nimeshawa-*challenge* watu wangu ni lazima pia tutoe taarifa na kuwekeza katika afya ya akili na bahati mbaya Tanzania afya ya akili tunaichukulia kama *criminal issue* kama suala la jinai hapana ni suala la afya na hapa tunaweza tukajiona wote tuko sawa lakini afya ya akili ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jesca kama utaridhia naomba nimteuwe Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kuwa balozi wa Afya ya Akili nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hili jambo lazima tusione aibu kulisema hata nyumbani ndoa *divorce frustration* ni kwa sababu pia ya afya ya akili, hata huu ukatili nilikuwa naongea na Waziri Gwajima wiki iliyopita hivi baba mzazi unambaka

vipi mtoto wako wa miaka minne, mitano kama sio tatizo la Afya ya Akili tumeongea kwa kweli hili jambo tutalipa kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la afya kwa watu wenye ulemavu Mheshimiwa Hadija Taya umeliongea vizuri na hili bahati nzuri nimeshaongea na wataalam wangu nimewaambia taarifa zetu za Wizara ya Afya nataka pia tulipoti kuhusu *rehabilitative services* huduma za utengamao ikiwemo huduma kwa watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Stella Ikupa amekuwa akizungumza huduma za wanawake wenye ulemavu katika kujifungua kwa hiyo tumeshapeleka maombi tunaifumua Wizara ya Afya pia nimesema lazima tuwe na kitengo maalum *unit* ambayo itahusika na masuala ya *rehabilitative services* huduma za utengamao ikiwemo huduma kwa watu wenye ulemavu na watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nimepigiwa kengele ya kwanza niseme tu kuna suala la gharama za kuwaona daktari ni kubwa ni kweli na hata jana nawa-*challenge* watu wangu tumegeuza hospitali kama vile *TRA*, hospitali kazi yetu ni kutoa huduma sio kukusanya mapato kwa hiyo, sasa hivi unakuta gharama kubwa na nimemuomba Waziri Mkuu ridhaa ukiangalia mwongozo ule ni wa 1997 nitatoa mwongozo wa kusema zahanati ya kumuona daktari isizidi kiasi gani, Kituo cha Afya isizidi kiasi gani, Hospitali ya Wilaya isizidi kiasi gani Hospitali ya Rufaa ya Mkoa isizidi kiasi gani na Hospitali za Taifa isizidi kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaumiza watanzania na ndio maana wanakimbilia kwenda kuwaona waganga wa kienyeji, Mheshimiwa Tabasam pia nimpokea mchango wako wa maandishi gharama za *dialysis* ni *very expensive* mtanzania gani ataweza kulipa laki mbili na nusu kwa siku mara tatu ni laki saba na nusu kwa wiki, kwa hiyo, ni eneo hili nalo Rais Samia ameshatuelekeza tunalifanyia kazi na tutahakikisha huduma bora za wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunarudi kulekule kabla hujaenda kuhitaji *dialysis* tunataka tuepuke tujikinge na magonjwa haya yasiyoyakuambukiza watanzania nawaomba sana tuwekeze kwenye afya zetu kwa kujali tunavyokula tujiulize wangapi mmekula mboga, wangapi mmekuala matunda katika wiki hii tumeambiwa angalau bia usinywe nyingi bia mbili tatu kwa siku lakini watu wanapiga mpaka bia 10/15 sigara kupita kiasi, pombe.

Mheshimiwa Spika, muda hautoshi. Nimalize kwa kukushukuru wewe kwa kusimamia vizuri mjadala huu. Narudia tena kwa Waheshimiwa Wabunge, afya siyo jambo la kuchekea chekea, afya ni jambo kubwa. Tunatambua dhamana kubwa ambayo tumepewa ya kusimamia afya za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuwa mwepesi sana wa kufanya ziara katika majimbo, lakini amekuwa mwepesi sana wa kusimamia

masuala ninayoyaelekeza. Mheshimiwa Dkt. Mollel nakushukuru sana. Nimshukuru Katibu Mkuu Prof. Makubi pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Shekalaghe pamoja na Mganga Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema; samahani mtani wangu Mheshimiwa Kabula na Mheshimiwa Mkundi wa Ukerewe, hii tunavyofumua, fedha ziko Wizara ya Afya. Nataka kuwaambia, fedha zipo. Tunakwenda kununua *ambulance boat* mbili kwa ajili ya Ukerewe na Mafia ili tuwezeshe pia rufaa za wagonjwa katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nimeshamwelekeza Katibu wangu Mkuu kuwasiliana na Katibu Mkuu TAMISEMI tufanye *assessment* ya zahanati zote nchini, wana vipimo gani na vipi hawana? Vituo vya afya na hospitali, tutakwenda kununua kwa kutumia fedha hizi ambazo zipo, zinatumika kwa ajili ya semina, kwa ajili ya safari, kwa ajili ya kongamano, kwa ajili ya mambo ambayo hayawagusi wananchi moja kwa moja. Jana nimewauliza wenzangu Wizarani, mnaposema tumefanya hivi, mimi Waziri na Naibu Waziri tutasimama kwenye mkutano wa hadhara kuwaambia Watanzania, tumetumia Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya semina, kwa ajili ya kongamano, kwa ajili ya matamasha, Hapana. Fedha tutaipeleka kwenye mambo yanayowagusa Watanzania hususan wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kukushukuru, pia kuishukuru sana familia yangu, kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jiji la Tanga. Tanga tunasema, jiji la mahaba na ukarimu, lakini tunataka liwe la mahaba, ukarimu na maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 7,344,615,864

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na Mheshimiwa Anastazia Wambura anahitaji ufafanuzi wa jambo mahususi la kisera. Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**Mhe. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nia yangu siyo kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ni kutaka tu ufafanuzi kidogo. Kumekuwa na mgongano wa miongozo kati ya *NHIF* na Wizara. Hili tunaliona na zimetokea *incidence* kwamba unakuta daktari ana-*prescribe* dawa kulingana na *Standard Treatment Guidelines* lakini *NHIF* mwongozo wake anasema kwamba kuna baadhi ya dawa zisitolewe katika baadhi ya vituo vya afya. Sasa matokeo yake ni kwamba wanapopeleka madai kule *NHIF* wanakuwa hawalipwi na inatokea kwamba wakati wa ukaguzi *CAG* anaichukulia ile kama ni hoja ya ukaguzi. Naomba kupata ufafanuzi lakini pia nijue kama Serikali itakuwa tayari sasa kuhakikisha kwamba inakuwa na mwongozo mmoja kwa ajili ya ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie kweli hilo tatizo lilikuwepo, lakini Mheshimiwa Waziri alishaelekeza; na kwa sababu moja, kwenye *STG* kulikuwa kuna dawa chache sana ukilinganisha na dawa zilizoko sehemu nyingine ambapo sasa bima walikuwa wanafuata ile *STG*. Sasa hivi zimeongezeka dawa mpaka zaidi ya 400 na kuanzia tarehe 1/7/2022 zinaenda kutumika ambapo itaondoa hilo tatizo ambalo Mheshimiwa anasema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa amekaa, kwa hiyo, ameridhika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit..... Sh.1,964,242,360*
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* .................. Sh.1,776,964,016
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit* ....................... Sh. 538,952,447
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit* ................................................Sh. 258,437,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* ...............................................Sh. 988,091,660
Kifungu 1007 – *Legal Service Unit* ........................Sh. 326,930,029
Kifungu 1008 – *Information and Communication and Technology Unit* ...................Sh. 762,165,415
Kifungu 2001 – *Curative Services Delivery* .. Sh. 463,663,312,844
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*............. Sh.18,474,931,060
Kifungu 2004 – *Nursing and Midwifery Services Division* ..........................................Sh. 672,458,253
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Units* ............................................Sh.1,120,028,000
Kifungu 3001 – *Preventive Services* .................Sh. 25,961,606,227
Kifungu 3002 – *Health Assurance Division* .......... Sh. 748,969,984
Kifungu 3003 – *Health Emerg. Preparedness Response Unit* ..................................................Sh. 290,670,000
Kifungu 4002 – *Social Welfare* ............................... Sh. 62,000,000
Kifungu 5001 – *Human Resource*

*Development*..........................Sh. 29,335,290,841

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 60 - *Regional Referral Hospitals***

Kifungu 6001 - *Amana Regional Referral Hospital Dar es Salaam* ....................................................................Sh.00
Kifungu 6002 - *Bombo Regional Referral Hospital – Tanga*Sh.00
Kifungu 6003 - *Dodoma Regional Referral Hospital* ..........Sh.00
Kifungu 6004 - *Geita Regional Referral Hospital* ................Sh.00
Kifungu 6005 - *Iringa Regional Referral Hospital*.................Sh.00
Kifungu 6006 - *Kagera Regional Referral Hospital* .............Sh.00
Kifungu 6007 - *Katavi Regional Referral Hospital* ...............Sh.00
Kifungu 6008 - *Ligula Regional Referral Hospital – Mtwara*Sh.00
Kifungu 6009 - *Manyara Regional Referral Hospital*...........Sh.00
Kifungu 6010 - *Mara Regional Referral Hospital*.................Sh.00
Kifungu 6011 - *Maweni Regional Referral Hospital – Kigoma* .........................................................................................Sh.00
Kifungu 6012 - *Mawenzi Regional Referral Hospital – Kilimanjaro*..............................................................Sh.00
Kifungu 6013 - *Mbeya Regional Referral Hospital*..............Sh.00
Kifungu 6014 - *Morogoro Regional Referral Hospital*.........Sh.00
Kifungu 6015 - *Mount Meru Regional Referral Hospital – Arusha* .........................................................................................Sh.00
Kifungu 6016 - *Mwananyamala Regional Referral Hospital – DSM*.................................................................................Sh.00
Kifungu 6017 - *Njombe Regional Referral Hospital* ............Sh.00

Kifungu 6018 - *Sekoutoure Regional Referral Hospital – Mwanza*.................................................................. Sh.00
Kifungu 6019 - *Shinyanga Regional Referral Hospital* ........ Sh.00
Kifungu 6020 - *Simiyu Regional Referral Hospital*................ Sh.00
Kifungu 6021 - *Singida Regional Referral Hospital*.............. Sh.00
Kifungu 6022 - *Sokoine Regional Referral Hospital – Lindi* . Sh.00
Kifungu 6023 - *Songea Regional Referral Hospital – Ruvuma* ........................................................................... Sh.00
Kifungu 6024 - Songwe *Regional Referral Hospital* ............ Sh.00
Kifungu 6025 - *Sumbawanga Regional Referral Hospital – Rukwa*.......................................................................... Sh.00
Kifungu 6026 - *Tabora Regional Referral Hospital* .............. Sh.00
Kifungu 6027 - *Temeke Regional Referral Hospital – Dar es Salaam* ....................................................................... Sh.00
Kifungu 6028 - *Tumbi Kibaha Regional Referral Hospital Pwani* ........................................................................... Sh.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu havikutengewa Fedha)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, vifungu vilivyotajwa na Katibu havijatengewa fedha kwa hivyo tunaendelea.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

***Fungu 52 – Wizara ya Afya***

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ....... Sh. 20,399,909,868
Kifungu 2001 – *Curative Service*.................... Sh.112,917,251,819

Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer* ........... Sh. 65,000,000,000
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*..........................................Sh.200,142,800,000
Kifungu 3001 – *Preventive Service* ................ Sh.134,572,094,313
Kifungu 3003 – *Health Emerg. Preparedness Response Unit*.............................................Sh.00
Kifungu 5001 – *Human Resources Development*..........................Sh. 22,100,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake ya kupitia Bajeti ya Wizara ya Afya Fungu 52 kwa Mwaka 2022/2023. Naomba kutoa hoja

kwamba, taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii ni mojawapo ya Bajeti ambazo Bunge zima limesema ndiyo. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana. Nachukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote ambao wanaongozwa na Katibu Mkuu kwa hotuba yenu ambayo mmeiwasilisha leo hapa Bungeni, na pia mlishaiwasilisha kwenye Kamati yetu ya Huduma za Jamii. Kwa hiyo, kwa namna ambavyo mmewasilisha leo, imeashiria kwamba mnafanya kazi kwa karibu kabisa na Kamati na mnasikiliza ushauri mnaopewa na Wajumbe wa Kamati, na

mawazo yao mengi mmeyachukua. Kwa hiyo, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Pamoja na pongezi hizo, kwa niaba ya Bunge Zima, naishukuru sana Kamati yetu ya Huduma za Jamii na Wajumbe wote na Viongozi wa hiyo Kamati; Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa kazi nzuri sana ya kuisimamia Wizara hii kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma wanayostahili. Yale yote ambayo Waziri ameyasema hapa pamoja msaidizi wake, Naibu Waziri, kwamba wanaenda kuyafanyia kazi, hata yale ambayo yalikuwa pengine hayajatajwa kwenye hotuba, ni wazi ninyi ndio mmeyaanzisha kutoka kwenye Kamati yenu. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika wachangiaji humu ndani, wapo Wabunge ambao wamechangia ambao hawatoki kwenye Kamati hii nao wametoa mawazo yao na Mheshimiwa Waziri amesema yote wameyachukua na wanaenda kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge ambao mmeweza kupata nafasi ya kuchangia na wengine tumewasikia hapa na wengine mmechangia kwa maandishi. Kwa hiyo, wote nia ni njema, tunakataka wananchi wapate huduma bora kabisa kwenye eneo hili afya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, niseme sasa rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara

ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamepitishwa Rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunawatakiwa kila la heri katika ahadi zenu zote ambazo mmesema mnaenda kuzifanya na mabadiliko makubwa ambayo tunayategemea kutoka kwenye Wizara hii, kwa sababu kama mlivyosema wenyewe kwamba bajeti hii inaenda kuleta mapinduzi makubwa kwenye utoaji wa huduma za afya tunayatarajia hayo kwa wananchi wetu mtakapoanza utekelezaji wa bajeti hii. Tunawatakia kila la heri.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hapa, amesema kwamba mimi kama naridhia Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kuteuliwa kuwa Balozi wa Afya ya Akili, sasa kwa yale maelekezo niliyokuwa nimeyatoa huko nyuma, sikukusudia kwamba mimi ndiye nitakuwa naridhia hapa mbele; lakini Mheshimiwa Waziri nataka kuamini kwamba hajamteua kuwa Balozi wa Afya ya Akili kwa sababu tu ya mchango wake wa leo. Nataka kuamini anayo na mambo mengine yanayoashiria yupo vizuri kwenye hilo eneo, kwa hiyo, anaweza akaisaidia pengine Wizara kwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri huo ni uchaguzi wako, lakini pia vigezo ulivyojiwekea wewe kwenye Wizara. Pia kwenye bajeti humu wakati napitia mafungu, sijaona sehemu ambapo mabalozi wametengewa kwa ajili ya kufanya kazi yao vizuri. Kwa sababu mabalozi lazima wawezeshwe kusafiri hapa na

pale kutoa elimu, kufanya uhamasishaji na mambo kama hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wewe utaangalia mwenyewe, siyo kwa sababu ya maneno uliyosema hapa, lakini utatazama ukirudi ofisini kama ni muda muafaka wa kuteua balozi ukiwa umejipanga kabisa na mafungu. Kwa sababu namfahamu huyu Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ni mtu wa pilika. Sasa ukishamwambia yeye ni balozi, basi utamsikia kila mahali ana kazi hizo. Kwa hiyo, uwe na utayari wa kumpa huduma stahiki huyo atakayekuwa anaitwa Mheshimiwa Balozi. Sijajua kama atakuwa ameshapita vigezo ama vipi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 17 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*